1 JUNI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Arobaini – Tarehe 1 Juni, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tumshukuru Mwenyezi Mungu, leo tumekutana tena tarehe 1 Juni, 2026 katika Kikao chetu cha Arobaini, Mkutano wa Tatu.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. MOHAMMED KASSIM SALUM K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali yetu, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki. Kwa niaba Mheshimiwa Isack.

Na. 471

Ujenzi wa Barabara za Lami Mji wa Ngarenanyuki Arumeru

MHE. ISACK J. COPRIANO K.n.y. MHE. JOSHUA S. NASSARI aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwenye Mji wa Ngarenanyuki kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na ujenzi wa barabara mbalimbali katika halmashauri ya Arumeru kupitia *TARURA*. Katika mwaka fedha 2026/2027 Serikali imeweka katika bajeti kiasi cha shilingi milioni 168.5 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na kufanya usanifu wa ujenzi wa Barabara za Mwakei – Orkung'wado (kilometa 3.94) na Ngarenanyuki – Kisimiri *Primary School* (kilometa 3.66) zilizopo katika Mji wa Ngarenanyuki kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea kuboresha mfumo wa barabara, Wilaya ya Arumeru kwa miaka mitatu ya fedha 2023/2024 hadi 2025/2026 iliidhinishwa bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 19.4 zilizotumika katika ujenzi na matengenezo ya barabara. Aidha, mwaka wa fedha 2025/2026 Wilaya ya Arumeru imeidhinishiwa shilingi bilioni 7.8 kwa ajili ya ujenzi wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 91.2 ambazo zitajengwa ama kufanyiwa matengenezo ikiwa pamoja na madaraja madogo na makubwa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa barabara za mijini nchini ikiwemo katika Mji wa Ngarenanyuki. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Isack Joseph.

MHE. ISACK J. COPRIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anajua fika barabara ni kiungo cha Wilaya zaidi ya tatu Longido, Siha na ni lango la kuingia kwenye hifadhi zetu. Je, hamwoni sasa ni wakati mwafaka wa Serikali kupeleka fedha ili barabara hizo zitengenezwe ili kuleta maendeleo kwa wananchi hawa walioko katika maeneo hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Isack Kadogoo, Mbunge wa Jimbo la Monduli kwa uchapakazi wake kwa Wananchi wa Monduli, lakini nimhakikishie kwamba Serikali inatambua umuhimu wa barabara hizi katika Mji wa Ngarenanyuki, lakini pia na barabara za vijijini katika Halmashauri ya Arumeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika kipindi cha miaka mitatu zaidi ya shilingi bilioni 19 zimepelekwa kwa ajili ya kujenga, kukarabati na kuboresha barabara zetu na katika bajeti ya mwaka huu, tayari tumetenga shilingi bilioni 7.8 na fedha hizi zitapelekwa kuhakikisha kwamba barabara hizo zinajengwa na zinakarabatiwa, lakini madaraja na makalavati ili kuwezesha barabara ambazo zinaunganisha halmashauri za jirani kama Longido na maeneo mengine ya utalii ziweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha tunafanya hivyo na hili kwa Arumeru lakini pia Jimboni kwako Monduli tuna bajeti nzuri tutahakikisha kwamba tunapeleka fedha ili kuboresha barabara katika Halmashauri ya Monduli. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bahati Ndingo.

MHE. BAHATI K. NDINGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri tuna barabara yetu ya Igalako - Mwatenga mpaka Mapala iko katika hali mbaya sana na wakulima wanashindwa kupitisha mazao yao msimu huu wa mavuno. Nini mkakati wa dharura wa Serikali kuhakikisha barabara hii inapitika? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mbunge wa Jimbo la Mbarali na jirani yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Jimbo la Mbarali lina shughuli nyingi hususan kilimo cha mpunga, na kuna changamoto kubwa ya barabara. Changamoto hii imeongezeka kufuatia mvua nyingi ambazo zimenyesha msimu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali na qananchi wote wa Mbarali kwamba kwanza Serikali imeshatoa maelekezo kwa Mameneja wa *TARURA* kote nchini akiwepo Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Mbarali, watangaze zabuni 60% ya bajeti yetu yote kwa ajili ya kuanza marekebisho ya barabara zote zilizoharibika katika Wilaya ya Mbarali; na kujenga madaraja na kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea na shughuli zao za ujasiriamali na usafirishaji kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, barabara hiyo tutaipa kipaumbele cha hali ya juu ili itengenezwe mapema iwezekanavyo. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Mbeya na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Mbarali wafike mara moja kwenye barabara hiyo, waifanyie tathmini na kuona kiasi cha fedha kinachohitajika ili iweze kufanyiwa matengenezo kwa haraka. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Regina Malima.

Na. 472

10% ya Mapato ya Halmashauri Kutowafikia Wanawake Vijijini

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA K.n.y. MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha 10% ya fedha za mapato ya halmashauri inawafikia wanawake wa vijijini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya 10% hutolewa kwa kutumia mfumo wa kieletroniki wa *Wezesha Portal* ambao unatoa fursa kwa makundi maalumu ikiwemo kundi la wanawake wa vijijini kuomba mikopo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea kusimamia huduma za mikopo huku watendaji wa kata na vijiji wakiwasaidia wananchi wa vijijini, hususan wanawake, kujisajili na kuwasilisha maombi yao ili kuwezesha hata wale wasiokuwa na uelewa wa TEHAMA au vifaa vya mawasiliano kupata huduma hiyo kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha uwazi na kuhakikisha walengwa halisi wananufaika, maombi yote ya mikopo hufanyiwa uhakiki kuanzia ngazi ya Kamati za Maendeleo

za Kata ili kuhakikisha vikundi vinavyopitishwa vinatoka katika maeneo husika ya vijijini na kuzuia matumizi yasiyo sahihi ya anwani za vijijini na vikundi visivyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa utoaji mikopo kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2026 unaridhisha, ambapo Serikali ilipanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 112.29 kwa wanawake na jumla ya shilingi bilioni 136.01 zimetolewa sawa na 121%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kuwa vikundi vya wanawake vinapata mikopo zaidi kuliko vijana na watu wenye ulemavu kutokana na mabadiliko ya kanuni yaliyowezesha kuhamisha fedha za kundi moja endapo hakitatumika kwa robo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango huo ili kuhakikisha wanawake wa vijijini wanapata fursa stahiki za kiuchumi kupitia mikopo hiyo, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Regina Malima.

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi kwa wanawake wanaoishi vijijini katika kutumia mfumo huu ambao unahitaji matumizi ya simujanja katika masuala ya *application,* na wanawake wengi wanaoishi vijijini hawana simu hizo. Je, Serikali ina mpango gani mbadala wa kuwasaidia wanawake hawa ambao wengi wao ndio wanufaika wa hizi fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa nini Serikali imeamua kuzipeleka fedha hizi benki ilhali kuna mifuko mingi ya wanawake ambako hizi fedha zingeweza kuwekwa na wanawake waweze kupata fursa ya kuweza kukopa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, benki kunakuwa na *procedure* nyingi sana na wanawake wengi hawawezi kufikia hiyo mikakati ambayo inatolewa na benki. Serikali haioni kwamba ni vizuri fedha hizi zikawekwa katika mifuko mingine ambako wanawake wanaweza wakakopa? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Malima kwa namna ambavyo anawakilisha Watanzania katika Bunge hili Tukufu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza Serikali inatambua kwamba kuna changamoto ya baadhi ya akina mama kupata mikopo hii na hususan akina mama wa vijijini kwa sababu kwa sababu tunatumia Mfumo wa kieletroniki wa *Wezesha Portal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo huu ulianzishwa kwa makusudi baada ya kuona bila kutumia mifumo hii, kwa utaratibu wa mwanzo kulikuwa na udanganyifu wa kiasi kikubwa kwa vikundi ambavyo vinapokea mikopo ya 10% na wanawake, wengi wenye sifa na haki ya kupata mikopo hiyo hawakuweza kupata kwa sababu hatukuwa na mfumo mzuri wa kufanya *tracking.* Kwa hiyo, Serikali ikafanya maamuzi ya kuhakikisha tunatumia mfumo wa kieletroniki ili kudhibiti matumizi yasiyo sahihi ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mafanikio yana changamoto zake. Changamoto ni kwamba baadhi ya wanawake wa vijijini hawana uwezo wa kuwa na simu hizo (simujanja) na Serikali imeweka utaratibu, kwanza, tunao Maafisa Watendaji wa Vijiji, Maafisa Watendaji wa Kata tunazo Kamati za Mikopo kwenye ngazi ya kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vikundi vya wanawake katika maeneo ya vijijini wanapata huduma hizo kupitia kwenye Kamati, na Maafisa Maendeleo wetu wa jamii wanafika katika

maeneo hayo kuwezesha vikundi ambavyo haviwezi ku-*access smartphone* ili waweze kupata huduma ya simujanja na kuomba mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kutoa elimu na kuendelea kuhamasisha Maafisa Maendeleo na Watendaji wa Serikali katika vijiji na kata zetu ili waweze kuwasaidia akina mama ambao wanahitaji huduma hiyo ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, Serikali ilifanya utaratibu wa kujifunza ufanisi wa mikopo ya 10% kwa njia ya benki na kwa njia ya utaratibu wa sasa uliopo. Ndiyo maana zile halmashauri 10 kati ya 184 ndizo ambazo zilipelekwa kwenye upande wa benki kama *pilot* ili kuona kama tukienda kwa utaratibu wa benki tutakuwa na mafanikio makubwa kuliko utaratibu wa halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafahamu na taarifa zinaonesha kwamba mikopo ile ambayo imetolewa kwenye halmashauri zetu inakwenda kwa ufanisi mkubwa zaidi kuliko ile mikopo inayotolewa kwenye benki, na hivyo Serikali inaendelea kufanya tathmini kuona uwezekano wa kuhimiza benki zifanye vizuri zaidi au kuondokana na utaratibu huo ili twende kwenye mifuko mingine ambayo akina mama wanaweza wakapata mikopo hiyo kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumepokea maoni yake na Serikali itayafanyia tathmini na kuona utaratibu mzuri zaidi wa kuboresha huduma za mikopo ya 10%. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Motto.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, mfuko huu ulianza muda mrefu, je, Serikali imewahi kufanya tathmini ya kujua ni vikundi vingapi vya wanawake vimefikiwa hapa nchini? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishafanya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 mpaka 2023/2024 tuliitisha taarifa za vikundi vyote ambavyo vimewahi kukopeshwa na kuona vimerejesha kiasi gani. Hili ndilo lililosababisha kuanza na mfumo huu wa maboresho ya kwenda sehemu benki na sehemu kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anahitaji vikundi vingapi, na ni suala la takwimu, ninaomba baada ya kipindi hiki nimpatie takwimu hizo kwa uhakika, ni vikundi vingapi tangu tumeanza vimewahi kunufaika na mikopo hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 473

Uhitaji wa Watumishi wa Afya Mkalama

MHE. JESCA D. KISHOA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka watumishi katika zahanati na vituo vya afya vilivyopo Wilaya ya Mkalama?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Iramba Mashariki, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa kada za afya za miaka mitano mfululizo, ambapo

kati ya mwaka 2021 hadi 2025, jumla ya watumishi 37,921 wa kada ya afya wameajiriwa na kupelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021 hadi 2026 Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imepokea jumla ya watumishi 316. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 ilipokea watumishi 11 na mwaka wa fedha 2025/2026 ilipokea watumishi 149 wa kada mbalimbali za afya. Watumishi hawa wamepangwa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti na kuajiri watumishi wa afya na kuwapanga katika vituo vyenye upungufu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuendelea kutupatia watumishi katika kada hii ya afya. Takwimu zinaonyesha kwamba tumevuka nusu ya *target*, uhitaji ulikuwa ni watumishi 962 na sasa tuna watumishi 485, tunashukuru sana. Mwaka 2025 mmetuletea watumishi 87, mwaka huu mmetuletea watumishi 62. Changamoto ni moja tu ambayo ni fedha za kujikimu kwa hawa watumishi, zaidi ya milioni 120 zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni haja ya kutoa fedha kulingana na idadi ya watumishi wanaokuwa *posted* kwenye nafasi hizi za kazi ili kuondoa changamoto ya wao kufanya kazi wakiwa wana *stress*, wakiwahudumia wananchi wa Mkalama kwa kukosa fedha za kujikimu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca David Kishoa. Kwanza nianze kwa kumpongeza kwa

maana anafuatilia sana wananchi wa Jimbo la Iramba Mashariki, na kwa hakika wamepata Mbunge ambaye anawasemea kwa ajili ya changamoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga fedha na kutoa motisha kwa watumishi wetu. Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 Serikali imetenga jumla ya bilioni 13 kwa ajili ya watumishi hawa kwa maana ya zile posho za kuitwa kazini. Pia imetenga jumla ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya posho ya likizo na imetenga jumla ya shilingi bilioni 7.5 kwa ajili ya posho za uhamisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto za watumishi wetu na namna inavyoweza kutoa motisha hizi ili kuwafanyia *retention mechanism* katika makazi yao hasa kwenye zile Halmashauri za pembezoni ili waendelee kuchapa kazi na kuleta tabasamu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kutoa motisha hizi ili kuhakikisha watumishi wetu nao wanapata tabasamu la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Lyabukande iliyopo katika Jimbo la Solwa, kuna kituo kizuri cha afya kimejengwa. Kuna jengo la upasuaji, kuna vifaa vyote, kuna madaktari, lakini hakuna mtaalamu wa kutoa dawa za usingizi. Je, ni lini Serikali itapeleka mtaalamu wa kutoa dawa za usingizi ili huduma ziweze kufanyika? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Christina Mnzava kwa swali hili kwa maana ya kwamba kweli tuna upungufu wa watumishi hawa wa kutoa dawa za usingizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwelekeze Mkurugenzi pamoja na *DMO,* wakae pamoja, waone namna ya kuajiri watumishi hawa angalau kwa mkataba ili waweze kutoa huduma katika kituo chetu cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli Serikali imejenga, tumejenga vituo vyetu vya afya maeneo mengi, ndiyo maana utaona tumekuwa na changamoto hii ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelichukua hilo na tunalifanyia kazi kuhakikisha kwamba tunapeleka watumishi wa kutoa huduma hizi katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri mwenzako, ninawashukuru sana kwa majibu hayo Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, aulize swali lake.

Na. 474

Ujenzi wa Jengo la Kisasa la TAKUKURU - Muleba

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga jengo la kisasa la TAKUKURU Wilayani Muleba?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha TAKUKURU, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwenye bajeti ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya ofisi kulingana na uwezo wa kibajeti. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Muleba katika kiwanja Namba 326 Kitalu "A" Bomani, Muleba Mjini, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya, na Waziri pamoja na Naibu Waziri na TAKUKURU. Kwa hiyo, sitakuwa na swali la nyongeza, ila ni pongezi tu kwa Serikali yangu kwa hii hatua ambayo wameichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika haina jengo la TAKUKURU wala ofisi ya *DSO*. Ni lini Serikali itaenda kujenga majengo hayo kwenye Wilaya ya Tanganyika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza

Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na ofisi za TAKUKURU katika kila eneo kwa maana ya Mkoa, Wilaya pamoja na vile vituo maalum. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma hizi zinasogezwa karibu na wananchi. Kwa sasa, tunatambua kwamba kuna uhitaji mkubwa wa kuwa na ofisi za mikoa, wilaya pamoja na vituo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhitaji wa ofisi nne za mikoa, ofisi 55 za wilaya na ofisi tano za vituo maalum ikiwemo Wilaya ya Tanganyika ambapo tunatambua kwamba hawana ofisi za TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaendelea kutenga bajeti kulingana na uwezo wa Serikali. Kwa hiyo, hata sasa kulingana na uwezo huo wa Serikali, tuko tayari kuanza ujenzi kwenye baadhi ya Wilaya ambazo hazina mahali pa kupangisha au kuna maeneo ambayo kodi ya pango ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, inailazimu Serikali kuanza ujenzi kwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo au Wilaya ambazo wako wanaopata nyumba za kupangisha, lakini zipo ambazo zinapangishwa kwa bei nafuu. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia maeneo hayo, na kwa kadri ambavyo bajeti inaruhusu, basi tutakwenda kujenga hizo ofisi kwenye mikoa, wilaya pamoja na vituo maalum.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana na ninakushukuru kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge, kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Dkt. Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Handeni, aulize swali lake.

Na. 475

Miradi ya Umwagiliaji – Handeni

MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji katika maeneo ya Masatu, Mumbwi, Kwaingoma na Sezakofi?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Handeni. Utekelezaji huo unahusisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa saba katika vijiji vya Masatu, Kwaingoma, Msangazi (Magamba), Nkale, Msasa, Kibaya na Sezakofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bwawa la Masatu umekamilika. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa ya Kwaingoma, Msangazi, Mkale, Msasa, Kibaya na Sezakofi umefikia wastani wa 73.6%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na utekelezaji wa mpango wa uchimbaji wa visima vya umwagiliaji katika maeneo ya Mumbwi, Manga, Mandera na Kwenkwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, tathmini za kitaalam zinaendelea zikihusisha upatikanaji wa rasilimali maji chini ya ardhi, ubora wa maji pamoja na usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji itakayounganishwa na visima hivyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Charles Sungura.

MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ni dhahiri kuwa miradi hii ni uti wa mgongo wa uchumi wa wananchi wa vijiji hivyo alivyovitaja ambavyo ni Kwaingoma, Masatu, Mumbwi na Sezakofi. Je, Waziri yuko tayari kuungana nami katika ziara ya kikazi akajionee hali halisi ya miradi hii, na pia atoe kauli rasmi mbele ya wananchi wangu juu ya utekelezwaji wa miradi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wakati tukiendelea kusubiri kukamilika kwa miradi hii, je, Serikali sasa ina mpango gani wa dharura wa kuleta msukumo katika kukamilisha vile visima ambavyo vimeshaanzwa, pamoja na kuchimba visima vingine ili iwe kama suluhu ya muda mfupi kwa wananchi wale wanaoendelea na kilimo wakati wanasubiri kukamilishwa kwa miradi hii mikubwa ambayo imejibiwa na Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Charles Jacob Sungura kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya ndani ya Jimbo la Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ombi lake la kuambatana na mimi Jimboni kwake mara baada ya Bunge hili kukamilika, nitalitekeleza. Nitaenda mwenyewe ili kujionea kile ambacho amesema Mheshimiwa Mbunge, hasa kwa sababu wote tunajua kilimo cha umwagiliaji ndicho kilimo cha uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo wa Serikali hii sasa hivi ni kuweka nguvu kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa sababu ni kilimo cha uhakika na kinawatengenezea mazingira ya uhakika ya uzalishaji wananchi na wakulima wetu. Kwa hiyo, nimhakikishie, tutaongozana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwenye hili la visima, sasa hivi tayari visima kadhaa vimeshachimbwa katika

maeneo ya Mumbwi, Manga, Mandera na Kwenkwale. Kilichokuwa kimebakia ni ufungaji wa pampu. Sasa hivi taratibu zinakamilika ili pampu zile zianze kufungwa kwenye visima hivyo vianze kutumika kwa umwagiliaji kwenye maeneo hayo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Arif Premji.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ukizingatia Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya 2025 - 2030 Jimbo la Mtwara Vijijini limeahidiwa kuchimbiwa visima vitano kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji. Je, utekelezaji huo utaanza lini? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Premji kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwawakilisha wananchi wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la visima vitano ambavyo vimeshachimbwa na vinasubiri tu pampu kwa ajili ya ufungaji, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zinakamilika kwa ajili ya upelekaji wa pampu kwenye Jimbo la Mtwara. Mara zitakapowasili kule vitafungwa ili zianze kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji kwa wananchi waliopo kwenye maeneo hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Uyui, aulize swali lake.

Na. 476

Ajira kwa Wenyeji Ujenzi wa *SGR*

MHE. SHAFFIN A. SUMAR aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ajira kwa vijana na akina mama wenyeji kwenye ujenzi wa *SGR* katika kituo kidogo cha abiria Nzubuka?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Jimbo la Uyui, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa ajira kwenye mradi wa *SGR* hufuata utaratibu wa ushirikishwaji wa wananchi hasa katika kutoa uelewa kwa wananchi, ambapo hujulishwa ujio wa reli ya *SGR* pamoja na fursa zilizopo katika mradi ikiwa ni pamoja na ajira za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kupata wafanyakazi wa mradi limekuwa ni zoezi la wazi linaloshirikisha Serikali za Kijiji na Mtaa ambapo matangazo yamekuwa yakitolewa katika ofisi hizo ambapo wananchi wanaalikwa kujitokeza. Aidha, kwa wale wanaoomba wanapata msaada wa kusaidiwa kufanya maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya wanaopeleka maombi ya kuajiriwa ni vijana na ajira hizi zimekuwa na uzingatiaji wa ajira za akina mama, ambapo baadhi ya kazi zimetengwa mahsusi kwa ajili ya wanawake na akina mama. Mradi unaendelea kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki na kupewa ajira hasa kazi ambazo zinaleta staha na kulinda heshima za wanawake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shaffin Sumar.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri sana ambayo yanatoa mwanga kwa wananchi wajue utaratibu ulivyokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa, huu mradi unatekelezwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi yetu, na kwa kuwa, tunafahamu kwamba mradi huu unapopita basi Halmashauri husika inatakiwa ifaidike kwa kupata *Service Levy*, je, ni mpango gani wa Serikali wa kuhakikisha kwamba Halmashauri yangu ya Wilaya ya Uyui inapata *Service Levy* inavyotakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mradi huu ni wa kimkakati na umepita katika Jimbo langu kwenye Kata ya Ilolanguru, Kalola na Ndono. Wananchi wameipokea kwa mikono miwili na wamepisha maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa mradi, lakini katika kupisha huo mradi walikuwa wameshafanyiwa tathmini ya kupewa fidia, fedha ambazo hadi leo hawajalipwa na hawaendelei tena kushughulika katika hayo maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kupata kauli ya Serikali, fedha za fidia zitatolewa lini kwa wananchi wangu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Sumar kwa jinsi ambavyo anafuatilia maendeleo ya wananchi wa Jimbo lake la Uyui na kipekee jinsi ambavyo yeye na wananchi wanaopitiwa na reli ya kisasa ya *SGR* inayotoka Dar es Salaam – Kigoma – Mwanza, walivyoupokea mradi huu wa kimkakati ambao ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza maswali mawili. Kwanza, kuhusiana na suala la *City Service Levy*. Ninapenda kumkubalia kwamba ni kweli kabisa panapokuwepo na wakandarasi, wanawajibika na kulazimika kupeleka sehemu ya faida kwenye jamii husika. Hivyo, nitoe maelekezo kwa wakandarasi wa maeneo mbalimbali, kutazama; moja, eneo hili la Uyui na maeneo mengine ili ikiwezekana wananchi wa pale na Halmashauri ya pale iweze angalau kuanza kupata kile sehemu ya faida kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusiana na fidia, ninapenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa yako madai ya fidia ya maeneo mbalimbali nchi nzima. Hii ni kutokana na kwamba miradi yetu inatekelezwa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma ukiunganisha mpaka Mwanza. Ni takribani kilometa 2,292 reli hii ya *SGR* inajengwa. Urefu ambao hakuna nchi nyingine Barani Afrika imeweza kuwa na ujasiri wa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazohitajika ukichukua na kipande mpaka Burundi ni karibu dola bilioni 12 na kidogo. Ukiishia pale kwetu hapa Tanzania ni karibu dola bilioni 11 na kidogo, karibu trilioni 30. Hivyo basi, tutakuwa tunalipa fidia kidogo kidogo kulingana na upatikanaji wa fedha katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba wananchi wa Uyui na maeneo mengine wavumilie na tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali ili miradi hii ijengwe, fidia zao watalipwa kwa sababu kwanza ni haki yao na ni kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa nimeona jina lako hapa unataka kuuliza swali la nyongeza. Nimeona jina liko hapa kwenye kisemeo.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Temeke.

Na. 477

Ujenzi wa Kivuko Eneo la *SGR* Keko – Temeke

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kivuko eneo la *SGR* – Keko ili kurahisisha Wananchi wa Keko kufika Mjini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *Standard Gauge* kutoka Dar es Salaam – Mwanza kilometa 1,219, Tabora – Kigoma kilometa 506 na Uvinza – Msongati kilometa 282. Aidha, ujenzi wa reli ya kisasa pamoja na masuala mengine unazingatia usalama kwa jamii kwa kujenga vivuko vya magari na wapita kwa miguu ili kuepusha ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Keko ambapo reli ya *SGR* inayoingia Bandarini *(Port Link)* inapita, Serikali kupitia *TRC* imejenga kivuko katika daraja Mkuki na pia kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *TANROADS*, Serikali imejenga kivuko katika daraja la Gerezani, hivyo wananchi wa Keko wanashauriwa kutumia vivuko hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na vivuko hivyo, katika mikakati ya kuimarisha zaidi usalama, uzio umejengwa pembezoni mwa njia ya reli ili kuzuia wananchi kukatiza njia ya reli katika maeneo ambayo siyo salama. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa, usalama unazingatiwa katika maeneo yanayoendelezwa kujengwa miundombinu mbalimbali ikiwemo reli ya *SGR*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo, ninaipongeza sana Serikali kwa mpango wake wa kujenga reli ya *SGR* katika nchi yetu ya Tanzania kurahisisha usafiri kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia eneo la mizigo *SGR* inayotoka bandarini. Wananchi wa Keko, eneo la Keko Mwanga *MSD*, eneo la Keko Magurumbasi, Keko Machungwa na Keko Akida, hawana *TLB* ya magari ya daladala na hawana njia yoyote ya usafiri, ni zaidi ya kuvuka reli na kwenda mjini kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo ya Keko Mwanga yana viwanda mbalimbali. Keko kuna Kiwanda cha Singasinga kina takribani wafanyakazi vijana 5,000; Kiwanda cha *T-shirts*, hawa wote wanatarajia kuvuka kwenda mjini kwa kupitia njia ya miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya mikakati yake na mipango yake, kuwajengea hata kivuko cha miguu wananchi wa eneo la Keko Mwanga, ili kuwarahisishia? Kama tunavyoona *SGR* ya kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kuna maeneo wananchi wamewekewa ngazi juu, je, Serikali haioni haja ya kuwaangalia wananchi hawa wa Keko ambao, mimi kama Mbunge niliteseka sana katika eneo hili na Mheshimiwa Diwani wangu wakiwaombea kivuko wananchi wale? Ninaomba Serikali iangalie upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, changamoto inayowapata wananchi wa Keko inafanana kabisa na wananchi wa Chang'ombe, Kata ya Chang'ombe eneo la Toroli. Wananchi hawa wa Chang'ombe Toroli walizoea kukatisha reli kwenda maeneo ya llala, lakini maeneo hayo sasa nayo yamefungwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na mipango yote, yuko tayari kufuatana na mimi kwenda akazione changamoto hizi zinazowakuta wananchi wa Keko na Chang'ombe uweze kushuhudia kwa macho yako?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza mama yangu Mheshimiwa Kisangi kwa jinsi ambavyo anafuatilia maendeleo ya wananchi wake kwa ukaribu na anawapigania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, hiyo ndiyo maana halisi ya Wabunge wa CCM jinsi wanavyopigana kuhakikisha kwamba wananchi wa nchi hii wanapata maendeleo. Pia nimshukuru sana, na nimepokea kwa niaba ya Serikali pongezi zake kwenda kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya kazi

kubwa anayoifanya ya kujenga reli ya kisasa kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nikubaliane naye, nipo tayari kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Uchukuzi, Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa Mnyaa, kwenda kuona changamoto alizozieleza. Mimi pamoja na yeye na timu yangu ya watalaamu, ili ushauri alioutoa, ambao kimsingi ndilo jukumu la Bunge la kuishauri Serikali, tukatazame anachokizungumza na uhalisia uliopo *field*. Kwa sasa, Serikali imeshaimarisha ulinzi eneo lile, imejenga fensi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kulinda miundombinu, kwa sababu pale ndipo ambapo reli inaingia Bandarini. Kwa namna ya kawaida, tuna wajibu sisi wote kama Taifa kulinda miundombinu yetu kuhakikisha tunaweka usalama ili Bandari yetu na reli yetu ibaki kuwa salama. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Josephine Kapoma.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuishukuru Serikali kwa mradi mkubwa sana wa *SGR,* hasa sisi wakazi wa Morogoro. Sasa, Kata ya Kihonda, reli imekata ile kata chini na juu, ambapo wakazi wengi wanatakiwa kutembea zaidi ya kilometa nane kwenda na kurudi hasa wanafunzi na walimu wa Shule ya Uhuru. Tulishatuma maombi kwa *Station Master,* tuone jinsi kama tunaweza tukatumia daraja la dharura, hasa kwa wanafunzi na walimu, kwa sababu wanatembea kwa umbali wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulikuwa tunaiomba Serikali ione kabla kututengenezea kivuko, inaweza ikatusaidiaje kutumia hili daraja la dharura kwa kipindi hiki? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Josephine kwa kuwasemea wananchi wa Morogoro katika eneo husika. Kwanza kwa kuomba

mpango wa muda mrefu kuhakikisha kwamba tunatafuta ufumbuzi, lakini pia maombi yake ya kutumia daraja la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, amekiri kwamba ameshapeleka maombi kwa *Station Master,* nimwelekeze *Station Master,* aende atazame eneo hilo kama maombi hayo yanaweza kutekelezeka hayaingiliani na mipango yetu ya shirika, kwa maana ya kulinda reli yetu, basi yaweze kufanyiwa kazi, na kama yatakuwa na changamoto, basi tuone namna bora ya kuweza pengine kulifanya kazi jambo hilo.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mbunge wa Tunduru Kaskazini aulize swali lake.

Na. 478

Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai

MHE. ADO S. ADO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza kwa ukamilifu mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mkakati wa utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai. Mkakati huo umeainisha shughuli zitakazotekelezwa katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Aidha, Wizara za kisekta na taasisi za Haki Jinai nchini zinatekeleza mkakati huo kupitia mpango na bajeti za kila mwaka. Serikali imejenga mfumo wa kielektroniki unaoitwa *e-Maboresho* wa utoaji taarifa katika kipindi

cha robo mwaka, nusu mwaka na mwaka. Kupitia mfumo huo, taasisi za haki jinai hutoa taarifa ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katimba ambaye nikiri, yeye pamoja na Mheshimiwa Judith Kapinga ni *classmates* wangu na tulipata huduma ya mafunzo na malezi kutoka kwa Mheshimiwa Kabudi na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Hiyo ni *historical facts* ambayo inanipa faraja ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili. Swali la kwanza, kwa kuwa mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Haki Jinai, baadhi ya mapendekezo hayo yanahitaji mabadiliko ya kikatiba na kisheria ili kuleta ufanisi, weledi na uhuru kwenye Taasisi za Haki Jinai kama vile Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, Jeshi la Polisi na taasisi nyingine za Haki Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hadi sasa siyo ndani ya Bunge hili wala kwingineko, Serikali haijaleta programu inayoonesha mchakato wa kupata Katiba mpya utakwendaje, wala haijaleta programu ya mabadiliko ya sheria ambazo zinakuwa na ufanisi wa vyombo vya haki jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa Serikali italeta mchakato wa kupata Katiba mpya ili kututoa wasiwasi baadhi ya wadau, ikiwemo mimi, tunavyodhani kwa mwenendo huu, Serikali na Chama cha Mapinduzi haina nia ya dhati ya kuleta Katiba mpya bali inaitumia ajenda hiyo kama turufu ya kisiasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa muhtasari wa Ripoti ya Haki Jinai hasa ukirejea ukurasa wa 34, aya ya 3.14, imeweka bayana kuwepo kwa malalamiko ya wananchi dhidi ya Jeshi la Polisi, ikitaja vitendo kama matumizi ya nguvu kupita kiasi wakati wa ukamataji, pamoja na kutesa watuhumiwa na

kubambikia watu kesi. Kwa sababu vitendo hivi vinaathiri sana taswira na heshima na kukubalika kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa Serikali itatekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, hasa lile pendekezo na kuleta mageuzi ya kimfumo, kimuundo na kimafunzo, kulitoa Jeshi la Polisi kutoka taasisi ya mabavu kupindukia kwa maana ya *Police Force*, kulipeleka katika taasisi ya huduma za kipolisi kwa maana ya *Police Service?*

MWENYEKITI: Umeeleweka Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukubaliana na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado kwamba ni kweli mimi na yeye tumekuwa katika darasa moja Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, walimu wetu wakiwa pamoja na wengine Mheshimiwa Prof. Kabudi na Mheshimiwa Dkt. Tulia. Kwa msingi huo huo, ninaomba nijibu swali lake la kwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kabisa kuna masuala ya aina mbili. Kuna *normative principles* ambayo ni masuala ya msingi na kuna masuala ambayo ni *operational principles,* masuala ya kiutendaji. Sasa Tume yetu hii ya Haki Jinai, ni kweli ilifanya kazi na ikaja na mapendekezo 333 ambayo baada ya tume kutoa taarifa ile, Serikali tayari imeanza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa masuala ya Tume ya Haki Jinai yaliyotoka, hakukuwa na mapendekezo yoyote ambayo yanagusa zile *normative principles* kwa maana ya kanuni za kimsingi, ikiwemo mabadiliko ya Katiba kama alivyosema yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kuwa masuala yaliyogusiwa katika mapendekezo ya Haki Jinai, ni masuala ambayo yaligusa kwenye *operational principles* ambazo tayari zipo katika Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, kwenye

Bill of Rights, Article 12, Ibara ya 12, Ibara ya 13 inaenda hadi Ibara ya 29.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Ado ni zuri, Serikali tayari ipo katika utekelezaji na ndiyo maana kwenye majibu ya msingi nimeeleza bayana kwamba kuna yale ya kutekeleza ndani ya muda mfupi, kuna yale ya kutekeleza ndani ya muda wa kati na kuna yale ya kutekeleza ndani ya muda mrefu. Serikali imeunda mfumo rasmi wa kutoa taarifa. Taasisi zote za haki jinai, Wizara zote zinazohusika zinatoa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo haya ya Tume ya Haki Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, swali lake ni zuri sana na Serikali itaendelea na utaratibu huu kuhakikisha kwamba mapendekezo yote ya Tume ya Haki Jinai yanatekelezwa ili kuleta ubora na ufanisi kama alivyoainisha yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, nalo linaunganika na swali la kwanza. Amezungumza kuhusiana na Jeshi la Polisi kwamba sasa litoke lisiwe tena ni Jeshi la Polisi, iwe ni *service*. Swali zuri na ni kweli kwenye mapendekezo yale tayari yameshapokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapendekezo ambayo yanagusa sera, yanaenda kwa utaratibu huo, yanapita kwenye *cabinet*. Septemba mwaka huu 2026, kuna Miswada itakuja kwa ajili ya kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake, ninaomba nimpe *comfort* Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote wafahamu kwamba Serikali inafanyia kazi kwa umuhimu mkubwa sana mapendekezo yote ya Tume ya Haki Jinai. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria kwa majibu hayo. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, ninaomba pia kwa sababu wamegusia kuhusiana na Jeshi la Polisi pamoja na masuala ya Haki Jinai na haki kwa ujumla, kwa maana haki za binadamu, kuna maeneo mawili ambayo niongezee pia kwenye majibu mazuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja la kwanza kuhusiana na marekebisho ya Katiba au mabadiliko au Katiba mpya alichokisema, tayari Serikali imekuwa na utashi huo tangu kipindi cha awamu ya nne. Hatua mbalimbali zilifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ado atakumbuka vizuri zaidi wakati wakiwa chuo, mimi nilikuwa kaka yao nimetangulia kidogo. Hata mchakato ule ulikuja kuharibikia kwenye Bunge hili, kwa maana ya upande wa wenzetu kuleta hoja ambazo zilikuwa zinakinzana kidogo. Hivyo, mchakato ule ulisitishwa kwa taratibu ambazo Mheshimiwa Ado anazijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara 98 inaeleza namna ambavyo kwanza imetambua uwepo wa mahitaji kulingana na matakwa na mahitaji ya kijamii na maendeleo, kwamba kuna wakati tunaweza tukafanya aidha kurekebisha, kufuta au kuboresha matakwa ya kikanuni na kikatiba kwa kufuata taratibu ambazo zimeainishwa kwenye Ibara 98 na Bunge linakuwa na fursa ya kutunga sheria kwa ajili ya kufanya michakato hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la Katiba hata kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeelezwa na tuko tayari nalo. Wakati utakapofika, asiwe na shaka haya mambo yanaenda kwa utaratibu na taratibu kwanza za *procedures* za kisheria pamoja na kibajeti. Kwa hiyo, jambo hili liko tayari, na Serikali imekuwa tayari na imekuwa ni ajenda yetu wala siyo ya mtu mwingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye kuhusiana na masuala ya sheria, haki jinai, amegusia masuala ya taratibu za

kusimama na nini. Mheshimiwa Ado kwa sababu ni mwanasheria anaweza kuwa na faida nzuri zaidi ya kukumbuka au kurejea *notes* zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tuna *generations* za *human rights.* Tuna *first generations,* tuna *second generation* na *third generation* ambayo tunaenda nayo sasa. Nchi nyingi za Afrika sasa, wengine wako kwenye *first generation* na wengine sasa wanaenda kwenye *second generation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *third generation,* ndiyo hiyo ambayo wamekuwa wakiisema. Tukipata muda mzuri tutajaribu kukumbushana kwenye masuala haya, hatujafika huko. Kuna wenzetu haki za kiuchumi, wengine wanalipwa mshahara inakuwa ni haki na ni wajibu kama *fundamental and basic rights*. Kwetu katika nchi nyingi ambazo bado zinaendelea na zilizoendelea kuna tofauti kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ni mambo ya msingi. Sasa kwenye suala la kuhusiana na mabadiliko ya sheria mbalimbali, tunayo hiyo nafasi, Bunge lako Tukufu mwezi wa Tisa litakuwa ni Bunge la mabadiliko pia ya sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeleta Miswada mbalimbali ya mabadiliko ya sheria, tuna sheria ambazo tayari tumeshazibadilisha, lakini pia hata utendaji wa kawaida ambao wanaelezea kuhusu Jeshi la Polisi. Tatizo, neno "*force*" lazima tuangalie tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza neno "polisi," hata ukiangalia kwenye tafsiri, ni jukumu ambalo limewekwa kikatiba na kisheria. Namna ya wao kufanya kazi, tunayo sheria ya *Police Force* na *Auxiliary Services*, lakini pia ndani ya hapo tunazo sheria nyingine ambazo zinasimamia utaratibu wa kijeshi ambao ni *PGO (Police General Orders)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatoa taratibu ya namna zote ambazo zimeelezwa kikatiba na kwa kuzingatia haki za binadamu na utawala wa sheria. Namna ya kukamata, namna ya kufuatilia

makosa ya jinai na namna ya kufanya upelelezi. Tunayo *Criminal Procedure Act* ambayo ni ya mwaka 1985 na mabadiliko yake. Mheshimiwa Ado anayajua haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nimetaka kusema leo hapa, kumekuwa na upotoshaji mkubwa wa sheria katika kuangalia upande mmoja wa *norms*, wanasahau *norms* na kuelezea zaidi kuhusiana na zile *procedurals,* lakini *substantive laws* hazielezi, na *norms* hazielezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yote yamekuwa yakitengenezwa na kupotoshwa wananchi kwenye masuala ya sheria. Hata ukiangalia kwenye Katiba yetu, mabadiliko ya mwaka 2005 yaliondoa *claw-back clause* zote kwamba sheria ilikuwa unapewa haki kwa mkono wa kulia unanyang'anywa mkono wa kushoto. Zilizitolewa kwa mabadiliko mwaka 2005. Kwa hiyo, tufike sehemu, sitaki kutumia neno baya, lakini niseme tusipotoshe umma. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa majibu ya nyongeza. Vilevile ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa majibu hayo kwa Mheshimiwa Ado. Ninaamini majibu yamejitosheleza na Mheshimiwa Ado ameridhika.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, aulize swali lake.

Na. 479

Kugawa Eneo la Jeshi la Magereza kwa Wananchi

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kugawa hekari chache za eneo la Jeshi la Magereza kwa wananchi wa Ludewa, kwa kuwa kuna upungufu wa ardhi?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Jeshi la Magereza Ludewa ni eneo la Serikali lilopimwa na kupewa Hati Miliki yenye Namba 5381-*NJO,* ambalo linatumika kwa ajili ya uzalishaji wa chakula cha kulisha wafungwa na mahabusu magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, eneo la Gereza Ludewa ni miongoni mwa maeneo ya Magereza ambayo yapo kimkakati katika uzalishaji wa chakula kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula katika Magereza yetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kutoa sehemu ya ardhi katika eneo hilo ni kudhoofisha juhudi za Jeshi la Magereza za kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu Magerezani, sambamba na kuipunguzia mzigo Serikali kama agizo la Serikali na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilivyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii, kupitia Bunge lako Tukufu, kumshauri Mheshimiwa ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, ili kuwezesha wananchi hao kupatiwa ardhi kwa ajili ya shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Kamonga.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Hata hivyo, nitakuwa na maswali madogo mawili ya nyongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Ludewa lina eneo lenye ukubwa wa hekari zaidi ya 6,000, lakini ambalo linatumika hazizidi hekari 400 kwa miaka 30 mfululizo. Kwa hiyo, kuna zaidi ya hekari 5,000 ambazo zimekaa tu hazitumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo dhana ya Jeshi la Magereza kujitegemea ni pamoja na kuweka majengo ya vitega uchumi lakini limejitenga sana na wananchi. Je, Serikali haioni haja ya kutuma wataalamu wakashirikiana na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Kamati yake ya ulinzi na usalama kufanya tathmini na kuona uwezekano wa kutoa maeneo kwa ajili ya stendi ya malori?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu Ludewa tuna tani milioni 420 za makaa ya mawe ambazo zitavutia malori mengi kwenda kule na stendi ya mabasi ambayo itahudumia miaka 70 au 80 ijayo ukizingatia Ludewa ina madini mengi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu watakuwa wengi hivyo, watu watakavyosogea jirani na Magereza itakuwa ni fursa pia kwa jeshi kuweka majengo ya vitega uchumi. Je, Serikali kwa nini isitume wataalamu wakashirikiane na Mkuu wa Wilaya kufanya tathmini na kuona uwezekano wa kutoa maeneo hayo ya muhimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ninatambua kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na sasa kumekuwa na kero kwa madereva wa malori na mabasi katika kuhuisha leseni zao za udereva, wengine wanalazimika waende mafunzo. Kwa kuwa hii imekuwa kero, sasa Serikali haioni haja, pamoja na nia yake njema ya kupunguza ajali barabarani kukaa na madereva hawa na kuwasikiliza maoni yao, kwa sababu mtu kuacha familia kwenda Dar es Salaam kuhudhuria mafunzo na gharama imekuwa kama kero; je, Serikali kwa nini isikae na madereva hawa na kusikiliza maoni yao ili ione namna nzuri ya kuziweka hizi sheria? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Kamonga swali lako la pili ulilete kama swali la msingi kwa hasabu halihusiani na swali la Magereza. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kumjibu swali la nyongeza Mheshimiwa Joseph, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamwomba Mheshimiwa Mbunge tuweke *Hansard* vizuri kuhusiana na ukubwa wa eneo la Gereza la Ludewa. Gereza la Ludewa lina ukubwa wa hekta 3,306.4 na kati ya ukubwa wa eneo hilo, hekta 701 zinatumika kwa ajili ya kilimo, hekta 2,228 zinatumika kwa ajili ya hifadhi ya milima, hifadhi ya miti asili na hifadhi kwa ajili ya vyanzo vya maji. Vilevile hekta 279.4 hizo zipo kwa ajili ya makazi na hekta 98 zimelengwa kuongezea hifadhi kwa ajili ya upandaji wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya msingi ya kuhusu eneo hilo na matumizi yake, nimepokea rai au Wizara inapokea rai aliyoitoa Mheshimiwa Mbunge ya kuona namna gani tunaweza kupeleka wataalamu kwa ajili ya kufanya tathmini ili hilo lengo ambalo analipendekeza liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara kupitia Ofisi ya Katibu Mkuu, itaandaa timu ya wataalamu kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza na *crew* ya wilaya na mkoa kule pamoja na Mkuu wa Magereza Mkoa pamoja na Mkuu wa Gereza husika kwa ajili ya kupata tathmini ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye dhana ya uwekezaji kwa sasa Serikali inakwenda kwenye suala la *PPP* kupitia Dira yetu ya 2050, hivyo katika mwelekeo huo na katika dhamira ile ile ya kuliona Gereza hili ni la kimkakati kama jibu la msingi lilivyokuwa, tutaendelea kuona kwamba yale mapendekezo ya hiyo Kamati yanazingatia suala la eneo hili ni la kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushuru sana kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Chemba aulize swali lake.

Na. 480

Ujenzi wa Majosho Wilaya ya Chemba

MHE. KUNTI Y. MAJALA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majosho katika Wilaya ya Chemba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hilo.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi na ukarabati wa majosho katika kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe na mbung'o nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ilianza kutekeleza mpango wa ujenzi wa majosho tangu mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo hadi sasa jumla ya majosho 754 yamejengwa kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilijenga majosho matano yenye thamani ya shilingi milioni 90 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kwenye Vijiji vya Mlongia, Msaada, Mondo, Masimba na Tumbakose. Majosho hayo yalikamilika kwa 100% na yanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuratibu ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa miundombinu muhimu ya mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo majosho ya Wilaya ya Chemba kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za mifugo kwa wananchi kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninatoa rai kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kutenga fedha kutoka katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majosho katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi nimwulize Mheshimiwa Waziri maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, sisi Wilaya ya Chemba ni wafugaji na wewe unajua vizuri na tuna adha kubwa ya upungufu wa majosho kiasi kwamba mifugo yetu mingi imeendelea kutokuwa bora kwa sababu ya magonjwa mbalimbali yanayoendelea kuwakabili wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru kwanza kwa hayo majosho matano mliyotupatia, lakini bado hayatoshi na mmetuambia halmashauri tutenge. Mheshimiwa Waziri halmashauri tunahangaika na kukarabati hata yale ambayo yalikuwa ya nyuma ambayo yana muda mrefu na yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ipo tayari kutuongezea kwa mwaka huu wa fedha majosho 11 kwenye vijiji vya Magungu, Bugelika, Umepa, Gonga Chini, Chambalo, Kidoka, Kombiri, Kaachini pamoja na Njoeni Muone?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mheshimiwa Waziri yupo tayari kufika kwa wakulima na wafugaji wa Wilaya ya

Chemba aende akakutane nao wakamwoneshe adha kubwa wanayoipata kwa ajili ya kukosa majosho na malambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda kuwasikiliza na kuweza kuwasaidia kuwatatulia changamoto zinazoendelea kuwakabili kwenye tasnia yao ya ufugaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Kunti kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Nianze na hili la pili ambalo ni jepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo tayari kufanya ziara na nimeanza kufanya ziara kwa mpangilio na haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba viongozi wote ambao amewateua kumsaidia washushe mabega yao ya vyeo waende kwa wananchi, wawasikilize kero zao, hofu zao, na mapendekezo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kufanya hiyo na mimi ninamwahidi, kwa sababu Chemba ni karibu, ninaweza nikaenda hata kabla ya Bunge hili katika moja ya siku za Jumamosi na Jumapili nikawasikilize wafugaji wa Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ambalo lilikuwa la kwanza la nyongeza ni gumu kwa sababu na niwe mkweli mahitaji ya majosho nchi nzima ni makubwa na uwezo wa Serikali wa kuhudumia majosho hayo unategemea na upatikanaji wa fedha kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi. Tutaendelea kuongeza idadi ya majosho na miundombinu mingine kama mabwawa kutegema na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakuhaidi kama hali ya fedha itakuwa nzuri tutaongeza majosho katika Wilaya ya Chemba siyo hayo 11 lakini kutegemeana na upatikanaji wa fedha na mambo mengine yatategemea pia na ziara nitakayoifanya na kufanya tathmini kuzungumza na wafugaji

tushauriane namna ya kukabiliana na changamoto ya majosho. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusherehekea wiki ya maziwa ambapo Kitaifa ilikuwa Mkoani Iringa, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu. Kwa kuwa Wilaya ya Kilolo, Kata ya Uhambingeto Wananchi wa Kijiji cha Kipaduka na Ng'osi wameungana na kuanza kujenga josho pamoja na bwawa kwa nguvu zao wenyewe. Je, Serikali sasa ipo tayari kuwasaidia hawa wananchi ili waweze kukamilisha hayo malengo yao na kuondoa changamoto katika vijiji hivyo viwili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kama una majibu ya Iringa, maana tumetoka Chemba.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ritta tulikuwa wote katika shughuli ya kuadhimisha wiki ya maziwa, na amehusika katika kufanya kampeni ya kuhamasisha unywaji wa maziwa kwa kunywa maziwa yeye mwenyewe nikimwona kwa macho yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jitihada za wananchi, ninaomba kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. Ritta niwapongeze wananchi wa vijiji alivyovitaja kutoka kwenye Jimbo lake la Kilolo kwa moyo wa kujitegemea na moyo wa kujitolea kutatua changamoto za majosho na mabwawa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo tayari kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kuunga juhudi za wananchi ili mipango yao waliyoiweka iweze kutekelezeka na tutafanya hivyo kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Kigoma Mjini.

Na. 481

Kuwasaidia Wavuvi wa Ziwa Tanganyika

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi wa Ziwa Tanganyika kwa kuwapatia vifaa vya kisasa, kupunguza tozo na kuboresha teknolojia ya uvuvi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaomba kujibu swali namba 481 la Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa jamii ya wavuvi katika maendeleo ya Sekta ya Uvuvi nchini. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imenunua boti za kisasa 16 na kuzigawa kwa wavuvi katika Mikoa ya Kigoma 12, Rukwa boti tatu na Katavi boti moja na kunufaisha jumla ya wavuvi wadogo 444 ambapo kati yao wanawake ni 146 na wanaume ni 292 kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imefanikiwa kusanikisha vizimba 29 katika Wilaya ya Kigoma ili kuwasaidia wavuvi kuendeleza shughuli za ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa samaki katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya pili Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaongeza boti tatu katika Wilaya ya Kigoma kwa ajili ya kuwezesha wavuvi wadogo kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepunguza tozo ya kusafirisha dagaa nje ya nchi kutoka dola 0.5 hadi dola 0.3 kwa kilo kwa dagaa wa Ziwa Tanganyika, ada za leseni za kusafirisha dagaa kutoka dola 1,000 hadi dola 250 kwa mwaka, na baadhi ya leseni kuunganishwa ili kupunguza gharama za uendeshaji kwa wadau wa uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeruhusu matumizi ya leseni moja ya uvuvi katika eneo la maji, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo kila halmashauri ilikuwa inatoza leseni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye vifaa na zana za uvuvi zikiwemo nyavu, nyuzi za kutengenezea nyavu, injini za kupachika, ndoano, maboya, boti za *fibber*, magari ya ubaridi, mitambo ya ubaridi na mitambo ya kuzalisha barafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuondoa kodi hiyo ni kupunguza gharama za uendeshaji kwa wavuvi na wadau wa Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza asiyeshukuru kwa kweli hata kwa Mwenyezi Mungu anapata kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutusikiliza Waheshimiwa Wabunge ambao tunatoka kwenye Ziwa Tanganyika kwa kutolifunga Ziwa Tanganyika. Tulimwomba na tukaweka hoja hajalifunga mpaka leo. Tunashukuru sana, wavuvi wanamwombea sana Mheshimiwa Waziri, ataendelea kuwa Waziri hivyo hivyo mpaka miaka mitano inakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Ni juzi Mheshimiwa Waziri amekutana hapa na wavuvi 30 ambao wamefunga safari kutoka

Kigoma wamemfuata kwa ajili ya kujadiliana suala ambalo walikubaliana wao wenyewe kuhusiana na upana wa matundu ya nyavu na unene wa nyuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyavu zinazovua Ziwa Tanganyika na nyavu zinazovua Ziwa Victoria zinatofautiana kwa sababu Ziwa Victoria ni ziwa lenye tope, na Ziwa Tanganyika ni ziwa lenye mchanga. Kwa hiyo kwa upana ule wa matundu yanayotumika Ziwa Victoria yakitumika Ziwa Tanganyika samaki hawapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina lengo gani la kukubaliana na wavuvi wa Kigoma Mjini kutumia nyavu ambazo walikubaliana tangu mwanzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kumekuwa na *operation* ambazo zinaendelea za kutokomeza uvuvi haramu na mimi ninaunga mkono, sikubaliani na uvuvi haramu, lakini zimekuwa zikiambatana na rushwa na mateso makubwa kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waliopewa kazi ya kwenda kufanya *operation* wamekuwa wakiwakamata wavuvi na kuwaomba hela. Wanakamata mashine, wanataka shilingi 300,000 au shilingi 200,000. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari tufunge safari mimi na yeye uende tukawasikilize wavuvi uso kwa uso? Maana mimi nimechoka kuwasikiliza na sina majibu, na yeye ndio mwenye majibu kama Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando almaarufu Baba Levo. Nimepokea shukrani lakini shukrani siyo za kutofunga Ziwa, shukrani ninazipokea kwa sababu ya kukaa tukasikilizana, na tukajadiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maziwa, (na ninarudia mbele yako) ni mbaya na lazima tuchukue hatua kulinda rasilimali

hizo kwa sababu zina manufaa makubwa kiuchumi na kwa maisha ya wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufunga ziwa ni suala la kimkataba na la kisheria baina ya nchi zetu tatu. Tulichokubaliana ni kwamba tufanye tathmini kuona matokeo tuliyoyapata na pengine tukianza hatua nyingine tuweze kufanya vizuri kutokana na tathmini tutakayoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kulinda rasilimali za uvuvi ni suala la kufa na kupona na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi tushirikiane kwa manufaa ya uchumi wetu. Sasa nijibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilifanya kikao na Waheshimiwa Wabunge, Mbunge wa Kigoma Kaskazini na Kigoma Kusini pamoja na wananchi kutoka katika Wilaya ya Kigoma, kutoka Kigoma Ujiji anapotoka Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tayari nimeshakutana na wataalamu na wameshanipa maelezo ya kitalaamu kuhusu nyavu gani zinafaa katika Ziwa Tanganyika na vyavu gani hazifai katika Ziwa Tanganyika kwa sababu hizo hizo tu za kulinda rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wale waliokuja na wananchi nitawaalika ama wiki hii au wiki ijayo tukae na wataalamu tufafanue kwa undani ni nyavu gani zinafaa? Kwanini zinafaa? Nyavu gani hazifai? Kwa nini hazifai? Baada ya hapo nitaomba tuelewane, tuheshimu utaalamu kwa lengo hilo hilo tu la kulinda rasilimali za uvuvi ili ziweze kuwanufaisha Wanakigoma na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu operesheni, hakuna operesheni yoyote tunayoifanya. Tumeacha utaratibu wa operesheni, sasa hivi tunasimamia sheria saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna mtu huko anasema, "ninafanya operesheni," huyo nipeni taarifa nimshughulikie kwa mujibu wa taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutafanya operesheni kama ilivyokuwa huko nyuma. Suala la kulinda rasilmali siyo la operesheni, ni suala la kufanya kazi ya kusimamia sheria kwa njia endelevu saa 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kinachoendelea ni kufanya elimu kwa vitendo. Nimetuma watu watoe elimu kwa vitendo. Halafu baada ya hapo kuanzia Julai tutaanza kutekeleza kanuni mpya ambazo tumepata maoni ya wadau zitakazotusaidia kusimamia rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametaja jambo la rushwa. Nikiri mbele yako taarifa hizo ninazo, siyo kutoka Kigoma tu, ni nchi nzima. Tunao baadhi ya watendaji wetu, Maafisa Uvuvi katika ngazi za Halmashauri na Maafisa Uvuvi katika ngazi ya Wizara ambao sio waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wapo katika taasisi nyingine kama maliasili kwa mamlaka kama *TAWA*. Tumeshapokea malalamiko hayo, na kwanza nimeanza kufanya mazungumzo na Waziri wa TAMISEMI pamoja na Waziri wa Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tusimamie nidhamu ya watumishi wetu na kuchukua hatua kwa wale ambao wanachafua taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tumepanga kukutana na Mamlaka ya TAKUKURU ili watusaidie kwa sababu rushwa ina sheria zake na inatakiwa isimamiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nimewahi kutangaza namba yangu ya simu na hapa nirejee tena. Namba yangu ya simu ni 0754 022915. Ninaomba wavuvi mnaodaiwa fedha tuwekeane mitego kwa simu hii tuwakamate hawa watu, lakini mjue kutoa rushwa ni kosa na kupokea rushwa ni kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatafuta kuwanasa wanaotoa rushwa na wanaopokea rushwa. Kwa hiyo, waache wananchi wavuvi wasitoe rushwa, na wakitoa rushwa nikiwanasa watakwenda mbele ya sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abubakari Asenga swali fupi la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwa kuwa Wilaya ya Kilombero wavuvi na wafugaji wana changamoto kubwa zaidi kuliko hata hizo za Kigoma, na kwa kuwa wavuvi wamenielekeza niombe Mheshimiwa Waziri awatembelee, azungumze nao ili waweze kumwelezea vizuri na ushahidi kuhusu changamoto zao, na kwa kuwa Morogoro, Kilombero ni karibu zaidi kuliko Kigoma, je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenda Kilombero kuzungumza na wavuvi wangu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu katika Wilaya ya Kilombero na jimbo analoliongoza kuna rasilimali za uvuvi kupitia Mto Kilombero na nimeshapokea malalamiko kutoka kwa wavuvi kwa njia hii hii ya simu, ninapata taarifa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua wanachangamoto za kimahusiano kati ya mamlaka za Serikali na wavuvi. Pia wana changamoto za kiuvuvi ambazo pia Wizara ina jukumu la kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafanya ziara Kilombero kukutana na hao wavuvi kwa lengo hilo hilo tu la maelekezo ya Mheshimiwa Rais kukutana na wadau wa Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuwasikiliza na kutatua changamoto zao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, Mbunge wa Ulyankulu aulize swali lake.

Na. 482

Kutatua Migogoro ya Wananchi na Wahifadhi
Jimbo la Ulyankulu

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA aliuliza:-

Je, lini Serikali itatatua migogoro ya mipaka kati ya wananchi na Hifadhi katika Vijiji vya Mwaduti, Mtwiga, Imagi, Sasu na Mkiligi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, Mbunge wa Ulyankulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Mwaduti, Mtwiga, Imagi, Sasu na Mkiligi ni mojawapo ya vijiji 22 vilivyokuwa vimeanzisha makazi na shughuli nyingine za kibanadamu ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Mto Igombe kinyume cha Sheria ya Misitu sura 323 inayolenga matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa jamii zinazopakana na haifadhi kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 Serikali kupitia Baraza la Mawaziri wa Kisekta ilipitia maeneo ya vijiji hivyo 22 vilivyokuwa vimeanzishwa ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Mto Igombe uliopo Wilaya ya Kaliua na kumega eneo la hekta 90,583.98 sawa na

ekari 226,459.90 kwa ajili ya matumizi ya makazi, malisho na kilimo ili kuondoa mgogoro wa mipaka kati ya hifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baada ya kumegwa kwa eneo hilo, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa hifadhi kwa kuweka jumla ya vigingi 30 ili kuonyesha mipaka mipya kwa lengo la kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu mipaka mipya ya hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba nitoe rai kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Wilaya ya Kaliua kwa ujumla kuendelea kushirikiana na watendaji wetu ili kutunza na kulinda hifadhi hiyo kwa maslahi mapana ya Taifa. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhael Lufungija.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, nianze kwa kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa niaba ya wananchi wa Ulyankulu kwamba tulipata kweli vile vijiji 22 mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mheshimiwa Waziri, ni muhifadhi na wananchi wa Ulyankulu tutaendelea kulinda hifadhi. Ninalo swali moja la muhimu ambalo ninataka Mheshimiwa Waziri anisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ya Serikali na Wizara iliyofanya, Kijiji cha Mwaduti kwenye Kata ya Mwongozo, Kitongoji cha Kipendamoyo na Kata ya Nhwande, Kijiji cha Ntwigu, Kitongoji cha Kabanga, Kasandawala, Isozi pamoja na Didia, Sasu, Kijiji cha Ibilingo na Kwa Ilege, Kitongoji cha Shininga, eneo la Mtakuja, wakati Serikali inafanya urekebishaji wa mipaka, hayo ni maeneo ya vitongoji ambayo yalisahaulika. Wapo wananchi wamekaa kwa muda mrefu huko, lakini tunapata changamoto kubwa ya maeneo ya malisho na eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini sasa Serikali itafanya mapitio upya ili kufanya marekebisho madogo madogo kwenye hayo

maeneo ili wananchi wapate fursa na kupata maeneo ya kupumua kwa ajili ya malisho na kilimo kwenye maeneo ya vitongoji hivyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Lufungija kwa jinsi ambavyo amekuwa mtetezi wa kweli wa wananchi wa jimbo lake kwa masuala haya ya kuwahakikishia usalama wa ardhi ya kuishi, ya kulima na yakufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake hili moja amaalo anasema kuna maeneo yalisahaulika wakati wa marekebisho ya mipaka iliyofanywa kupitia ile *task force* ya Baraza la Mawaziri wa Kisekta, nimhakikishie kwamba Serikali ipo tayari kupeleka wataalamu wakapitie hiyo mipaka kwa kushirikiana na halmashauri ya wilaya na pamoja na ofisi yake na nimwombe sana ahakikishe na yeye anashiriki katika zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nimhakikishie kwamba Serikali baada ya kufanya mapato hayo, na kama kuna haja ya kufanya marekebisho stahiki ili wananchi hawa ambao amewaelezea na maeneo aliyoyataja wapate maeneo ya kufanya shughuli zao za maisha, ninaomba nitoe wito kwa wataalamu wetu kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii waendelee kutoa elimu ya tafsiri ya mipaka sahihi ya maeneo ya hifadhi na maeneo ya wananchi ili kuondoa migogoro hiyo ambayo inaweza ikatokea kwa kutoelewa mipaka sahihi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela, Mbunge wa Maswa Mashariki aulize swali lake.

Na. 483

Ujenzi wa Barabara ya Maswa - Lalago

MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Maswa – Lalago itajengwa kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. George Lugomela, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Maswa - Lalago ni sehemu ya barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom - *Sibiti River* - Lalago hadi Maswa kilometa 389. Ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kazi ya ujenzi zinaendelea kwa sehemu ya Mbulu Garbabi kilometa 25 na Labai hadi Haydom kilometa 25 pia. Aidha, taratibu za malipo ya awali ya mkandarasi zinaendelea kwa sehemu ya Nkoma hadi Lalago kilometa 65 ili kumwezesha mkandarasi kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu zilizobaki ikiwemo Maswa hadi Lalago kilometa 34 Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. George Lugomela.

MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha Maswa mpaka Lalago takribani kilometa 34 ni kiungo muhimu kati ya barabara kuu ya Mwigumbi hadi Lamadi na kitaunganisha na barabara ambayo ameitaja kwamba mkandarasi anaenda kulipa malipo ya awali cha Nkoma hadi Lalago. Kipande hiki pia kikikamilika pamoja na Nkoma - Lalago na maeneo mengine aliyoyataja barabara kuu inayoenda mpaka Mbulu na Karatu kuunganisha Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara ambayo inategemewa kuunganisha na Mkoa wa Singida kitaifanya barabara hii iwe ndiyo njia fupi kabisa ya kutokea Kanda ya Kaskazini kwenda Kanda ya Ziwa, pia na kutokea Kanda ya Kati kwenda Kanda ya Ziwa. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuharakisha kipande hiki kwa lami kilometa 34 kutoka Lalago hadi Maswa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, jambo la kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Lugomela kwa swali hili zuri la wananchi wa Maswa na mkoa mzima wa Simiyu. Jambo la pili, nimechukua *concern* yake inayohusu kipande cha kutoka Maswa mpaka Lalago kilichobaki ambacho ni kilometa 34 ili tuweze kukamilisha kufika pale Maswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama nilivyojibu katika jibu la msingi kwamba Serikali itakapopata fedha tutahakikisha kwamba tunaunganisha hiki kipande kilichobaki ili sasa wananchi wa maeneo haya waweze kutoka Maswa mpaka kufika Singida na kuja katika mikoa ya kati na hadi Dar es Salaam kwa urahisi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa wabunge muda wetu wa maswali umefikia mwisho. Kwa hiyo, sasa tutakuwa na matangazo. Nitaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Spika ambao ni Ndugu Claude Kimu, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanaume Tanzania; Ndugu Faidin Vuai, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanaume Zanzibar; Ndugu Privatus Evarest, Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Wanaume Zanzibar; Ndugu Mema Juma, Naibu Mwenezi Taifa Umoja wa Wanaume; Ndugu Wadi Ally, Mnadhimu Umoja wa Wanaume; Ndugu Abdulkarim Said, Naibu Mwenezi wa Mahusiano Umoja wa Wanaume; Ndugu Kibozero Khaji, Afisa Miradi Umoja wa wanaume; na Ndugu Mazengo Mazengo, Chifu wa Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana Umoja wa Wanaume kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Naibu Spika, Ndugu Daniel Sarwat, mpigakura wake kutoka Babati, Mkoani Manyara. Karibu sana mpigakura wa Naibu Spika wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokaa kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wageni tisa kutoka Bunge la Zambia; Ndugu Tronne Nyirenda, Mkurugenzi Msaidizi Masuala ya Fedha na Kiongozi wa Msafara; Ndugu Fabian Lwizi, Mkurugenzi Msaidizi, Ukaguzi wa Ndani; Ndugu David Phiri, Afisa Mipango na Uajiri Mwandamizi; Ndugu Ndiyoyi Sikopo, Mkaguzi wa Ndani; Ndugu Peter Nyirongo, Afisa Manunuzi Mwandamizi; Ndugu Kennedy Bwalya, Afisa Manunuzi Mwandamizi; Ndugu Chola Kaoma, Mkalimani wa Lugha ya Alama; Ndugu Jason Manda, Mkalimani wa Lugha ya Alama; na Ndugu Lewis Mambwe, *Chief Inspector* na Katibu wa Msafara. Karibuni sana wageni wetu kutoka Bunge la Zambia. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Doroth Onesphoro Gwajima Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni Ndugu Eliakim Maswi, Katibu Mkuu; Ndugu Amon Mpanju, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Felista Mdemu, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Adela Adam, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu; Dkt. Bakari George, Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru; Dkt. Joyce Nyoni, Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii; Ndugu Geofrey Mafungu, Mwenyekiti wa Wakuu wa Vyuo Vya Maendeleo ya

Jamii; Ndugu Jaspar Makala, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali; Ndugu Emmanuel Mwasota, Mwenyekiti wa Chama cha Wataalam wa Ustawi wa Jamii Tanzania; Ndugu Victor Kabuje, Rais wa Chama cha Watalaam wa Maendeleo ya Jamii; Ndugu Azza Hajji, Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake katika Uongozi; na Ndugu Zainab Shomari, Makamu Mwenyekiti wa UWT Taifa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, hongera. Makofi hayo ni yako Ndugu Suzani Kunambi, Katibu Mkuu wetu wa UWT. Karibu sana Katibu Mkuu wetu. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge wamefurahi sana. Mheshimiwa Ndugu Riziki Khamisi, Naibu Katibu Mkuu UWT, karibuni sana viongozi wetu wote hao waliotajwa, pia na viongozi wetu wa UWT karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Dkt. Avemaria Semekafu, Mwenyekiti wa Jumuiya za Wanawake wa Vyama vya Siasa Tanzania. Karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Waziri ni Wakili Methusela Gwajima, Mume wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Tunakushukuru sana Ndugu yetu Wakili Methusela kwa kututunzia vizuri Ndugu yetu Mheshimiwa Dorothy. *(Makofi)*

Wageni wengine wawili ni wa Mheshimiwa Gwajima, haw ani Wadau wa Maendeleo ya Jamii kutoka Taasisi ya *So They Can* kutoka Babati Mkoani Manyara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wawili ni wa Mheshimiwa Gwajima kutoka Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambao ni Ndugu Saci Mbaraka Alhaji Batenga, Mkuu wa Wilaya ya Chunya; Ndugu Langaeli

Akyoo, Katibu wa Mkoa wa Mbeya. Karibu sana Katibu wetu wa CCM, Mkoa wa Mbeya.

Yupo pia Ndugu Edina Mwaigomole, Mwenyekiti wa UWT, Mkoa wa Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile ambaye ni Naibu Waziri wetu wa Uchukuzi. Hawa ni viongozi wa *Red Cross*, Ndugu Godfrey Kipngetich Korir, Rais wa *Red Cross* nchini Kenya; na Ndugu Lucia Pande, Katibu Mkuu wa *Red Cross* Tanzania. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutoka Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 12, wa Mheshimiwa Revocatus Clayton Chipando, ni Watumishi wa Ofisi ya Mbunge Jimbo la Kigoma Mjini. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Revocatus Chipando ni Dkt. Melenda Omar, Askofu Mstaafu wa *TAG*; na Mwandishi wa vitabu vya Ndugu Abdillah Juma Mkurugenzi wa *Mandas Store* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tuna mawakili wanne kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika *(TLS)*. Karibuni sana mawakili wetu kutoka *TLS*; walimu 58 kutoka shule ya msingi Nane Nane na Shule ya Sekondari Alfagems za mkoani Morogoro. Karibuni sana walimu wetu kutoka huko Morogoro. *(Makofi)*

Pia wapo Viongozi 28 wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe cha Mkoani Morogoro. Karibuni sana *(Makofi)*.

Pia, tunao wanafunzi 124 na walimu nane kutoka shule ya awali na msingi Weslay ya Mkoani Morogoro. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Weslay mkoani Morogoro. Karibuni sana wageni wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunalo tangazo linatoka kwa Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limekuwa na utaratibu wa kuhamasisha Wabunge vijana kujiunga na kupata mafunzo ya uzalendo yanayotolewa na Jeshi letu la Kujenga Taifa.

Mafunzo haya ambayo hutolewa katika Kambi mbalimbali za JKT hapa nchini yanalenga kuenzi tunu za Taifa ambazo ni uzalendo, utu, umoja, uwajibikaji, uadilifu, uwazi na Lugha ya Taifa Kiswahili.

Kwa kuzingatia manufaa yanayopatikana kwa kushiriki mafunzo hayo, Bunge kwa kushirikiana na JKT linapanga kuendesha mafunzo hayo kwa mwaka huu ili kutoa fursa kwa Wabunge wa Bunge la Kumi na Tatu, ambao wengi ni vijana, kupata nafasi ya kujiunga mafunzo maalumu ya JKT kwa Wabunge, ambayo hutolewa kwa kipindi cha mwezi mmoja. *(Makofi)*

Kwa sababu hiyo, Wabunge wote wenye nia ya kupata mafunzo hayo ya uzalendo, kupitia JKT, wanaombwa kujiorodhesha katika Ofisi ya Katibu wa Bunge. Mara baada ya kupata idadi ya Wabunge wenye nia ya kujiunga, utaratibu kamili wa ushiriki wa mafunzo hayo utatolewa.

Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kutumia fursa hii adhimu kabisa. *(Makofi)*

Katibu, tuendelee.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa nimkaribishe Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wetu wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ili aweze kuwasilisha Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dorothy Gwajima, karibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote kwa idhini yako, ninaomba kufanya masahihisho madogo, kwenye ukurasa wa 82 wa kitabu changu cha hotuba, kutoka juu mstari wa sita, inaposoma aya ya 147 isome 154. Baada ya hapo ninaomba kitabu changu cha hotuba kiingie kama kilivyo kwenye Kumbukumbu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa mwaka 2025/2026, na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema na Neema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo ili kuwasilisha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua tena kuiongoza Wizara hii muhimu kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa nchi yetu. Ninatambua kuwa Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii, malezi na makuzi ya watoto na uwezeshaji wa kiuchumi kwa makundi maalum unafanyika kwa kasi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaahidi kwamba Wizara itaendelea kutimiza majukumu yake kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa tena na Watanzania na kuchaguliwa kwa kishindo kuendelea kuongoza nchi yetu kwa kipindi kingine. Aidha, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawaombea viongozi wetu afya njema, hekima na mafanikio katika kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha pili kupitia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza kwa uongozi wake madhubuti na juhudi zake za kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii. Tunatambua na kuthamini mchango wake mkubwa katika kuimarisha ushiriki wa wanaume katika kukuza usawa wa kijinsia kupitia kampeni ya "*He for She*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa 12 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 1 Aprili, 2026 ambayo imeainisha vipaumbele na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilala na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani Mheshimiwa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge, nikianza na wewe mwenyewe Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso kwa umakini wenu katika kutusaidia kuongoza vikao vya Bunge. Ninawaombea na kuwatakia kazi njema katika majukumu yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, na Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, kwa ushauri na maelekezo yao wakati wa maandalizi ya bajeti hii. Hakika, ushauri na maelekezo ya Kamati yamekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara yangu kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa afua za maendeleo na ustawi wa jamii. Vilevile, ninawashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ahadi yangu kwamba Wizara itaendelea kushirikiana nao kwa karibu ili kuhakikisha tunatekeleza

kwa vitendo maono na dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwa na jamii yenye ustawi na maendeleo endelevu na jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kila siku. Amekuwa msaada mkubwa katika kusimamia shughuli za Wizara, kutoa ushauri na kuhakikisha utekelezaji wa majukumu unafanyika kwa ufanisi. Hakika, Wanawake wa Mkoa wa Mbeya hawakukosea kumchagua mwakilishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaishukuru Menejimenti na wataalamu wote wa Wizara, ninayoiongoza, wakiongozwa na Bwana Eliakim Chacha Maswi, Katibu Mkuu, na wasaidizi wake, Wakili Amon Mpanju, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia maendeleo ya jamii na makundi maalum, na Bi. Felister Mdemu, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia maendeleo ya jinsia na wanawake, kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama na Maendeleo ya Jamii Tengeru, pamoja na Wakuu wa Vyuo Nane vya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao mkubwa unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa salamu za pole. Ninatoa pole kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, na wenye Ulemavu; pia, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Iddi Nassor, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), waliotoa mchango mkubwa katika Taifa kupitia Bunge na Serikali. Tunawaombea pumziko la amani na tunawakumbuka kwa utumishi uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pole kwa kifo cha Mheshimiwa Julie Catherine Manning, mwanamke wa kwanza Tanzania kusoma Shahada ya Sheria na kuhudumu kama Jaji wa Mahakama Kuu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, pamoja na kuwa Waziri wa kwanza wa Sheria mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu maono ya kimageuzi katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/2026, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya kimkakati vya Wizara kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, imebeba ujumbe mkuu kwamba, Maendeleo ya Taifa hayawezi kupimwa kwa miundombinu pekee, bali kwa ubora wa maisha ya watu, uimara wa jamii, usalama wa kijamii, ushiriki wa wanawake katika maendeleo, ustawi wa watoto na wazee, pamoja na uwezo wa wananchi kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapenda kunukuu maneno ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipotoa hotuba yake ya kufungua Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025 Dodoma, alisema, ninanukuu: "Ninamwomba Mungu kuwa mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita usipimwe tu kwa vitu, bali pia kwa tabasamu la utu litakaloachwa kwenye nyuso za Watanzania." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Wizara hii ni mhimili mahususi wa maendeleo ya watu na *engine* ya uchumi jumuishi nchini. Aidha, ni nyenzo ya kuleta mageuzi ya fikra katika jamii ambayo ni msingi muhimu katika kufanikisha Dira ya 2050 yenye lengo la kujenga Taifa lenye demokrasia, haki, na uhuru. Taifa linalozingatia utu, amani, na umoja, Taifa lenye uwezo wa kumiliki na kutumia kikamilifu rasilimali zake kwa manufaa ya wananchi,

pamoja na kuhifadhi, kukuza, na kulinda maadili na tamaduni chanya za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ninayoiwasilisha haiainishi tu takwimu za kibajeti, bali inaeleza maono na mwelekeo wa Taifa katika kujenga Taifa lenye ustawi, mshikamano, maadili, na ushiriki mpana wa wananchi katika maendeleo. Tunaamini kwamba maendeleo ya kweli na endelevu hayawezi kupatikana kwa ukuaji wa uchumi pekee, bali pia kwa kuwa na jamii imara inayojali makundi yote ya wananchi na inayowezesha kila mmoja kushiriki katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, sekta hii ni ya kimkakati na kimageuzi inayojenga msingi wa Taifa lenye watu wenye utu, uwajibikaji, uzalendo, na uwezo wa kuchangia kikamilifu katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusisitiza kwamba msingi mkuu wa Dira 2050 unaojengwa juu ya utawala bora, amani, usalama, na utulivu si kauli ya kawaida ya sera, bali ni uamuzi wa kimkakati wa Taifa letu unaoendelea kuimarishwa na uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kuonesha kwa vitendo nafasi muhimu ya mwanamke kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo imejidhihirisha katika Dira 2050 inayolenga kupunguza pengo la kijinsia kwa angalau 85% na kuiwezesha Tanzania kuwa kinara barani Afrika na kuwa miongoni mwa nchi 10 bora duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuelekea Dira 2050 tunategemea kujenga Tanzania ya wanawake na wanaume wenye uwezo sawa wa kushiriki, kuamua, kumiliki, kuzalisha, kuongoza, na kunufaika na maendeleo ya Taifa. Kwa mtazamo wa kimkakati, Dira 2050 inabainisha kuwa usawa wa kijinsia siyo ajenda ya kijamii tu, bali ni ajenda ya kimageuzi ya kiuchumi na ajenda ya Kitaifa ya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu, ninaomba sasa kusoma Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2025/2026. Katika kuboresha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii kwa mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele vitano ambavyo kwenye kitabu changu nimevitaja kwenye aya ya 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato na matumizi ya fedha za Wizara (Fungu 53). Katika mwaka 2025/2026 Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 9.040 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato. Vyanzo hivyo ni pamoja na ada ya vyuo vya maendeleo ya jamii, ada za malazi kwa wanafunzi wa vyuo hivyo, ada za mwaka za mashirika yasiyo ya Kiserikali, uuzaji wa mitaala ya vyuo vya ustawi na maendeleo ya jamii, na ada za usajili wa wafanyabiashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 3.570 sawa na 39.5% ya lengo la makusanyo ya mapato. Hata hivyo, miongoni mwa sababu iliyochangia kutofikiwa kwa lengo hilo ni pamoja na uhaba na uchakavu wa miundombinu katika vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inaendelea na jitihada za kukusanya mapato katika kipindi kilichobakia ili kufikia lengo la makusanyo yaliyokadiriwa kwa mwaka wa utekelezaji 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu shilingi bilioni 76.057 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 49.115 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 26.941 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 22.646 ni mishahara, na shilingi bilioni 26.469 ni fedha za matumizi mengineyo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 15.415 ni fedha za ndani na bilioni 11.526 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia Aprili, 2026, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 60.456 sawa na 79.49% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 40.740 sawa na 82.95% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 19.719 sawa na 73.19% ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na mchanganuo wa fedha hizo uko jedwali namba 01 ukurasa wa 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara Fungu 53. Hadi Aprili, 2026 Wizara kwa kushirikiana na taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo imetekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika bajeti ya mwaka 2025/2026 na utekelezaji huo umewezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali katika maeneo ya maendeleo na ustawi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuendeleza rasilimali watu katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii. Habari hii nimeieleza kwenye aya ya 29 – 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya jamii. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, inatekeleza kampeni ya mageuzi ya kifikra na mitazamo ya jamii kwa kujenga fikra na mitazamo chanya inayowezesha wananchi kufanya kazi kwa bidii, kuongeza uwajibikaji, kuwa wazalendo, waadilifu, wabunifu na wenye moyo wa kujitolea. Lengo ni kuondoa mitazamo hasi kama utegemezi, kutotumia fursa, kukosa maadili, kukosa uzalendo na kutowajibika, mambo yanayosababisha kutopata maendeleo yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampeni hiyo inakuza ari ya wananchi kushiriki katika kuibua, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kufuatilia shughuli za maendeleo na kuwafanya kuwa kitovu cha maendeleo yao na kuhakikisha miradi ya maendeleo wanayoitekeleza ni endelevu na jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ilitekeleza kampeni ya amsha ari katika Mikoa minne na

kufanya jumla ya Mikoa 21 iliyofikiwa na kampeni hiyo, maelezo kwa kina yako aya ya 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kampeni hiyo jumla ya wananchi 7,184 walishiriki kama walivyoainishwa kwenye aya ya 36. Kampeni hiyo imeimarisha mshikamano wa jamii katika kufanya kazi kwa pamoja, kuongeza uelewa na uwajibikaji wao katika kusimamia na kuendeleza miradi yao, kupunguza utegemezi kwa kuimarisha hali ya wananchi na kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imeendelea kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kutambua umuhimu wao mkubwa katika kuamsha ari ya jamii kushiriki katika masuala ya maendeleo yao na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Maafisa Maendeleo ya Jamii 830 wameajiriwa na kufanya jumla yao kuwa 4,806 sawa na 89.8% kati ya mahitaji ya watumishi 5352 wanaohitajika nchini. Kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii hao ambao wengi wao wapo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wameendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia Aprili, 2026 miradi ya maendeleo imeongezeka kutoka 31,802 hadi kufikia 38,443, ikiwemo miradi ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya 1,632, ujenzi wa madarasa ya shule za awali na msingi 26,467 na madarasa ya shule za sekondari 10,344.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, inaendelea kuratibu kampeni nyingine ya ujenzi wa nyumba bora kupitia kaulimbiu isemayo, ‘Piga Kazi, Boresha Makazi.’

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kampeni hiyo Maafisa Maendeleo ya Jamii wamehamasisha ujenzi wa nyumba bora 944 zenye gharama nafuu na hivyo kufanya jumla ya nyumba bora

zilizojengwa katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kufikia 15,296 tangu kuanza kwa kampeni hiyo mwaka 2022. Taarifa nyingine kuhusu eneo hili la maendeleo ya jamii ziko aya ya 40 - 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha kuhusu utambuzi, uratibu na uendelezaji wa wafanyabiashara ndogondogo. Wizara imeendelea na shughuli za utambuzi, uratibu na usimamizi wa *program* za kuwezesha makundi mbalimbali kiuchumi kama ilivyotajwa kwenye aya ya 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha juhudi za Serikali za kuwatambua na kuwarasimisha wafanyabiashara ndogondogo nchini, Wizara imeendelea na utekelezaji wa zoezi la utambuzi na usajili wao kupitia mfumo wa usajili wa wafanyabiashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki cha utekelezaji jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 56,039 wakiwepo wanaume 25,589 na wanawake 30,450 wamesajiliwa na kufanya jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 143,053 ambao hawa wamesajiliwa kwa hiari yao tangu zoezi lilipoanza mwaka 2024. Kati yao wafanyabiashara 63,246 wamelipia gharama za uchapishaji wa vitambulisho vya kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wafanyabiashara 51,333 sawa na 81.2% ya waliolipia tayari wamepatiwa vitambulisho vyao, huku maombi 11,913% sawa na 18.8% yakiwa katika hatua za uchapishaji na usambazaji. Katika kipindi hiki cha utekelezaji kufikia Aprili, 2026, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 10.5 kwa ajili ya utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zinafanya jumla ya shilingi bilioni 18.5 zilizopokelewa na Wizara na kupelekwa Benki ya *NMB* kwa ajili ya utoaji wa mikopo tangu zoezi hilo lianze Januari, 2025. Kufikia Aprili, 2026, jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 8,426, wanaume 3,906, na wanawake 4,520 wamekopeshwa kiasi cha shilingi bilioni 17.9. Mchanganuo wa mikopo hii kwa kina uko

kiambatisho namba moja mwishoni mwa ukurasa wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 60 - 64 ni maelezo kuhusu makongamano na maonesho mbalimbali ya wafanyabiashara ndogondogo likiwemo la hivi karibuni la Mama na Baba Lishe, Aprili, 2026 ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze kwenye eneo la malezi, maadili, maendeleo na ustawi wa watoto. Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia malezi, maadili, matunzo na ustawi wa watoto pamoja na familia, ambao ni msingi wa kujenga Taifa lenye nguvu kazi yenye tija. Malezi chanya ya watoto yanayoambatana na maadili mema ni nguzo katika kujenga Taifa imara kwa ustawi na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Wizara inaratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya malezi chanya kwa wazazi au walezi na vijana balehe ikiwa ni juhudi za pamoja za kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto. Programu hiyo inalenga kuhakikisha kuwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka nane anapata huduma jumuishi za malezi na makuzi ili kuongeza kiwango cha ukuaji timilifu kutoka 47% ya sasa hadi 90% kama ilivyobainishwa katika Dira 2050. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara imeratibu uandaaji wa mfumo wa upimaji wa matokeo ya malezi na makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ili kufuatilia utekelezaji wa viashiria vya programu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na ongezeko la matumizi ya vifaa vya kielektroniki kwa watoto hali inayochangia upatikanaji wa maudhui yasiyofaa kwa watoto. Tafiti zinaonesha kuwa 67% ya watoto wenye umri wa miaka 12 hadi 17% hutumia simujanja, ambapo 4% kati yao wamekumbana na aina mbalimbali za ukatili mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto dhidi ya changamoto hizo, Wizara ilitoa mafunzo kwa timu ya wawezeshaji 516 kuhusu usalama wa watoto mtandaoni kwa lengo la kuwawezesha kutoa elimu kwa wanafunzi, walimu na watumishi wasio walimu katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mafunzo hayo, wawezeshaji waliweza kuwaelimisha wanafunzi milioni 1.8, walimu 679 na watumishi wasio walimu 232 kutoka Mikoa yote 26 nchini. Ili kuhakikisha Serikali inaendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, ilianzisha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu Usalama wa Mtoto Mtandaoni Mwaka 2024 kama inavyoelezwa kwa kina kwenye aya ya 73.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinavyoathiri afya mwili na akili, jumla ya walimu 4,388 wamepata mafunzo kuhusu namna ya kuanzisha kusimamia na kuratibu afua za ulinzi na usalama wa mtoto shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maelezo kuhusu madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi na sekondari nchini na maelezo kuhusu mabaraza ya watoto yapo katika aya ya 75 na76.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na vitendo vya ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto wa kike ambavyo ni ukiukwaji wa haki za binadamu, Serikali imezindua Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji wa mwaka 2025/2026 unakwenda hadi 2029/2030. Mkakati huu unalenga kuimarisha juhudi za kutokomeza vitendo vya ukeketaji nchini. Mkakati huu unalenga kupunguza kiwango cha ukeketaji kutoka 8% hadi kufikia 4% ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na mikakati iliyopita, mkakati huu umeweka kipaumbele cha ushiriki wa wanaume katika harakati za kutokomeza ukeketaji. Hatua hiyo inatokana na baadhi ya mila na desturi na mitazamo hasi ya jamii inayochochea vitendo vya ukeketaji hususan kwa baadhi ya

wanaume kutokuwa tayari kuoa wanawake ambao hawajakeketwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi husika Wizara imeendesha kampeni rafiki ya kuokoa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani katika mikoa yote nchini. Kupitia kampeni hiyo, jumla ya watoto 6,182 wameokolewa. Watoto 5,663 wameunganishwa na familia zao, kati yao watoto 52 wamehitimu mafunzo mbalimbali ya ufundi. 448 wako katika makao ya watoto na 71 wako chini ya walezi wa kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuzuia watoto kuingia mtaani, sambamba na hilo Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imeanzisha madawati 14 ya huduma za ustawi wa jamii kama nilivyoainisha kwenye aya ya 81 hadi 83. Hii hii ipo kwenye vituo mbalimbali vya mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, inapotokea watoto wamekosa malezi ya kifamilia, Wizara imeweka utaratibu wa malezi mbadala kama vile huduma za watoto wanaolelewa katika makao ya watoto, malezi ya kambo na kuasili kwa lengo la kutoa matunzo ya watoto hao kama nilivyoeleza kwa kina kuhusu huduma hizi kwenye aya ya 84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu na kuimarisha afua zinazolenga kuwaandaa vijana kuingia katika majukumu ya ndoa na familia. Kadhalika, Wizara imeweka msisitizo wa umuhimu wa utatuzi wa migogoro ya familia kwa njia ya usuluhishi, ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imepokea jumla ya mashauri ya ndoa 49,573. Kati ya mashauri hayo mashauri 9,995 yamesuluhishwa na kufungwa, mashauri 836 yalipelekwa mahakamani na mashauri 31,542 bado tunayo tunaendelea kusuluhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya mashauri ya matunzo ya watoto 19,425 yalitokana na watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Kati

ya mashauri hayo 3,500 yamepelekwa Mahakamani na 15,925 yanaendelea kushughulikiwa na Maafisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, Wizara inasajili vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga kama nilivyoeleza kwa kina mchanganuo wake kwenye aya ya 92.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wake wa kisekta imeendelea kuratibu ushirikiano wa wadau mbalimbali wa maendeleo ili kushirikiana na jamii ya makundi yote katika kupambana na kutokomeza ukatili wa kijinsia na kwa watoto ambapo kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jeshi la Polisi, idadi ya watoto walioripotiwa kufanyiwa ukatili wa kingono, imepungua kutoka 10,937 mwaka 2024 hadi 9,902 kwa mwaka 2025. Takwimu hizi ziko kwenye kiambatisho namba mbili mwishoni mwa kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na mafanikio haya, takwimu hizi zinaonesha ukubwa wa changamoto ya ukatili dhidi ya watoto katika jamii yetu na zinatoa wito kwa Taifa kuendelea kuchukua hatua madhubuti zaidi kulinda kizazi cha sasa na kijacho. Wizara itaendelea kwa kasi zaidi kuratibu wadau wake ili kuhakikisha ukatili wa kingono dhidi ya watoto unatokomezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine watoto wameendelea kukabiliwa na ukatili wa kutupwa, kuibwa na kutelekezwa ambapo kwa mwaka 2025 taarifa ya Jeshi la Polisi inaonesha kwenye Kimbatisho Namba 2(b) kuwa, jumla ya watoto 165 waliripotiwa kutupwa, 137 kutelekezwa na 86 kuibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya ni kinyume kabisa na haki za watoto kuishi kama ilivyoainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Mtoto na Sheria ya Mtoto. Ijulikane kwetu sote kuwa mapambano dhidi ya ukatili wa watoto si jukumu la Serikali pekee bali ni wajibu wa Taifa zima. Hivyo, tunapaswa kama jamii kuungana kwa dhati kwani bila kufanya hivyo tutakuwa

tunahatarisha msingi wa kizazi chenye jukumu la kubeba maono uchumi na uongozi wa Tanzania ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha wazazi wanatekeleza wajibu wao wa kusimamia maadili, malezi na matunzo ya watoto na familia, Serikali kupitia Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu kuhusu maadili, malezi chanya na matunzo ya watoto na familia yenye kaulimbiu isemayo 'Familia Bora, Taifa Imara.'

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi husika jumla ya wazazi na walezi 469,634 wakiwemo wanaume 157,291 na wanawake 312,343 walipatiwa elimu ya malezi chanya kupitia majukwaa ya wazazi, viongozi wa dini na wahamasishaji jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, elimu hiyo ilitolewa kwa waandishi wa habari kutoka vyombo vya habari 29 vya Kitaifa pamoja na redio za kijamii 16 zinazosikika nchi nzima. Vikundi vya malezi ni majukwaa ya kuwafikia wazazi na walezi kwa urahisi katika lengo la kuimarisha malezi, matunzo na maadili ya watoto ndani ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeandaa mwongozo wa kuwezesha uwezeshaji na uanzishaji na uendeshaji wa vikundi vya malezi na matunzo ya watoto. Katika kipindi husika jumla ya vikundi vya malezi 4,526 vimeanzishwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuanzisha na kuhuisha vikundi 200,000 vya malezi na matunzo ya watoto ifikapo 2030. Hatua hiyo ni sehemu ya makubaliano ya Bogota Colombia ya Mwaka 2024 kuhusu uanzishaji wa majukwaa ya wazazi au walezi kwa ajili ya malezi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye huduma za ustawi wa jamii. Wizara imeendelea kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa mtu binafsi, familia na makundi mbalimbali katika jamii kwa lengo la kuzuia na kutatua athari zinazotokana

na changamoto mbalimbali. Maelezo kwa kina juu ya huduma hizi yapo aya ya 103 hadi aya ya 104.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na washirika wake wa maendeleo inaendelea kutoa huduma za msingi kama vile huduma za matibabu, malazi ya muda, huduma za kisheria na msaada wa kisaikolojia kwa manusura na wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha utekelezaji jumla ya manusura 1,313 wanaume 53, wanawake 1,260 wamehudumiwa katika nyumba salama 20 zilizopo katika Mikoa mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, jumla ya wahanga na manusura wa vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto 108,819 wakiwemo watoto 32,150, wapo wavulana na watu wazima pia ambao wameripotiwa katika vituo mbalimbali vinavyotoa huduma za afya kwa manusura wa ukatili nchini. Takwimu kwa kina zipo aya ya 104.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii kwa lengo la kusogeza huduma za ustawi kwa wananchi ambapo katika mwaka huu wa fedha 2025/2026 jumla ya Maafisa Ustawi wa Jamii 401 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi, hivyo, kufanya idadi yao kufikia 2,315 sawa na 12.5% ya Maafisa 18,481 wanaohitajika nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika kusongeza huduma za ustawi wa jamii kwa wananchi Wizara imewapatia simu janja Maafisa hawa wa ngazi za Mikoa kwa Mikoa yote 26 ili waweze kuharakisha utoaji wa huduma kwa mawasiliano na wananchi. Namba za simu kupitia Bunge lako Tukufu zipo kiambatisho namba tatu ya kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani ulionesha kuwa takribani watu 25 kati ya 100 hukabiliwa na changamoto za afya ya akili na saikolojia. Takwimu hizi

zinaonesha wazi kuwa, changamoto za afya ya akili siyo suala la mtu mmoja mmoja, bali ni suala linalohitaji juhudi za pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha utekelezaji jumla ya wataalamu 95 wamejengewa uwezo juu ya kutoa huduma ya afya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua na kuthamini mchango wa wazee kama tunu muhimu ya Taifa. Hapa dhamira hiyo imeainishwa katika Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2024, inayosisitiza kuhusu ulinzi, matunzo, hifadhi ya jamii na ustawi wa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lisilojali wazee linapoteza hazina ya maarifa, uzoefu, historia na utamaduni ambavyo ni msingi wa kujenga mshikamano na maadili ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha utekelezaji Wizara imetoa huduma za matunzo kwa wazee wasiojiweza 229; wanaume 139, wanawake 90 katika makazi ya wazee 13 yanayosimiwa na Wizara. Makazi hayo yapo katika maeneo mbalimbali nchini, nimeyataja aya ya 112.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Wizara imeratibu huduma za utoaji wa matunzo kwa ujumla ya wazee 268, wakiwepo kwenye makazi ya wazee 16 yanayomilikiwa na taasisi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za afya kwa wazee nchini ikiwa ni utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imewezesha upatikanaji wa Bima za Afya kwa Wazee Wote 229 wanaohudumiwa katika makazi 13 ya Serikali. Kadhalika, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imefanikisha upatikanaji wa huduma za msamaha wa matibabu na upimaji wa afya kwa wazee 586,638 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wanawake, Wizara inasimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2003, yenye lengo la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikia azma hiyo, Wizara imeendelea kuratibu na kutekeleza programu ya afua mbalimbali zinazolenga kuimarisha ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika nyanja zote za maendeleo. Habari hizi nimeainisha kwenye aya ya 119, na hapa sera ni ya 2023, kwa makosa nilitamka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na wadau wa maendeleo imefanikisha utekelezaji wa uandaaji wa bajeti yenye mlengo wa kijinsia *(gender responsive budget)* kwa mwaka 2026/2027. Kupitia Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango na Bajeti ya 2026/2027 umebainisha wizara tisa za mfano ambazo ni kinara wa utekelezaji wa bajeti yenye mlengo wa kijinsia. Nimetaja Wizara hizi kwenye aya ya 120, na lengo ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mipango na bajeti ya Serikali unatoa matokeo chanya na kuimarisha usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili limewezesha Serikali kwa mara ya kwanza kuweza kuandaa tamko la uzingatiaji wa masuala ya kijinsia kwenye mipango ya bajeti. Tamko hili litawasilishwa katika Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka huu 2026/2027. Maelezo ya kina kuhusu maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wanawake yanaendelea kwa wingi kwenye aya ya 123 hadi 163.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, kwenye aya ya 141 hadi 142 nimetoa maelezo mafupi kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia kwamba, ukatili wa kijinsia ni changamoto inayodhuru uimara wa wanawake na wanaume katika kufikia ndoto zao za kujiletea maendeleo na ustawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi, zinaonyesha ukatili wa kingono kwa jinsia

zote umeshuka kutoka matukio 12,749 mwaka 2024 hadi 11,625 mwaka 2025. Aidha, katika kipindi chote wanaokatiliwa zaidi kingono ni wanawake ukilinganisha na wanaume. Mathalani, wanawake 10,976 na 10,057 walikatiliwa kingono mwaka 2024 na mwaka 2025 mtawalia ukilinganisha na wanaume 1,773 na 1,568 katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2024 na 2025 mtawalia. Habari zaidi zipo Kiambatisho Namba nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya uongozi wenye maoni wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanawake wameendelea kujipambanua kama nguzo ya uongozi, umoja wa Kitaifa na maendeleo jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhamira hiyo, tarehe 14 Januari, 2026 Wizara ilisajili *Women in Leadership Forum* (Jukwaa la Wanawake Viongozi Tanzania) taasisi ya kipekee iliyoanzishwa na wanawake viongozi 12 kutoka vyama 10 vya siasa wakiongozwa na mwasisi na mbeba maono wake, Mheshimiwa Dkt. Evaline Wilbard Munisi, ambaye tuko naye humo ndani kama Mbunge mwenzetu. Pia yeye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Ajira na Mahusiano. Wapo pamoja na viongozi wenzake ambao wapo katika jukwaa la wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nadra duniani kuona viongozi kutoka vyama vingi vyenye itikadi tofauti tofauti wakivuka mipaka ya ushindani wa kisiasa na kuungana kwa ajili ya amani, mshikamano, kwa uongozi wa wanawake na maslahi mapana ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa *WLF* ni kielelezo cha mazingira wezeshi, siasa za staha na falsafa ya Mheshimiwa Rais ya kulileta Taifa pamoja; falsafa inayowafanya wanawake kuwa madaraja ya umoja, sauti za matumaini na wabeba maono ya Tanzania imara na jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika kila mkoa ambapo Wizara iliungana na Mkoa wa Geita kuadhimisha siku hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na maadhimisho hayo, Wizara ilizindua rasmi mradi wa kukuza usawa wa kijinsia Tanzania unaojulikana kwa jina la *Pamoja Project*, *Advancing Gender Equality in Tanzania*. Lengo la mradi huu ni kukuza usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake kiuchumi na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika mikoa 10 yenye jumla ya halmashauri 40. Maelezo ya kina kuhusu mradi huu mkubwa yapo eneo la 10 la utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uratibu wa mashirika yasiyo ya Kiserikali; usajili na uratibu wa shughuli za mashirika yasiyo ya Kiserikali ni majukumu muhimu yanayotekelezwa na Wizara ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki yao ya kikatiba ya kujumuika na kuchangia maendeleo kwa kutoa huduma kwa jamii zenye uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha utekelezaji mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yamesajiliwa ni 1,066 kati ya mashirika 1,000 yaliyopangwa kusajiliwa. Katika jitihada za Serikali za kupunguza utegemezi kwa wafadhili kuhusu mashirika haya na kuimarisha uendelevu wa mashirika hayo, Serikali imezindua Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Mchango wa Uanzishwaji wa Mfuko wa Pamoja wa Ruzuku wa Mashirika hayo ya Kiserikali (*NGOs Basket Fund)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hiyo inaongozwa na Dkt. Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya *CRDB*. Kamati hiyo inatarajia kukamilisha kazi yake ndani ya mwaka ujao wa fedha 2026/2027. Maelezo kuhusu mchango wa mashirika yasiyo ya Kiserikali nimeeleza kwa kina kwenye aya ya 172, jinsi gani mashirika haya yanatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kushirikiana kwa karibu na Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali nchini katika kuimarisha uratibu wa sekta ya mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kujenga ushirikiano madhubuti, kuongeza uwajibikaji na kuimarisha mchango wa sekta hiyo katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza juhudi dhidi ya ukatili, Aprili, 2026 Wizara iliratibu kikao maalum cha Wabunge wa Viti Maalum wanaowakilisha mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa ajili ya kupitia taarifa mbalimbali za utekelezaji pamoja na mwelekeo wa sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia majadiliano hayo mrejesho ulionyesha kuwa, kati ya hoja 19 zilizowasilishwa na sekta kupitia majukwaa mbalimbali za mwaka, hoja 15 sawa na 80% tayari zimefanyiwa kazi na Serikali, na hoja nyingine tunaendelea kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mafanikio hayo, Wizara inapenda kutumia fursa hii tena kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uamuzi wake wa kizalendo, wenye maono na tija kwa Taifa wa kuongeza idadi ya Wabunge wanaowakilisha mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoka wawili hadi watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi huo ni hatua kubwa ya kihistoria inayoonyesha dhamira dhabiti ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuendelea kuimarisha ushiriki wa wadau wa maendeleo katika ujenzi wa Taifa, kuongeza uwakilishi wa sauti za wananchi na kuipa sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali nafasi pana zaidi ya kushiriki katika majadiliano ya maamuzi muhimu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme machache kuhusu uratibu wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto II, habari inayopatikana kwa kina kwenye aya ya 179 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto II wenye lengo la kuhakikisha jamii inakuwa huru dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto na inapata fursa sawa za kushiriki katika masuala ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu una maeneo makuu nane; yametajwa vyema kabisa kwenye aya ya 179 yakiwepo masuala ya maadili, masuala ya sheria mbalimbali na uwezeshaji kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni shirikishi kwa kuhusisha Serikali, washirika wa maendeleo, mashirika yasiyo ya Kiserikali, taasisi binafsi na jamii kwa ujumla. Aidha, mpango huo unasisitizwa kujadiliwa katika ngazi za maamuzi, ikiwemo Kamati ya Maendeleo ya Kata, *(WDC)* ambako Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa ni Madiwani wakirudi kule huwa wanaketi. Kamati za Ushauri za Wilaya *(DCC)* na Kamati za Ushauri za Mikoa *(RCC)* ambazo zinaongozwa na Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango huo kwa kila eneo unaratibiwa na Wizara mbalimbali kulingana na usimamizi wa kisera. Mchanganuo wa Wizara hizo upo aya ya 181 hadi 203.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika aya ya184 hadi 185 nimetambua na kupongeza juhudi za Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa kuzindua mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kwa miaka 10 ijayo, kuanzia mwaka 2026/2027 hadi 2036/2037.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu unalenga kujenga jamii yenye maadili, uzalendo, uwajibikaji na mshikamano wa Kitaifa; na ni mkakati pacha unaoenda sambamba na huu mpango niliotoka kuuelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, nimetoa maelezo ya kina kwenye aya ya 204 hadi 218.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze kwenye miradi ya maendeleo. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo nane ikijumuisha

miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika taasisi, vyuo vya maendeleo ya jamii na vituo vya ustawi wa jamii na miradi ya kutoa huduma katika jamii. Miradi hii ni mikubwa na taarifa yake ni ya kina sana. Kutokana na muda, ninaomba Bunge lako Tukufu lirejee kwenye aya ya 219 hadi 230. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijielekeze kwenye vipaumbele vya Wizara na bajeti ya mapato, matumizi ya kawaida, na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Wizara itajikita katika maeneo machache yenye matokeo chanya kwa Taifa, uwezo wa kuleta mageuzi na mchango mkubwa katika kujenga Tanzania yenye jamii imara, jumuishi na yenye maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivyo, Wizara itatekeleza mpango na bajeti kwa kuzingatia vipaumbele saba ambavyo ni vifuatavyo; kwanza; kujenga mtaji wa watu wa Taifa na kizazi cha Tanzania ya 2050 kinachozingatia maadili, uzalendo, haki, usawa, ustawi, na maendeleo jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuimarisha huduma za ustawi, malezi na makuzi ya watoto, ulinzi wa kijamii na uthabiti wa Taifa ili kuendeleza Taifa lenye mshikamano, ustahimilivu na utu wa kibinadamu kwa kuzingatia kuwa watu ndiyo mtaji mkuu wa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuimarisha mifumo ya uwezeshaji wa wanawake, usawa wa kijinsia na kutokomeza ukatili wa kijinsia ili kuhakikisha kuwa mwanamke anashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kufanya mageuzi ya uchumi wa makundi maalum na sekta isiyo rasmi kutoka uchumi wa kujikimu kwenda uchumi rasmi wa kibiashara wenye tija, ushindani na wenye mchango katika pato la Taifa kwa kuwa makundi hayo ni muhimu katika kujenga uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuimarisha matumizi ya kidigitali na takwimu katika huduma za kijamii ikihusisha uchambuzi wa takwimu ili kurahisisha utendaji na kufanya maamuzi yenye ushahidi wa kitakwimu. Sita, kujenga jamii ya Kitanzania yenye amani, uwajibikaji na mshikamano ili kuimarisha ushiriki wa wananchi katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, kuimarisha ushirikiano wa Kitaifa wa kimkakati kati ya Serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi, taasisi za dini na wadau wa maendeleo kwa kuwa maendeleo ya Taifa yanahitaji juhudi za pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele hivi vimefafanuliwa na kuelezwa kwa kina maana yake nini pamoja na kazi zitakazotekelezwa na matokeo tarajiwa yatakayotokea, na vyote hivi viko aya ya 233 hadi 267. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi mbalimbali marafiki kwa ushirikiano wanaotupatia ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayashukuru mashirika na taasisi za Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara ikiwa ni pamoja na *UNICEF*, *UNFPA*, *UN Women*, *WHO*, *UNDP*, *UNEP*, *IOM* na *UNESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ninashukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki, Umoja wa Afrika, *SADC*, *EU*, Benki ya Dunia, *AfDB*, *Enabel Foundation*, *Abbott Fund*, *Global Fund* na *Hilton Condrad Foundation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazishukuru taasisi za kifedha nchini ambazo ni *CRDB Bank*, *NBC*, *NMB*, *TCB*, Benki ya Maendeleo - *TADB*, *Stanbic*, *Azania, Equity Bank*, Benki ya Watu wa Zanzibar, *ACB*, *DCB* na Benki ya Mkombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayashukuru mashirika yasiyo ya Kiserikali na mashirika ya dini; *Hope for Young Girls Tanzania*, *World*

Vision, *PACT Tanzania*, *HelpAge Tanzania*, *Compassion International*, *ROT*, *CIC*, *RCT*, *ICS*, *SOS*, *BRAC Maendeleo*, *Plan International*, *Kivulini*, *C-SEMA*, *Amani Girls*, *Girls Effect*, *TECDEN*, *EGPAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu ziende kwa taasisi za umma; *TPA*, *TPRA*, *TPDC*, *WCF*, *UTT*, *TISEZA*, Mgodi wa Geita, *PMM Group*, *Bakhresa Group of Companies*, *Total Energies*, *Asas Group of Company* na *Oryx Gas*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani zangu kwa jumuiya za makundi mbalimbali; Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee, CHAMWAPITA, Machifu na Viongozi wa Kimila, *CCWWT*, Jukwaa la Ulingo, Baraza la Watoto, SHIUMA na UMALITA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi ziende kwa mabinti wa timu yetu ya *Tanzanite Queens* ambao wamefuzu na wataiwakilisha nchi katika mashindano ya Kombe la Dunia Septemba 5, 2026 nchini Poland. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru wafanya kampeni za kijamii; SMAUJATA, LeMaChu, SAWATA pamoja na vyombo vyote vya habari. Shukrani pia ziende kwa viongozi wa dini; *CPCT*, *TEC*, *BAKWATA*, *CCT* na *SDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru bodi ya mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NaCoNGO)*. Vile vile kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ninawashukuru Wakuu wa Mikoa yote nchini kwa ushirikiano wanaonipa na timu zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu hususan mume wangu mpenzi, wakili msomi, Methusela Gwajima na watoto wetu wote ambao wamekuwa sehemu yangu wakati wote ninapokuwa ninafanya kazi hizi. Wamekuwa sehemu ya familia yangu kwa uvumilivu wao wa kipekee na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Ninawapenda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru wananchi wote wa Tanzania kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba fedha. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 7,040,129,000 kutoka vyanzo mbalimbali kama ilivyoainishwa katika ukurasa wa 148. Matumizi ya kawaida kwa mwaka 2026/2027, Wizara inakadiriwa kutumia kiasi cha shilingi 50,137,801,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 23,315,207,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na 26,822,594,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maendeleo, Wizara inakadiria kutumia shilingi 57,886,442,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 36,915,404,000 ni fedha za ndani na shilingi 20,971,038,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2026/2027, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Fungu 53, tunaomba shilingi 108,024,243,000 ili kutekeleza majukumu yetu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum *www.jamii.go.tz*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

HOTUBA YA MHE. DKT. DOROTHY GWAJIMA (MB), WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo

imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka 2025/26 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2026/27. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na neema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo ili kuwasilisha hotuba yangu. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua tena kuiongoza Wizara hii muhimu kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa Nchi yetu. Natambua kuwa, Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii; malezi na makuzi ya watoto; na uwezeshwaji kiuchumi kwa makundi maalum unafanyika kwa kasi na ufanisi mkubwa. Ninaahidi kwamba Wizara itaendelea kutimiza majukumu yake kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

SALAMU ZA PONGEZI

3. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa tena na Watanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuendelea kuongoza nchi yetu kwa kipindi kingine. Aidha, ninapenda kumpongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawaombea viongozi wetu afya njema, hekima na mafanikio katika kuwatumikia watanzania.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha pili kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Ninampongeza kwa uongozi wake madhubuti na

juhudi zake za kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii. Tunatambua na kuthamini mchango wake mkubwa katika kuimarisha ushiriki wa wanaume katika kukuza usawa wa kijinsia kupitia kampeni ya "***He for She"***.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb),** kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa 12 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe **1 Aprili, 2026** ambayo imeainisha vipaumbele na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka 2026/27.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninakupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilala na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb),** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge, **Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb**), **Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb)** na **Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso (Mb)** kwa umakini wao katika kusaidia kuongoza vikao vya Bunge. Ninawaombea na kuwatakia kazi njema katika majukumu yenu.

7. ***Mheshimiwa Spika***, pia ninapenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya **Mwenyekiti Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma (Mb)** na **Makamu wake, Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima (Mb)** kwa ushauri na maelekezo yao wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Hakika, ushauri na maelekezo ya Kamati yamekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha utendaji wa Wizara. Aidha, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara yangu kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa afua za maendeleo na ustawi wa jamii nchini.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Ni ahadi yangu kwamba, Wizara itaendelea kushirikiana nao kwa karibu ili kuhakikisha tunatekeleza kwa

vitendo maono na dhamira ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwa na jamii yenye ustawi na maendeleo jumuishi na endelevu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninamshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi (Mb),** Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Amekuwa msaada mkubwa katika kusimamia shughuli za Wizara, kutoa ushauri na kuhakikisha utekelezaji wa majukumu unafanyika kwa ufanisi. Hakika, wanawake wa Mkoa wa Mbeya hawakukosea kumchagua kuwa mwakilishi wao.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninaishukuru Menejimenti na Wataalam wote wa Wizara wakiongozwa na **Bw. Eliakim Chacha Maswi,** Katibu Mkuu na wasaidizi wake **Wakili Amon Anastaz Mpanju,** Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum na **Bi. Felista Peter Mdemu**, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Maendeleo ya Jinsia na Wanawake kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama na Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao mkubwa unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu.

SALAMU ZA POLE

12. ***Mheshimiwa Spika***, ninatoa pole kwa kuondokewa na wabunge wenzetu, **Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Mb)** na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); **Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa **Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi)**, waliotoa mchango mkubwa katika Taifa kupitia Bunge na Serikali. Tunawaombea pumziko la amani na tunawakumbuka kwa utumishi uliotukuka.

13. ***Mheshimiwa Spika***, ninatoa pole kwa kifo cha **Mheshimiwa Julie Catherine Manning**, mwanamke wa kwanza Tanzania kusoma Shahada ya Sheria na kuhudumu kama Jaji wa Mahakama Kuu katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, pamoja na kuwa Waziri wa kwanza wa Sheria mwanamke.

Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, wadau na Watanzania wote walioguswa na vifo hivyo kwa namna moja au nyingine. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa marehemu pumziko la amani. Amina!

14. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa utangulizi huu, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu Maono ya Kimageuzi katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/26, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya kimkakati vya Wizara kwa mwaka 2026/27.

MAONO YA KIMAGEUZI KATIKA SEKTA YA MAENDELEO NA USTAWI WA JAMII

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu imebeba ujumbe mkuu kwamba, Maendeleo ya Taifa hayawezi kupimwa kwa miundombinu pekee, bali kwa **ubora wa maisha ya watu**; **uimara wa jamii**; **usalama wa kijamii**; **ushiriki wa wanawake katika maendeleo**; **ustawi wa watoto na wazee pamoja na uwezo wa wananchi kushiriki kikamilifu katika kujiletea Maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.** Hapa pia napenda kunukuu maneno ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** alipotoa Hotuba yake ya kufungua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba 2025, Dodoma alisema nanukuu "**Namuomba Mungu kuwa mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita usipimwe tu kwa vitu bali pia, kwa Tabasamu la Utu litakaloachwa kwenye nyuso za Watanzania"**. Mwisho wa kunukuu.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa msingi huo, Wizara hii ni mhimili

mahsusi wa maendeleo ya watu na injini ya uchumi jumuishi nchini. Aidha, ni nyenzo ya kuleta mageuzi ya fikra katika jamii ambayo ni msingi muhimu katika kufanikisha DIRA 2050 yenye lengo la kujenga Taifa lenye Demokrasia, Haki na Uhuru; Taifa linalozingatia Utu; Amani na Umoja. Taifa lenye uwezo wa kumiliki na kutumia kikamilifu rasilimali zake kwa manufaa ya wananchi pamoja na kuhifadhi, kukuza na kulinda maadili na tamaduni chanya za kitanzania.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii ninayoiwasilisha haiainishi tu takwimu za kibajeti, bali inaeleza maono na mwelekeo wa Taifa katika kujenga Taifa lenye ustawi, Mshikamano, maadili na ushiriki mpana wa wananchi katika maendeleo. Tunaamini kwamba, maendeleo ya kweli na endelevu hayawezi kupatikana kwa ukuaji wa uchumi pekee bila kuwa jamii imara inayojali makundi yote ya wananchi na inayowezesha kila mmoja kushiriki katika kujiletea maendeleo. Kwa mantiki hiyo, Sekta hii ni ya kimkakati na kimageuzi inayojenga msingi wa Taifa lenye watu wenye utu, uwajibikaji, uzalendo na uwezo wa kuchangia kikamilifu katika kufikia malengo ya DIRA 2050.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** mwelekeo wa Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa jamii unajengwa katika misingi ya kutambua kuwa watu ndiyo rasilimali kuu ya Taifa. Kwa msingi huo, wanawake ni nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa, watoto ni msingi wa Taifa la kesho, wazee ni hazina ya Taifa na jamii imara ndiyo nguzo ya amani, mshikamano na maendeleo endelevu. Aidha, Wizara inaendelea kutambua na kuthamini mchango wa makundi mbalimbali ya wananchi wakiwemo machinga, bodaboda, mama/baba lishe pamoja na wafanyabiashara ndogondogo wengine ambayo ni sehemu muhimu ya uchumi rasmi wa Taifa.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kusisitiza kwamba, msingi mkuu wa DIRA 2050 unaojengwa juu ya Utawala bora, Amani, Usalama na Utulivu si kauli ya kawaida ya sera, bali ni uamuzi wa kimkakati wa Taifa letu unaoendelea kuimarishwa na uongozi madhubuti wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kuonesha kwa vitendo nafasi muhimu ya mwanamke kwa maendeleo ya Taifa.

Hali hiyo imejidhihirisha katika DIRA 2050 inayolenga kupunguza pengo la kijinsia kwa angalau asilimia 85 na kuiwezesha Tanzania kuwa kinara Barani Afrika na kuwa miongoni mwa nchi 10 bora Duniani.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** kuelekea DIRA 2050 tunategemea kujenga Tanzania ya wanawake na wanaume wenye uwezo sawa wa kushiriki, kuamua, kumiliki, kuzalisha, kuongoza na kunufaika na maendeleo ya Taifa. Kwa mtazamo wa kimkakati, DIRA 2050 inabainisha kuwa usawa wa kijinsia si ajenda ya kijamii tu, bali ni ajenda ya kimageuzi ya kiuchumi (Economic Transformation Agenda) na ajenda ya kitaifa ya ushindani (National Competitiveness Agenda).

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Sheria, Mipango, Mikataba na Makubaliano ya Kikanda na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 (Toleo la Mwaka 2024); Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); na Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023). Aidha, Wizara inazo sheria tatu (3) inazozitekeleza ambazo ni Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56; na Sheria ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Sura ya 110.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2025/26, umezingatia miongozo mbalimbali ya Taifa na Kimataifa. Baadhi ya miongozo hiyo ni pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/ 26); Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 – 2025/26); Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya II (MTAKUWWA II, 2024/25 – 2028/29); Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na

Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi (Bottom Up 2022/23 - 2025/26); Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM 2021/22 – 2025/26); Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (2021/22 - 2024/25); Mkakati wa Taifa wa kutokomeza Ukeketaji (2021/22 – 2024/25); Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 – 2026/27); Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals, 2030*); na Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063). Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum – GEF, 2021 – 2026).

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa katika ngazi ya msingi;

ii) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii ikiwa pamoja na kukuza usawa wa kijinsia, kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji wanawake kiuchumi na upatikanaji wa malezi bora katika familia;

iii) Kutambua, kuratibu na kuimarisha maendeleo na ustawi wa makundi maalum wakiwemo watoto, wazee na wafanyabiashara ndogondogo;

iv) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na

v) Kuimarisha mazingira ya ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

Mapato na Matumizi ya Fedha za Wizara (Fungu 53)

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha **shilingi bilioni tisa, milioni arobaini, mia moja ishirini na tisa elfu** (shilingi 9,040,129,000) kutoka katika vyanzo

mbalimbali vya mapato. Vyanzo hivyo ni pamoja na Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Ada za Malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo hivyo; Ada za Mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Ada za usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2026, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,570,588,691.45** sawa na **asilimia 39.50** ya lengo la makusanyo ya mapato. Hata hivyo, miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikiwa kwa lengo hilo ni pamoja na uhaba na uchakavu wa miundombinu katika Vyuo; kuongezeka kwa fursa mbalimbali za mikopo zenye masharti nafuu kutoka sekta binafsi na sekta ya umma; na kupungua kwa ufadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutokana na mabadiliko ya sera za nchi wafadhili. Aidha, Wizara inaendelea na jitihada za kukusanya mapato katika kipindi kilichobaki ili kufikia lengo la makusanyo yaliyokadiriwa kwa mwaka 2025/2026.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu **Shilingi 76,057,153,000** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 49,115,697,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 26,941,456,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 22,646,148,000** ni Mishahara na **Shilingi 26,469,549,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo, kiasi cha **Shilingi 15,415,404,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 11,526,052,000** ni fedha za nje.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2026, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 60,459,559,340.07**, sawa na **asilimia 79.49** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 40,740,367,581.40** sawa na **asilimia 82.95** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 19,719,191,758.67** sawa na **asilimia 73.19** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika ***Jedwali Na. 1.***

Jedwali 1: Fedha zilizopokelewa katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026.

Eneo	Fedha zilizoidhinishwa	Fedha zilizotolewa	Asilimia
Matumizi ya Kawaida			
Mishahara	22,646,000,000.00	18,548,952,761.00	81.91
Matumizi mengineyo	26,469,549,000.00	22,191,414,820.40	83.84
Jumla Ndogo (a)	**49,115,549,000.00**	**40,740,367,581.40**	**82.95**
Fedha za Miradi ya Maendeleo			
Fedha za Ndani	15,415,404,000.00	13,400,000,000.00	86.93
Fedha za Nje	11,526,052,000.00	6,319,191,758.67	54.83
Jumla Ndogo (b)	**26,941,456,000.00**	**19,719,191,758.67**	**73.19**
JUMLA KUU	**76,057,005,000.00**	**60,459,559,340.07**	**79.49**

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA (FUNGU 53)

28. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo imetekeleza vipaumbele vilivyoanishwa katika bajeti ya mwaka 2025/26. Utekelezaji huo umewezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali katika maeneo ya maendeleo na ustawi wa jamii kama ifuatavyo: -

ENEO LA 1: KUENDELEZA RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA MAENDELEO NA USTAWI WA JAMII

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua kuwa rasilimali watu ni msingi muhimu katika kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma bora za maendeleo na ustawi wa jamii. Ili kufanikisha lengo la kuwa na sekta yenye ufanisi, uwajibikaji inayozingatia mahitaji ya wananchi, Wizara pamoja na Taasisi zake imeendelea kuimarisha uwezo wa watumishi kupitia ajira mpya, mafunzo ya kitaaluma ya muda mfupi na mrefu yanayotolewa ndani na nje ya nchi. Aidha, kuimarisha programu za kuendeleza ujuzi na weledi na kuhimiza maadili ya utumishi wa umma.

WIZARA

30. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imeendelea kuimarisha rasilimali watu kwa kuajiri watumishi 17 na hivyo kuwa na jumla ya **watumishi 685**. Aidha, Wizara imewathibitisha kazini watumishi 108, imewapandisha vyeo watumishi 76. Vilevile, imepokea Watumishi 25 waliohamia kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na kuhamisha watumishi 13 kwenda taasisi nyingine.

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho, Wizara imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa **watumishi 25** na mafunzo ya muda mfupi kwa **watumishi 31** katika fani mbalimbali ndani ya nchi. Aidha, kwa mwaka 2025/26 jumla ya **watumishi 17** wamestaafu kwa mujibu wa Sheria na taratibu za utumishi wa umma.

TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ina jumla ya **watumishi 241**. Katika mwaka 2025/26 Taasisi hiyo imeajiri **watumishi 23**, watumishi nane (8) wamehamia kutoka taasisi mbalimbali na watumishi saba (7) wamehama kwenda taasisi nyingine. Aidha, Taasisi imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa **watumishi 45** ikiwemo mafunzo ya ngazi ya Shahada ya Uzamivu (PhD).

TAASISI YA USTAWI WA JAMII

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii ina jumla ya **watumishi 192**. Katika mwaka 2025/26, Taasisi ya hiyo imeajiri **watumishi wawili (2)** na kuwathibitisha kazini **watumishi wawili (2)**. Aidha, imewapandisha vyeo **watumishi saba (7)**, imemteua mtumishi mmoja katika nafasi ya uongozi, imepokea watumishi saba (7) waliohamia kutoka taasisi mbalimbali na kuwahamisha watumishi watano (5) kwenda taasisi nyingine. Hata hivyo, watumishi wanne (4) wamestaafu kwa mujibu wa sheria na taratibu za utumishi wa umma.

ENEO LA 2: MAENDELEO YA JAMII

34. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI inatekeleza Kampeni ya Mageuzi ya Kifikra na Mitazamo ya Jamii kwa kujenga fikra na mitazamo chanya inayowezesha wananchi kufanya kazi kwa bidii, kuongeza uwajibikaji, kuwa wazalendo, waadilifu, wabunifu na wenye moyo wa kujitolea. Lengo likiwa ni kuondoa mitazamo hasi kama utegemezi, kutotumia fursa, kukosa maadili, uzalendo na kutowajibika inayosababisha kutopata maendeleo yanayotarajiwa. Kampeni hiyo inakuza ari ya wananchi kushiriki katika kuibua, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kufuatilia shughuli za maendeleo na kuwafanya kuwa kitovu cha maendeleo yao na kuhakikisha miradi ya maendeleo wanayoitekeleza ni endelevu na jumuishi.

35. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI ilitekeleza Kampeni ya Amsha Ari katika mikoa minne (4) na kufanya jumla ya Mikoa 21 iliyofikiwa na kampeni hii. Kampeni hiyo ilifanyika kwa kushirikisha viongozi mbalimbali kuanzia ngazi ya kata hadi Taifa ili kuonesha kwa vitendo umuhimu wa jamii kushiriki na kuchangia kwa hiari katika miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao. Kampeni hiyo ilifanyika katika Mikoa ya Mbeya - Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Mara - Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, Morogoro - Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Mwanza - Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na Manispaa ya Ilemela.

36. ***Mheshimiwa Spika***, katika kampeni hiyo, jumla ya wananchi **7,184** (Wanaume 3,190 na Wanawake 3,994) walishiriki wakiwemo Viongozi wa Dini, Wazee wa Mila, Watu Maarufu, Vijana, Wajumbe wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, Wafanyabiashara Ndogondogo, wajumbe wa kikundi cha Baponyamaswa na Wanafunzi wa Vyuo vya Buhare na Misungwi. Kampeni hiyo imeimarisha mshikamano wa jamii katika kufanya kazi kwa pamoja, kuongeza uelewa na uwajibikaji wa wananchi katika kusimamia na kuendeleza miradi yao, kupunguza utegemezi kwa kuimarisha ari ya wananchi kujitegemea.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM-

TAMISEMI imeendelea kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kutambua umuhimu wao mkubwa katika kuamsha ari ya jamii kushiriki katika masuala ya Maendeleo yao na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha 2025/26 Maafisa Maendeleo ya Jamii **830** wameajiriwa na kufanya jumla yao kuwa **4,806** sawa na **asilimia 89.8** kati ya mahitaji ya watumishi **5,352** wanaohitajika nchi nzima.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii hao ambao wengi wao wapo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wameendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika mikoa 26 ya Tanzania Bara. Hadi kufikia Aprili, 2026 miradi ya maendeleo imeongezeka kutoka **31,802** hadi kufikia **38,443**, ikiwemo miradi ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya **1,632**, ujenzi wa madarasa ya shule za awali na msingi **26,467** na madarasa ya shule za sekondari **10,344**.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI inaendelea kuratibu Kampeni ya Ujenzi wa Nyumba Bora kupitia Kaulimbiu isemayo "**Piga Kazi, Boresha Makazi".** Kupitia Kampeni hiyo, Maafisa Maendeleo ya Jamii wamehamasisha ujenzi wa nyumba bora **944** zenye gharama nafuu na hivyo kufanya jumla ya nyumba bora zilizojengwa katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kufikia **15,296** tangu kuanza kwa kampeni hiyo mwaka 2022.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kuhuisha Mwongozo wa Majukumu ya Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Mwaka 2018 na kuandaa Toleo la Mwaka 2026. Mwongozo huo umeboreshwa ili kuwawezesha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao ikiwemo uratibu na utekelezaji wa Sera mbalimbali za Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwongozo huo umejumuisha majukumu na muundo mpya wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali

za Mitaa ambapo Kitengo cha Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Mkoa kimeanzishwa na hivyo kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Maafisa Maendeleo ya Jamii kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninatoa Shukrani za kipekee kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia uundwaji wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa ambacho kimeongeza ufanisi katika utendaji kazi na baadaye kinatarajiwa kuwa sehemu inayojitegemea.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na zoezi la kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Jamii ya Mwaka 1996, ili iendane na hali halisi ya sasa kwa kuzingatia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Tathmini ya utekelezaji wa Sera hiyo imeonesha kuwa kuna umuhimu wa kuihuisha Sera hiyo. Wizara imekamilisha Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996, Toleo la mwaka 2026 ambayo imewasilishwa kwa wadau ili kupata maoni na inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/27.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa Sera hiyo, kutajenga msingi wa kutungwa kwa Sheria mahsusi ya wataalam wa maendeleo ya jamii. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine itaimarisha usimamizi na udhibiti wa maadili, weledi na uwajibikaji wa wataalam hao ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa wananchi.

44. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia Vyuo sita (6) vya Maendeleo ya Jamii ambavyo ni Ruaha (Iringa), Rungemba (Iringa), Uyole (Mbeya), Mlale (Ruvuma), Buhare (Mara) na Monduli (Arusha); pamoja na Vyuo viwili (2) vya Maendeleo ya Jamii Ufundi ambavyo ni Misungwi (Mwanza) na Mabughai (Tanga). Katika mwaka wa masomo 2025/26 Vyuo hivyo vimedahili jumla ya wanafunzi **5,152 (Wanaume 1,683** na **Wanawake 3,469)**

45. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza thamani na ubora wa wahitimu wa Taasisi na Vyuo, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa

dhana ya uanagenzi ambayo inawaunganisha wanafunzi na taasisi, Mashirika au Kampuni kwa ajili ya kuongeza ujuzi wanaohitaji. Aidha, iliratibu utekelezaji wa dhana ya ushirikishwaji jamii, ambapo wanafunzi kwa kushirikiana na wakufunzi na jamii inayozunguka Vyuo wanaibua changamoto zilizopo katika jamii husika na kuainisha mbinu za kuzitatua. Vilevile, iliwezesha utekelezaji wa dhana ya ubunifu ambayo inawawezesha wanafunzi kutoa mawazo yao ya kibunifu ambayo yanasaidia kutatua changamoto za jamii.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya wanafunzi 180 wameunganishwa na Taasisi mbalimbali kama vile Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kwa ajili ya mafunzo ya uanagenzi. Kupitia dhana hiyo wanafunzi wameweza kupata ujuzi katika maeneo ya uandishi na usimamizi wa miradi, uanzishaji wa biashara na matumizi ya teknolojia mbalimbali.

47. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Vyuo inatekeleza programu ya ushirikishwaji jamii inayolenga kuiwezesha jamii kutatua changamoto zinazoikabili kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao. Katika mwaka 2025/26, jumla ya wananchi 1,499 walinufaika na programu hiyo kupitia mafunzo mbalimbali kama vile ushonaji, kilimo cha parachichi, lishe bora na elimu dhidi ya ukatili. Aidha, kupitia programu hii Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale kiliwakatia Bima za Afya watoto 65 wa kituo cha watoto yatima cha Chipole pamoja na kuwapatia chakula na vifaa vya shule.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya mawazo 9 ya kibunifu yameibuliwa kwenye Taasisi na vyuo hivyo, hivyo kufanya mawazo yaliyoibuliwa tangu kuanzishwa kwa vituo vya ubunifu mwaka 2019 kufikia mawazo 53; kati ya hayo, mawazo 21 yako hatua ya dhana (*Ideation)*, mawazo 13 yako katika hatua ya uatamiaji, mawazo 9 yako hatua ya sampuli kifani, na mawazo 10 yamekamilika na kuwa bidhaa na huduma kama vile:- niuzie *point of sale* – POS (Tengeru) ambao ni mfumo wa kijasiriamali unaowezesha wajasiriamali kutunza kumbukumbu za mauzo, matumizi na manunuzi; na mfumo wa kielekroniki wa

connect (Tengeru) ambao umesaidia kusajili wajasiriamali wanawake Mkoani Arusha.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** pia mawazo mengine ambayo tayari ni bidha ni mitungi inayotengenezwa kwa saruji (Misungwi) ambayo inatumika kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi pamoja na kifaa cha kugundua madini ardhini (Misungwi) ambacho kitawawezesha wachimbaji wadogo kutambua maeneo yenye madini. Vilevile, kuna wazo la karata lishe na draft lishe (Rungemba) ambalo linatumika kuelimisha na kuhamasisha jamii kutumia vyakula bora.

50. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ruaha, Rungemba, Mlale na Monduli imeendelea kutoa mafunzo ya ushonaji kwa wanafunzi na wananchi ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya wanafunzi na wananchi 399 wamenufaika. Mafunzo haya yameendelea kuwavutia wadau mbalimbali wakiwemo Shirika la *SOS Children's Villages Tanzania* ambalo limewezesha wasichana 26 waliopata watoto katika umri mdogo kupata mafunzo hayo katika Chuo cha Rungemba. Wasichana hao wanapatiwa ujuzi wa ushonaji ili waweze kujikwamua kimaisha, kuwalea watoto wao vema pamoja na kuepukana na vitendo vya ukatili. Mafunzo haya yanafanyika kwa kutumia vyerehani 258 vilivyopatikana kwa ushirikiano na Ubalozi wa China.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi na Mabughai imeendelea kuwajengea ujuzi na uzoefu wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo hivyo kwa kutekeleza mafunzo kwa vitendo. Aidha, vyuo hivyo vimekuwa vikitoa huduma ya usimamizi elekezi (consultancy) kwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa taasisi za Wizara kama vile mahabusu ya watoto Bukumbi na hosteli za wasichana katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Monduli na Uyole. Usimamizi huo umesaidia kuipunguzia gharama Wizara na kuongeza uzoefu kwa wanafunzi na wakufunzi wa vyuo hivyo.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na mchakato wa kuviunganisha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ili viweze kujiendesha kiutendaji

(autonomous). Hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara ilishirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kufanya upembuzi yakinifu wa rasilimali watu, miundombinu na taaluma katika Vyuo hivyo. Matokeo ya tathmini hiyo yameonesha kuwa kuna manufaa kupitia muunganiko huo ikiwemo kupunguza utegemezi wa rasilimali fedha kutoka Serikali Kuu pamoja na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Aidha, Wizara imepokea maoni ya wadau muhimu wakiwemo Wizara ya Fedha, OR - UTUMISHI na Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao kwa pamoja wameunga mkono azma hiyo. Hivyo, muunganiko huo unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/27.

ENEO LA 3: UTAMBUZI, URATIBU NA UENDELEZAJI WA WAFANYABIASHARA NDOGONDOGO

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na shughuli za utambuzi, uratibu na usimamizi wa programu za kuwezesha Makundi Maalum kiuchumi. Makundi hayo yanajumuisha wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo machinga; mama na baba lishe; waendesha bodaboda na bajaji; wasusi; washonaji wa nguo na wafanyabiashara ndogondogo wengine wenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni nne (4) kwa mwaka. Makundi hayo yanalengwa kwa kuwa yanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kutofikiwa na fursa za kiuchumi kama elimu ya ujasiriamali, mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha na maeneo wezeshi ya kufanyia biashara zao.

54. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha juhudi za Serikali za kuwatambua na kuwarasimisha wafanyabiashara ndogondogo nchini, Wizara imeendelea na utekelezaji wa zoezi la utambuzi na usajili wao kupitia Mfumo wa Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo (WBN-MIS). Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 56,039 (Wanaume 25,589 na Wanawake 30,450) wamesajiliwa na kufanya jumla ya Wafanyabiashara ndogondogo 143,053 (wanaume 57,221 na wanawake 85,832) kusajiliwa kwa hiari yao tangu zoezi lilipoanza Machi 2024.

55. ***Mheshimiwa Spika***, kati yao, wafanyabiashara 63,246

(Wanaume 24,965 na Wanawake 38,281) wamelipia gharama za uchapishaji wa vitambulisho vya kidijitali. Aidha, wafanyabiashara 51,333 sawa na asilimia 81.2 ya waliolipia tayari wamepatiwa vitambulisho vyao, huku maombi 11,913 sawa na asilimia 18.8 yapo katika hatua za uchapishaji na usambazaji. Vitambulisho hivi vinachapishwa na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC) kilichopo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambacho kina mkataba na Wizara wa kutekeleza jukumu hilo. Kituo hicho ni maalum kwa ajili ya kuchakata na kuhifadhi taarifa mbalimbali kidijitali.

56. ***Mheshimiwa Spika***, kitambulisho cha kidijitali cha wafanyabiashara ndogondogo ni muhimu kwa kuwa, hubeba taarifa za msingi kama vile taarifa za biashara, eneo la biashara na shughuli za kiuchumi za mhusika tofauti na kitambulisho cha NIDA ambacho kina taarifa binafsi za mhusika ikiwemo uraia wake. Mfumo huo unawawezesha wafanyabiashara hao kutambulika rasmi na kurahisisha upatikanaji wa mikopo, huduma za kifedha, masoko na fursa nyingine za uwezeshaji wa kiuchumi.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kitambulisho hicho kimeunganishwa na mifumo mingine kama vile NIDA, mifumo ya hifadhi ya jamii, mifumo ya kibenki na Wezesha Portal ambapo muunganiko huo umewezesha kusomana na kubadilishana taarifa za waombaji wa mikopo hiyo.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya mafunzo kuhusu Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa wafanyabiashara ndogondogo (Wafanyabiashara Ndogondogo *Management Information System - WBN-MIS)* kwa washiriki 139 ambao ni maafisa wa Serikali kutoka ngazi ya Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Viongozi wa Wafanyabiashara Ndogondogo. Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha uratibu, usimamizi na utekelezaji wa zoezi la utambuzi na usajili wa wafanyabiashara ndogondogo nchini.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 10.5 kwa ajili ya utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo. Fedha hizo zinafanya jumla ya shilingi bilioni 18.5

zilizopokelewa na Wizara na kupelekwa Benki ya NMB kwa ajili ya utoaji wa mikopo tangu zoezi hilo lianze mwezi Januari, 2025. Aidha, hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 8,426 (Wanaume 3,906 Wanawake 4,520) wamekopeshwa kiasi cha shilingi bilioni 17.9. Mchanganuo wa Mikopo hiyo kwa kila Mkoa umeambatishwa katika ***Kiambatisho Na.1.***

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI pamoja na Viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) iliratibu makongamano na mikutano ya Wafanyabiashara Ndogondogo katika Mikoa yote 26 kuanzia mwezi Agosti, 2025 hadi Aprili, 2026, ambapo jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 25,458 (Wanaume 10,184 na Wanawake 15,274) walishiriki. Kupitia makongamano na mikutano hiyo, washiriki walipata elimu ya biashara, kujadili mafanikio na changamoto zinazowakabili pamoja na kuunganishwa na fursa zinazotolewa na Taasisi mbalimbali. Taasisi zilizoshiriki ni pamoja na Benki ya NMB, CRDB, Benki ya Azania, TRA, SIDO, TANESCO, NSSF, Tanzania Agricultural Development Bank – TADB na NHIF.

61. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Sekta nyingine hutoa nafasi za ushiriki wa wafanyabiashara ndogondogo katika maonesho ya biashara za ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI, iliratibu ushiriki wa wafanyabiashara ndogondogo 1,374 (Wanaume 632 na Wanawake 742) katika Maonesho ya Kitaifa ya Wakulima na Wafugaji (Nanenane) mwezi Agosti, 2025 yaliyofanyika Jijini Dodoma ambapo waliweza kuuza na kutangaza biashara zao. Aidha, jumla wafanyabishara ndogondogo 697 (Wanaume 237 na Wanawake 460) walitembelea banda la Wizara na kuelimishwa kuhusu fursa ya mikopo yenye masharti nafuu inayoratibiwa na Wizara kupitia Benki ya NMB.

62. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na OWM – Kazi, Ajira na Mahusiano pamoja na Wizara nyingine za Kisekta iliwawezesha wafanyabiashara 271 (Wanaume 122 na Wanawake 149) kushiriki katika Maonesho ya 25 ya wajasiriamali wadogo na wa kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

(Juakali/Nguvukazi) yaliyofanyika Jijini Nairobi – Kenya mwezi Novemba 2025. Kupitia Maonesho hayo wafanyabiashara hao walipata fursa ya kuonesha na kuuza bidhaa zao, kupata uzoefu kutoka kwa wenzao na hatimaye kukuza mtandao wa kibiashara.

63. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Umoja wa Mamalishe na babalishe Tanzania (UMALITA), OWM - TAMISEMI, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na sekta binafsi, iliandaa Kongamano la Kitaifa lilishirikisha mamalishe na babalishe 3,500 kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, lililofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 21 Aprili 2026. Pamoja na masuala mengine, kongamano hilo lililenga kuimarisha nafasi ya mamalishe na babalishe katika uchumi wa familia na Taifa kwa ujumla kwa kuwaunganisha, kuwajengea uelewa na kuwawezesha kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo katika mnyororo wa thamani wa chakula.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** kongamano hilo pia lililenga kuweka msingi wa kuwawezesha wafanyabiashara hao kushiriki kikamilifu katika uchumi rasmi kupitia mafunzo, teknolojia, masoko, mitaji na matumizi ya nishati safi, ili kujenga uchumi jumuishi, shindani na unaozalisha ajira kwa wananchi wengi zaidi. Vilevile, kongamano hilo lilisisitiza umuhimu wa kuwaandaa mamalishe na babalishe kunufaika na fursa za kiuchumi zitokanazo na matukio mbalimbali makubwa ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo **AFCON 2027**, hususan katika huduma za chakula, utalii, biashara na huduma nyingine zitakazochochea ongezeko la kipato na ukuaji wa biashara zao. **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuwa Mgeni Rasmi katika tukio hilo kubwa. Kongamano liliongozwa na kauli mbiu isemayo ***"Shiriki Kulinda Amani na Mshikamano wa Taifa; Amani ni Hazina Yetu, Mamalishe na Babalishe".***

65. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa mikopo pamoja na elimu ya fedha na ujasiriamali kwa wafanyabiashara ndogondogo kupitia Benki za Biashara nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya wafanyabiashara ndogondogo **60,737** (Wanaume 42,137 na

Wanawake 18,600) wamenufaika na mikopo yenye thamani ya **Shilingi trilioni 1.8**. Kati ya Fedha hizo, Wanaume walipata mikopo yenye thamani ya **shilingi trilioni 1.357**, sawa **na asilimia 75.4** na wanawake walipata mikopo yenye thamani ya **Shilingi trilioni 0.443**, sawa na **asilimia 24.6**. Hatua hii imeendelea kuchochea ukuaji wa biashara ndogondogo nchini, kuongeza ujumuishwaji kifedha na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uchumi rasmi.

66. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo zinaendelea kutolewa kupitia programu mbalimbali za benki za biashara nchini. Programu hizo ni pamoja na mikopo ya kilimo na biashara kupitia Benki ya NMB; Mikopo ya wajasiriamali wadogo kupitia benki ya kupitia Benki ya *Equity;* mikopo ya mtu mmoja mmoja na vikundi kupitia Benki ya TCB*;* Mikopo ya Kua Nasi kupitia Benki ya NBC; na Mikopo ya IMBEJU kupitia *CRDB Foundation*.

67. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Benki ya Azania inaendelea kutoa mikopo ya Fanikisha Wewe ni Hodari, mikopo ya viwanda skimu na mikopo ya biashara ndogondogo. Aidha, Benki ya *DCB* inatoa Mikopo ya Tausi, Sokoni, mikopo ya bajaji na bodaboda huku Benki ya Maendeleo ikitoa mikopo ya Wezesha Machinga, mikopo ya vikundi (Solidarity Group Lending - SGL) na mikopo ya Bajaji kwa kushirikiana na Chama Cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (CMPD).

ENEO LA 4: MALEZI, MAADILI, MAENDELEO NA USTAWI WA WATOTO

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia malezi, maadili, matunzo na ustawi wa watoto pamoja na familia, ambayo ni msingi wa kujenga Taifa lenye nguvukazi yenye tija. Malezi chanya ya watoto yanayoambatana na maadili mema ni nguzo katika kujenga Taifa imara kwa ustawi na maendeleo endelevu. Sambamba na hilo, Wizara inaratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya malezi chanya kwa wazazi au walezi na vijana balehe, ikiwa ni juhudi za pamoja za kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** watoto ni rasilimali muhimu na mtaji

wa Taifa, hivyo wanapaswa kulindwa, kupendwa, kuendelezwa na kulelewa katika misingi ya maadili na tamaduni za Taifa letu, ambapo mazingira bora na sahihi ya malezi ya watoto yanapaswa kuanzia ndani ya familia. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo hali duni ya kipato cha familia, ukatili, migogoro ya familia, na vifo vya wazazi au walezi, husababisha watoto kuishi katika mazingira hatarishi hivyo kuhitaji huduma za malezi mbadala.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/22–2025/26). Programu hiyo inalenga kuhakikisha kuwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka nane (8) anapata huduma jumuishi za malezi na makuzi ili kuongeza kiwango cha ukuaji timilifu kutoka asilimia 47 ya sasa hadi asilimia 90 kama ilivyobainishwa katika DIRA 2050. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara imeratibu uandaaji wa mfumo wa upimaji wa matokeo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (Early Childhood Development – ECD Scorecard) ili kufuatilia utekelezaji wa viashiria vya Programu hiyo.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa mfumo kwa ajili ya kukusanya takwimu na taarifa kuhusu afua za malezi na makuzi ya awali ya mtoto kutoka katika mifumo ya Wizara za kisekta na Taasisi mbalimbali za Serikali (ECD Dashboard). Mfumo huo unalenga kubaini ulinganifu wa utekelezaji wa nguzo tano (5) za Malezi na Makuzi ya watoto wadogo ambazo ni afya bora, lishe toshelevu, uchangamshi na ujifunzaji wa awali; malezi yenye mwitikio; na ulinzi na usalama wa watoto wadogo. Nguzo hizo zote zina umuhimu sawa katika malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kuhusu mifumo hiyo kwa maafisa wasimamizi 227 kutoka Mikoa na Halmashauri zote nchini. Kati yao, maafisa 17 walitoka ngazi ya Wizara, maafisa 26 kutoka ngazi ya Mkoa, na maafisa 184 kutoka ngazi ya Halmashauri.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwepo na ongezeko la matumizi ya vifaa vya kielektroniki kwa watoto, hali inayochangia upatikanaji wa maudhui yasiyofaa kwa watoto. Tafiti zinaonesha kuwa asilimia 67

ya watoto wenye umri wa miaka 12–17 hutumia simu janja, ambapo asilimia 4 kati yao wamekumbana na aina mbalimbali za ukatili mtandaoni. Katika kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto dhidi ya changamoto hizo, Wizara ilitoa mafunzo kwa timu ya wawezeshaji 516 kuhusu usalama wa watoto mtandaoni, kwa lengo la kuwawezesha kutoa elimu kwa wanafunzi, walimu na watumishi wasio walimu katika shule za msingi na sekondari. Baada ya mafunzo hayo, wawezeshaji waliweza kuwaelimisha wanafunzi 1,811,212, walimu 679 na watumishi wasio walimu 232 kutoka mikoa yote 26 nchini.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Serikali inaendana na kasi ya maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, ilianzisha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu Usalama wa Mtoto Mtandaoni mwaka 2024 kwa lengo la kuishauri Wizara kuhusu afua mahsusi zinazokidhi mahitaji ya wakati wa sasa. Kamati hiyo hukutana kila robo mwaka. Moja ya ushauri uliotolewa na Kamati ni uwezekano wa matumizi ya utaratibu maalum wa kuchuja na kuzuia maudhui yasiyofaa kwa watoto wanapotumia mitandao. Sambamba na hilo, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ipo katika hatua ya majadiliano ya kuanzisha matumizi ya Laini Maalum ya Simu kwa Mtoto (Child SimCard) kwa lengo la kuimarisha usalama wa mtoto katika matumizi ya teknolojia na mawasiliano.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za kundi la vijana balehe ikiwemo maambukizi ya VVU na UKIMWI, mimba za utotoni, vitendo vya ukatili, lishe duni, watoto kuacha shule, pamoja na ukosefu wa ujuzi na fursa za kiuchumi, Wizara imeratibu utekelezaji wa Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (2021/2022 – 2024/2025). Katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ilifanya tathmini ya utekelezaji wake, na imependekezwa kuanzishwa kwa Programu Jumuishi ya Taifa inayolenga kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe wenye umri wa miaka 9 hadi 19.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinavyoathiri afya ya mwili na akili. jumla ya walimu 4,388 wamepata mafunzo kuhusu namna ya kuanzisha, kusimamia na kuratibu afua za ulinzi na usalama wa mtoto shuleni. Aidha, Wizara imeanzisha na kuimarisha madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi na sekondari nchini. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, Madawati 3,204 ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto yameanzishwa katika shule za msingi na sekondari nchini na hivyo kufikisha jumla ya madawati 11,156 kati ya lengo la madawati 20,772 ifikapo mwaka 2027/28.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara imeratibu na kusimamia uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto kwa lengo la kuwapa watoto fursa ya kushiriki katika mijadala ya masuala yanayowahusu kulingana na umri wao. Katika kipindi hicho, mabaraza 223 yalianzishwa na kufanya jumla ya mabaraza kufikia 8,427 kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa. Hata hivyo, Wizara inaendelea na jitihada za kuanzisha mabaraza kwenye vijiji/Mitaa ili kufikia azma ya Serikali ya kuwa na mabaraza 16,602 ifikapo 2027/28.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na vitendo vya ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto wa kike ambavyo ni ukiukwaji wa haki za binadamu, Serikali imezindua Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji (2025/26 – 2029/30), unaolenga kuimarisha juhudi za kutokomeza vitendo vya ukeketaji nchini. Mkakati huo unalenga kupunguza kiwango cha ukeketaji kutoka asilimia 8 hadi kufikia asilimia 4 ifikapo mwaka 2030. Tofauti na mikakati iliyopita, mkakati huu umeweka kipaumbele cha ushiriki wa wanaume katika harakati za kutokomeza ukeketaji. Hatua hiyo inatokana na baadhi ya mila, desturi na mitazamo hasi ya jamii inayochochea vitendo vya ukeketaji hususani kwa baadhi ya wanaume kutokuwa tayari kuoa wanawake ambao hawajakeketwa

78. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hatua hiyo, kwa mwaka 2026 Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji katika Mikoa yenye vitendo vya ukeketaji nchini. Aidha, Wizara iliungana na Mkoa wa Arusha katika Maadhimisho ya

kupinga vitendo vya ukeketaji yaliyofanyika mwezi Februari, 2026 katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Katika maadhimisho hayo jumla ya wananchi 3,227 walipata elimu kuhusu madhara ya ukeketaji na umuhimu wa ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za kuelimisha jamii.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu afua za ulinzi na usalama wa watoto wanaokinzana na kukutana na sheria pamoja na watoto walio katika mazingira hatarishi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya watoto 284,308 (Wavulana 183,124 na Wasichana 101,184) walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani na watoto waliokinzana na sheria wametambuliwa na kupatiwa afua mbalimbali za kiustawi ikiwemo malezi mbadala, elimu, mafunzo ya ufundi stadi, huduma za afya, vifaa vya shule na kuwaunganisha na familia zao.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani wamegawanyika katika makundi mawili, wanaotegemea mtaa kama makazi ya kudumu na wanaofanya kazi mtaani na kurudi kwenye familia ya wazazi au walezi wao. Katika kipindi husika Wizara imeendesha Kampeni rafiki ya kuokoa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani katika mikoa yote nchini. Kupitia kampeni hiyo, jumla ya watoto 6,182 (Wavulana 3,407 na Wasichana 2,775) wameokolewa, watoto 5,663 wameunganishwa na familia zao, kati yao watoto 52 wamehitimu mafunzo mbalimbali ya ufundi, 448 wako katika Makao ya Watoto na 71 wako chini ya walezi wa kuaminika.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuzuia watoto kuingia mtaani, Sambamba na hilo, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imeanzisha Madawati 14 ya huduma za Ustawi wa Jamii katika Bandari ya Dar es Salaam na stendi za mabasi katika Mikoa ya Shinyanga (2), Mwanza (2), Dar es Salaam (2), Arusha, Kagera, Mbeya, Morogoro, Dodoma, Njombe, Tabora na Ruvuma. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya watoto 3,366 (Wavulana 1,679 na Wasichana 1,687) wameokolewa kupitia madawati hayo na kuunganishwa na familia na wengine kupata huduma katika makao ya watoto.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** madawati hayo hutumika pia kutoa huduma za Ustawi wa Jamii kwa watu wazima wenye changamoto mbalimbali ikiwemo waliopotezana na ndugu zao, waliokosa nauli, waliotelekezwa, waliotapeliwa na waliopitia kadhia ya usafirishaji haramu wa binadamu. Jumla ya watu wazima 3,139 (Wanaume 1,672 na Wanawake 1,467) wamepatiwa huduma katika madawati hayo. Afua hizi zinatekelezwa kupitia Kiongozi cha Uratibu, Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii cha mwaka 2025.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasisitiza kwamba, watoto wote walelewe katika familia. Wazazi na walezi wawajibike katika matunzo na ulinzi wa watoto wao. Mkakati wa kuzuia watoto kuingia na kuishi mtaani ni endelevu ambapo Wizara imepanga kuanzisha madawati mengine nane (8) katika vituo vya usafirishaji kwenye mikoa mingine, sambamba na kuimarisha uwezo wa watoa huduma, mifumo ya uratibu na ufuatiliaji, pamoja na kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu malezi, makuzi na ulinzi wa watoto.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, inapotokea watoto wamekosa malezi ya kifamilia, Wizara imeweka utaratibu wa malezi mbadala kama vile huduma za watoto wanaolelewa katika Makao ya Watoto, Malezi ya Kambo na Kuasili kwa lengo la kutoa matunzo kwa watoto hao. Katika kipindi husika jumla ya Makao ya Watoto 33 yanayomilikiwa na kuendeshwa na Taasisi Binafsi yamesajiliwa na kufanya kuwa na jumla ya makao 426 yaliyosajiliwa nchini (Serikali 2 na Binafsi 424). Makao hayo yanahudumia jumla ya watoto 16,648 (Wavulana 8,423 na Wasichana 8,225).

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji, jumla watoto 39 (Wavulana 18 na Wasichana 21) wamepatiwa huduma ya malezi ya kambo na jumla watoto 28 (Wavulana 11 na Wasichana 17) wamepatiwa huduma ya malezi ya kuasili. Wito unatolewa kwa wote wenye mapenzi mema na watoto na wanaohitaji huduma za kutoa malezi ya kambo na kuasili watoto wafanye maombi yao kupitia Afisa Ustawi wa Jamii kwenye eneo lao kwa hatua stahiki.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa mfano kwa kuendesha Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo - Dodoma na Kurasini - Dar es Salaam yanayotoa huduma jumuishi kwa watoto. Huduma hizo ni pamoja na mahitaji ya msingi, afya, unasihi, elimu ya awali, mafunzo ya ufundi stadi, elimu ya ujasiriamali, kilimo, ufugaji na kuwaunganisha watoto na familia. Jumla ya watoto 418 (Wavulana 231 na Wasichana 187) wamehudumiwa; ambapo Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo yamehudumia watoto 229 (Wavulana 119 na Wasichana 110) na Makao ya Watoto Kurasini yamehudumia watoto 189 (Wavulana 112 na Wasichana 77). Kati ya hao, jumla ya watoto 90 (Wavulana 49 na Wasichana 41) wameunganishwa na familia zao au familia mbadala.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Katiba na Sheria imefanya usimamizi shirikishi kuhusu utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya utoaji huduma za Ustawi wa Jamii katika makao ya watoto katika Mkoa wa Dar es Salaam na Arusha. Zoezi hilo limefanyika kwa kutembelea makao ya watoto 25 katika Mkoa wa Dar es Salaam na Makao ya watoto tisa (9) katika Mkoa wa Arusha. Kupitia zoezi hilo wamiliki wa makao ya watoto 34 pamoja na maafisa ustawi wa jamii 85 walijengewa uwezo wa kuandaa mipango ya huduma kwa watoto.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha haki, ulinzi na ustawi wa watoto kupitia mfumo wa sheria na kijamii, Serikali imeweka mazingira rafiki yanayowezesha watoto waliokinzana au kukutana na sheria kusikilizwa katika Mahakama za Watoto, kwa kuzingatia maslahi mapana ya mtoto na haki zake za msingi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya mashauri 1,367 (Wavulana 731 na Wasichana 636) yalisikilizwa katika Mahakama za Watoto. Kati ya mashauri hayo, mashauri 1,248 ni ya madai na mashauri 119 ni ya jinai. Kati ya mashauri ya madai yaliyosikilizwa, mashauri 1,231 yalihusu matunzo ya watoto, uangalizi wa watoto, haki ya kuwaona watoto pamoja na kuasili watoto na mashauri 17 yalihusu vipimo vya vinasaba.

89. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa huduma za haki za mtoto Kisheria na Marekebisho ya tabia kwa watoto

waliokinzana na sheria katika Mahabusu za Watoto 6 nchini (Arusha, Mbeya, Tanga, Moshi, Upanga – Dar es Salaam na Mtwara) na shule ya Maadilisho ya Irambo Mkoani Mbeya ambapo jumla ya watoto 154 (Wavulana 148 na Wasichana 6) wamepatiwa huduma za msingi ikiwemo chakula, malazi, mavazi, afya, stadi za maisha, msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa lengo la kuwezesha marekebisho ya tabia na utengamao. Huduma hizo zimewezesha watoto kurekebishwa tabia na kupata stadi za maisha za kuwasaidia kujitegemea.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kuimarisha afua zinazolenga kuwaandaa vijana kuingia katika majukumu ya ndoa na familia. Kadhalika, Wizara imeweka msisitizo wa umuhimu wa utatuzi wa migogoro ya familia kwa njia ya usuluhishi ambapo, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imepokea jumla ya mashauri ya ndoa 49,573. Kati ya mashauri hayo, mashauri 9,995 yamesuluhishwa na kufungwa, mashauri 8,036 yalipelekwa mahakamani na mashauri 31,542 yanaendelea kusuluhishwa.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya mashauri ya matunzo ya watoto 19,425 yalitokana na watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Kati ya mashauri hayo 3,500 yamepelekwa Mahakamani na mashauri 15,925 yanaendelea kushughulikiwa na Maafisa Ustawi wa Jamii. Juhudi za kushughulikia migogoro ya familia na ndoa zinachangia kuimarisha mahusiano, ustawi wa familia, na kuwezesha wahusika kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo pindi changamoto zao zinapotatuliwa.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, Wizara inasajili vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana 922 vimesajiliwa na kufikia jumla ya vituo 4,916 kote nchini vinavyohudumia jumla ya Watoto 565,508 (Wavulana 267,922 na Wasichana 297,586). Vilevile, jumla ya Vituo 282 vya Malezi ya Watoto vya Kijamii vimeanzishwa katika ngazi ya jamii vilivyotoa huduma kwa watoto 23,137 (Wavulana 9,875 na Wasichana 13,262). Uwepo wa vituo hivyo umesaidia malezi na

matunzo ya awali ya watoto na kuwezesha wazazi kupata muda wa kujishughulisha na shughuli za kiuchumi.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuimarisha usajili na ufuatiliaji wa vituo hivyo ili kuhakikisha vinazingatia viwango na miongozo iliyowekwa; kujenga uwezo wa watoa huduma kupitia mafunzo ya malezi, lishe na ulinzi wa mtoto; pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na jamii katika uwekezaji wa huduma za malezi ya awali.

94. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau wake wa kisekta imeendelea kuratibu ushirikiano wa wadau mbalimbali wa maendeleo ili kushirikiana na jamii ya makundi yote katika kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa watoto ambapo, kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi, idadi ya watoto walioripotiwa kufanyiwa ukatili wa kingono imepungua kutoka 10,937 mwaka 2024 hadi 9,902 kwa mwaka 2025 (Mchanganuo wa takwimu husika kwa watoto wa kike na kiume na kwa aina ya matukio upo kwenye ***Kiambatisho Na.2A***).
Hata hivyo, pamoja na mafanikio haya, takwimu hizi zinaonesha ukubwa wa changamoto ya ukatili dhidi ya watoto katika jamii yetu na zinatoa wito kwa Taifa kuendelea kuchukua hatua madhubuti zaidi za kulinda kizazi cha sasa na kijacho hivyo, Wizara itaendelea kwa kasi zaidi kuratibu wadau wake ili kuhakikisha ukatili wa kingono dhidi ya watoto unatokomezwa.

95. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, watoto wameendelea kukabiliwa na ukatili wa kutupwa, kuibwa na kutelekezwa ambapo, kwa mwaka 2025 taarifa ya Jeshi la Polisi inaonesha kwenye ***Kiambatisho Na.2B*** kuwa, jumla ya watoto 165 waliripotiwa kutupwa, 137 kutelekezwa na 86 kuibwa. Matukio haya ni kinyume na haki za watoto kuishi kama ilivyoainishwa katika sera ya maendeleo ya mtoto na sheria ya mtoto. Wizara kwa kuunganisha nguvu na wadau wake itaendelea kuelimisha jamii kuimarisha ulinzi wa watoto na iwapo kuna mzazi wa mwenye changamoto yoyote, taarifa iwasilishwe ustawi wa jamii ili hatua zinazostahili zichukuliwe ikiwemo kutoa huduma ya malezi mbadala na kwa wale wenye uhitaji wa watoto badala ya

kuwaiba wafahamu kuhusu uwepo wa huduma rasmi ya kisheria ya kuasili watoto. Tofauti na mwelekeo huu Serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wote wanaojihusisha na vitendo vya ukatili na kuhujumu haki za watoto.

96. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha haki za watoto zinalindwa, wizara kupitia maafisa ustawi wa jamii imeendelea kufuatilia mashauri ya kesi mbalimbali mahakamani ambapo, wakati tunaanza mwaka wa fedha Julai 2025 kulikuwa na mashauri 1,237 ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto yaliyokuwa yanaendelea Mahakamani. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2025 hadi 30 Aprili, 2026 mashauri mapya 1,909 yaliwasilishwa Mahakamani, hivyo kufanya jumla ya mashauri ya ukatili dhidi ya watoto yaliyofikishwa Mahakamani kufikia **3,146**. Kati ya mashauri hayo, mashauri **2,517** yamekwishapatiwa maamuzi huku mashauri **629** yakiendelea kusikilizwa Mahakamani.

97. ***Mheshimiwa Spika***, ni ukweli usiopingika kuwa, Taifa lenye maono ya kufikia DIRA ya Taifa ya Maendeleo 2050 haliwezi kujengwa juu ya mazingira yanayoruhusu watoto kuishi katika hofu, manyanyaso na kukosa ulinzi stahiki hivyo, tunapoelekea DIRA 2050 ni lazima tutambue kuwa, msingi wa Taifa imara, lenye uchumi shindani na maendeleo endelevu ni uwekezaji katika malezi bora, usalama na ustawi wa watoto.

98. ***Mheshimiwa Spika***, ijulikane kwetu sote kuwa, mapambano dhidi ya ukatili wa watoto si jukumu la Serikali pekee bali ni wajibu wa Taifa nzima hivyo, tunapaswa kama jamii kuungana kwa dhati wazazi, walezi, viongozi wa dini, viongozi wa mila, walimu, vyombo vya dola na wananchi wote kuhakikisha watoto wanalelewa katika mazingira salama, yenye maadili, upendo na heshima kwa utu wa binadamu kwani, bila kufanya hivyo, tutakuwa tunahatarisha msingi wa kizazi chenye jukumu la kubeba maono, uchumi na uongozi wa Tanzania ya mwaka 2050.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wazazi wanatekeleza wajibu wao wa kusimamia maadili, malezi na matunzo ya watoto na familia, Serikali kupitia Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu kuhusu maadili, malezi chanya na

matunzo ya watoto na familia, yenye kaulimbiu isemayo "**Familia Bora, Taifa Imara."** Katika kipindi husika, jumla ya wazazi na walezi 469,634 (Wanaume 157,291 na Wanawake 312,343) walipatiwa elimu ya malezi chanya kupitia majukwaa ya wazazi, viongozi wa dini na wahamasishaji jamii. Sambamba na hilo, elimu hiyo ilitolewa kwa waandishi wa habari kutoka vyombo vya habari 29 vya Kitaifa pamoja na redio za kijamii 16 zinazosikika nchi nzima.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** vikundi vya malezi ni majukwaa ya kuwafikia wazazi na walezi kwa urahisi katika lengo la kuimarisha malezi, matunzo na maadili ya watoto ndani ya familia. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeandaa Mwongozo wa kuwezesha uanzishaji na uendeshaji wa Vikundi vya Malezi na Matunzo ya Watoto. Katika kipindi husika, jumla ya vikundi vya malezi 4,526 vimeanzishwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Lengo la Serikali ni kuanzisha na kuhuisha vikundi 200,000 vya malezi na matunzo ya watoto ifikapo mwaka 2030. Hatua hiyo ni sehemu ya Makubaliano ya Bogota, Colombia ya mwaka 2024 kuhusu uanzishaji wa majukwaa ya wazazi au walezi kwa ajili ya malezi ya watoto (Bogota Parenting Platforms Agreement, 2024).

101. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua umuhimu wa ushiriki wa wazazi na walezi katika programu za malezi na matunzo ya watoto nchini. Hata hivyo, imebainika kuwa wazazi wengi hawashiriki ipasavyo katika programu hizo. Kwa kutambua hali hiyo, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) imeratibu utafiti wenye lengo la kubaini tabia na vikwazo vinavyowakabili wazazi na walezi katika kushiriki programu mbalimbali za malezi na matunzo ya watoto.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuwa, vikwazo vinavyosababisha wazazi na walezi kutokamilisha programu za malezi ni pamoja na uelewa mdogo wa maudhui ya afua za malezi, umbali wa kufikia maeneo ya huduma hizo, na mwingiliano kati ya shughuli za kiuchumi na muda wa kushiriki programu hizo. Kupitia matokeo hayo, Wizara inaendelea kuimarisha utekelezaji wa programu za malezi, zikiwemo matumizi

ya teknolojia kupitia programu ya malezi kwa njia ya mtandao (Parenting App) ili kuongeza ushiriki wa wazazi na walezi.

ENEO LA 5: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

103. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa mtu binafsi, familia na makundi mbalimbali katika jamii kwa lengo la kuzuia na kutatua athari zinazotokana na changamoto mbalimbali. Huduma za ustawi wa jamii zinazotolewa kwa makundi hayo zinalenga kukidhi mahitaji ya msingi, kulinda utu wao, na kuwawezesha wanufaika kujenga ustahimilivu wa maisha na hatimaye kujitegemea. Huduma hizo ni pamoja na huduma za msingi za malazi, mavazi, chakula na matibabu; msaada wa kisaikolojia na kijamii; elimu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto; usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia; hifadhi kwa manusura wa vitendo vya ukatili; malezi mbadala; marekebisho ya tabia; na kuunganishwa na mifumo mingine ya utoaji huduma ikiwemo huduma za kisheria, afya na uchumi. kwa ujumla, juhudi hizo zinaakisi dhamira ya serikali ya kuhakikisha makundi hayo yanapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika uchumi na maendeleo ya taifa.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo inaendelea kutoa huduma za msingi kama vile huduma za matibabu, malazi ya muda, huduma za kisheria na msaada wa kisaikolojia kwa manusura na wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto. Miongoni mwa vituo vya kutolea huduma hizo ni pamoja na nyumba salama na vituo vya huduma jumuishi vilivyopo katika vituo vya afya. Katika katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya manusura 1,313 (wanaume 53, wanawake 1,260) wamehudumiwa katika nyumba salama 20 zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini. Sambamba na hilo, jumla ya wahanga na manusura wa vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto 108,819 ikijumuisha watoto 32,150 (Wavulana 6,592 na Wasichana 25,558) na watu wazima 76,669 (Wanaume 16,882 na Wanawake 59,787) wameripotiwa katika vituo mbalimbali vinavyotoa huduma za afya kwa manusura wa ukatili nchini.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii kwa lengo la kusogeza huduma za ustawi kwa wananchi ambapo, katika mwaka wa fedha 2025/26 jumla ya Maafisa Ustawi wa Jamii 401 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi, hivyo kufanya idadi yao kufikia 2,315 sawa na asilimia 12.5 ya Maafisa 18,481 wanaohitajika nchi nzima. Aidha, katika kusogeza huduma za ustawi wa jamii kwa wananchi, Wizara imewapatia Simu Janja Maafisa Ustawi wa Jamii wa ngazi za mikoa ili waweze kuharakisha utoaji wa huduma za kiustawi. Namba za simu kwa kila Mkoa zimeainishwa katika ***Kiambatisho Na.3***.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI, Wizara za kisekta na Wadau wa Maendeleo iliandaa Wiki ya Ustawi wa Jamii yaliyofanyika katika Halmashauri zote nchini kuanzia tarehe 25 - 30 Agosti, 2025 iliyoongozwa na kaulimbiu isemayo **"Pata Msaada wa Kisaikolojia; Imarisha Afya ya Akili"**. Tukio hilo lilitoa fursa kwa wananchi kuzifahamu huduma za ustawi wa jamii sambamba na kufanikisha utolewaji wa huduma muhimu kwa wananchi.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kilele cha Wiki ya Ustawi, Wizara kwa kushirikiana na Mkoa wa Dar es Salaam ilitoa huduma mbalimbali zikiwemo: - Usajili wa Vituo vya kulelea Watoto Wadogo mchana (122); Kutolewa kwa Vyeti vya Kuzaliwa (53); Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa (86); Uchunguzi wa Afya na matibabu kwa wananchi (62); Uchunguzi wa Afya ya Ngozi na Matibabu kwa Watu Wenye Ualbino (263); Kutolewa kwa Huduma ya Msaada wa Kisheria kwa Wananchi (117). Aidha, Wananchi (83) walijiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Wananchi (117) Walipatiwa Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Watoto (43) wanaoishi na kufanya kazi Mtaani waliunganishwa na familia zao; na Manusura (22) wa vitendo vya ukatili walipatiwa usaidizi wa haraka wa huduma za kisaikolojia, Afya na kisheria. Huduma hizo pia zilitolewa katika Halmashauri na Mikoa yote nchini.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO, Tanzania STEPS Survey - 2023) ulionesha kuwa, takribani watu 25 kati ya watu 100 hukabiliwa na changamoto za afya ya akili na saikolojia. Takwimu hizi zinaonesha wazi kuwa changamoto za

afya ya akili si suala la mtu mmoja mmoja, bali ni suala linalohitaji juhudi za pamoja. Katika kipindi cha mwezi Julai 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya Wataalam 95 wakiwemo Maafisa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii, Madaktari na Wauguzi wanaotoa huduma kwa Watoto na Vijana balehe kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Kagera na Songwe wamejengewa uwezo juu ya kutoa huduma ya Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii (Mental Health and Psychosocial Support – MHPSS).

109. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, watoa huduma ngazi ya jamii 280 wamejengewa uwezo wa utoaji wa huduma ya msaada wa afya ya akili na msaada wa kisaikolojia wakati wa majanga katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Katavi, Kigoma, Dodoma, Mbeya na Dar es Salaam. Aidha, wahudumiwa 490 (Wanaume 286 na Wanawake 204) katika vituo vya Ustawi wa Jamii wamepata huduma ya Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii. Pia, jumla ya watoto 208,921 (Wavulana 99,744 na Wasichana 109,177) walio katika mazingira hatarishi na jumla wa wananchi 99,136 (Wanaume 49,568 na Wanawake 49,568) wamepata huduma hiyo. Mafunzo haya yameimarisha uwezo wa wataalam kutambua mapema changamoto za afya ya akili kwa watoto na vijana, kutoa huduma stahiki za ushauri nasaha na msaada wa kisaikolojia, pamoja na kushughulikia athari za msongo wa mawazo, ukatili na majanga mbalimbali.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuimarisha utolewaji wa huduma za Ustawi wa Jamii nchini kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kuongeza ubora wa huduma hizo kwa jamii. Katika kufanikisha hilo, Wizara inashughulikia uanzishwaji wa Idara Huru Inayojitegemea ya Ustawi wa Jamii ambapo kwa sasa iko kwenye hatua ya kupokea maoni kutoka Wizara za Kisekta. Hatua hii inakwenda sambamba na kukamilisha mchakato wa utungwaji wa sheria mahsusi ya wataalam wa huduma za ustawi wa jamii yenye lengo la kusimamia, kudhibiti maadili na weledi kwa wataalamu wanaotoa huduma za ustawi wa jamii.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua na kuthamini mchango wa Wazee kama Tunu muhimu ya Taifa. Dhamira hiyo imeainishwa katika Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Toleo

la Mwaka 2024, inayosisitiza kuhusu ulinzi, matunzo, hifadhi ya jamii na ustawi wa wazee. Taifa lisilojali wazee linapoteza hazina ya maarifa, uzoefu, historia na utamaduni ambavyo ni msingi wa kujenga mshikamano na maadili ya jamii.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026 Wizara imetoa huduma za matunzo kwa wazee na wasiojiweza 229 (Wanaume 139 na Wanawake 90) katika makazi ya Wazee 13 yanayosimamiwa na Wizara. Makazi hayo yapo katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Nunge - Dar es Salaam, Kibiriz - Kigoma, Njoro - Kilimanjaro, Ipuli - Tabora, Kolandoto - Shinyanga, Bukumbi - Mwanza, Magugu - Manyara, Kilima-Kagera, Nyabange - Mara na Mwanzange na Misufini Mkoani Tanga. Sambamba na hilo, Wizara imeratibu huduma za utoaji wa matunzo kwa jumla ya wazee 268 (Wanaume 218 na Wanawake 50) kwenye Makazi ya Wazee 16 yanayomilikiwa na Taasisi Binafsi.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za afya kwa Wazee nchini ikiwa ni utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imewezesha upatikanaji wa Bima za Afya kwa Wazee wote 229 (Wanaume 139 na Wanawake 90) wanaohudumiwa katika Makazi 13 ya Serikali. Kadhalika, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI imefanikisha upatikanaji wa huduma za Msamaha wa Matibabu na Upimaji wa afya kwa Wazee 586,638 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.2.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee, jumla ya madirisha 1,066 ya kutolea huduma za afya kwa wazee yameanzishwa katika hospitali 187 na vituo vya afya 879 katika Halmashauri 184. Sambamba na hilo, jumla ya Watoa Huduma za Afya 140 katika ngazi ya msingi pamoja na Waandishi wa Habari 20 kutoka vyombo mbalimbali vya habari wamejengewa uwezo juu ya afua zinazohusu huduma na ustawi wa wazee. Pia, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Help Age Tanzania imeendelea kutoa elimu na hamasa kuhusu umuhimu wa mazoezi kwa wazee nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya Klabu 195 za mazoezi ya Wazee zimeanzishwa na

kupatiwa vifaa vya mazoezi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Morogoro, Kigoma na Shinyanga.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imeratibu uanzishaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee, ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya mabaraza 20,768 yameanzishwa kuanzia ngazi ya Kata hadi Taifa. Mabaraza hayo yanatumika kama majukwaa ya kuwakutanisha wazee na kujadili masuala yanayo wahusu na nafasi yao katika jamii ikiwa ni pamoja na kurithisha mila, tamaduni na maarifa chanya kwa watoto na vijana.

Sambamba na hilo, Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Singida, Simiyu, Mbeya na Morogoro imeanzisha Ofisi za Mabaraza ya Ushauri wa Wazee ambayo yamerahisisha uratibu wa shughuli za mabaraza hayo.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Aprili, 2026, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) imefanya utambuzi wa jumla ya wazee 1,014,005 wenye uhitaji na kuwajumuisha katika mpango wa uwezeshaji wa kaya maskini utakaowasaidia kuboresha hali zao za kiuchumi kwa ustawi na maendeleo yao. Hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa hakuna kundi linaachwa nyuma katika mchakato wa maendeleo.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee tarehe 01 Oktoba, 2025 yenye kauli mbiu ya **"Wazee tushiriki uchaguzi kwa Ustawi wa Jamii yetu".** Maadhimisho hayo yalianzia katika ngazi za Mikoa na Wilaya yaliyoambatana na makongamano ya wazee na utoaji wa huduma mbalimbali zikijumuisha huduma za afya na afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii ambapo jumla ya wazee 7,917 walipatiwa huduma hizo. Kilele cha maadhimisho hayo Kitaifa yalifanyika Mkoani Ruvuma na kuhudhuriwa na washiriki 814 (Wanaume 511 na Wanawake 303). Lengo la maadhimisho hayo lilikuwa ni kujenga uelewa kwa jamii kuhusu kuwatunza wazee, kuwashirikisha na kuamsha ari ya jamii katika kujiandaa na uzee mwema.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** usalama wa wazee umeendelea kuimarika kutokana na jitihada kubwa za Serikali za kuhakikisha wanapata ulinzi na kuishi katika mazingira salama. Kutokana na hatua hizo, matukio ya ukatili na mauaji dhidi ya wazee yameendelea kupungua kwa kiwango kikubwa. Takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2024 kuliripotiwa matukio 152 (Wanaume 36, Wanawake 116) ya ukatili na mauaji dhidi ya wazee ikilinganishwa na wazee 101 (Wanaume 26 na Wanawake 75) walioripotiwa kwa mwaka 2025.

ENEO LA 6: MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE

119. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 yenye lengo la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeendelea kuratibu na kutekeleza programu na afua mbalimbali zinazolenga kuimarisha ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika nyanja zote za maendeleo. Programu na afua hizo ni pamoja na Programu ya Kizazi Chenye Usawa, Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama, Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia, Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na Ujumuishwaji wa Masuala ya Jinsia katika Sera, Sheria, Mipango na Bajeti.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Wadau wa Maendeleo imefanikisha utekelezaji wa uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia (*Gender Responsive Budget*) kwa Mwaka 2026/27. Kupitia Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango na Bajeti (2026/27), ulibainisha Wizara Tisa (9) za mfano ambazo ni kinara wa utekelezaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia. Wizara hizo ni pamoja na Wizara ya Afya; Maji; Katiba na Sheria; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Viwanda na Biashara; na Mambo ya Ndani ya Nchi; Mikoa Miwili (2) ya Singida na Geita; na Halmashauri mbili (2) za Chalinze na Tandahimba. Lengo ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mipango na bajeti ya Serikali unatoa matokeo chanya na kuimarisha usawa wa kijinsia.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi hili limewezesha Serikali kwa mara

ya kwanza kuweza kuandaa tamko la uzingatiaji wa masuala ya kijinsia kwenye mipango na bajeti (Gender Budget Statement) ambayo itawasilishwa katika Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka 2026/27. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa na kuzindua Kitini cha Mafunzo ya Uandaaji wa Bajeti yenye Mrengo wa Kijinsia cha mwaka 2026. Kitini hicho kitatumika kufundishia Maafisa na wadau wote wanaohusika na uandaaji wa bajeti. Aidha, Wizara imewajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge (Kamati za Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Katiba na Sheria na kamati ya Bajeti) kuhusu bajeti yenye mrengo wa kijinsia na itaendeleza mafunzo haya kwa wadau wote.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuhakikisha bajeti zinaandaliwa na kutekelezwa kwa kuzingatia mrengo wa kijinsia, imeshirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la Wanawake - UN WOMEN na Shirika la *Plan International* katika kutoa mafunzo kwa wataalam 486 ikijumuisha wataalam 167 (Wanaume 84, Wanawake 83) wa ngazi ya Wizara, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 319 (Wanaume 174, Wanawake 145). Mafunzo hayo yalishirikisha Wakurugenzi wa Sera na Mipango, Ufuatiliaji na Tathimini na maafisa wa uandaaji wa bajeti, Makatibu Tawala Wasaidizi sehemu ya Mipango na Uratibu (M), Waganga Wakuu (M), Maafisa Elimu (M), Maafisa Ustawi wa Jamii (M) na Maafisa Maendeleo ya Jamii (M) na Maafisa Habari (M).

123. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Kizazi Chenye Usawa (2021/22 - 2025/26), ikiwa ni utekelezaji wa eneo la Haki na Usawa wa kiuchumi ambalo **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kinara wa utekelezaji kidunia. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, Wizara iliratibu Kongamano lililolenga kuonesha mafanikio ya programu yaliyojumuisha utekelezaji wa miradi ya kiuchumi iliyotekelezwa na wanawake ikiwemo miradi ya uongezaji wa thamani katika bidhaa mbalimbali na teknolojia zinazorahisisha uzalishaji. Kongamano hilo lilishirikisha Waratibu 280 kutoka Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

124. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha mafanikio ya Programu

hiyo yanafahamika na kuenezwa kwa umma, Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini wa Wizara, Taasisi za Umma na Sekretarieti za Mikoa wapatao 63, pamoja na Wahariri 30 kutoka vyombo mbalimbali vya habari vya Umma na binafsi. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uelewa wanahabari na wahariri kuhusu utekelezaji na mafanikio ya Programu kwenye nyanja mbalimbali.

125. ***Mheshimiwa Spika***, mafunzo hayo yamewezesha wanahabari kuibua, kujadili na kuandaa makala katika vyombo vya habari vya Kitaifa na Kijamii, pamoja na mitandao ya kijamii yakionesha mafanikio yaliyopatikana katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake. Vilevile, Wizara inaendelea na uratibu wa kujenga uelewa kuhusu Programu hii katika ngazi za Mabaraza ya Madiwani, kwa lengo la kujenga uelewa ili waweze kusimamia utekelezaji wa Programu kwenye maeneo yao, ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 Mabaraza ya Madiwani katika Halmashauri za Chemba, Mpwapwa, Manyoni na Ikungi yamejengewa uelewa.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) imeendelea kuwatumia Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi na Taasisi; ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Kizazi chenye Usawa. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya majiko banifu 13,575, mitungi ya gesi asilia 28,653 na majiko janja ya umeme 7,292 yametolewa kwa wananchi katika Mikoa yote Tanzania bara kwa utaratibu wa ruzuku. Aidha, Taasisi 1,136 zimehamasishwa kutumia nishati safi ya kupikia ikiwemo Taasisi na Vituo vilivyo chini ya Wizara ambazo ni Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Kijitonyama, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii - Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Jamii Ufundi, Makao ya Watoto, Mahabusu za watoto, Shule ya Maadilisho na Makazi ya Wazee.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imewezesha uandaaji wa Mwongozo wa Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Mwongozo huo, unalenga kuziwezesha Taasisi na jamii kutoa fursa

sawa kwa wanawake na wanaume katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Aidha, sekta ya kilimo imeendelea kuwa kinara katika kuimarisha ushiriki wa wanawake katika ajira zenye staha na shughuli za kilimo chenye tija kupitia uwezeshaji upatikanaji wa ardhi ya kilimo, ushiriki katika mashamba makubwa ya pamoja (BBT Block farms), upatikanaji wa mikopo kwa wanawake (BBT Mitaji) pamoja na kuwawezesha wanawake kuongeza thamani ya mazao.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza muda wa wanawake na wasichana kutafuta maji safi na salama, Serikali imeimarisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya mijini na vijijini. Hali ya upatikanaji wa maji imeongezeka na kufikia **asilimia 85.2** kwa vijijini na **asilimia 92.5** mijini kwa mwezi Desemba, 2026 ikilinganishwa na asilimia 91.6 kwa mijini na asilimia 83 vijijini mwaka 2025.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ushiriki wa wanawake na wasichana kwenye kazi zenye staha, Serikali imeendelea kuhamasiha wasichana kushiriki kwa kusoma masomo ya Sayansi, TEHAMA, Uhandisi na Hisabati kupitia ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wa Programu ya Samia *Scholarship*. Wanafunzi 936 wamedahiliwa katika mwaka wa masomo 2025/26 ambapo kati ya hao wanawake ni 288 na wanaoendelea na masomo ni wanafunzi 850 ambapo wanawake ni 325 wa shahada ya kwanza na shahada ya uzamili 66 ambapo wanawake ni 24.

130. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (Women Development Fund - WDF) unaotoa mikopo kwa Wanawake wajasiriamali walio kwenye vikundi na mwanamke mmoja mmoja. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026, mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 337.9 imetolewa kwa wajasiriamali 45 na kuzalisha jumla ya ajira za watu 114.

131. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wanawake wanafikiwa na fursa za mikopo, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha imeendelea kuhamasisha kutumia madirisha maalum ya wanawake yaliyoanzishwa kwenye Benki mbalimbali nchini. Baadhi

ya madirisha hayo ni pamoja na Jasiri Bond (NMB), Malkia Akaunti (CRDB), Fanikiwa Wewe ni Hodari (Azania), Tabasamu (TCB), *Women Suit Loans* (Access Bank Tanzania), *Group and Small* (BRAC Microfinance Tanzania), *Women Entreprenuership Loans* (SELF Microfinance fund), *SME and Micro loans* (Selcom Microfinance Bank), *Women Empowerment Loans* (GADATH Microcredit Company Limited), *Pink* Mwanamke Loan (Mwanga Hakika Bank), Johari Akaunti (NBC Bank), Vikundi Akaunti (Stanbic bank) na *Mwanamke Plus* (Equity Bank). Kati ya kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026, jumla ya Shilingi **Bilioni 422.9** zimekopeshwa kwa **wanawake 82,699.**

Natoa rai kwa wanawake wajasiriamali kujiepusha na mikopo yenye masharti magumu ijulikanayo kama mikopo kausha damu, badala yake watumie mikopo iliyopo kwenye utaratibu rasmi unaotambuliwa na Serikali.

132. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa uundaji na uratibu wa Majukwaa ya Uwezeshaji wanawake Kiuchumi, Toleo la mwaka 2024. Katika kuimarisha majukwaa hayo, Waratibu 26 wa Mikoa na viongozi 130 wa majukwaa ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara walijengewa uwezo kuhusu majukumu na wajibu wao. Vilevile, Sekretarieti ya Kitaifa imeundwa ikiwa na jukumu la kusimamia utekelezaji na kuelimisha fursa za kiuchumi zinazopatikana nchini katika kuwezesha wanawake kiuchumi.

133. ***Mheshimiwa Spika***, wanawake wajasiriamali wameelimishwa kuhusiana na uundaji wa majukwaa na upatikanaji wa fursa za mitaji na mikopo. Jumla ya wanawake 5,096 kutoka Mikoa ya Iringa, Dar es Salaam, Simiyu, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Tanga, Mara, Pwani, Kilimanjaro, Dodoma, Shinyanga, Manyara, Njombe na Songwe walipata elimu hiyo kwa njia mbalimbali ikiwemo kupitia mikutano ya kidijitali.

134. ***Mheshimiwa Spika***, jitihada hizi zimewezesha jumla ya Majukwaa 15,147 kati ya majukwaa 20,748 sawa na asilimia 73 kuhuishwa. Mchanganuo wa majukwaa hayo ni kama ifuatavyo: Ngazi ya Mikoa (Majukwaa 26); Ngazi ya Halmashauri (Majukwaa

184); Ngazi ya Kata (Majukwaa 3,956); Ngazi ya Mitaa (Majukwaa 4,263) na Ngazi ya Vijiji (Majukwaa 6,718).

135. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya ufuatiliaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa na Dodoma. Ufuatiliaji huo ulihusisha kukagua uhai wa vikundi vinavyounda majukwaa, utekelezaji wa shughuli za majukwaa na upatikanaji wa mikopo na mitaji. Kupitia ufuatiliaji huo ilibainika kuongezeka hamasa kwa wanawake kuunda vikundi ili kujiunga na majukwaa. Aidha, majukwaa haya yameendelea kuwa msaada kwa wanawake kuendelea kukutana na kupata taarifa za fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo fursa za masoko.

136. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha mazingira ya ushiriki wa wanaume katika afua za kukuza usawa wa kijinsia na kupinga ukatili wa kijinsia. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imefanya vikao vilivyohusisha majukwaa ya umoja wa wanaume, ambapo kupitia vikao hivyo kikosi kazi chenye wajumbe sita (6) kiliundwa ili kuunganisha majukwaa hayo kuwa na ushiriki mpana, endelevu na wenye tija. Kutokana na umuhimu huo, Wizara imeanza kuandaa Mwongozo mahsusi wa kuhimiza ushiriki wa wanaume katika kuimarisha usawa wa kijinsia.

137. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imeendelea kuhamasisha vikundi vya wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu kujisajili kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma (National e-Procurement System of Tanzania - NeST) ili waweze kunufaika na zabuni zinazotolewa na Wizara na Taasisi za umma kwa makundi hayo kwa kiwango cha asilimia 30 kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410. Katika kuhakikisha makundi hayo yananufaika, Mafunzo yametolewa kwa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii 978 kutoka Mikoa nane (8) ya Mwanza, Iringa, Mbeya, Songwe, Ruvuma, Katavi, Rukwa na Njombe.

138. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2026 vikundi 1,478 vimepata zabuni za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 39.8, ikijumuisha bilioni 17 zilizonufaisha vikundi vya wanawake 539, bilioni 20.3 kwa vikundi vya vijana 853; bilioni 2.1 kwa vikundi vya

Wazee 57 na milioni 295.1 kwa vikundi vya Watu wenye Ulemavu 29. Kupitia zabuni hizo vikundi vimeweza kuongeza uwezo wa kuajiri na kujiajiri, kukuza ujuzi na ushindani wa kufanya kazi za mikataba ya Serikali na kampuni mbalimbali ili kukuza kipato chao.

139. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilifanya Kongamano la Kiuchumi kwa Wanawake na wajasiriamali lililofanyika mwezi Agosti, 2025 Jijini Mbeya lenye Kauli mbiu ya **"Changamkia Fursa: Jenga Leo na Kesho yako".** Kongamano hilo lilihudhuriwa na jumla ya washiriki 3,989 (Wanaume 1,679, Wanawake 2,310). Lengo la Kongamano lilikuwa ni kutoa elimu kuhusu fursa mbalimbali ikiwemo mikopo yenye masharti nafuu, kuwaunganisha na Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, pamoja na kuwahamasisha kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ikiwa pamoja na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) imeendelea kuboresha utendaji wa madawati ya jinsia katika kukabiliana na Ukatili wa Kijinsia, kwa kuandaa mfumo wa kidijitali wa ukusanyaji wa taarifa za Dawati la Jinsia (Gender Desk Information System - GDIS). Mfumo huo utawezesha manusura kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia kwa njia ya faragha. Vilevile, utaimarisha uwezo wa mamlaka kupokea taarifa, kufuatilia na kushughulikia malalamiko kwa wakati na kwa ufanisi.

141. ***Mheshimiwa Spika***, ukatili wa kijinsia ni changamoto inayoathiri uimara wa wanawake na wanaume katika kufikia ndoto zao za kujiletea maendeleo na ustawi. Takwimu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi zinaonesha ukatili wa kingono kwa jinsia zote umeshuka kutoka matukio 12,749 mwaka 2024 hadi 11,625 mwaka 2025. Aidha, katika kipindi chote, wanaokatiliwa zaidi kingono ni wanawake ukilinganisha na wanaume mathalani, wanawake 10,976 na 10,057 walikatiliwa kingono mwaka 2024 na mwaka 2025 mtawalia ukilinganisha na wanaume 1,773 na 1,568 katika kipindi hicho cha mwaka 2024 na 2025 mtawalia ***Kiambatisho Na.4***.

142. ***Mheshimiwa Spika***, Takwimu za ukatili wa kijinsia kwa watu wazima zinabainisha wazi kuwa, juhudi zaidi zinahitajika katika kuwakomboa wanawake dhidi ya ukatili wa kijinsia kwani, mama akikatiliwa mtoto naye huwa kwenye mashaka makubwa ya kuathiriwa na ukatili huo. Wizara kwa kushirikina na Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Mambo ya Ndani imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuepuka ukatili wa kijinsia, kutumia huduma za dawati la jinsia lililopo katika vituo vyote vya Jeshi la Polisi na kutumia huduma za huduma za msaada wa kisheria chini ya uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria.

143. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, Wizara imeratibu uanzishwaji wa Madawati ya kupinga na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Kati, pamoja na maeneo ya umma yakiwemo maeneo ya masoko. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya madawati 580 yalianzishwa na kufikisha jumla ya madawati 1,150. Mchanganuo wa madawati hayo ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

Jedwali Na.2: Madawati yaliyoanzishwa hadi kufikia Aprili, 2026

Na.	Eneo	Malengo	Julai, 2025 hadi Aprili, 2026	Jumla yaliyoanzishwa hadi Aprili, 2026	Asilimia
1	Taasisi za Elimu ya Juu na Kati	612	30	362	59
2	Maeneo ya soko	2,429	550	788	32
	Jumla	**3,041**	**580**	**1,150**	**38**

144. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya Matukio ya ukatili wa kijinsia 150 (41 Maeneo ya masoko na 109 Taasisi ya Elimu ya Juu na Kati) yameripotiwa. Kati ya matukio hayo yaliyoripotiwa, matukio 134 yalipatiwa ufumbuzi. Vilevile, matukio 14 yalitolewa rufaa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na matukio mawili (2) yalipelekwa Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi kwa hatua zaidi.

145. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaratibu utekelezaji wa Azimio Na. 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama ambalo Tanzania iliridhia kutekeleza tangu mwaka 2000. Azimio hilo linalenga kuimarisha ulinzi na ushiriki wa wanawake katika ajenda ya Amani na Usalama kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa. Katika kutekeleza azimio hilo, Wizara, ilizindua Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama (2024/25 - 2028/29) mwezi Agosti, 2025 Jijini Dar es Salaam. Mpango huu unalenga kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki kikamilifu katika kuzuia migogoro, kujenga na kudumisha amani na kushiriki katika mazungumzo ya usalama katika jamii na nchi.

146. ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa Na. 1325, Wizara zote za Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zina umuhimu kutokana na majukumu yao katika kuhakikisha usawa wa kijinsia, amani na ushirikishwaji wa wanawake katika maendeleo na ulinzi wa jamii. Aidha, Wizara 12 za kipaumbele kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ambazo ni Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Zanzibar; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - (Bara); Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - (Zanzibar); Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara nyingine ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara ya Mambo ya Ndani-Jeshi la Polisi; Wizara ya Fedha - Bara; Wizara ya Fedha na Mipango- (Zanzibar); Wizara ya Katiba na Sheria- (Bara); Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora-(Zanzibar); na OWM-TAMISEMI (Bara na Zanzibar). Wizara hizi zimeteuliwa maalum kutokana na uzito wa majukumu yao yanahusiana moja kwa moja na masuala ya usalama, haki, afya, elimu, maendeleo ya jamii, ulinzi wa watoto na wanawake, pamoja na uratibu wa Sera na mipango ya utekelezaji wa Azimio hilo.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango huo, Wizara imeratibu vikao kazi vya mashauriano vilivyowashirikisha wataalam 50 wa masuala ya bajeti, ufuatiliaji na tathmini pamoja

na watakwimu kutoka katika Wizara za Kisekta 12, Taasisi tatu (3), Mamlaka za Serikali za Mitaa nane (8) na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali matano (5). Kupitia vikao hivyo, Mpango kazi wa mwaka wa utekelezaji kwa kila Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa umeandaliwa na utekelezaji wake unaendelea.

149. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilishiriki mkutano wa sita (6) kuhusu Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama uliofanyika mwezi Desemba, 2025 nchini Tunisia. Mkutano huo uliandaliwa na Uongozi wa Umoja wa Afrika kupitia Ofisi ya Mjumbe Maalum wa Umoja wa Afrika anayeshughulikia masuala ya Wanawake, Amani na Usalama kwa kushirikiana na Serikali ya Tunisia na Mtandao wa Wanawake Viongozi ujulikanao kwa jina la *African Women Leadership Network (AWLN)*. Kupitia mkutano huo Tanzania iliahidi kuendelea na utatuzi wa changamoto za wanawake katika nyanja zote na pia kuendelea kuimarisha ushirikiano na umoja wa Afrika na Wadau wengine ili kuhakikisha wanawake wanapata nafasi stahiki katika jitihada zote za ujenzi na ulinzi wa amani.

150. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilizindua Kampeni yenye jina la ***"Inspire to Lead"*** tarehe 07 Julai, 2025 ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kuhamasisha wanawake na wasichana kushiriki na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na maamuzi. Kupitia kampeni hiyo, Wizara imeandaa video fupi 14 za viongozi wanawake wakielezea uwezo wa mwanamke katika nafasi za uongozi kwa ajili ya kutumika kuhamasisha wanawake na wasichana kupitia mitandao ya kijamii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-Government Authority - eGA) imeanzisha dirisha maalum katika tovuti ya Wizara liitwalo **KAMPENI** kwa ajili ya kurusha kampeni zote za Wizara zinazoelimisha jamii. Hadi kufikia mwezi Aprili 2026 kampeni nne (4) zimerushwa kupitia dirisha hilo.

151. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Uratibu wa Wajane, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imehamasisha wajane kuunda vikundi, kuvisajili na kujiunga na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ili waweze kupata fursa za mitaji na masoko. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya vikundi 121 vya wajane vimeanzishwa na kuunganishwa na fursa za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kupata mikopo na taarifa

za masoko. Vikundi hivyo vimeanzishwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Mtwara, Lindi, Songwe na Dodoma.

152. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imeendelea na ufuatiliaji wa vikundi mbalimbali vya wajane kupitia majukwaa ya Uwezeshaji wanawake kiuchumi na Taasisi zinazotoa huduma kwa wajane kama TAWIA, TUYATA na nyinginezo ili kuhakikisha wajane wanapata haki stahiki na kwa wakati.

153. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilishiriki Mkutano wa Wajane Barani Afrika uliofanyika Jijini Windhoek, Namibia mwezi Septemba, 2025. Katika mkutano huo Ujumbe wa Tanzania uliambatana na Mama Anna Mkapa, mjane wa Rais Mstaafu wa awamu ya tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Benjamini William Mkapa. Kupitia Mkutano huo, Mama Anna Mkapa alipata heshima ya kuzindua Mpango wa Afrika wa Ukuaji na Maendeleo ya Wajane (Pan - Africa Widows Growth and Development Initiatives - PAWGADI). Mkutano huo uliazimia kuendeleza jitihada za kutetea, kulinda na kukuza haki na ustawi wa wajane Barani Afrika.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya uongozi wenye maono wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanawake wameendelea kujipambanua kama nguzo ya uongozi, umoja wa kitaifa na maendeleo jumuishi. Kwa dhamira hiyo, tarehe 14 Januari, 2026, Wizara ilisajili Women in Leadership Forum (WLF) — Jukwaa la Wanawake Viongozi Tanzania, taasisi ya kipekee iliyoanzishwa na wanawake viongozi 12 kutoka vyama 10 vya siasa, wakiongozwa na muasisi na mbeba maono wake, Mheshimiwa Dkt. Evaline Wilbard Munisi ambaye tupo naye ndani ya Bunge hili, pamoja na viongozi wenzake ambao wapo katika Jukwaa la Wageni. Ni nadra duniani kuona viongozi kutoka vyama vingi vyenye itikadi tofauti wakivuka mipaka ya ushindani wa kisiasa na kuungana kwa ajili ya amani, mshikamano, uongozi wa wanawake na maslahi mapana ya Taifa. Usajili wa WLF ni kielelezo cha mazingira wezeshi, siasa za staha na falsafa ya Mheshimiwa Rais ya kulileta

Taifa pamoja; falsafa inayowafanya wanawake kuwa madaraja ya umoja, sauti za matumaini na wabeba maono ya Tanzania imara na jumuishi.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika ngazi za Mikoa, ambapo Wizara iliungana na Mkoa wa Geita kuadhimisha siku hiyo katika kata ya Kalangalala, Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Geita. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa; ***"Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana: Msingi Jumuishi kufikia DIRA 2050***". Kaulimbiu hiyo ilijikita kujenga uelewa wa pamoja ili kuwekeza katika maendeleo jumuishi kwa kutambua na kutekeleza haki za wanawake na wasichana kwa vitendo.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipokea salamu za viongozi na wadau mbalimbali wakiwemo wawakilishi kutoka Benki ya Dunia, Asasi za Kiraia na kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania Shirika la Wanawake Viongozi (Women Leaders Forum - WLF) linaloundwa na wanawake waliokuwa wagombea kwa nafasi ya Urais na Makamu wa Rais katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kama nilivyoeleza awali kwenye aya ya 147.
Pamoja na ushiriki wao katika maadhimisho hayo pia walihimiza wanawake na wasichana kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni ili kujenga Taifa lenye usawa wa kijinsia lisilokuwa na tofauti za kiitikadi, kidini ama kikabila. Hakika, WLF ni kielelezo cha ukomavu wa demokrasia nchini na alama ya mshikamano wa wanawake pasipo itikadi katika kutafuta maendeleo endelevu.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na maadhimisho hayo, Wizara ilizindua rasmi Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Advancing Gender Equality in Tanzania) unaojulikana kwa jina la "PAMOJA Project". Lengo la mradi huo ni kukuza usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake kiuchumi na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika mikoa 10 yenye jumla ya Halmashauri 40. Maelezo ya kina ya kuhusu Mradi wa PAMOJA yapo katika eneo la kumi linalobainisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli mbalimbali zilifanyika wakati wa maadhimisho katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na kutoa misaada kwenye vituo vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; na kusaidia kaya za watoto wenye ulemavu kwa kutoa misaada ya kifedha na taulo za kike kwa wanafunzi wasichana wa shule za Msingi na Sekondari. Vilevile, kufanya usafi wa mazingira maeneo ya stendi za mabasi; kutoa elimu kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, lishe na malezi bora kupitia mikutano na makongamano; kutoa elimu ya msaada wa kisheria kupitia kampeni ya Mama Samia *Legal Aid Campaign;* na mashindano ya michezo mbalimbali (Bonanza).

159. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilishiriki kwenye Mkutano wa 70 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Nchini Marekani Mwezi Machi 2026 uliokuwa na kaulimbiu isemayo; ***"Kuhakikisha na Kuimarisha upatikanaji wa haki kwa Wanawake na Wasichana wote, ikiwa ni pamoja na kukuza mifumo ya kisheria yenye usawa na jumuishi, kuondoa sheria, sera na desturi za kibaguzi na kushughulikia vikwazo vya kimuundo".*** Kaulimbiu hiyo imejikita kujadili utekelezaji na jitihada za nchi katika kuimarisha upatikanaji wa haki za msingi na huduma za kisheria kwa wanawake na wasichana wote.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilifanikiwa kuwasilisha mafanikio yaliyopatikana katika upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana katika mkutano huo. Miongoni mwa wawasilishaji wa Taarifa ya Nchi ni pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria, Chama cha Majaji Wanawake (TAWJA), Shirika la LANDESA na Chama cha Wahandisi Wanawake. Kupitia Mkutano huo nchi ilionesha mafanikio yaliyofikiwa kwa wanawake na wasichana kwa kuakisi utekelezaji wa Mipango na programu za nchi, sambamba na mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** ujumbe wa nchi katika mkutano huo uliambatana na Waziri wa Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar pamoja na viongozi, wataalamu na wanaharakati wanaojihusisha na masuala ya uwezeshaji wanawake, ukatili wa Kijinsia na masuala ya sheria kutoka Wizara za Kisekta, Taasisi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wenye jumla ya washiriki 138. Aidha, Nchi iliandaa mikutano minne (4) ya

pembeni, (side events) kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Katiba na Sheria, Chama cha Wanawake Majaji (TAWJA) na Taasisi ya Wahandisi (Kitengo cha Wanawake Wahandisi) ambao walitumia majukwaa hayo kuelezea utekelezaji wa nchi sanjari na kaulimbiu ya mwaka huu.

162. ***Mheshimiwa spika,*** kupitia Mkutano huo, nchi yetu ilipata mialiko ya kushiriki mikutano mbalimbali kutoka nchi nyingine ikiwa ni pamoja na mkutano ulioandaliwa na nchi ya Misri, Liberia, Morrocco, Uholanzi (Netherland), Uingereza (United Kingdom), Sweeden, Ujerumani, FAO na mikutano iliyoandaliwa na Afrikan Union (AU) na United Nations (UN). Majukwaa hayo yalisaidia kutambua fursa na namna ya kutatua changamoto zinazohusu masuala ya uimarishaji na upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuleta ufanisi na uendelevu wenye tija wa mikutano hii, Wizara imeratibu kikao cha tathimini na Wadau wote walioshiriki mkutano huo tarehe 09 Mei, 2026 ambapo wadau walijadili mafanikio, changamoto na mikakati ambayo itazingatiwa katika mikutano ijayo hususan mkutano wa 71 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani.

Aidha, katika mkutano huo ulizinduliwa Mwongozo wa Kuratibu Ushiriki wa Wadau wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa wa mwaka 2024 ambao utasaidia kuratibu ushiriki wa mikutano hiyo kabla, wakati na baada ya kufanyika kwa mikutano hiyo kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa maendeleo.

ENEO LA 7: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

164. ***Mheshimiwa Spika,*** usajili na uratibu wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni majukumu muhimu yanayotekelezwa na Wizara, ili kuhakikisha wananchi wanapata haki yao ya kikatiba ya kujumuika na kuchangia maendeleo kwa kutoa huduma kwa jamii zenye uhitaji. Uratibu wa Mashirika haya umeendelea kuimarisha mahusiano kati Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika utekelezaji wa miradi na utambuzi wa mchango wa Mashirika hayo katika maendeleo

ya nchi. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini yanasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 na Kanuni zake.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,066 (Kimataifa 49, Kitaifa 973, Kimkoa 23 na Kiwilaya 21) yamesajiliwa kati ya Mashirika 1,000 yaliyopangwa kusajiliwa. Mafanikio hayo yamechangiwa na uboreshaji wa huduma za usajili kupitia mfumo wa kielektroniki na kutanua wigo wa watumiaji wa mfumo huo. Mashirika yaliyosajiliwa yamejikita katika utekelezaji wa afua za sekta mbalimbali za maendeleo ikiwemo uwezeshaji wa jamii kiuchumi, afya, mazingira, elimu, ulinzi wa jamii, kilimo, utawala bora, maji, miundombinu, haki za binadamu na jinsia.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wasajili Wasaidizi waliopo ngazi za Halmashauri na Mikoa imeendelea kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo katika kipindi husika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,547 yalifikiwa katika Halmashauri 154 nchini. Ufuatiliaji huo ulibainisha kuwa kati ya Mashirika yaliyofuatiliwa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,432 yanatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayosimamia uendeshaji wa Mashirika hayo, pamoja na vipaumbele vya Taifa.
Aidha, Mashirika 115 yalibainika kutozingatia Sheria na taratibu za uendeshaji wake kwa kutowasilisha taarifa za mwaka. Mashirika hayo yamejengewa uwezo na kupewa muda maalum wa kuwasilisha taarifa hizo ili kuendana na matakwa ya Sheria.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inashirikiana na Wizara ya Fedha katika uratibu wa pamoja na ufuatiliaji wa miradi yenye uendelevu ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kwa mujibu wa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara (2025). Kupitia ufuatiliaji huo, mwaka 2025/2026 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 250 yalifuatiliwa katika mikoa 10 ya Kilimanjaro, Mbeya, Dodoma, Arusha, Iringa, Manyara, Tanga, Mwanza, Tabora na Dar es Salaam. Ufuatiliaji huo ulilenga kuhakiki utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye uendelevu na kutathmini tija ya miradi hiyo kwa jamii.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ufuatiliaji huo, ilibainika kuwa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalipokea jumla ya shilingi bilioni 296.5. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 275.6 sawa na asilimia 93 zilitoka katika vyanzo vya nje ya nchi na shilingi bilioni 20.9 sawa na asilimia 7 zilitoka katika vyanzo vya ndani ya nchi. Aidha, tathmini hiyo ilionesha kuwa Mashirika mengi yanajiendesha kwa kiasi kikubwa kwa kutegemea ufadhili kutoka nje ya nchi ambapo kwa sasa wafadhili wengi wamepunguza ufadhili.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutegemea wafadhili, baadhi ya Mashirika yameendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 - 2026/27). Mkakati huo unahimiza Mashirika kuwekeza mitaji katika miradi ya kijamii yenye kujiendesha kibiashara ili kuongeza uendelevu wa shughuli zao. Kwa mfano, Shirika la *Ilula Orphan Program (IOP)* la Mkoani Iringa limekuwa la mfano katika utekelezaji wa Mkakati huo ambapo kati ya shilingi bilioni 3 inazotumia katika uendeshaji wa shughuli zake, bilioni 1.8 sawa na asilimia 60 zinatokana na miradi ya uendelevu ya Shirika ambayo ni shule, chuo cha ufundi, nyumba za malazi pamoja na miradi ya kilimo na ufugaji. Miradi hiyo imechangia utoaji wa huduma kwa jamii na kutoa ajira kwa wananchi wa maeneo hayo.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kupitia **Mradi wa Wajibika** unaofadhiliwa na Ubalozi wa Uswisi na Ubalozi wa Uingereza imeandaa mwongozo wa utekelezaji wa Mkakati huo. Mwongozo huo unalenga kuongeza uelewa kuhusu uhimilivu na uendelevu wa Mashirika hayo pamoja na kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mkakati huo. Kutokana na juhudi hizo baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameanzisha Taasisi za Fedha zinazotoa mikopo hususani kwa wanawake na vijana.Mashirika hayo ni Shirika la *World Vision* Tanzania iliyoanzisha *VisionFund* Tanzania, Shirika la BRAC Maendeleo lililoanzisha BRAC Tanzania *Finance Limited* na Shirika la Pastoral Women's Council (PWC) lililoanzisha *Engison Microfinance Limited*.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali za kupunguza utegemezi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa wafadhili wa nje

na kuimarisha uendelevu wa Mashirika hayo, Serikali imezindua Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Mchakato wa Uanzishwaji wa Mfuko wa Pamoja wa Ruzuku kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs Basket Fund - NBF). Kamati hiyo inaongozwa na Dkt. Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB. Mfuko huo utayawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupata rasilimali fedha zitakazoratibiwa kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi visivyo na masharti magumu. Kamati hiyo inatarajia kukamilisha kazi hiyo ndani ya mwaka ujao wa fedha 2026/27.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2025 ikitoa taarifa ya mchango wa Mashirika hayo kwa mwaka 2024 kwa mujibu wa utaratibu wa utoaji wa taarifa hizo. Taarifa hiyo ilionesha kuwa, jumla ya shilingi trilioni 1.2 zilitumika katika shughuli za utekelezaji wa miradi. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 980.3 kilitumika kutekeleza miradi ya afya, nishati, mazingira, uwezeshaji jamii, ulinzi wa jamii, elimu, kilimo, utawala bora, maji, haki za binadamu na jinsia na kiasi cha shilingi bilioni 219.7 kilitumika kwa ajili ya shughuli za kiutawala za Mashirika hayo. Aidha, tathimini hiyo ilibaini kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametoa ajira 18,529 ambapo wanawake walikuwa 10,504 na wanaume 8,025. Vilevile, afua zilizotekelezwa na Mashirika hayo zimenufaisha wananchi 208,300.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** Waratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ngazi za Mikoa na Hamashauri ni Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi hizo ambao ndio Wasajili Wasaidizi. Katika kuhakikisha kada hiyo inajengewa uwezo kuhusu uratibu wa Mashirika hayo, Wizara imewajengea uwezo Wasajili Wasaidizi 210 wa Mikoa na Halmashauri zote nchini. Aidha, Wajumbe 30 wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), pamoja na Wawakilishi 2,636 wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pia wamejengewa uwezo kuhusu Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara (2025), Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali (2025/26), Mwongozo wa Uzingatiaji wa Uwazi wa Masuala ya Kifedha na Ushirikiano kati ya Serikali na Asasi Zisizo za Serikali (2025), pamoja na Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Lengo la mafunzo hayo ni

kuwawezesha kuandaa miradi yao kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa na kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwenye Bajeti ya Serikali.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) iliratibu Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Jijini Dodoma. Kupitia jukwaa hilo huduma mbalimbali zilitolewa kwa wananchi ikiwemo huduma ya msaada wa Kisheria ambapo wananchi 2,094 walifikiwa na kwamba migogoro ya ardhi 50 ilishughulikiwa. Aidha, wananchi 138 (Wanaume 77 na Wanawake 61) walipata huduma ya afya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kurudisha kwa jamii

175. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana kwa karibu na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini katika kuimarisha uratibu wa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kujenga ushirikiano madhubuti, kuongeza uwajibikaji na kuimarisha mchango wa Sekta hiyo katika maendeleo ya Taifa. Katika kuendeleza juhudi hizo, tarehe 22 Aprili, 2026, Wizara iliratibu kikao maalum cha Wabunge wa Viti Maalum wanaowakilisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ajili ya kupitia taarifa ya utekelezaji pamoja na mwelekeo wa Sekta hiyo. Kikao hicho kilitoa fursa muhimu ya kujadili mafanikio yaliyopatikana, changamoto zinazoikabili Sekta, pamoja na mikakati ya kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na kuchochea maendeleo jumuishi ya Taifa. Aidha, kikao hicho kilisisitiza umuhimu wa kuongeza utambuzi wa mchango unaotolewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya jamii, ustawi wa wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

176. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia majadiliano hayo, mrejesho ulionesha kuwa, kati ya hoja 19 zilizowasilishwa na Sekta kupitia majukwaa mbalimbali ya mwaka, hoja 15 sawa na asilimia 80 tayari zimefanyiwa kazi na Serikali. Mafanikio hayo yanajumuisha kuimarishwa kwa utendaji wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) pamoja na kuboreshwa kwa Mwongozo

wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini ili kuyawezesha Mashirika hayo kushiriki kikamilifu katika vikao rasmi vya Serikali katika ngazi za Halmashauri, Wilaya na Mikoa. Hatua hizi zinaendelea kuimarisha mazingira wezeshi ya ushiriki wa wadau katika maendeleo na kuifanya Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa mshirika muhimu wa Serikali katika kufanikisha agenda ya maendeleo ya Taifa kuelekea DIRA 2050.

177. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na mafanikio hayo, Wizara inapenda kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan**, kwa uamuzi wake wa kizalendo, wenye maono na tija kwa Taifa wa kuongeza idadi ya Wabunge wanaowakilisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka wawili hadi watatu. Uamuzi huo ni hatua kubwa na ya kihistoria inayoonesha dhamira thabiti ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuendelea kuimarisha ushiriki wa wadau wa maendeleo katika ujenzi wa Taifa, kuongeza uwakilishi wa sauti za wananchi na kuipa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nafasi pana zaidi ya kushiriki katika majadiliano na maamuzi muhimu ya kitaifa.

Hatua hiyo imekuwa ni chachu muhimu ya kuimarisha mahusiano kati ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kuongeza ari ya uwajibikaji wa Sekta hiyo, na kuifanya kuwa mshirika imara zaidi katika utekelezaji wa agenda ya maendeleo ya Taifa kuelekea DIRA 2050.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa ushirikiano kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mamlaka za Serikali katika ngazi za Mikoa kumewezesha kufungamanisha agenda za maendeleo za Mashirika hayo na vipaumbele vya maendeleo vya Mikoa husika, hali inayoongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi na mchango wa Sekta hiyo katika maendeleo ya Taifa. Sambamba na mafanikio hayo, Wizara inaendelea kushirikiana kwa karibu na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kushughulikia hoja zilizobakia ikiwemo kuharakisha upatikanaji wa vibali vya utekelezaji wa miradi kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuhakikisha maombi ya msamaha wa kodi yanawasilishwa na kupatiwa mrejesho kwa wakati kutoka

Mamlaka ya Mapato Tanzania, hatua ambazo zinalenga kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji wa Mashirika hayo na kuyawezesha kuchangia kwa ufanisi zaidi katika kufanikisha DIRA ya Taifa ya Maendeleo 2050 inayohitaji mshikamano wa dhati wa wadau wote wa maendeleo wakiwemo Asasi za Kiraia.

ENEO LA 8: URATIBU WA MPANGO KAZI WA TAIFA WA KUTOKOMEZA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO AWAMU YA PILI (MTAKUWWA II)

179. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya Pili (MTAKUWWA II – 2024/25 - 2028/29) wenye lengo la kuhakikisha jamii inakuwa huru dhidi ya vitendo wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto na inapata fursa sawa za kushiriki katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mpango huu una maeneo makuu nane (8) ambayo ni (i) Kuimarisha Uchumi wa Kaya; (ii) Mila na Desturi; (iii) Mazingira Salama katika Maeneo ya Umma na Mtandaoni; (iv) Malezi, Familia na Mahusiano; (v) Usimamizi na Utekelezaji wa Sheria; (vi) Utoaji wa Huduma za Mwitikio kwa Wahanga wa Ukatili; Ulinzi wa Mtoto Shuleni na Stadi za Maisha; na (viii) Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Washirika wa Maendeleo imeendelea kuratibu utekelezaji wa mpango huo ili kuimarisha utekelezaji wa afua mbalimbali. Mpango huo ni shirikishi kwa kuhusisha Serikali, Washirika wa Maendeleo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Taasisi Binafsi na jamii kwa ujumla. Aidha, Mpango huo unasisitizwa kujadiliwa katika ngazi za maamuzi ikiwemo Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC), Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) na Kamati za Ushauri za Mikoa (RCC) zinazoongozwa na Wakuu wa Mikoa na zinazoongozwa na Wakuu wa Wilaya.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango huo kwa kila eneo unaratibiwa na Wizara mbalimbali kulingana na usimamizi wa Kisera wa eneo husika ambapo, eneo la kuimarisha uchumi

wa kaya linaratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuwezesha mazingira ya upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa makundi ambayo yapo katika sekta isiyo rasmi hususan wananchi wasio na sifa za kuweza kupata mikopo mikubwa katika Taasisi za Fedha.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** fursa hizo ni pamoja na mikopo isiyo na riba kutokana na mgawanyo wa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri, Mikopo ya wafanyabiashara ndogondogo, ushiriki wa Makundi maalum katika zabuni za manunuzi ya Umma, ushiriki wa wanawake katika Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na uwepo wa madirisha ya mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake yaliyopo katika Benki mbalimbali hapa nchini. Vilevile, eneo hili linatambua pia Mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania - TASAF ambapo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, mfuko umetoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 43.5 kwa Kaya zilizotambuliwa 896,746 katika maeneo 186 ya utekelezaji wa programu ya TASAF.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mpango huo Wizara inaratibu pia eneo la kuimarisha Mila na Desturi kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ambayo imezindua. Miongoni mwa kazi zinazofanyika katika eneo hili ni pamoja na kuendesha majadiliano ya mmomonyoko wa maadili ngazi ya jamii kuhusu mila na desturi kwa lengo la kushawishi jamii kubadili mitazamo na kuachana na mila na desturi hasi zinazochochea ukatili wa kijinsia.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** majadiliano hayo yamefanyika katika Mikoa 10 ambayo ni Manyara, Mara, Shinyanga, Geita, Arusha, Singida, Mwanza, Simiyu, Lindi na Tanga ambapo jumla ya washiriki 19,215 (Wanaume 10,560 na Wanawake 8,655) wa rika na nyadhifa mbalimbali walifikiwa. Makundi yaliyofikiwa ni wazee wa mila (350), Ngariba (15), Viongozi wa dini (200), watu mashuhuri (50), Viongozi wa Kisiasa (100), Watumishi wa Serikali (500), na Wananchi wa kawaida (18,000). Kupitia majadiliano hayo, jamii zilitambua baadhi ya mila zenye madhara na kuweka mikakati

mbalimbali ya kuzitokomeza. Aidha, katika kuimarisha masuala ya maadili pia, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo imezindua **Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmmonyoko wa Maadili (2026/27 – 2036/ 37)** unaolenga kujenga jamii yenye maadili, uzalendo, uwajibikaji, na mshikamano wa kitaifa.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Mipango hii miwili (2) yaani Mpango wa MTAKUWWA na Mkakati wa Kupambana na Mmomonyoko wa Maadili ni Mipango pacha ambayo inalenga kuhakikisha jamii ya Tanzania inakuwa salama dhidi ya ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya watoto pamoja na kuimarisha mila, desturi na tamaduni chanya miongoni mwa jamii.

Nitoe pongezi zangu za Dhati kwa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo inayoongozwa na Mhe. Paul Makonda (Mb.) kwa kuona umuhimu wa kupambana na mmomonyoko wa maadili na kuandaa Mkakati huo.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, imewajengea uwezo wataalam mbalimbali kuhusu mbinu za kuelemisha jamii katika masuala mbalimbali ikiwemo: Fursa za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Kutokomeza Mila na Desturi zenye Madhara; Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Sheria; Kuanzisha Dawati la ulinzi wa Mtoto Shuleni; na kuanzisha Dawati la Jinsia katika Maeneo ya Umma. Mafunzo haya yalitolewa kwa jumla ya Wataalamu 238 kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Wataalamu waliojengewa uwezo ni Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa TEHAMA, Watangazaji wa Redio za Kijamii, Maafisa Habari wa Serikali, Viongozi wa Kidini na Viongozi wa Kimila. Kupitia mafunzo hayo, masuala mbalimbali yaliibuliwa na kujadiliwa na wataalamu hao ikiwemo namna ya kukabiliana na mila zenye madhara.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafunzo hayo, jumbe mbalimbali ziliandaliwa kwa lengo la kuelimisha jamii ikiwemo ujumbe usemao ***"Tuseme Hapana kwa Ukatili wa Kijinsia, mila na desturi zinazozuia heshima na ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika maendeleo ya familia na Taifa. Usawa kwa Wote Maendeleo kwa Taifa"***. Aidha, waandishi na watangazaji wa

redio mbalimbali za kijamii walishiriki mafunzo hayo na wameanza kurusha maudhui ya kuelimisha jamii kulingana na maeneo waliojengewa uwezo. Wanahabari hao walitoka katika vituo vya redio za Mpanda FM (Katavi), Joy Radio (Kigoma), Nyemo FM (Dodoma), CG FM (Tabora), Afya Radio (Mwanza), Kasibante FM Radio (Kagera), Mazingira FM (Mara), Sunrise Radio (Arusha), Mbeya Highlands FM (Mbeya), Nuru FM (Iringa), Abood FM (Morogoro), Hopaje FM (Mtwara) na Ruangwa FM (Lindi).

Nitoe Rai kwa Waandishi wa Habari katika Maeneo yote ikiwemo Waandishi wa Habari wa Mtandaoni kutumia Taaluma zao kutangaza Habari zenye kuelimisha na kuhabarisha ili kujenga jamii yenye uelewa mpana na si kutangaza na kurusha maudhui yanayochangia mmomonyoko wa maadili kwa lengo la kupata wafuasi wengi katika vyombo vyao na kusababisha mmomonyoko wa maadili.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu kikao ngazi ya Mawaziri kwa lengo la kujadili hali ya maadili katika jamii kufuatia ongezeko la matukio ya ukiukwaji wa maadili katika jamii. Aidha, kikao hicho pia kilijadili athari za matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, changamoto zinazokwamisha juhudi za kudhibiti mmomonyoko wa maadili, pamoja na kuweka maazimio kuhusu hatua stahiki kudhibiti hali hiyo.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** kikao hicho kilihudhuriwa na Mawaziri kutoka Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Afya; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Fedha; Wakuu wa Taasisi kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); pamoja na Wakurugenzi na wataalam kutoka Wizara hizo.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia kikao hicho, masuala mbalimbali yanayochochea mmomonyoko wa maadili yalijadiliwa ikiwemo: -

i) Kufanya mapitio ya Sera na Sheria zote zinazoendana na masuala ya maadili kwa lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti na kuanisha adhabu kwa makosa yanayochochea mmonyoko wa maadili;

ii) Kuimarisha utekelezaji wa sheria kwa kuwachukulia hatua watuhumiwa wote watakaobainika kuvunja sheria au kuchochea mmomonyoko wa maadili kwa namna yoyote ile;

iii) Kuongeza ushirikiano wa Wizara na Taasisi zote zenye mamlaka ya kudhibiti mmomonyoko wa maadili ikiwemo Mamlaka ya Mawasiliao Tanzaia TCRA na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA);

iv) Kuhakikisha masuala ya mmomonyoko wa maadili yanajadiliwa katika vikao mbalimbali vya maamuzi kuanzia ngazi ya Taifa, hadi Kamati za Ushauri za Mikoa (RCC), Wilaya (DCC) na ngazi Kata (WDC); na

v) Kuandaliwa kwa Mpango Kazi jumuishi wa utekelezaji wa afua za kupambana na mmomonyoko wa maadili.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuanza utekelezaji wa hatua za haraka za kupambana na mmomonyoko wa maadili, Serikali imefanya utambuzi wa baadhi ya matukio yanayochochea mmomonyoko wa maadili ambapo orodha ya watuhumiwa wanaohusika kwenye matukio hayo imeandaliwa na kuwasilishwa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ajili ya hatua zaidi.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, katika kuimarisha jitihada za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili; Serikali imeandaa **Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania (2022)** na **Mwongozo wa Uzingatiaji Maadili katika Kazi za Sanaa (2023)**. Miongozo hiyo ni jitihada za pamoja katika kuimarisha maadili na misingi ya utamaduni wa Taifa na kudhibiti maudhui ya kazi za sanaa zinazochochea mmomonyoko wa maadili yasiyoendana na mila na desturi za Kitanzania.

Nitoe rai, kwa jamii kwamba suala la maadili sio ajenda ya Serikali peke ya yake bali ni ajenda ya Taifa kwa ujumla, hivyo ni wajibu wetu sote kulinda maadili ya Taifa letu kwani Taifa ni letu na maadili ni ya kwetu kama ilivyoainishwa katika misingi ya DIRA 2050 kuwa na Taifa linalohifadhi, kukuza na kulinda maadili na

tamaduni chanya kwa lengo la kuimarisha umoja na utambulisho wa kitaifa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Mazingira Salama Katika Maeneo ya Umma na Mtandaoni ni eneo lingine la MTAKUWWA II ambalo linalenga kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii. Mazingira hayo yanajumuisha maeneo ya kijiografia yanayokutanisha watu wengi kupata huduma kama vile sokoni, vituo vya usafiri, viwanja vya michezo na fukwe pamoja na maeneo ya mtandaoni. Eneo hili linaratibiwa na OWM – TAMISEMI pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha usalama katika mazingira hayo ikiwemo, ujenzi wa mfumo wa kutambua matukio na kuhifadhi takwimu za Uhalifu Mtandaoni na kuimarisha mazingira ya TEHAMA katika maabara za Jeshi la Polisi Tanzania na Kitengo cha Uchunguzi wa Kidijitali (Cybercrime Unit). Hatua hizi zinalenga kuongeza uwezo wa uchunguzi wa uhalifu mtandaoni na kuimarisha usalama wa matumizi ya mifumo ya kidijitali hususan kukabiliana na ukatili wa mtandaoni.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo lingine la Huduma na Msaada wa Kisheria linaloratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria, Mpango umetambua jitihada za Serikali na wadau wengine ikiwemo utoaji huduma ya Msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Mama Samia *Legal Aid Campaign*. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya wananchi 7,462,387 (Wanaume 3,611,286 na Wanawake 3,851,101) walifikiwa na kupatiwa huduma za msaada wa kisheria.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa manusura wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, Wizara inaratibu kituo cha Kijamii cha Huduma kwa Wateja (Community Contact Center) chenye lengo la kusogeza huduma kwa jamii. Kupitia kituo hicho, wananchi wanaweza kupiga simu bure kwa ajili ya kupata huduma zinazoratibiwa na Wizara au kutoa taarifa ya changamoto mbalimbali. Namba za kituo cha Wizara ni **0262160250**, **0734986503**, **0766400168**, **0769608130**, **0774112233**.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya mashauri 753 yalipokelewa kupitia kituo cha kijamii cha huduma kwa wateja. Kati ya mashauri yaliyopokelewa, mashauri 660 yamefanywa kazi na kufungwa na mashauri 93 yanaendelea kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya mashauri yaliyopokelewa, mashauri 272 yalihusu huduma za ustawi wa jamii ikiwemo masuala ya ndoa na familia, ukatili wa kijinsia, mahitaji ya msaada wa afya ya akili na kisaikolojia, malezi ya kambo na kuasili pamoja na usajili wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana; Mashauri 101 yalihusu masuala mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo ambapo; Mashauri 373 yalihusu Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Mashauri mawili (2) yalihusu masuala ya kijamiii; na Mashauri Matano (5) yalihusu huduma za maendeleo ya mtoto.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo la Ulinzi wa Mtoto Shuleni na Stadi za Maisha linaratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo mambo mengi yamefanyika katika kuimarisha ulinzi wa mtoto shuleni. Miongoni mwa masuala yaliyofanyika ni pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu 6,024 wa shule za awali na shule za msingi kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia kupitia mpango wa shule salama kwa lengo la kuboresha huduma za malezi, ushauri na unasihi shuleni. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha masuala mtambuka ikiwemo mazingira, usawa wa kijinsia na elimu ya afya katika taasisi za elimu ya juu kwa kutoa mafunzo kwa wanafunzi 34,000 kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili na kupinga ukatili wa kijinsia ili kufanya vyuo kuwa sehemu salama ya kuishi, kufanya kazi na kupata ujuzi na mafunzo.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo la Uratibu wa MTAKUWWA linafanyika kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Katika kuimarisha uratibu wa MTAKUWWA, Wizara imeandaa Mwongozo wa uratibu wa MTAKUWWA II (2024/25 -2028/29) unaofafanua kwa kina majukumu ya utekelezaji wa mpango kwa ngazi zote. Malengo ya mwongozo huo ni pamoja na kuimarisha

uratibu wa mpango; kuimarisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto; na kuimarisha utoaji wa huduma za msaada kwa wahanga na waathirika vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imeandaa Kitini cha Mafunzo (Training Manual) na Kitabu cha Mshiriki kwa ajili ya Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika ngazi zote. Lengo ni kuimarisha uelewa na uwezo wa wajumbe wa kamati hizo katika kutekeleza majukumu yao. Nyenzo hizo zipo katika hatua ya majaribio kabla ya kuanza kutumika.

201. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imeratibu uandaaji wa Mipango Mikakati ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto, kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele maalum vya kila mkoa. Hadi kufikia Aprili, 2026 Mikoa 10 ya Mwanza, Geita, Dodoma, Iringa, Mbeya, Njombe, Shinyanga, Songwe, Dar es Salaam na Mtwara imeandaa na kuzindua mipango hiyo, na mikoa 16 ipo katika hatua za ukamilishaji. Mipango ya MTAKUWWA ngazi ya Mkoa inaimarisha utekelezaji wa kukabiliana na kupunguza vitendo vya ukatili kwa kuzingatia mahitaji na mazingira ya Mkoa husika.

202. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utekelezaji wa MTAKUWWA, jumla ya vikundi kazi nane (8) vimeundwa kwa kuzingatia maeneo ya utekelezaji wa mpango. Ili kuongeza ufanisi wa vikundi kazi hivyo, Wizara imeandaa hadidu za rejea (Terms of Reference – TOR) kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa wajumbe wanaounda vikundi kazi hivyo. Vilevile, Wizara imefanya uzinduzi wa Vikundi Kazi hivyo kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa afua za mpango, pamoja na kuimarisha uratibu, ushirikiano na mawasiliano kati ya waratibu wa vikundi kazi na wadau mbalimbali. Uzinduzi wa vikundi kazi ulifanyika mwezi Februari, 2026 ambapo Wakuu wa Vikundi kazi walipata fursa ya kueleza utekelezaji, mafanikio changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha utekelezaji wa mpango.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI imewajengea uwezo Wakuu wa Idara za Mipango na Uratibu184 kutoka Halmashauri zote nchini kuhusiana na umuhimu wa kutenga fedha za utekelezaji wa MTAKUWWA katika maeneo yao. Mafunzo hayo ni miongoni mwa utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali wa mwaka 2026/27 unaoelekeza Maafisa Masuhuli kutenga fedha za utekelezaji wa MTAKUWWA.

Nitoe Rai wa Waheshimiwa Wabunge kufuatilia utekelezaji wa ajenda ya MTAKUWWA katika vikao rasmi ambavyo Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe wa kudumu ikiwemo vikao vya ushauri ngazi ya Mikoa na Wilaya ili kuhimiza utengaji wa Bajeti na kufuatilia utekelezaji wa MTAKUWWA katika Majimbo yao.

ENEO LA 9: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA.

204. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbili (2) zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Maelezo ya kina kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo: -

TAASISI YA USTAWI WA JAMII

205. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Ustawi wa Jamii ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Ustawi wa Jamii ya Taifa Na. 26 ya mwaka 1973, kwa lengo la kuandaa rasilimali watu wenye sifa stahiki kwa ajili ya kuimarisha muundo wa utoaji wa huduma za kijamii nchini. Taasisi imepitia maboresho na mabadiliko mengi ambapo kwa sasa Taasisi inatoa huduma mbalimbali za ustawi wa jamii zikiwemo: mafunzo ya kada ya ustawi wa jamii kuanzia ngazi ya cheti hadi uzamili; tafiti za kijamii; na kutoa utaalamu elekezi unaohusiana na masuala ya ustawi wa jamii. Taasisi hii ina kampasi mbili (2) ambapo kampasi kuu ipo eneo Kijitonyama, Jijini Dar es Salaam na Kampasi nyingine ipo eneo la Kisangara, Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii ina programu 20 za mafunzo, ambapo katika mwaka wa masomo 2025/26, hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 imesajili jumla wanafunzi 5,868 (Wanaume 2,045 na Wanawake 3,823) ikilinganishwa na wanafunzi 5,400 (Wanaume 1,871 na Wanawake 3,529) walisajiliwa katika mwaka wa masomo 2024/2025. Wanafunzi wapya waliodahiliwa kati ya hao ni 3,000 (Wanaume 1,028 na Wanawake 1,972). Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na wanafunzi 2,731 (Wanaume 1,022 na Wanawake 1,709) waliodahiliwa mwaka wa masomo 2024/25.

207. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imefanikiwa kuhuisha mitaala ya kozi ya Ustawi wa Jamii kwa Ngazi ya Cheti na Diploma (NTA 4, 5 na 6). Mitaala hiyo tayari imethibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) na imeanza kutumika Novemba, 2025 ambapo inatarajiwa kufikia ukomo wa matumizi ifikapo Desemba, 2030.

208. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 jumla ya wanafunzi 3,121 (Wanaume 1,108 na Wanawake 2,013) wamehitimu masomo yao ikilinganishwa na wanafunzi 3,112 (Wanaume 1,028 na Wanawake 2,084) waliohitimu katika mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 0.3.

209. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ina Kituo kinachotoa Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia. Katika kipindi husika jumla ya wananchi 403 (Wanaume 190, Wanawake 213) ambapo kati ya hao wananchi 356 (Wanaume 169, Wanawake 187) na watumishi 47 (Wanaume 31 na Wanawake 16) wa Taasisi mbalimbali za Serikali walipata elimu, ushauri na msaada wa kisaikolojia.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi inaratibu programu ya uanagenzi yenye lengo la kuwasaidia wahitimu kupata ujuzi wa vitendo na uzoefu unaohitajika katika fani walizohitimu. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya wahitimu 21 walishiriki programu hiyo kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo Manispaa ya Tabora, Halmashauri ya Jiji la Ilala, Kituo cha Utetezi wa Haki za Binadamu pamoja na Shirika la *Plan International*. Aidha, hadi

kufikia Aprili, 2026, jumla ya wanafunzi 35 walipata ajira kupitia fursa inayotolewa na Programu hiyo.

TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU

211. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ilianzishwa mwaka 1963 kama Kituo cha kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mabwana na mabibi maendeleo waliokuwa na jukumu la kuhamasisha maendeleo ngazi ya jamii. Taasisi hii imepitia maboresho na mabadiliko mengi ambapo kwa sasa inajishughulisha na masuala mengi ya kijamii ikiwemo utoaji wa mafunzo ya kada ya Maendeleo ya Jamii kuanzia ngazi ya Cheti hadi Uzamili; kufanya utafiti mbalimbali wa masuala ya kijamii; na kutoa ushauri elekezi.

212. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ina programu 50 za mafunzo, ambapo hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya wanafunzi 3,648 (Wanaume 1,469 na Wanawake 2,179) walidahiliwa. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 12 ikilinganishwa na udahili wa mwaka wa masomo 2024/25, ambapo wanafunzi 3,219 (wanaume 1,286 wanawake1,933) walidahiliwa.

213. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26 Taasisi ilifanya mahafali ya
15 ambapo jumla ya wanafunzi 1,813 (Wanaume 758 na Wanawake 1,055) walihitimu. Idadi hii ya wahitimu imeongezeka kwa asilimia 9.8 ikilinganishwa na wahitimu wa mwaka 2024/25, ambapo wanafunzi 1,672 (Wanaume 554 na Wanawake 1,118) walihitimu.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Kituo cha Huduma Tandaa na Ubunifu wa Kidigitali (Jamii Outreach Digital Innovation Center – JODIC), Taasisi imetekeleza dhana tatu (3) ambazo ni Uanagenzi, Ushirikishwaji Jamii na Ubunifu. Jumla ya wanafunzi 2,445 walipata mafunzo na kuunganishwa na mashirika kwa ajili ya kuongeza ujuzi kulingana na taaluma zao ili iwasaidie kujiajiri, kuajiriwa na kuajiri wengine.

215. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu dhana ya ushirikishwaji jamii, wanafunzi wa Taasisi hushiriki na jamii inayowazunguka katika

kubaini changamoto zinazoikabili na kuzitafutia utatuzi ambapo katika kipindi hiki elimu ya upimaji wa VVU/UKIMWI ilitolewa kwa watu 420 katika kijiji cha Patandi ambapo watu 66 walipima kwa hiari.

216. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kuhusu dhana ya ubunifu, wanafunzi watatu (3) waliwezeshwa kushiriki mashindano ya *Afrinnovate Youth Challenge Competition* yaliyoandaliwa na Taasisi ya *E3 Empowered Africa* yaliyoshirikisha vyuo vikuu na vyuo vya kati kumi kutoka Tanzania. Mashindano hayo yalilenga kuibua bunifu zinazosaidia wanafunzi kuweza kujiajiri, kuajiriwa na kuajiri wengine ambapo bunifu zao zilihusisha teknolojia ya kubangua karanga. Wanafunzi wa Taasisi waliibuka washindi wa kwanza na kupata zawadi ya Dola za Kimarekani 3,500. Aidha, wanafunzi hao walishinda pia mashindano ya *Afrinnovate Youth Challenge Competition* ya Afrika na kuwa washindi wa kwanza barani Afrika na kuzawadiwa Dola za Kimarekani 5,000.

217. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Kituo cha Kitaifa cha utafiti na uhifadhi wa machapisho ya wanawake (National Women's Research and Documentation Center - NWRDC) imefanyika midahalo 10 kuhusu fursa za ubunifu na ujasiriamali katika Taasisi nane (8) za elimu ambapo jumla ya wanafunzi 969 (Wanaume 487 na Wanawake 482) walifikiwa na hivyo kuongeza uelewa, kujiamini na kutambua fursa zinazowazunguka ili kukabiliana na changamoto zilizopo.

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kilifanya tafiti mbili (2) zinazohusu ukatili wa kijinsia na kimewezesha utoaji wa msaada wa kisheria kwa wanawake 15 katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, ambapo wanawake wenye kipato kidogo na wasiokuwa na fursa ya kuwalipa mawakili walipewa ushauri wa kisheria na taratibu za kufuata ili kupata haki zao. Vilevile, mafunzo ya uongozi yametolewa kwa wanafunzi wa kike 40 katika vyuo vikuu na vyuo vya kati sita (6), ambapo mafunzo hayo yamesaidia wanafunzi kuongeza uelewa wa misingi ya uongozi bora, kujiamini, ubunifu na kuwaandaa kuwa viongozi wa baadae wenye weledi na kujituma.

ENEO LA 10: UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

219. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo nane (8) ikijumuisha miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Taasisi, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vituo vya Ustawi wa Jamii; na miradi ya kutoa huduma katika jamii.

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama, ambapo mradi huo umefikia asilimia 85 ya utekelezaji. Mradi huu unakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi 626,405,367.66, ambapo hadi sasa shilingi 366,119,211.65 zimeshatumika. Hatua hii inaendelea kuimarisha ubora wa miundombinu na mazingira ya kitaaluma ndani ya Taasisi.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya utendaji kwa watumishi, Wizara inaendelea na ujenzi wa jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru lenye Ofisi 44 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 94 na kumbi tano (5) zenye uwezo wa kuhudumia watu 545. Jengo hilo litagharimu shilingi bilioni 5.7, ambapo katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imepokea shilingi bilioni 1.2, na kufanya jumla ya shilingi bilioni 3.9 zimetolewa katika mradi husika na kufanya utekelezaji wa mradi huo kufikia asilimia 71.

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na ujenzi wa hosteli ya Wasichana ya ghorofa mbili (2) yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 600 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole, ambapo hadi kukamilika Mradi huu utagharimu kiasi cha shilingi Bilioni 5.1. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2025/26 Mradi huu umepokea shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa awamu ya tatu (3) na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa tangu mradi huo kuanza Mwezi Aprili, 2022 kuwa ni shilingi bilioni 2.6. Aidha, utekelezaji wa mradi huo umefika asilimia 65 ya ujenzi.

223. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza mradi wa Ujenzi wa Hosteli Katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli

unaokadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 4.7 hadi kukamilika ikijumuisha na gharama za ununuzi wa samani. Hosteli hiyo ya wasichana ya ghorofa tatu (3) itakuwa na uwezo wa kuhudumia jumla ya wanafunzi 576. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2025/26 kiasi cha shilingi milioni 600 kimepokelewa na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa katika mradi huo kuwa ni shilingi Bilioni 2.1 ambapo utekelezaji wa mradi huo umefika asilimia 67 ya ujenzi.

224. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Upangaji wa Rasilimali za Kutekeleza Afua za Kijinsia (Resource Planning for Gender Project). Mradi huu unalenga kutekeleza shughuli za kutokomeza ukatili wa kijinsia pamoja na kuwezesha uratibu wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II 2024/25 – 2028/29).

225. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi mwaka 2025/26, mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 1.15 ikijumuisha fedha za ndani shilingi milioni 705.4 na fedha za nje shilingi milioni
449.3. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imepokea kiasi cha shilingi milioni 119.6 ambapo fedha hizo zimetumika kuratibu Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto.

226. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Uhai na Maendeleo ya Mtoto (Child Survival and Development) ambapo Wizara imepokea fedha za nje kiasi cha **shilingi milioni 294.4** katika kuimarisha afua za kutoa elimu ya malezi chanya kwa watoto katika ngazi zote nchini. Aidha, Wizara imeratibu na kufanya Mkutano wa wadau wanaotekeleza afua za Vijana Balehe Nchini; kugharamia maandalizi ya mkutano wa Tano wa Nchi wanachama kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Afrika na Haki na Ustawi wa Mtoto; utekelezaji wa afua za Ulinzi na usalama wa mtoto Mtandaoni; kugharamia afua za MMMAM; na kuzuia aina zote za ukatili dhidi ya watoto ikiwemo ukeketaji na ukatili mitandaoni.

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI inatekeleza Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Advancing Gender Equality in Tanzania) unaojulikana kwa jina la "PAMOJA Project". Mradi huo unatakelezwa Tanzania Bara na

Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano (5) na utagharimu Dola za Marekani milioni 100 kutoka Benki ya Dunia. Kati ya fedha hizo, Wizara imetengewa Dola za Marekani 38,000,000, OWM - TAMISEMI imetengewa Dola za Marekani 49,000,000 na Zanzibar imetengewa Dola za Marekani 13,000,000. Hata hivyo, Mradi huu ukitekelezwa ipasavyo, Serikali itapata ruzuku ya Dola za Marekani milioni nne.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wanawake waishio vijijini; kujenga vituo vya kulelea watoto wadogo mchana 200 (184 Tanzania Bara na 16 Zanzibar); kuwajengea wanaume uwezo na kuwa vinara wa kutokomeza ukatili wa kijinsia; ujenzi wa nyumba salama 10; na ujenzi na ukarabati wa Ofisi 40 za Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii.

229. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, mradi umetengewa Shilingi 6,576,717,000 ambapo hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya shilingi 5,836,716,758.67 zimetolewa. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya utambuzi wa maeneo ya ujenzi wa vituo vya kulelea Watoto wadogo mchana, nyumba salama na vikundi vitakavyonufaika na mikopo; kufanya utafiti wa msingi (baseline survey) ili kupata taarifa za awali kabla ya kuanza kutekeleza mradi; ununuzi wa magari sita (6); na kuandaa mifumo ya kuimarisha upatikanaji wa masoko kwa wajasiriamali na mifumo ya kidijitali ya kukusanya takwimu za mradi.

230. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii (Support to Social Welfare Services) ambapo katika kipindi cha mwaka 2025/26, kiasi cha **shilingi bilioni 3** kilitengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu ya vituo vya ustawi wa jamii. Hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara, imepokea fedha kiasi cha **shilingi milioni 568.3** (Fedha za ndani shilingi milioni 500 na fedha za nje shilingi milioni 68.3) zilizotumika kuendeleza ujenzi wa Mahabusu ya Watoto Jijini Mwanza awamu ya pili; ukarabati wa miundombinu ya Mahabusu za Watoto Upanga, Mbeya, Mtwara na Kilimanjaro; ukarabati wa majengo na miundombinu ya umeme na mifumo ya vyoo katika

makazi ya Wazee na Wasiojiweza Bukumbi, Nyabange, Misufini, Kiilima, Magugu na Ipuli; na kufanya tathmini ya mifumo ya takwimu ya *Most Vulnerable Children Management Information Sytem (MVC – MIS)* na *Disctrict Case Management Information Sytem* (DCMIS).

VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2026/27

Mwelekeo wa Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii katika Mwaka 2026/2027

231. ***Mheshimiwa Spika,*** mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/27 umeandaliwa kwa kuzingatia misingi ifuatayo: -

i) DIRA 2050 inayosisitiza kuhusu Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii;

ii) Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 inayoelekeza kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii;

iii) Mpango wa Taifa wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV), katika ya nguzo ya pili inayosisitiza kujenga uwezo wa watu na Maendeleo ya Kijamii;

iv) Mpango Mkakati wa Wizara na Mipango Mkakati ya Taasisi za Wizara kwa kipindi cha 2026/2027 – 2030/2031; na

v) Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27 pamoja na Sera, Sheria, Programu nyingine zinazotelezwa na Wizara.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itajikita katika maeneo machache yenye matokeo chanya kwa Taifa, uwezo wa kuleta mageuzi na mchango mkubwa katika kujenga Tanzania yenye jamii imara, jumuishi na yenye maendeleo endelevu. Hivyo, Wizara itatekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele saba (7) ambavyo ni:-

i) **Kujenga mtaji watu wa Taifa na kizazi cha Tanzania ya 2050**, kinachozingatia maadili, uzalendo, haki, usawa, ustawi na maendeleo jumuishi;

ii) **Kuimarisha huduma za ustawi, malezi na makuzi ya watoto, ulinzi wa kijamii na uthabiti wa Taifa** ili kuendeleza Taifa lenye mshikamano, ustahimilivu na utu wa kibinadamu kwa kuzingatia kuwa watu ndiyo mtaji mkuu wa Maendeleo ya Taifa;

iii) **Kuimarisha mifumo ya uwezeshaji wa wanawake, usawa wa kijinsia na kutokomeza ukatili wa kijinsia** ili kuhakikisha kuwa mwanamke anashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo;

iv) **Kufanya mageuzi ya uchumi wa makundi maalum na sekta isiyo rasmi kutoka uchumi wa kujikimu, kwenda uchumi rasmi wa kibiashara wenye tija, ushindani na wenye mchango katika pato la Taifa** kwa kuwa makundi hayo ni muhimu katika kujenga uchumi jumuishi;

v) **Kuimarisha matumizi ya kidijitali na takwimu katika huduma za kijamii ikihusisha uchambuzi wa takwimu** ili kurahisisha utendaji na kufanya maamuzi yenye ushahidi wa kitakwimu;

vi) **kujenga jamii ya Kitanzania yenye amani, uwajibikaji na mshikamano** ili kuimarisha ushiriki wa wananchi katika maendeleo; na

vii) **Kuimarisha ushirikiano wa Kitaifa wa kimkakati kati ya Serikali, Asasi za Kiraia, Sekta binafsi, Taasisi za dini na wadau wa maendeleo** kwa kuwa maendeleo ya Taifa yanahitaji juhudi za pamoja.

233. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia vipaumbele hivyo, Serikali inalenga kujenga jamii imara na salama; wanawake wenye nguvu kiuchumi; watoto waliolelewa vyema; uchumi jumuishi na endelevu; jamii yenye maadili, mshikamano na amani ya kudumu;

na Taifa lenye maendeleo yanayoongozwa na maarifa, teknolojia na ubunifu katika kufikia malengo ya DIRA 2050.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inapendekeza bajeti inayoweka vipaumbele katika ustawi na maendeleo ya jamii ikiwemo kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; huduma za watoto na wazee; ulinzi wa wanawake na wanaume; na makundi mengine maalumu kwa kuwa hizi si huduma za pembeni, bali ni **mfumo wa kulinda amani, usalama na uthabiti wa Taifa**. Hivyo, mafanikio ya bajeti hii hayatapimwa kwa kiasi cha fedha kilichotumika, bali kwa kiwango cha matokeo yaliyopatikana kwa familia, jamii/wananchi, Serikali na Taifa kwa ujumla.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii haulengi tu kutekeleza shughuli za Serikali, bali umeandaliwa mahsusi ili kuleta matokeo ya kimkakati yanayopimika yenye tija na mchango wa moja kwa moja wa kila mdau katika utekelezaji wa DIRA 2050. Lengo ni kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utoaji huduma, kupunguza umaskini uliokithiri, kulinda makundi yaliyo hatarini, kujenga jamii salama, kuimarisha mshikamano wa Kitaifa na kujenga Taifa jumuishi.

236. ***Mheshimiwa Spika***, leo nasimama mbele ya Bunge hili Tukufu kuzungumzia jambo moja kubwa sana ambalo linaamua mustakabali wa Taifa letu kuliko hata jambo jingine lolote. Na jambo lenyewe ni ***Malezi, Maadili, Makuzi na Ustawi wa Watoto wa Tanzania kwa Mwelekeo wa DIRA 2050.***

237. ***Mheshimiwa Spika,*** Tunaweza kujenga reli za kisasa, Tunaweza kujenga bandari kubwa, Tunaweza kujenga viwanja vya ndege, miji ya kisasa na uchumi mkubwa. Lakini tukishindwa kujenga mtoto wa Kitanzania mwenye maadili, nidhamu, uzalendo, utu na uwezo wa kuhimili ushindani wa dunia ya mwaka 2050 tutakuwa tumeshindwa kujenga Taifa imara.

238. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sababu ukweli ni huu Taifa lolote hujengwa kwanza kwenye malezi kabla halijajengwa kwenye uchumi. Naomba Bunge hili Tukufu litambue kuwa mtoto wa leo ndiye Mtendaji wa Serikali wa kesho; Daktari wa kesho; Mwalimu

wa kesho; Jaji wa kesho; Askari wa kesho; Mwekezaji wa Kesho na kiongozi wa Taifa wa kesho. Kwa hiyo tukiharibu malezi ya mtoto leo, tutakuwa tumeharibu Tanzania ya mwaka 2050.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** leo Taifa letu linaanza kuona dalili ambazo hatupaswi kuzipuuza. Tunaona Kuporomoka kwa maadili katika jamii; Kuongezeka kwa ukatili dhidi ya watoto; Watoto kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya; Kuongezeka kwa mimba za utotoni; Athari kubwa za matumizi holela ya mitandao ya kijamii; Watoto kukosa malezi ya karibu; Kuongezeka kwa migogoro ya kifamilia; na kupungua kwa uwajibikaji wa pamoja katika malezi ya mtoto.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** jambo la kutisha zaidi siyo tu changamoto hizi kuwepo; jambo la kutisha zaidi ni pale jamii inaanza kuziona changamoto hizi kama ni mambo ya kawaida. Hapo ndipo Taifa huanza kupoteza mwelekeo wake wa maadili.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwelekeo wa DIRA 2050, Tanzania haiwezi kuwa Taifa lenye ushindani wa kimataifa kama Familia zitakuwa dhaifu; Malezi yatakuwa dhaifu; Watoto hawatakuwa salama na maadili yataendelea kuporomoka. DIRA 2050 inahitaji Taifa lenye watu wenye uwezo mkubwa wa kufikiri; Wenye nidhamu ya kazi; Wenye uzalendo; Wenye maadili; Wenye afya ya akili na wenye uwezo wa kuishi katika ushindani wa dunia ya kisasa. Na msingi wa yote hayo unaanzia kwenye malezi ya mtoto.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** ni lazima sasa kama Taifa tufanye mabadiliko makubwa ya kimkakati katika eneo la malezi na ustawi wa watoto. Naomba nitoe maeneo sita (6) muhimu ambayo Taifa linapaswa kuyaangalia kwa uzito mkubwa:

243. ***Mheshimiwa Spika,*** moja, **Kurejesha Nguvu ya Familia**. Familia ndiyo taasisi ya kwanza ya Taifa. Mtoto wa Kitanzania hapaswi kulelewa na simu wala kulelewa na TikTok. Hapaswi kulelewa na mitandao ya kijamii bali Mtoto wa anahitaji Mzazi; Malezi; Muda; Maadili na uwepo wa familia. Ni lazima turejeshe mfumo wa wazazi kushiriki kikamilifu katika maisha ya watoto wao. Leo tuna

Taifa ambalo linaanza kuwa na watoto wengi wenye mahitaji ya kiakili, kihisia na kimaadili kwa sababu ya kukosa malezi ya karibu.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** mbili, **Kujenga Mfumo wa Taifa wa Maadili**. Tukijenga uchumi bila maadili tutakuwa tumejenga hatari kubwa kwa Taifa. Tunapaswa kuwa na *National Moral Regeneration Programme;* Mfumo wa Taifa wa Malezi; Kampeni ya Taifa ya Maadili na elimu ya maadili kuanzia ngazi za awali kabisa. Tunataka Watoto Wanaoheshimu Taifa lao; Wanaopenda kazi; Wenye utu; Wenye heshima na wanaolinda utamaduni wa Kitanzania.

245. ***Mheshimiwa Spika,*** tatu, **Kuimarisha Ulinzi wa Mtoto**. Mtoto anatakiwa kuwa salama Nyumbani; Shuleni; Kwenye mitandao; na katika jamii. Ni lazima tuimarishe madawati ya watoto; Mifumo ya kuripoti ukatili; Huduma za ushauri nasaha; Ulinzi wa mtoto mtandaoni na mifumo ya ufuatiliaji wa watoto waliyo kwenye mazingira hatarishi. Mtoto wa Tanzania hapaswi kuishi kwa hofu ndani ya Taifa lake mwenyewe.

246. ***Mheshimiwa Spika,*** nne, **Kuwekeza Kwenye Makuzi ya Awali ya Mtoto**. Tafiti zinasema ubongo wa mtoto unajengwa kwa asilimia 90 katika umri wa miaka 0 - 8. Tukiharibu hatua hiyo Taifa hupoteza ubunifu; Taifa hupoteza akili; Taifa hupoteza nguvu kazi; na Taifa hupoteza ushindani wa baadaye. Ni lazima tuwekeze zaidi katika Lishe ya mtoto; Afya ya mtoto; Elimu ya awali na mazingira bora ya ukuaji wa mtoto.

247. ***Mheshimiwa Spika,*** tano, **Kulinda Afya ya Akili ya Watoto**. Dunia ya sasa imeleta changamoto mpya kwa watoto wetu. Watoto wengi wana msongo wa mawazo; Wanaishi kwenye upweke; Wanapitia ukatili wa kimtandao; na wengine wanakosa hata mtu wa kuwasikiliza. Tunapaswa kuanzisha mifumo imara ya mental wellness kwa watoto wetu.

248. ***Mheshimiwa Spika,*** sita, **Kujenga Jamii Inayowajibika kwa Mtoto.** Malezi ya mtoto siyo jukumu la mzazi pekee. Ni jukumu la Serikali; Jamii; Viongozi wa dini; Walimu; Vyombo vya habari; na

Taifa lote kwa ujumla. Tunapaswa kurejesha falsafa ya "Mtoto wa mmoja ni mtoto wa jamii."

249. ***Mheshimiwa Spika,*** Tukitaka kuondoa kero zilizopo leo kama vile Ukatili; Dawa za kulevya; Watoto wa mitaani; Mmomonyoko wa maadili; Uhalifu wa vijana; na changamoto za kijamii ni lazima tuanze na malezi. Kwa sababu matatizo mengi tunayoyaona leo yanaanzia kwenye kuporomoka kwa mfumo wa malezi.

250. ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba niseme jambo moja kubwa mbele ya Bunge hili Tukufu "**Taifa lisipoamua kuwekeza kwa nguvu katika watoto wake leo, kesho litaingia gharama kubwa sana kurekebisha jamii**".
Tutatumia fedha nyingi Magerezani; katika vita dhidi ya dawa za kulevya; katika mapambano dhidi ya uhalifu; katika migogoro ya kijamii; na katika kurekebisha kizazi ambacho kingeweza kujengwa mapema. Ndiyo maana wahenga walisema "**Samaki mkunje angali mbichi**"

251. ***Mheshimiwa Spika,*** DIRA 2050 siyo tu kuhusu uchumi mkubwa. DIRA 2050 ni kuhusu kujenga Taifa lenye utu. Taifa lenye maadili; Taifa lenye watoto wenye ndoto; na Taifa lenye kizazi kinachojiamini. Na Taifa lenye watu wanaolitanguliza Taifa lao mbele ya maslahi binafsi. Naomba Bunge lako Tukufu, pamoja na Taifa letu, na kila mzazi wa Kitanzania tukubaliane jambo moja "**Hakuna uwekezaji mkubwa kwa Taifa kuliko uwekezaji kwa mtoto**." Na tukubaliane pia kuwa "**Malezi bora ya mtoto wa leo ndiyo usalama, maadili, amani, uchumi na mustakabali wa Tanzania ya mwaka 2050**."

252. ***Mheshimiwa Spika,*** kuna haja ya kukuza ujuzi wa wataalamu wa Ustawi na Maendeleo ya Jamii, hivyo, Wizara itajielekeza katika kuboresha dhana ya uanagenzi, ushirikishaji jamii na ubunifu kwa kutumia teknolojia rahisi ili kuleta ufumbuzi wa changamoto zilizopo kwenye jamii. Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya Taasisi, vyuo na vituo vya kibunifu ili kuwavutia vijana wengi kujiunga na masomo na kuongeza ushindani wa vyuo hivyo Kimataifa.

253. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuleta mageuzi yatakayochochea ukuaji wa uchumi jumuishi katika sekta isiyo rasmi, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta pamoja na wadau kufanya utambuzi, usajili na urasimishaji wa wafanyabiashara ndogondogo kijiditali. Lengo la hatua hii ni kupata takwimu sahihi za wafanyabiashara hao kupitia kanzidata iliyohuishwa na kuwaunganisha na fursa za kiuchumi.

254. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo. Aidha, Wizara itahamasisha uanzishwaji na uimarishwaji wa vikundi vya fedha ikiwemo SACCOS na VICOBA kwa lengo la kujenga utamaduni wa kuweka akiba na uwekezaji. Vilevile, Wizara itajielekeza katika kuwajengea uwezo wafanyabiashara ndogondogo kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali, elimu ya fedha, usimamizi wa biashara kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia za kidijitali.

255. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara itahuisha na kuboresha Ajenda ya Taifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe, sambamba na mwelekeo wa DIRA 2050 inayolenga kukuza ujuzi, ubunifu na matumizi ya teknolojia, hususan kwa vijana.

256. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ongezeko la ukatili unaofanyika kupitia mitandao, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na wadau itaanzisha utaratibu maalum utakaowezesha kuchuja maudhui yasiyofaa kwa watoto. Sambamba na hilo, elimu kuhusu matumizi salama ya mitandao na uzuiaji wa ukatili itaendelea kutolewa kwa watoto, wazazi na walimu kupitia majukwaa mbalimbali, yakiwemo vyombo vya habari na taasisi za dini. Vilevile, mkakati wa usalama wa mtoto mtandaoni unaandaliwa ili kutoa mwongozo wa utekelezaji wa hatua hizi za kipaumbele, kwa lengo la kuhakikisha mazingira salama kwa watoto katika ulimwengu wa kidijitali na katika jamii kwa ujumla.

257. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma katika vituo vya Ustawi wa Jamii kwa makundi

mbalimbali yenye uhitaji maalum wakiwemo wazee, watoto walio katika mazingira hatarishi, wananchi wasiojiweza, familia zenye migogoro, manusura wa ukatili wa kijinsia na watoto, pamoja na wananchi wenye changamoto za afya ya akili na kisaikolojia. Huduma hizi zinalenga kuimarisha ustawi wa jamii, mshikamano wa kijamii na kuwawezesha wananchi kurejea katika maisha ya kawaida ili kushiriki shughuli za maendeleo.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la uwezeshaji wa wanawake kiuchumi halina maana kumkandamiza mwanaume bali ni kumtoa mwanamke kutoka nafasi ya mnufaika wa maendeleo, na kumpeleka kwenye nafasi ya mshiriki mkuu katika uzalishaji, uwekezaji, ubunifu, na uchumi wa Taifa. Katika kufanikisha hilo Wizara itajielekeza katika kuimarisha upatikanaji wa mikopo na teknolojia rahisi kwa wanawake ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa bidhaa na huduma kupitia shughuli zao za ujasiriamali, sambamba na kuhamasisha matumizi ya biashara mtandao (e-commerce); na kujenga uwezo wa makundi maalum (wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu) kunufaika na fursa za uwezeshaji kiuchumi.

259. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na maamuzi, Wizara itaanzisha na kuendeleza programu atamizi za kuibua na kuendeleza viongozi wanawake na wasichana wanaochipukia ikiwa ni jitihada za kufikia malengo ya DIRA 2050 inayobainisha Tanzania kuwa kinara wa usawa wa kijinsia barani Afrika na miongoni mwa nchi kumi duniani katika kupunguza pengo la kijinsia kwa asilimia 85.

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Washirika wa Maendeleo itaendelea kujenga uelewa wa ujumuishaji wa masuala ya kijinsia katika mchakato wa uandaaji wa mipango na bajeti za Wizara, Taasisi za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za mitaa (Gender Responsive Budgeting) kuhakikisha rasilimali za Taifa zinawanufaisha wanawake na wanaume kwa usawa.

261. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuweka mkazo katika kulinda haki na ustawi wa wajane kupitia Mwongozo wa Uratibu

wa Huduma kwa Wajane (2025). Serikali itaimarisha mifumo ya uratibu wa huduma, ulinzi wa mirathi, pamoja na upatikanaji wa haki za msingi kwa kundi hili. Aidha, hatua mbalimbali zitachukuliwa kuhakikisha wajane wanapata huduma stahiki za kisheria, kijamii na kiuchumi, ili kuwawezesha kurejea katika maisha yenye tija na heshima.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaweka mkazo katika kuanzisha na kuimarisha vikundi vya wanaume vinavyolenga mabadiliko ya mitazamo na mila zinazokwamisha usawa wa kijinsia, kuendesha kampeni za Kitaifa za uhamasishaji zinazowalenga wanaume na wavulana kuhusu wajibu wao katika kulinda haki za wanawake na kuzuia ukatili wa kijinsia, pamoja na kuwashirikisha kikamilifu katika programu za kiuchumi na kijamii ili kujenga mshikamano wa pamoja katika maendeleo.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi zinalenga kubadilisha dhana ya usawa wa kijinsia kutoka kuwa ajenda ya wanawake pekee na kuwa ajenda ya wote, ambapo wanaume wanakuwa washirika wa mabadiliko (change agent), hivyo kupunguza mitazamo hasi, kuimarisha ushirikiano ili kuwa na msingi imara wa jamii yenye usawa, amani na maendeleo endelevu.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** DIRA 2050 imeweka msisitizo mkubwa katika ushiriki thabiti wa wadau mbalimbali, zikiwemo Asasi za Kiraia na wananchi kwa ujumla, ambapo ushirikiano wa kimkakati baina ya wadau utaimarisha uratibu na kuhakikisha malengo ya kitaifa yanatimizwa kwa ufanisi. Aidha, DIRA 2050 imebainisha kuwa Asasi za Kiraia zina mchango muhimu katika kukuza demokrasia, kulinda haki za binadamu na kuchangia jitihada za kuboresha huduma za jamii.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia ubia na mahusiano kati ya Serikali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kama ilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 - 2026/27). Hatua hiyo inakwenda sambamba na mwelekeo wa DIRA 2050 inayohimiza upatikanaji wa rasilimali

katika kutoa huduma jumuishi zikiwemo: hifadhi ya jamii, upatikanaji sawia wa maji safi, nishati na usafi wa mazingira, kuongezeka kwa ajira na kupunguza pengo la kijinsia, ambapo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni wadau muhimu na washirika katika kuchagiza utekelezaji wa afua hizo.

Kazi Zitakazotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027

266. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza vipaumbele, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (**Fungu 53**) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na:-

i) Kuboresha ustawi wa watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;

ii) Kutekeleza afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto;

iii) Kufanya maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS) na Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Wafanyabishara Ndogondogo (Wafanyabiashara Ndogondogo Management System - WBN – MIS);

iv) Kuendelea kuratibu utoaji wa mikopo kwa Wafanyabishara Ndogondogo, wanawake na makundi mengine nchini;

v) Kuandaa Kitabu cha Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2025;

vi) Kufanya tathmini na mapitio ya Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001) na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008) na kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996);

vii) Kuanzisha mfuko wa pamoja wa ruzuku kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs Basket Fund);

viii) Kujenga Nyumba Salama 10 na vituo 184 vya kijamii vya kulelea watoto wadogo wa mchana wenye umri chini ya miaka 5;

ix) Kuimarisha majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi;

x) Kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati vya wanawake kila Mkoa;

xi) Kuhamasisha uanzishaji wa madawati ya ulinzi na usalama wa watoto katika shule za msingi na sekondari;

xii) Kuendeleza uanzishwaji wa madawati ya kuzuia ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi za Elimu ya juu na Kati; na Maeneo ya umma;

xiii) Kutoa elimu kuhusu wajibu wa msingi wa wazazi na walezi katika malezi chanya ya watoto;

xiv) Kuhamasisha matumizi salama ya mtandao kwa watoto kadi maalum za simu kwa watoto (Child SIM Card) zitakazosaidia kuchuja na kudhibiti maudhui yasiyofaa;

xv) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii;

xvi) Kufanya Mapitio ya Mpango wa Kitaifa wa Uhamasishaji na Usimamizi wa Maendeleo Ngazi ya Msingi (*Bottom Up*);

xvii) Kuunganisha vyuo vinne (4) vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Jamii Ufundi kwenda Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru;

xviii) Kutoa huduma za msingi (chakula, mavazi, malazi na Matibabu) kwenye vituo 23 vya ustawi wa Jamii (Makazi ya Wazee 13, Mahabusu za watoto 7, Shule ya Maadilisho 1 na Makao ya Watoto 2);

xix) Kujenga Mfumo Jumuishi wa kidijitali wa Taarifa za Huduma za Ustawi wa Jamii (Comprehensive Social Welfare Information System); na Mfumo Jumuishi wa kidijitali wa Taarifa za Huduma za Maendeleo ya Jamii (Comprehensive Community Development Information System);

xx) Kuendelea na kampeni ya kuhamasisha ujenzi wa makazi bora ya gharama nafuu;

xxi) Kujenga makazi ya wazee ya kikanda katika Kanda ya Ziwa na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini;

xxii) Kuwajengea uwezo na kuwapatia vitendea kazi Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya msingi; na

xxiii) Kuhamasisha matumizi ya biashara mtandao kwa wanawake wajasiriamali ili kuongeza upatikanaji wa masoko.

267. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti hii ni mwelekeo wa kuwa na jamii imara, yenye kuthaminiana na inayojali utu kwa ustawi wa Taifa. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii unatarajiwa kuleta matokeo yafuatayo:

i) Kuongezeka kwa idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi;

ii) Kuongezeka kwa madawati na majukwaa ya kushughulikia matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto;

iii) Kuongezeka kwa idadi ya wanaume wanaoshiriki katika afua za kuzuia na kukabiliana na vitendo vya ukatili;

iv) Kuongezeka kwa fursa ya upatikanaji wa mikopo, mitaji na huduma za kifedha kupitia taasisi za fedha nchini;

v) Kuongezeka kwa idadi ya wanufaika wa mikopo yenye masharti nafuu kutoka Taasisi za fedha;

vi) Kuimarika kwa huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto, wazee na familia zenye dhiki;

vii) Kuongezeka kwa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa;

viii) Kuongezeka kwa idadi ya miradi inayotekelezwa kwa nguvu za wananchi;

ix) Uwepo wa Mifumo ya kidijitali ya kutoa huduma za Maendeleo na Ustawi wa jamii;

x) Uwepo wa Sera, mipango, sheria, miongozo iliyofanyiwa maboresho;

xi) Uwepo wa miundombinu iliyoboreshwa katika Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii;

xii) Kuongezeka kwa idadi ya vitendea kazi vya Maafisa Maendeleo ya jamii na Maafisa Ustawi wa jamii;

xiii) Ongezeko la vituo vya kijamii vya kulelea watoto wadogo mchana na uelewa wa umuhimu wa huduma jumuishi za malezi kwa watoto Wadogo; na

xiv) Kuongezeka kwa idadi ya wazazi na walezi waliopata elimu kuhusu malezi chanya ya watoto katika zama za sasa.

268. ***Mheshimiwa Spika,*** DIRA 2050 haitajengwa kwa saruji na majengo pekee, bali itajengwa kwa watu wenye uwezo, jamii zenye mshikamano, wanawake wenye nguvu, watoto wenye maadili, uzalendo na wananchi wanaoshiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. Na kwamba "Kupitia Wizara hii, Serikali inaendelea kujenga msingi wa Tanzania yenye ustawi, usalama wa kijamii, uchumi jumuishi na maendeleo endelevu kuelekea mwaka 2050."

SHUKRANI

269. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano

mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta binafsi zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Aidha, Ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi rafiki kwa ushirikiano wanaotupatia ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

270. ***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara ikiwa ni pamoja na: **Mashirika ya Kimataifa yakiwemo** UNICEF, UNFPA, UN-Women, WHO, UNDP, UNEP, IOM na UNESCO. Vilevile, ninashukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya (EU). Pia ninayashukuru **Mashirika ya Kimataifa** ambayo ni: - Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Enabel Foundation, Mfuko wa *Abbott Fund*, *Global Fund* na *Hilton Condrad Foundation*. Aidha, ninazishukuru **Taasisi za Kifedha** za hapa nchini zinazoshirikiana na Wizara ambazo ni pamoja na Benki ya CRDB, Benki ya NBC, Benki ya NMB, Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Benki ya Maendeleo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Benki ya Stanbic, Benki ya Azania, Benki ya Equity, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), *Akiba Commercial Bank* (ACB), Benki ya Biashara ya Dar es salaam (DCB) na Benki ya Mkombozi.

271. ***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** na **Mashirika ya Dini** kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na; *Hope Four Young Girls Tanzania*, *World Vision, PACT Tanzania, HelpAge Tanzania, Compassion International*, *Responsible Organization Tanzania*, *Children in Crossfire*, *Railway Children Tanzania*, ICS, *SOS Children's Village Tanzania*, BRAC Maendeleo Tanzania, *Plan International - Tanzania*, Kivulini, C-SEMA; *Amani Girls*, Girls Effect na TECDEN, EGPAF.

272. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe pia shukrani zangu kwa Taasisi za Umma na sekta binafsi ikiwemo, TPA, PPRA, TPDC, WCF, UTT, TISEZA, Mgodi wa Geita (GGM), PMM Group, Bakhresa Group of Company, Total Energies, Asas Group of Company na Oryx Gas.

273. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nitoe shukrani zangu kwa

Jumuiya za makundi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Wizara. Jumuiya hizo ni pamoja na: - Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania (CHAMWAPITA), Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT), Jukwaa la ULINGO, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) na Umoja wa Mama na Baba Lishe Tanzania (UMALITA).

274. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pongezi kwa mabinti zetu wa Timu ya mpira wa miguu ya wanawake chini ya miaka 20, (Tanzanite Queens), ambao wamefuzu na wataiwakilisha nchi katika mashindano ya kombe la Dunia yanayotarajia kufanyika kuanzia Septemba 5, 2026 nchini Poland. Tanzania ni moja kati ya nchi 4 za Afrika zitakazoshiriki mashindano hayo ya kuwania kombe la Dunia. ***Hakika Wanawake wameweza na hawajatuangusha***. Pia, navishukuru vikundi/kampeni za kijamii kama (Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), Lete Mabadiliko Chanya Ulipo (LeMaChu), Sauti ya Watoto Tanzania (SAWATA) pamoja na vyombo vyote vya habari.

275. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe shukrani zangu pia kwa viongozi na taasisi zetu za dini zikiwemo Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA).

276. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninaomba kuwashukuru Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO). Vilevile, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ninawashukuru sana Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala; Wakuu wa Wilaya; Wakurugenzi wa Halmashauri; na mitandao ya habari za kijamii ambao wamekuwa wakifuatilia na kutoa ushirikiano mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

277. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, hususan **Mume wangu mpendwa Wakili Msomi Methusela**

Gwajima na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, ninawashukuru **wananchi wote wa Tanzania** kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoisimamia wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu na pia kwa wao binafsi kuendelea kupambana kuhakikisha maendeleo na ustawi wa jamii kwa usawa wa jinsia huku wakitumia mawasiliano kupitia simu nilizozisema awali.

MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2026/27

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2026/27

278. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha **shilingi bilioni saba, milioni arobaini, mia moja ishirini na tisa elfu** (shilingi 7,040,129,000) kutoka katika vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivyo ni pamoja na: Ada za wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Mitaala, Ada za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na Ada za mwaka za vituo vya kulelea watoto.

MATUMIZI YA KAWAIDA

279. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2026/27, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **shilingi bilioni hamsini, mia moja thelathini na saba milioni, mia nane na moja elfu** (Shililngi 50,137,801,000) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni ishirini na tatu, milioni mia tatu kumi na tano, mia mbili na saba elfu** (shilingi 23,315,207,000) ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **shilingi bilioni ishirini na sita, milioni mia nane ishirini na mbili, mia tano tisini na nne elfu** (shilingi 26,822,594,000) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

MIRADI YA MAENDELEO

280. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi bilioni hamsini na saba, milioni mia nane themanini na sita, mia nne arobaini na mbili elfu** (shilingi

57,886,442,000) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni thelathini na sita, milioni mia tisa kumi na tano, mia nne na nne elfu** (Shilingi 36,915,404,000) ni Fedha za Ndani na **Shilingi bilioni ishirini, milioni mia tisa sabini na moja na thelathini na nane elfu** (shilingi 20,971,038,000) ni Fedha za Nje.

281. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** inaomba jumla ya **shilingi bilioni mia moja na nane, milioni ishirini na nne, mia mbili arobaini na tatu elfu** (shilingi 108,024,243,000) ili kutekeleza majukumu yake.

282. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum *www.jamii.go.tz*.

283. ***Mheshimiwa Spika,*** **Ninaomba Kutoa Hoja.**

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Hoja hiyo uliyotoa kwa umahiri mkubwa sana, na imeungwa mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea, ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mwenyekiti wa Kamati, karibu. *(Makofi)*

MHE. HAWA M. CHAKOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, ninapenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nitaomba taarifa yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurahisisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge inayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inahusu Msingi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa Wizara;

(iii) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(iv) Sehemu ya Nne inafafanua maoni na ushauri wa Kamati unaotolewa kwa Serikali; na

(v) Sehemu ya Tano inahitimisha taarifa ya uchambuzi na kuonesha msimamo wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum unawekwa na Masharti ya Kanuni za Bunge, Kifungu cha 6 (5)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka masharti yanayoitaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa. Taarifa ya Kamati inahusu Utekelezaji wa Wizara Fungu 53 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(b) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na

(c) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliiwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo inazitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 24 Machi, 2026, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Taarifa hiyo inajumuisha Mpango na Bajeti ya Wizara Fungu 53. Baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;

(b) Ukaguzi wa Miradi;

(c) Utekelezaji wa Vipaumbele;

(d) Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli; na

(e) Hali ya upatikanaji wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati. Katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 27 Mei, 2025 wakati wa uwasilishaji wa Hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo 11 kwa Fungu 53. Ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya maeneo ushauri wa Kamati umezingatiwa huku maeneo mengine utekelezaji wa ushauri wa Kamati haujafanyiwa kazi kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri uliozingatiwa ni wa kutoa fedha kwa ajili ya mikopo nafuu kwa wafanyabiashara

ndogondogo ambapo wafanyabiashara 6,306 wamenufaika na mikopo hiyo yenye thamani ya Shilingi bilioni 13,156,183,022. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya maoni na ushauri ambao utekelezaji wake hauridhishi nao ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuandaa mkakati maalumu unaotekelezeka wa kupima na kupata hati ya maeneo yote ya vyuo na vituo ambavyo havijapimwa;

(b) Kuendeleza maeneo makubwa yanayomilikiwa na Taasisi, Vyuo na vituo vilivyo chini ya Wizara kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi;

(c) Kuweka mikakati madhubuti ya ufuatiliaji na uhamasishaji wa mashirika yasiyo ya Kiserikali kulipa ada ili kuongeza mapato ya Serikali; na

(d) Kuandaa mkakati wa kutoa elimu juu ya faida za kujisajili na manufaa yatokanayo na usajili wa wafanyabiashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa ukomo wa bajeti na upatikanaji usioridhisha wa Fedha za Maendeleo ni moja ya sababu za Wizara kushindwa kutekeleza baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati kwa ufanisi. Hali hii inaweza kupunguza manufaa ya Wizara hii katika Taifa na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha. Kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa mitatu, nayo ni Arusha, Kilimanjaro, na Dar es Salaam. Katika mikoa hiyo, Kamati ilikagua miradi mitatu ambayo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha shilingi 26,941,456,000 kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kubainisha na kufafanua miradi hiyo pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 6330 ambao ni ujenzi wa Jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Mradi huu upo katika mwendelezo wa utekelezaji ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 ulipokea kiasi cha shilingi 600,000,000 ambapo mpaka Kamati inatembelea eneo la mradi, kiasi cha shilingi 1,200,000,000 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa tangu kuanza kwa mradi kuwa ni shilingi 3,900,000,000. Jengo hilo linaundwa kwa kumbi za mikutano na ofisi za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 6330. Mradi huu, utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa mihadhara katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama. Mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa *Force Account* wenye thamani ya shilingi 626,405,367.66 ambapo hadi Kamati inatembelea, ilikuwa imetumia kiasi cha shilingi 394,441,341.65 na mradi umefikia 82% na utakuwa na uwezo wa kubeba wanafunzi 400 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 6279 ambao ni ukarabati wa makazi ya wazee. Kamati ilitaka kujionea tija inayoweza kupatikana iwapo makazi ya wazee yataboreshwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali. Ili kufanikisha hilo, Kamati ilifanya ziara katika makazi ya wazee Njoro ambayo kwa kiasi kikubwa yamekarabatiwa na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hii, Kamati ilipata fursa ya kujionea kuwa ipo haja ya Serikali kuona namna ya kuongeza bajeti ili kuweka kwenye mpango makazi mengi zaidi tofauti na hali hivi sasa ambapo makazi machache huwekwa kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imebaini changamoto mbalimbali kwenye makazi haya zinazohitaji msukumo wa kibajeti. Mathalani, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 1,000,000,000 ambapo hadi Kamati ilipotembelea mradi, shilingi 568,000,000 zilikuwa zimepokelewa ikiwa ni robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatokanayo na ukaguzi wa miradi. Kamati ilipokea Taarifa za Utekelezaji wa Miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Lengo ilikuwa kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika. Tathmini ya Kamati imebainisha kuwa:-

(a) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati imezingatia thamani ya fedha *(value for money)* na hatua iliyofikiwa ina uwiano na muda wa utekelezaji wa miradi husika;

(b) Miradi iliyotembelewa na Kamati ingekuwa na tija kubwa zaidi na ufanisi kama fedha za maendeleo zingetolewa kwa wakati kama ilivyokusudiwa; na

(c) Sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa inatumia *Force Account* jambo linalopongezwa na Kamati na litakalochochea utekelezaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Fungu 53 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 9,040,129,000. Hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 2,991,829,587 sawa na 33.09% tu ya lengo la makusanyo ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti ambao ni 66.7%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, uwezekano wa Wizara kufikia lengo la ukusanyaji ni mdogo kwani katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo makusanyo ya Wizara yamekuwa chini ya 50% ya lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 53 kutoka Hazina kama ifuatavyo:-

(a) Upatikanaji wa jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Fungu 53 ni 67.8% ya bajeti ikiwa ndani ya utekelezaji wa kipindi kama hicho;

(b) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopatikana ni 66%;

(c) Fedha za Matumizi Mengineyo *(OC)* zimepokelewa kwa 67%;

(d) Fedha za mishahara zilizopokelewa ilikuwa 65% ikiwa na upungufu wa asilimia moja nukta saba ya fedha iliyotakiwa katika kipindi kama hiki;

(e) Fedha za kugharimia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa 70% ya bajeti; na

(f) Fedha za kugharimia miradi ya maendeleo ambazo fedha za ndani zilikuwa 87% na fedha za nje zilikuwa 48%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni wa kuridhisha na hivyo Kamati inaishauri Serikali kusimamia miradi kikamilifu ili ilete tija iliyokusudiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya mapato na matumizi, Kamati ilipokea ufafanuzi kuhusu lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ambapo Wizara Fungu 53 inakadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi 7,040,129,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makusanyo yamepungua kwa shilingi 2,000,000,000 sawa na 22.1% ikilinganishwa na makadirio ya makuasanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Pamoja na kupunguziwa maduhuli, Kamati ilipokea taarifa kuwa Wizara iliibua chanzo kipya cha mapato ambacho ni ulipaji wa kodi kwa shule za watoto za kulala

mchana *(daycare centres)* kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na heshima katika kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara Fungu 53 inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi 108,024,243,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli na vipaumbele vya Wizara hii. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:-

(i) Jumla ya bajeti ya Wizara Fungu 53 kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa 42.03% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026. Hii imetokana na kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni shilingi 50,137,801,000 sawa na 46.4% ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti hii imeongezeka kwa asilimia mbili nukta sifuri nane ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026. Hili ongezeko limetokana na kupatikana kwa kibali cha kuajiri watumishi; na

(iii) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni shilingi 57,886,442,000 sawa na 53.6% ya bajeti yote. Hata hivyo, bajeti hii imeongezeka kwa 114.86% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri. Maoni ya Jumla:-

(i) Wizara iendelee kutoa elimu kwa wanawake inayolenga kuwaonesha ni kwa namna gani wanaweza kunufaika na fursa mbalimbali zinazoweza kupatikana katika mchakato wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali; na

(ii) Wizara iendelee kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu na misingi bora ya malezi na makuzi ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa Maduhuli, Kamati inashauri Serikali kuwa:-

(i) Iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia uuzaji wa mitaala ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na ada ya malazi kwa wanafunzi wa vyuo hivyo kwani imekuwa na mwenendo usioridhisha;

(ii) Iendelee kuibua vyanzo vipya vya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na

(iii) Iweke mikakati madhubuti ya uhamasishaji na ufuatiliaji wa ulipaji wa ada za Mashirikia yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Fedha. Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Itoe fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuweza kutekeleza shughuli kama zilivyopangwa; na

(ii) Iongeze bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu na vipaumbele kama vilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Kamati inaishauri Serikali kuwa: -

(i) Iweke mikakati na jitihada za kubadili mitaala ya vyuo kwa lengo la kuzalisha Maafisa Maendeleo ya Jamii watakaoendana na kasi ya maendeleo iliyopo;

(ii) Itengeneze vituo atamizi *(Incubation Centres)* kwa shughuli mbalimbali ili kuwezesha makundi maalum kupata elimu za ujasiriamali, ujuzi, masuala ya fedha na biashara ili iweze kuwasaidia kuwa na shughuli endelevu pindi wanapopewa mikopo;

(iii) Iongeze kasi ya kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Jamii ya Mwaka 1996 ili iendane na wakati uliopo kwa lengo la kurahisisha mchakato wa kutunga Sheria ya Maendeleo ya Jamii; na

(iv) Ianzishe Bodi ya Utaalamu *(Professional Boards)* za Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya kupata wataalamu wabobezi watakaoendana na soko la ajira lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utoaji wa Mikopo ya Wafanyabiashara Ndogondogo. Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Iendelee kutoa elimu kwa wafanyabiashara ndogondogo juu ya kujiandikisha katika Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo;

(ii) Iongeze kasi katika utoaji wa mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo ili kuongeza idadi ya wanufaika wa fursa hiyo inayotolewa na Serikali; na

(iii) Iongeze kasi ya kufuatilia marejesho ya mikopo ya wafanyabiashara ndogondogo ili kutoa fursa kwa wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ustawi wa Jamii. Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Iendelee kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii ili kukidhi mahitaji yaliopo kwa sasa jambo litakalosaidia kuwepo watalamu hao katika maeneo muhimu kama vile Hospitalini, Mashuleni, Mahabusu, Mahakamani na sehemu nyingine;

(ii) Ianze mchakato wa kuandaa Bodi ya Watalamu wa Ustawi wa Jamii kwa lengo la kupata watalamu bora watakaoendana na soko la ajira la sasa;

(iii) Iongeze fedha kwa ajili ya kutoa huduma za ustawi wa jamii nchini ikiwa ni pamoja kutoa fedha kadri zilivyoidhinishwa na Bunge;

(iv) Itenge fungu maalum la kibajeti kwa ajili ya kutoa huduma za malezi na makuzi na maendeleo ya awali kwa mtoto;

(v) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi iongeze kasi ya Ujenzi wa Vituo Salama vya Malezi ya Mtoto ili maeneo mengi nchini yaweze kufikiwa na huduma hiyo;

(vi) Iongeze msisitizo kwenye malezi na makuzi ya mtoto ili kuendana na mikataba ya malezi ya Kimataifa;

(vii) Iongeze nguvu katika ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji kwa takwa la kisheria la kutenga asilimia tatu ya makusanyo ya halmashauri kwa ajili ya malezi na makuzi ya mtoto kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba niirudie hii.

(i) Serikali iongeze nguvu katika ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji wa takwa la kisheria la kutenga asilimia tatu ya makusanyo ya halmashauri kwa ajili ya malezi na makuzi ya mtoto kwenye maeneo husika;

(ii) Iweke msisitizo katika utoaji wa elimu inayohusu afya ya akili kwa shule za awali na msingi hapa nchini kujenga kizazi chenye fikra chanya;

(iii) Itafute namna ya bora ya kuweza kutekeleza sera ya matibabu bure kwa makundi maalum; na

(iv) Ihuwishe Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kwa ajili ya kuondoa kukinzana kwa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Ninapenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambayo maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Mbunge na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum, na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, Mbunge kwa kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi yao kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru Watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Eliakim Chacha Maswi na Manaibu Makatibu Mkuu Bwana. Amon Anastaz Mpanju na Bi. Felister Mdemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Idephonce Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum Fungu 53 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama ilivyowasilisha na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge,inayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (05) kama ifuatavyo: -

i) Sehemu ya Kwanza inahusu Msingi na Mawanda ya Uchambuzi;

ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum;

iii) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

iv) Sehemu ya nne inafafanua maoni na ushauri wa Kamati unaotolewa kwa Serikali; na

v) Sehemu ya Tano inahitimisha taarifa ya uchambuzi na kuonesha msimamo wa Kamati.

1.2 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum unawekwa na Masharti ya Kanuni za Bunge, Kifungu cha 6 (5)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa yaUtekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika,ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo,Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati inahusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika,uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:-

i) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa Fedha 2025/2026;

ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliiwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo inazitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo tarehe 24 Machi,2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Taarifa hiyo ilijumuisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum kwa **Fungu 53.**

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo,Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
ii) Ukaguzi wa Miradi;
iii) Utekelezaji wa Vipaumbele;
iv) Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli;na

v) Hali ya upatikanaji wa Fedha

Mheshimiwa Spika, mambo hayo kwa pamoja yanaweka msingi wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kupata uwiano utakaolisaidia katika kufikia uamuzi baada ya mjadala wa hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Maakundi Maalum kama ilivyowasilishwa na Mtoa hoja.

2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali tarehe 27 Mei,2025 wakati wa uwasilishaji wa hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo kumi na moja (11) kwa Fungu 53. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya maeneo ushauri wa kamati umezingatiwa huku maeneo mengine utekelezaji wa ushauri wa Kamati haujafanyiwa kazi kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Spika,Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni wa kutoa fedha kwa ajili ya mikopo nafuu kwa wafanya biashara ndogondogo ambapo wafanyabiashara **6306** wamenufaika na mikopo hiyo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 13,156,183,022/=**

Mheshimiwa Spika,hata hivyo,Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya maoni na ushauri ambao utekelezaji wake hauridhishi kama ifuatavyo:-

i) Kuandaa mkakati maalum unaotekelezeka wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Vyuo na Vituo ambavyo havijapimwa;

ii) Kuendeleza maeneo makubwa yanayomilikiwa na Taasisi,Vyuo na vituo vilivyo chini ya Wizara kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi;

iii) Kuweka mikakati Madhubuti ya ufuatiliaji na uhamasishaji wa

mashirika yasiyo ya kiserikali kulipa ada ili kuongeza mapato ya Serikali;na

iv) Kuandaa mkakati wa kutoa elimu juu ya faida za kujisajili na manufaa yatokanayo na usajili wa Wafanyabiashara ndogondogo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo,Kamati ilibaini kuwa ukomo wa bajeti na upatikanaji usioridhisha wa fedha za Maendeleo ni moja ya sababu za Wizara kushindwa kutekeleza baadhi ya maoni na ushauri wa kamati kwa ufanisi. Hali hii inaweza kupunguza manufaa ya Wizara hii katika Taifa na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi hapa Nchini.

2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

2.2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge,Kamati ilifanya ziara katika Mikoa mitatu (03) Arusha, Kilimanjaro, na Dar es Salaam. Katika mikoa hiyo Kamati ilikagua miradi mitatu ambayo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha **Shilingi 26,941456,000** kwa mwaka wa fedha 2025/2026.Naomba kubainisha na kufafanua miradi hiyo pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo:-

(A) Mradi 6330: Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Mheshimiwa Spika, mradi huu upo katika mwendelezo wa utekelezaji ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 ulipokea **Shilingi 600,000,000** ambapo mpaka Kamati inatembelea eneo la mradi **shilingi 1,200,000,000** zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa tangu kuanza kwa mradi kuwa ni **shilingi 3,900,000,000**. Jengo hilo linaundwa na kumbi za mikutano na ofisi za watumishi.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizowasilishwa mbele ya kamati zilibainisha kuwa mradi huu unapaswa kukamilika mwezi Mei Mwaka 2026 na umefika **asilimia 80**.

(B) Mradi 6330: Utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa mihadhara katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa *force accaunt wenye* thamani ya **Shilingi 626,405,367.66** ambapo hadi Kamati inatembelea ilikuwa imetumia kiasi cha **Shilingi 394,741,341.65** na mradi umefikia **asilimia 82** na utakuwa na uwezo wa kubeba Wanafunzi 400 kwa wakati mmoja.

(C) Mradi 6279: Ukarabati wa makazi ya wazee.

Mheshimiwa Spika, mradi huu kamati ilitaka kujionea tija inayoweza kupatikana iwapo makazi ya Wazee yataboreshwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali, ili kufanikisha hilo Kamati ilifanya ziara katika makazi ya Wazee Njoro ambayo kwa kiasi kikubwa yamekarabatiwa na wadau wa maendeleo. Katika ziara hii Kamati ilipata fursa ya kujionea kuwa ipo haja ya serikali kuona namna ya kuongeza Bajeti ili kuweka kwenye mpango makazi mengi zaidi tofauti na hali ya hivi sasa ambapo makazi machache huwekwa kutokana na ufinyu wa Bajeti, aidha Kamati imebaini changamoto mbalimbali kwenye makazi haya zinazohitaji msukumo wa kibajeti. Mathalani, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ilitengewa kiasi cha **shilingi 1,000,000,000** ambapo hadi Kamati ilipotembelea mradi **shilingi 568,000,000** zilikuwa zimepokelewa ikiwa ni robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti

2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

Mheshimiwa Spika, katika ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Lengo ilikuwa kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua

zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika

Mheshimiwa Spika,Tathmini ya Kamati imebainisha kuwa:-

i) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na kamati imezingatia thamani ya fedha na hatua iliyofikiwainawiana na muda wa utekelezaji wa miradi husika;

ii) Miradi iliyotembelewa na Kamati ingekuwa na tija kubwa zaidi na ufanisi kama fedha za maendeleo zingetolewa kwa wakati kama ilivyokusudiwa; na

iii) Sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa inatumia Force Account jambo linalopongezwa na kamati na litakalochochea utekelezaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua mbailmbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi chini ya Wizara ya Maendeleo ya jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum (**Fungu 53**) .Kamati inalitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza miradi hiyo thamani ya fedha, uwekezaji, ufanisi na tija vimezingatiwa.

2.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Machi,2026 kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, wakati wa uchambuzi wake Kamati ilizingatia vipaumbele vya wizara ambavyo ni:-

i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza Sera na Miradi ya Maendeleo iliyoibuliwa Ngazi ya Msingi;

ii) Kuratibu afua za Upatikanaji wa Haki, Ulinzi, Malezi na Matunzo ya watoto;

iii) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia,kutokomeza ukatili wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi;

iv) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii;

v) Utambuzi, uratibu na uendelezaji wafanyabiashara Ndogo ndogo

Mheshimiwa Spika,Wizara imefanikiwa kufanya baadhi ya shughuli ili kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea, baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na:-

i) mapitio ya Mwongozo wa majukumu ya wataalam wa maendeleo ya jamii wa Mwaka 2018, Toleo la Mwaka 2025;

ii) uanzishwaji wa Madawati ya ulinzi na usalama wa Mtoto;

iii) Imetoa mafunzo ya kujenga uelewa kuhusu programu ya kizazi chenye usawa;na

iv) Wizara kwa kushirikiana na OWM- TAMISEMI imeweza kuwapatia vitambulisho vya kidigitali kwa wafanyabiashara ndogo ndogo kwa ajili ya kuvitumia kuomba mkopo yenye masharti mafuu kutoka Taasisi za kifedha.

2.3.1 Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefanikiwa. Aidha, uchambuzi huu unaliweka Bunge katika nafasi ya kutumia uzoefu unaopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kubaini uhalisia inavyostahili kwa mwaka wa fedha 2026/2027.Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo; na

ii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2.3.2 Hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum **Fungu 53** ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 9,040,129,000/=.** Hadi kufikia Februari, 2026 wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 2,991,829,587/=** sawa na **asilimia 33.09 tu** ya lengo la makusanyo ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti ambao ni **asilimia 66.7**

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa uwezekano wa Wizara kufikia lengo la ukusanyaji ni mdogo kwani katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo makusanyo ya Wizara yamekuwa chini ya **asilimia 50** ya lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge.

2.3.3 Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Bajeti unategemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 53 kutoka hazina kama ifuatavyo:-

i) Upatikanaji wa jumla ya Fedha zilizoidhinishwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **Fungu 53** ni **asilimia 67.8** ya bajeti ikiwa ndani ya utekelezaji wa kipindi kama hicho;

ii) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopatikana kwa asilimia 66;

iii) Fedha za Matumizi mengineyo (OC) zimepokelewa kwa **asilimia 67;**

iv) Fedha za mishahara zilizopokelewa ilikuwa **asilimia 65** ikiwa na upungufu wa **asilimia 1.7** ya fedha iliyotakiwa katika kipindi kama hiki;

v) Fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa **asilimia 70** ya Bajeti; na

vi) Katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo,Fedha za Ndani zilifikia **asilimia 87** na Fedha za nje **asilimia 48.**

Upatikanaji wa fedha kutoka hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni wa kuridhisha na hivyo Kamati inaishauri Serikali kusimamia miradi kikamilifu ili ilete tija iliyokusudiwa kwa Wananchi.

Kielelezo Na. 1: Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 53

AINA YA MATUMIZI	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	KIASI KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
Mshahara	22,646,148,000	14,797,974,939	65
Matumizi mengineyo	26,469,549,000	17,799,823,321	67
Jumla Ndogo	49,115,697,000	32,597,798,260	66
Miradi ya Maendeleo	26,941,456,000	18,948,732,400	70
Jumla kuu	**76,057,153,000**	**51,546,530,666**	**67.8**

Chanzo: Randama za Wizara, 2026 na Usanifu wa Kamati

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika,Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na

ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

3.1 Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya Mapato na matumizi, kamati ilipokea ufafanuzi kuhusu lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ambapo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** inakadiriwa kukusanya maduhuli ya Shilingi **7,040,129,000/=**. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa makusanyo yamepungua kwa **Shilingi 2,000,000,000** sawa **na asilimia 22.1** ikilinganishwa na makadirio ya makuasanyo kwa mwaka wa Fedha 2025/2026. Pamoja na kupunguziwa maduhuli kamati ilipewa taarifa kuwa Wizara iliibua chanzo kipya cha mapato cha ulipaji wa kodi kwa shule za Watoto za kulala mchana (daycare centers) na kwa lengo la kuongeza uwajibakaji na heshima katika kutoa huduma.

Kielelezo Na. 2: Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli

FUNGU	Mwaka 2025/2026	Mwaka 2026/2027	Ongezeko/ pungufu	Asilimia
Wizara (53)	9,040,129,000	7,040,129,000	2,000,000,000	22.1

Chanzo: Randama za Wizara, 2026 na Usanifu wa Kamati

3.2 Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika,kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua, makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika,Wizara (Fungu 53) inakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 108,024,243,000/=** kwa ajili utekelezaji wa shughuli na

vipaumbele vya Wizara hii. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:- Jumla ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum (**Fungu 53)** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa **asilimia 42.03** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 hii imetokana na kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo;

i) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni **50,137,801,000/=** sawa na **asilimia 46.4** ya Bajeti yote ya Wizara hii. Bajeti hii imeongeka kwa **asilimia 2.08** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 hili ongezeko limetokana na kupatikana kwa kibali cha kuajiri Watumishi; na
ii) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni Shilingi **57,886,442,000/=** sawa na asilimia **53.6** ya bajeti yote. Hata hivyo,
iii) bajeti hii imeongezeka kwa **asilimia 114.86** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026

Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 - Fungu 53

AINA YA MATUMIZI	MWAKA 2025/2026	MWAKA 2026/2027	ASILIMIA Ongezeko/ Upungufu
Mishahara	22,646,148,000	23,315,207,000	2.95
Matumizi mengineyo	26,469,549,000	26,822,594,000	1.33
Jumla	49,115,697,000	50,137,801,000	2.084
Miradi ya Maendeleo	26,941,456,000	57,886,442,000	114.86
Jumla kuu	**76,057,153,000**	**108,024,243,000**	**42.03**

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI

4.1 Maoni ya Jumla

i) Wizara iendelee kutoa elimu kwa wanawake inayolenga kuwaonesha ni kwa namna gani wanaweza kunufaika na fursa mbalimbali zinazoweza kupatikana katika mchakato wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali; na

ii) Wizara iendelee kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu na misingi bora ya malezi na makuzi ya mtoto;

4.2 Ushauri wa Kamati

4.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Kamati inashauri Serikali kuwa:-

i) iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia uuzaji wa mitaala ya vyuo vya maendeleo ya jamii na ada ya malazi kwa wanafunzi wa vyuo vya Maendeleo ya jamii kwani imekuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji;

ii) iendelee kuibua vyanzo vipya vya ukuanyaji wa maduhuli ya Serikali;na

iii) iweke mikakati madhubuti ya uhamasishaji na ufuatiliaji wa ulipaji wa ada za Mashirikia yasiyo ya Kiserikali.

4.2.2 Upatikanaji wa Fedha

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i) itoe fedha za miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuweza kutekeleza shughuli kama zilivyopangwa; na

ii) iongeze bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu na vipaumbele kama ilivyopangwa;

4.2.3 Sekta ya Maendeleo ya Jamii

Kamati inaishauri Serikali kuwa

i) iweke mikakati na jitihada za kubadili mitaala ya vyuo kwa lengo la kuzalisha Maafisa maendeleo ya jamii watakaoendana na kasi ya maendeleo iliyopo;

ii) itengeneze vituo atamizi (incubation centres) vingi kwa shughuli

mbalimbali ili kuwezesha makundi maalum kupata elimu za ujasiliamali,ujuzi,masuala ya fedha na biashara ili iweze kuwasaidia kuwa na shughuli endelevu pindi wanapopewa mikopo;

iii) iongeze kasi ya kuhuisha sera ya maendeleo ya jamii ya mwaka 1996 ili iendane na wakati uliopo kwa lengo la kurahisisha mchakato wa kutunga Sheria ya Maendeleo ya Jamii; na ianzishe bodi ya utaalamu (professinal board) za maendeleo ya jamii kwa ajili ya kupata wataalam wabobezi na watakaoendana na soko la ajira lililopo;

4.2.4 Utoaji wa Mikopo ya Wafanyabiashara Ndogondogo

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i) iendelee kutoa elimu kwa Wafanyabiashara ndogondogo juu ya kujiandikisha katika Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo ;

ii) iongeze kasi katika utoaji wa mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo ili kuongeza idadi ya wanufaika wa fursa hiyo inayotolewa na Serikali; na

iii) iongeze kasi ya kufuatilia marejesho ya mikopo ya Wafanyabiashara ndogondogo ili kutoa fursa kwa wengi zaidi.

4.2.5 Sekta ya Ustawi wa Jamii

Kamati inaishauri Serikali kuwa

i) iendelee kuajiri Maafisa ustawi wa jamii ili kukidhi mahitaji yaliyopo kwasasa, jambo litakalosaidia uwepo wa wataalam hao katika maeneo muhimu kama vile hospitalini, shuleni, mahabusu, mahakamani na sehemu nyingine;

ii) ianze mchakato wa kuunda bodi ya Wataalam wa Ustawi wa jamii kwa lengo la kupata Wataalam bora na watakaoendana na soko la ajira la sasa;

iii) iongeze Fedha kwa ajili ya kutoa huduma za ustawi wa jamii nchini ikiwa ni pamoja kutoa fedha kadri zilivyoidhinishwa na Bunge;

iv) itenge fungu Maalum la Kibajeti kwa ajili ya kutoa huduma za malezi na makuzi na maendeleo ya awali kwa mtoto;

v) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Sekta binafsi iongeze kasi ya ujenzi wa vituo salama vya malezi ya mtoto ili maeneo mengi nchini yaweze kufikiwa na huduma hiyo;

vi) iongeze msisitizo kwenye malezi na makuzi ya mtoto ili kuendana na mikataba ya malezi ya kimataifa;

vii) iongeze nguvu katika ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji wa takwa la kisheria la kutenga asilimia 3% ya makusanyo ya Halmashauri kwa ajili ya malezi na makuzi ya mtoto kwenye maeneo husika;

viii) iweke msisitizo katika utoaji wa elimu inayohusu afya ya akili kwa shule za awali na msingi hapa nchini ili kujenga kizazi chenye fikra chanya;

ix) itafute namna bora ya kuweza kutekeleza Sera ya matibabu bure kwa makundi maalum;

x) ihuishe Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 kwa ajili ya kuondoa kukinzana na Sheria ya mtoto ya mwaka 2009.

SEHEMU YA TAN0

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika

kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe.Hawa Chakoma Mchafu, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe.Dkt. Regina C. Malima, Mb. - **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe.Mohamed Abrahman Mwinyi, Mb.
4. Mhe.Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
5. Mhe.Tinnar Andrew Chenge, Mb.
6. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb.
7. Mhe.Said Ibrahim Mzimba, Mb.
8. Mhe.Lucy Similya Kombani, Mb.
9. Mhe. Nasriya Nassir Ali, Mb.
10. Mhe. Shadya Haji Omary, Mb.
11. Mhe. Mohamed Kassim Salum, Mb.
12. Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar, Mb.
13. Mhe. Athumin Omary Mapalilo, Mb.
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
15. Mhe. Pascal Lucas Lutandula, Mb.
16. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola, Mb.
17. Mhe. Kafiti William Kafiti, Mb.
18. Mhe. Edefonce Joachim Canoni, Mb.
19. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
20. Mhe. Happiness Daniel Ngwando, Mb.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima, Mb, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri Mheshimiwa Marryprisca Winfried Mahundi, Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Eliakim Chacha Maswi na Manaibu Katibu Wakuu Bwn. Amon Anastaz Mpanju na Bi. Felister Mdemu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja**.**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Hawa Chakoma Mchafu, Mb
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII
01 Juni, 2026

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Hawa Chakoma Mchafu kwa taarifa hiyo tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea taarifa zote mbili, sasa tunaanza na uchangiaji na tutaanza hapa na Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga na Mheshimiwa Lucy Damas Simirya ajiandae. *(Makofi)*

(Hapa Mhe. Nassriya Nassir Ali Alichangia Kupitia Mtaalamu wa Lugha ya Alama)

MHE. NASSRIYA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nimshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama tena kwa mara nyingine hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia, kwanza ninaomba nimshukuru sana mama yangu, yuko hapa leo Bungeni amefanya kazi kubwa sana, amekuwa ni Balozi wa watoto wenye ulamavu hapa duniani. Mungu atakulipa mama yangu, endelea kuwa na moyo huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya kwenye Wizara hii katika kuhakikisha maendeleo ya jamii yanakuwa vizuri. Wizara hii imekuwa na jukumu kubwa sana kwenye jamii. Hii ni Wizara mama ambayo imebeba maono ya jamii nzima kwa watoto, wamama na wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nimpongeze Waziri, mama yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima, kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya. Mama wewe ni jembe, endelea na moyo huo huo umefanya kazi kubwa sana, Wizara hii kweli ni ngumu lakini Mungu anakusimamia, unakwenda vizuri. Usichoke endelea kupambana kuhudumia jamii usichoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nilishukuru Bunge kwa kuniteua mimi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Masuala ya Ustawi wa Jamii. Hii kwangu inanihusu mimi mwenyewe kwa sababu mambo mengi ya watu wenye ulemavu, wanawake, watoto na wazee mimi ninayafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana leo nimesimama hapa nikiwa na kofia mbili. Kwanza, ninasimama mbele yako kwa unyenyekevu mkubwa, mimi nimekuwa ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake na Watoto ndani ya Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ninafahamu changamoto ambazo watoto wenye ulemavu wanazipitia, kwa hiyo ninashukuru sana Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninatafuta mahali pa kusemea, sasa nimepata. Ninamshukuru Mungu leo nimesimama hapa na ninarudia tena kumshukuru mama yangu. Bila mama yangu, mimi nisingekuwa hapa. Pia ninamshukuru Mheshimiwa

Rais na Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipitisha kuwa Mbunge wa kuwakilisha Watu Wenye Ulemavu kuwa msemaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nitoe ushuhuda leo tunapitisha Bajeti ya Wizara hii, kabla sijasema yote ipitishwe kwa sababu yako mambo mengi sana ambayo Wizara inawajibika katika kuhudumia jamii. Kuna masuala ya watoto, wazee, watu wenye ulemavu na makundi yenye ulemavu, maalum kwa ujumla. Kwa hiyo, lazima Wizara ipewe nguvu ili iweze kutekeleza majukumu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Wizara hii siyo dogo, tusichukulie juu juu, kutembelea kituo kimoja tu cha wazee. Mimi nilienda kituo kimoja cha wazee kule Moshi, kwa kweli nilitamani kulia, kwani hali niliyowakutanayo haikuwa nzuri. Kwa hiyo, ninaomba Wizara hii ipitishiwe bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaja kituo cha wazee kule Moshi, Waheshimiwa Wabunge ninaomba tupitishe hii bajeti ili iweze kuongezwa kwa ajili ya ufanisi katika kutoa huduma kwa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nisiwe mchoyo tena kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Gwajima, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kipindi cha mashindano ya Miss Redds, Mwaka 2009 alikuwa Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima mwenyewe na Tanzania tulipata msindi wa kwanza. Kwa hiyo, tulipata *support* sana kutoka Wizara ya mama, Mungu akubariki sana endelea na moyo huo huo usichoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimeridhika na nimefarijika kwa uwezo wake, sina mashaka yoyote na pia pacha wake Naibu Waziri, Mheshimiwa Maryprisca, yeye mwenyewe ameniambia wakati anakwenda Mbeya na nitamsumbua, pia anafahamu changamoto za watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, nitamsumbua usiku na mchana kuhakikisha mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa sana ninaomba sisi watu wenye ulemavu katika programu zote ambazo zinaendeshwa tuweze kujumuishwa kwa sababu kwa kipindi kirefu tumekuwa tunapitia changamoto nyingi. Kuwa mlemavu halafu mwanamke, unakuwa na changamoto mara mbili. Tunapitia changamoto kubwa sana tofauti na wanawake ambao hawana ulemavu. Kwa hiyo, tunaomba katika programu mbalimbali tuweze kujumuishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nisisitize, tunaomba pia katika programu kama hizi nitumwe mimi kwa sababu nafahamu takwimu za watu wenye ulemavu wakiwemo wazee. Kwa hiyo, tutaweza kufanya kazi vizuri usiku na mchana. Wanisumbue tu, wanitumie, niko tayari kutumika kwenye Wizara hii ili kusaidia mambo yaende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kabla ya kuunga hoja, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, suala la wenye ulemavu linaunganisha Wizara mbili; TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu na Maendeleo ya Jamii. Ninaomba Wizara hizi zikae zifanye utafiti kuhusu wanawake wenye ulemavu wanaishije? Wazee pia wenye ulemavu na vijana wenye ulemavu wanaishije?

Mheshimiwa Mwenyekiti, itapendeza na sisi Wabunge kwa sababu wenye ulemavu pia sisi tumo, kwa hiyo, tukae pamoja Wizara watusikilize, tuwaeleze yale tunayoyapitia na nini kifanyike? Mheshimiwa Rais ni mama mwenye huruma sana, ana huruma kweli kweli, kwa hiyo, naomba tusikilizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, ahsante sana kwa mchango wako mzuri kabisa. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga ajiandae.

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimshukuru Mungu kwa nafasi hii, lakini pia kwa namna ya pekee sana nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa na mipango ya muda mrefu, mipango ya muda wakati hata mipango ya muda mfupi. Hivyo kwa sababu nchi yetu sasa ina mtazamo muhimu wa kuwa na mipango ya maendeleo ya jamii ambayo inaeleweka, hii ikiwemo Dira ya 2050, ni mambo muhimu sana ambapo Taifa letu na tupaswa kuipongeza Serikali hii kwa namna ambavyo imejipambanua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Gwajima, wakati akisoma hotuba yake ameongea habari ya kuleta tabasamu kwa wananchi wa Tanzania, kauli ambayo aliitoa Mheshimiwa Rais wakati akizindua Bunge la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii ni lugha ya picha. Kinachotakikana nyuma yake Mheshimiwa Rais anataka kuona wananchi wanapata majisafi na salama, wananchi wanapata miundombinu inayoeleweka, na kuona elimu inaboreka kwa Watanzania. Kwa maana hiyo, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa namna ambavyo imejipambanua na namna ambavyo Tanzania inapaswa kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Dkt. Gwajima, nimpongeze Naibu wake Muhandisi Maryprisca Mahundi, na pia bila kusahau, Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Eliakim Maswi na Manaibu Katibu Wakuu Mheshimiwa Mpanju na hata Mheshimiwa Mdemu na timu yote ya watalamu ambao wamekuja na bajeti hii ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii lazima tuipongeze kwa sababau uwiano wa bajeti hii unaonyesha kabisa Miradi ya Maendeleo ni 53.59%, lakini gharama ambazo zitatumika katika uendeshaji wa Ofisi ni 46.41%. Jambo hili ni la kupongeza na kwa bajeti hii tunaona tabasamu la Watanzania likifikiwa kwa sababu uwiano wa bajeti kubwa imeenda katika Miradi ya Maendeleo. Mheshimiwa Waziri, Dkt. Dorothy Gwajima hongera sana kwa hili na lazima tukupongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma ya maendeleo ya jamii ndiyo inayobeba dhana kubwa katika utekelezaji wa mipango ya muda mrefu wa Taifa hili, na pia mipango ya kati na hata muda mfupi. Taaluma hii ni kiungo kati ya Serikali na wadau wa maendeleo na pia taasisi nyingine zote zinazofanya shughuli za maendeleo na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza kuona namna ambavyo bila ku-*support*, taaluma ya maendeleo ya jamii bado utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya maendeleo katika Taifa letu unaweza ukawa na changamoto. Serikali inaweza kuwa na sera, mipango na fedha, lakini bila watalamu wa maendeleo ya jamii watu hawawezi kuhamasika, watu hawawezi kushirikishwa, watu hawawezi kuelimishwa lakini watu hawawezi kumiliki miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitoe tu rai yangu kwa Wizara yetu pendwa, namna ambavyo ina majukumu makubwa katika Taifa hili, lazima sasa ijipambanue wazi namna gani bora itaweza kuipa nguvu taaluma hii ya maendeleo ya jamii kuweza kuendana na wakati, na zaidi katika kutekeleza mipango hii ambayo imeletwa na Serikali ya Awamu ya Sita, iwe ni afya iwe ni lishe iwe ni malezi ya watoto, iwe ni mikopo, iwe ni mazingira, iwe ni uwezeshaji wanawake, wananchi kiuchumi, yote haya yanamhitaji Afisa Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona vipaumbele vya Wizara ni vingi kujenga mtaji wa watu wa Taifa na kizazi cha Tanzania, kuimarisha huduma za makuzi na kadhalika na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele hivi, mimi nilikuwa ninashauri Wizara lazima iwe na kipaumbele cha kuimarisha taaluma ya maendeleo ya jamii ili iweze kutekeleza vyema na kwa tija mipango hii ambayo Mheshimiwa Rais kwa dhati ameleta na anataka aone tabasamu katika nyuso za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo? Mpaka sasa taaluma hii haina sheria, na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati wakati akiwasilisha pia ameongea juu ya hili na katika Taifa hili taaluma muhimu sana ambayo ina-*deal* na *mind set* ya wananchi, ndiyo haina sheria, kitu ambacho Wizara inabidi ijitathimini sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia madaktari wana sheria, hata wasanii wana sheria zinazolinda taaluma. Kwa hiyo, ninaomba Wizara hii pendwa pamoja na mzigo mkubwa ilionao ihakikishe ndani ya mwaka huu; tumeambiwa sera iko katika mapitio, ni kweli, na tunapongeza, lakini lazima viende sambamba na uandaaji wa sheria ili viweze kusomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamuwezi kutengeneza sera ambayo haina *reflection* ya sheria, haina *reflection* ya *professional board* na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri na timu yake hili walichukue kwa umakini mkubwa na sisi kama Kamati tuta-*support initiatives* zote ambazo watazifanya kama Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninaomba tu yule mama aliyeko kijijini anayehamasishwa kujiunga kwenye vikundi vya uchumi anamtegemea Afisa Maendeleo ya Jamii; yule kijana anayesaidiwa kuacha madawa ya kulevya, anamtegemea Afisa Maendeleo ya Jamii; yule mtoto anayepatiwa malezi bora anamhitaji Afisa Maendeleo ya Jamii, lakini watu wote tukiwemo sisi, tunamhitaji Afisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, tunamwomba Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, sheria ni kipaumbele cha taaluma hii ili iweze kufanya

kazi katika tija inayotakiwa. Mheshimiwa Rais ameshasema tabasamu analolitaka liweze kuonekana, na watu wa kuleta tabasamu ni Maafisa Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ninaomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima. Nilimtaja Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mheshimiwa Lucy Kombani na Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando ajiandae. *(Makofi)*

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara hii muhimu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Bunge linisikilize vizuri, na leo hapa ninataka niongee nimetulia kabisa. Hapa nina Biblia na hapa nina Msahafu. Hivi vyote ni vitabu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye hotuba hii kwenye *angle* moja ya mapenzi ya jinsia moja. Kila nikitazama hotuba za Mheshimiwa Rais anapohutubia, akifika kwenye *angle* ya mmomonyoko wa maadili, unamtazama yule mama usoni unaona sura yake ina huzuni, kwa sababu ya kinachoendelea kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya na miongozo anayoitoa kwenye Serikali. Mimi ninataka nimwambie Mama yangu, sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuko hapa kukuunga mkono ili utimize matarajio ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpongeze dada yangu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, anafanya kazi nzuri sana na mimi toka nimemfahamu sijawahi kumwona ameweka

hata wigi. Ninawaza tatizo ni nini? Kumbe matatizo aliyonayo ni kwenye mmomonyoko wa maadili ya Taifa letu. Mama hongera sana, lakini hongera za dhati ninampa mume wako anayekuvumilia kwa yale ambayo unakutana nayo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu za tatu ziende kwa *Prophet IPM*. Huyu *Prophet*, mimi siyo muumini sana wa manabii hawa, lakini ninampongeza kwa sababu ameona lipo tatizo akachukua hatua. Kwenye tatizo la mmomonyoko wa maadili kinachonisikitisha, vita hii ameachiwa Mheshimiwa Dkt. Gwajima peke yake, lakini vita hii inahusu Wizara zaidi ya nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Sheria na Katiba kwa maana ya sheria zetu, zipo kesi nyingi zimewahi kutokea hapa. Hawa watu wanaofanya matendo kama haya wakipelekwa Mahakamani wanashinda kesi zile, na Wakili anasimama kwa kujimwambafai kabisa eti, hoja iliyokuwepo ni kwamba mtu ameingiliwa kinyume cha maumbile na kuingiliwa kinyume haieleweki ni nini? Imefika wakati sheria zetu ziwe wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Biblia Takatifu ukienda kwenye Walawi, unaanza na Walawi 20:13 inasema, "Mtu alalaye na mume, kama vile amelala na mwanamke, wote wanafanya machukizo, na wanafaa kuuawa hakika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kitabu cha 1Wakorintho 8 inasema, "Watu wa kunyang'anya mali zao, naam, hata na ndugu zenu, au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi Ufalme wa Mungu. Msidanganyike waasherati wala wazinzi, wala wafiraji..." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi kwenye sheria mnashindwa kuandika kuwa mtu siyo kuiingiliwa kinyume na maumbile, sheria zinakinzana na mawakili hapa ndipo wanapopata *loophole*. Andikeni kabisa huyu amekwenda kufirwa kama Biblia inavyosema. Mimi sikuandika Biblia. Hili ni neno la Mungu, ninyi sheria mnafichaficha mambo nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakienda Kanisani kule, Wachungaji wetu na Mapadri na wenyewe wanakwambia tutunze maadili, unyenyekevu. Maadili yapi? Nyookeni mtuambie. Ninawapongeza viongozi wa dini, wanafanya kazi kubwa sana ya kuikosoa Serikali. Wanatumia nguvu kubwa mno ya kuikosoa Serikali. Nguvu hiyo hiyo mnayoitumia, watumie kukosoa mmomonyoko wa maadili. Wasifanye mambo kwa mafumbo mafumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *Quran* Tukufu *Surat* mstari wa 78 – 83, Mwenyezi Mungu katika *Quran* aliwapa adhabu kubwa sana Kaumu Lutu, kwa kupigwa jiwe kichwani, ambapo kila mtu mmoja aliandikiwa jiwe lake na baadaye *Allah* alimwamrisha Jibril kuipindua ardhi *upside down*, kusiwepo kabisa hata alama yao baadaye. Mwenyezi Mungu alichukia hiki kitendo, akafikia mahali akaipindua dunia ili pasiwepo na kizazi kingine kinachofanana na Lutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo ninawaonya Watanzania msiponiunga mkono, Mwenyezi Mungu wa Mbinguni ananisikia. Siku anaipindua Tanzania *upside down* mimi nitakuwa kama Lutu ninaamini, sitakuwa sehemu ya adhabu atakayoitoa kwenye dunia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Quran* Tukufu bado inasisitiza. Ukienda kwenye *Surat al Qamal* aya ya 36 – 39, Nabii Lutu aliapa, lakini hawakusikia, akafadhaisha dunia. Pia mimi leo Mwenyezi Mungu anawaambia, ninawaapia *Allah* aifadhaishe dunia au Tanzania, ukumbusho unaofaa wenye kukumbuka milele na milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu, hali ya Tanzania tunakokwenda ni mbaya. TAMISEMI jambo hili wamemwachia Mheshimiwa Dkt. Gwajima. Matatizo makubwa yanaanza kwenye *Local Government*. Wanatunga sheria ya kutoa vibali vya utamaduni, ngoma zinazochezwa huko, ndugu zangu zinaharibu kabisa maadili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wanacheza uchi mbele ya watoto wao, TAMISEMI wapo, wanatoa vibali. Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo wanalo jukumu kubwa sana. Sasa hivi kumezuka ma-*designer*. Mambo haya yanaanzia mbali, wasanii wetu wakubwa ma-*celebrity* sasa wanavishwa vinguo vya kike vinaitwa *clop* sijui *crop top*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu zikipungua kidogo uniongeze tu kidogo, kwa sababu nina kazi ya kulikomboa Taifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliotoka Katavi ukitazama msanii mkubwa kabisa amevaa kale, sisi tunajua ni *blouse*. Hawa watu huwa wanawaandaa watu kisaikolojia ili tatizo linaloendelea lionekanane ni la kawaida. Ifike mahali wasanii; sasa hivi tunao waigizaji wengi sana wa kike, hakuna sababu ya mtoto wa kiume kuweka matako. Hakuna sababu ya mtoto wa kiume kutinda nyusi na kupaka wanja. Ifike mahali vitendo hivi Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo ichukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mambo ya Ndani, Mama Gwajima anafanya kazi kubwa. Kazi ya kuchunguza na kuchukua hatua na kukamata ni ya Mambo ya Ndani, wanashindwa nini? Hapa mimi ndipo ninapopata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba, ninasikia kuna watu sijui wasioonekana. Ninataka niwaombe wale wasioonekana, wafanye kazi ya kulisaidia Taifa, wachukue hawa ili Taifa hili libaki salama. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu inalo jukumu kubwa la kuhakikisha maadili kwenye shule zetu yanasimama. Wizara ya Mawasiliamo huko kwenye mitandao ni balaa. *TCRA* sijui hata wanafanya nini? Kuna shida zimetokea, sasa hivi kuna siku nimeona Waziri, Mheshimiwa Dkt. Gwajima anatoa *notice*, eti punga nalo linamjibu. *TCRA,* mpo! Waziri anajibiwa na punga. *TCRA* mnaiona ile akaunti inatembea na ninyi mpo! Haiwezi kuwa nchi ya namna hii. Nchi haiwezi kwenda hivyo. Serikali lazima iheshimiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie, hili tatizo Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapo, ninataka nipendekeze, tatizo hili tukimwachia Mheshimiwa Dkt. Gwajima peke yake hataliweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tuamue kutengeneza taasisi kama Taasisi ya Kupambana na Dawa za Kulevya kwa ajili ya kupambana na mmomonyoko wa maadili kwenye Taifa letu, *otherwise* tutakuwa tunapiga *mark time* tu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana Watanzania, ndugu zangu ninyi mnaokaa kwenye ma-*V8* huko hamwoni hili tatizo. Ukipita mtaani huko vitoto vidogo kwenye hizi ngoma, zamani Mheshimiwa Ridhiwani yuko hapa, sisi tunaotoka Bara kule tulikuwa tunajua hizi ngoma zenu za Kizaramo za Kipwani zinachezwa na wanawake na wanaoalika ni wanaume. Sasa hivi ngoma za Pwani wanatengeneza wanaume, wanaume wanaalika wanawake. Haya mambo yamekuwaje? Mheshimiwa Ridhiwani na wenzio watu wa Pwani, Mheshimiwa Ulega, mmebadilisha utaratibu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu mtusaidie sisi washamba tunaotoka Katavi, hizi ngoma zenu za Pwani sijui Kibao Kata...

MWENYEKITI: Mheshimiwa ninakuongezea dakika mbili. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ngoma zenu na ilitokea *scenario* moja Mheshimiwa Dkt. Gwajima nilimtumia *clip*. Mkaka mmoja amechukua ukumbi wa *Mlimani City* pale akatengeneza hayo makibao kata yake. Akaita akina mama wakaenda. *Clip* zilikuwa zinarushwa nje, mgeni rasmi alikuwa yule kaka sitaki kumpa umaarufu, yule Mheshimiwa Waziri alikuwa anapambana naye kwenye mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie, tukiacha Taifa hili hivi linavyokwenda na kuacha watu wanaji-*post* kwenye

mitandao, kuonekana kwamba eti mtu akiwa ana mambo ya kike kike eti ni kufanikiwa, hawa watoto wanaokua wakitazama kwenye mitandao, watakubaliana na hiyo hali kuwa ukiendeleza na vitendo vya ushoga ni kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niisihi sana Serikali, Taifa hili lina mpango wa miaka 50. Kama tuna mpango wa miaka 50 isije ikafika miaka huko, hii mipango ya miaka 50 itafika Taifa baada ya miaka 30 hatutakuwa na vijana. 70% itakuwa hali ni mbaya na msiponisikia, Wizara ya Viwanda na Biashara, muanze kuandaa *pampers* kwa ajili ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge.

Ahsante sana Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga kwa kukemea vikali vitendo vya mmomonyoko wa maadili katika Taifa letu. Siyo jambo la kufurahia wala kuchekelea, ni jambo la hatari. Endapo Mwenyezi Mungu hasira zake zikizidi na sisi tunaweza tukaangamia.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Kombani, Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando ajiandae.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuimarisha ustawi wa jamii, hususan katika kulinda haki za wanawake, watoto, wazee, pamoja na makundi mengine maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Wizara hii ikiunda programu mbalimbali kama SMAUJATA, itakuwa programu ambazo sasa kwenye jamii tumeshaanza kuona matokeo yake

chanya katika usawa wa kijinsia, ulinzi wa watoto na wanawake na hata katika uwezeshaji wa watu wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninawapongeza katika zoezi zima la kuwapeleka Maafisa Maendeleo ya Jamii kila Kata. Maafisa hawa ambao wamekuwa wakifanya kazi muhimu sana katika jamii zetu, hususan kushughulikia mambo mbalimbali yenye kuleta ustawi wa jamii kwenye jamii zetu. Maafisa hawa wamekuwa viungo muhimu sana kwenye Kata zetu hususan katika kushughulikia kesi za unyanyasaji, ukatili wa watoto, zoezi zima la uhamasishaji wa Bima ya Afya kwa wote na zoezi kubwa zaidi likiwa kuratibu zoezi zima la mikopo kwa ajili ya jamii zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia hawa maafisa wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana. hizi kazi zote wanazofanya, ukiangalia kuna mashirika, wangeweka watumishi zaidi ya 10 kwa ajili ya kufanya hizi kazi, lakini kwa upande mwingine, pamoja na hawa maafisa kubeba majukumu mazito sana, hawa maafisa wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto mbalimbali, kubwa ikiwa usafiri. Sisi tukichukulia Mkoa wetu wa Morogoro, ule Mkoa ni mkubwa sana. Kuna mabonde, milima, na misitu. Kwa hiyo, anaweza kukaa kwenye Kata moja, lakini kufika kwenye vijiji vingine ikawa taabu kwa sababu hawana usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *nature* ya majukumu yao hii imesababisha ku-*delay* kutimiza majukumu yao mengi sana, hasa likiwa kwenda kuokoa mwanamke au mtoto ambaye anafanyiwa ukatili. Hivyo, Wizara tunaomba iangalie hili suala la usafiri hususan kwa sehemu ambazo zinaonekana kabisa kwamba jiografia yake siyo rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, maafisa wamekuwa wakipata changamoto. Hawa ndiyo wamekuwa wakiratibu zoezi zima la mikopo ya 10% na ile ya asilimia saba, na siku hizi tunajua mambo ni teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo inahitaji watu wawe na katiba, inahitaji watu waombe *online*, lakini sasa utakuta Afisa Maendeleo ya Jamii huyu hana hata hiyo kompyuta. Inafika wakati anaishia kutoa elimu tu, yeye hawezi kuwasaidia wale wananchi, na wananchi hawawezi kujisaidia kwa kuwa vijiji vingi hamna mtu ana-*invest* kwenye *internet cafe* au *stationary*. Kwa hiyo, hili jukumu linabaki kwa Afisa Maendeleo ya Jamii ambalo na lenyewe linakuwa gumu kulitekeleza na kuna sehemu mikopo inakuwa migumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni udogo wa bajeti katika fedha ya OC. Kumekuwa kuna fedha inatoka kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizi mbalimbali ambapo kwa sasa hivi kama sikosei ni shilingi milioni tano kwa kila Halmashauri. Tukichukulia sisi tuna Halmashauri kama ya Kilosa ina Kata 40, hii shilingi milioni tano. Ukiigawanya kwa Kata hizi 40 kwa kweli haitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna maafisa wamekuwa wakifanya kazi kwa mazingira magumu na pia kumekuwa na malalamiko kuwa hizi fedha za *OC* hazifiki kwa baadhi ya Maafisa wa Maendeleo Kata. Kwa hiyo, Wizara iangalie ili hawa watu waweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna Halmashauri zimekuwa na changamoto, Wakuu wa Idara hawana hata magari. Wao kutimiza majukumu yao imekuwa wanasubiri Afisa Kilimo asiwe na shughuli, Afisa Biashara asiwe na shughuli yeye ndiyo aazime lile gari aende aka-*supervise* hizi kazi. Hili suala Wizara tunaomba mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ndiyo inayohusika na *NGOs* zote, wanahusika na mashirika haya yasiyokuwa ya Kiserikali. Kuna mashirika yamekuwa yakitoa magari, yamekuwa yakitoa *computers*. Jamani *charity begins at home*. Ungeni ujamaa na hawa watu ili watusaidie kwa ajili ya hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa kata zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kumekuwa na changamoto ya mafunzo. Hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata, wakishatupwa huko kwenye kata, basi hamna semina yoyote, hamna mafunzo yoyote. Wenyewe wanasubiri Wizara imeleta sera mpya, imeleta mpango mpya, au mfumo mpya wale wa mkoani waende wakajifunze waje wawafundishe wa wilayani, wa wilayani ndio waanze kuwaelezea Maafisa Maendeleo Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote mtu kukielewa kitu lazima afundishwe yeye kama yeye na siyo asimuliwe tu na mtu. Kwa hiyo, mwangalie hili suala la kuwapatia hawa Maafisa Maendeleo Jamii wa Kata mafunzo. Pia niishauri Wizara, hawa Maafisa wanafanya kazi nzuri sana, na kama tutaangalia ustawi wa kwao kwanza watafanya kazi vizuri zaidi. Waangalie mpango mzuri wa motisha ili kuwa-*motivate* hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afisa Maendeleo ya Jamii yeye mwenyewe simu kafunga na *rubber band*, anamweleza vipi mtu kuhusu maendeleo wakati yeye mwenyewe hana maendeleo. Kwa hiyo, mwaangalie vizuri hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii ya Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, kumekuwa na *ideology* kwamba hii mikopo ya halmashauri, tuna halmashauri hii mikopo ya 10%, haitoshi. Sasa kuna muda pale mikopo ndiyo imeshaisha, huu mzigo wote anaubeba Afisa Maendeleo ya Jamii. Yaani anashindwa hata kunywa soda yake hadharani, watu wanajua huyu ndiyo kasababisha sisi tunakosa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge, wenzangu, tunaomba tushirikiane na hawa watu kwenye suala hili, tushirikiane katika kuwaelimisha watu, tusiwaache hawa watu wana-*hang* wenyewe, kwa sababu hawa watu wanatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba kwa leo niishie hapo na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Kombani.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na kumalizia kazi yetu, ninaomba niwatangaze wageni ambao wapo mchana huu.

Tunao wageni ambao wamekaa kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika, wageni wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Tunaye Ndugu Jane Sembuche, Mkurugenzi Shirika la *Plan International*; Ndugu Mwajuma Noty, Katibu Mkuu Jukwaa la Wanawake katika uongozi; Ndugu Sharifa Nabalang'anya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo; Ndugu Lediana Mng'ong'o, Mbunge na Mwenyekiti wa Bunge Mstaafu, na Mkurugenzi Mtendaji wa *NGO TAHEA*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni Menejimenti ya Wizara na taaasisi zake. Menejimenti ya Wizara na taasisi zake karibuni. *(Makofi)*

Taasisi ya wanawake iliyogombea uongozi Tanzania Bara na Visiwani *(Women Leadership Forum)*, karibuni sana. *(Makofi)*

Wadau wa maendeleo na mashirika yasiyo ya Kiserikali, karibuni sana wadau wetu. *(Makofi)*

Wawakilishi kutoka taasisi za kifedha; *NMB*, *AZANIA*, *TCB* na Benki ya *EXIM*, karibuni sana wadau wetu wa fedha. *(Makofi)*

Vilevile, tuna Mabaraza ya watoto Tanzania; Umoja wa wamiliki Makao ya Watoto Tanzania; Chama cha Wataalamu wa Ustawi wa Jamii Tanzania *(TASO);* Chama cha Wagumba Wanawake na Wanaume Tanzania; na Chama cha Wazee Wanaume Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, vipo Vyama vya makundi maalumu; Jukwaa la Wanawake katika Uongozi (LEMACHO, SUMAUJATA, SHIUMA); na

vyombo mbalimbali vya Habari, karibuni sana wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambaye Ndugu Kelvin Shishi Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mahundi ni familia yake kutoka Jijini Mbeya. Yupo Ndugu Johnson Luhenga, mtoto wa Naibu Waziri; Ndugu Rose Chale, dada wa Naibu Waziri; Ndugu John Mahundi, kaka wa Naibu Waziri; Ndugu Kelini Mahundi, mpwa wa Naibu Waziri; Ndugu Colin Mahundi, mpwa wa Naibu Waziri; Ndugu Erick Mahundi, mpwa wa Naibu Waziri. Karibuni sana Familia ya Mheshimiwa Maryprisca Mahundi. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, ni Chama cha Wanawake Wahandisi Tanzania *(IET)*, karibu sana. *(Makofi)*

Washirika wa Taasisi ya *Maryprisca Women Empowerment Foundation*, karibuni sana. *(Makofi)*

Baraza la Madiwani wa Halmashauri, karibuni sana. Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Chunya, karibuni sana. Kamati ya Ulinzi na Usalama kutoka Wilaya ya Chunya, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao Machifu wa Mkoa wa Mbeya, karibuni sana machifu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa CCM, anawatangazia Wabunge wote wanawake wa CCM kwamba kutakuwa na kikao kifupi na viongozi wa UWT Taifa mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge mchana saa saba. Kikao kitafanyika katika ukumbi wa Msekwa. Kila mmoja anayesikia tangazo hili, amwaarifu mwenzake.

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia na mchangiaji wetu Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Kiuhalisia mambo mengi sana yamezungumzwa hapa na mimi ninaungana na watu wote ambao wanampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuletea Waziri ambaye yupo *active*, ninamaanisha Mheshimiwa Dkt. Gwajima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema Waziri yupo *active,* tunajua watu wote sisi ni mashahidi kwamba jambo lolote likitokea linalohusu jamii yetu utamwona Mheshimiwa Dkt. Gwajima yupo *front* nalo, liwe kwenye mitandao ya kijamii, liwe ni jambo la mtaani, utaona yupo nalo. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa unayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia mambo machache sana kwa sababu mambo mengi yameshazungumzwa. La kwanza, nitaanza na 10% ya mikopo ambayo inatakiwa kutolewa kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba Serikali iliamua kupeleka mikopo kwenye benki ili kulinda fedha. Watu wengi walikuwa wanakopa na kuondoka na fedha bila kurudisha, lakini bado kumekuwa na changamoto kubwa kwenye elimu ya wajasiriamali wetu kuhusiana na namna ya kuzifuata hizo fedha katika taratibu za benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki ina taratibu zake za kulinda fedha, na wananchi wetu kuzifikia hizo taratibu imekuwa ni kazi ngumu sana. Hivi ninavyokwambia, Jimbo la Kigoma Mjini kuna makundi zaidi ya 25 yaliandikwa na yakafuata taratibu zote, tangu mwezi wa kwanza mpaka leo hii bado hawajapata fedha yoyote kwenye makundi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengine waliomba shilingi milioni tano halafu wakapewa shilingi laki tano. Hii tafsiri yake ni

kwamba hiyo fedha haiwezi kwenda kufanya hiyo biashara ambayo hicho kikundi au huyo mtu alikuwa amei-*target*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, aende *front* na watu wake, waambie benki hizi fedha ni za Serikali, hizi siyo fedha za benki, watu waweze kupewa fedha zao, waweze kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu wanaume. Wizara hii imejikita zaidi kwenye kutetea wanawake, lakini tunapozungumzia maendeleo ya jamii, tunazungumzia jamii nzima kwa ujumla tukiwemo wanaume. Sasa leo nitakwambia na ninaomba Mheshimiwa Waziri, afungue masikio asikie vituko tunavyofanyiwa wanaume na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu nyingi imekuwa ikitolewa hata kwenye vipindi vya redio. Ukisikia vipindi vya redio, elimu inayotoa ni kama vinawafundisha wanawake waende wakapambane na wanaume kwenye nyumba zao. Lazima mjue, wanaume wapo humu, ni mashahidi, wanaume tunaoa wanawake kwa namna ambavyo tunataka sisi, kwa sababu sisi hatuolewi, sisi tunaoa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwanaume anaoa mwanamke anayetaka; huyo mwanamke aajiriwe yeye afanye kazi na mwanamke afanye kazi. Kuna mwanaume hataki mke wake aajiriwe na bosi...

MHE. MARY F. MASANJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu anakuwa na wasiwasi kwamba...

MHE. MARY F. MASANJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Taarifa wangezisubiri kwa...

MHE. MARY F. MASANJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Mary Masanja.

TAARIFA

MHE. MARY F. MASANJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa mzungumzaji. Vivyo hivyo na wanawake hatuolewi tu hivi hivi, isipokuwa tunaolewa na mtu ambaye tumemhitaji. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, unaipokea hiyo taarifa?

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo ambayo ninaenda kuyazungumzia huko mbele. Kama mwanaume anaongea na wewe unaongea, tafsiri yake... *(Kicheko/Makofi)*

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uulinde muda wangu kwa sababu nina mengi ya kuongea.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uulinde muda wangu, taarifa zao zipokee, lakini ninaomba unilindie muda wangu.

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wawe wavumilivu, wakati wanaume tunasemwa huwa tunavumilia, na wao...

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: …wawe wavumilivu, wakati...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Ninaomba utulivu tafadhali. Waheshimiwa siwezi kumsikia anasema nini kama mtakuwa mnaongea.

Mheshimiwa ninaomba uendelee.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimesema mnaongea sana, sikusikia nini anasema. Kwa hiyo, hiyo taarifa unayoomba sijajua ni ya nini? Ninaomba aendelee kuongea ili niweze kuelewa. *(Makofi)*

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie ukweli, hasa Wabunge wanawake waliomo humu ndani. Jeshi kubwa ambalo limenipa mimi Ubunge mpaka kuja hapa ni jeshi la akina mama. Kwa hiyo, njia pekee ya kuwatetea wanawake ni kuwaambia ukweli pia, siyo kuwadanganya na kuwabebesha mzigo ambao kiuhalisia ungemwambia ukweli mwanamke angejua namna bora ya kuanza kujikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wanisikilize ili wajifunze, wajue ni yapi tunapitia sisi wanaume, na tunayoteswa na wanawake. Kwa hiyo, watulie wasikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee na unilindie muda wangu, mama yangu. Wakati unamtetea mwanamke kuhusiana na ukatili wa kijinsia, ni lazima na yeye mwenyewe umfundishe namna ya kutojiingiza kwenye ukatili wa kijinsia. Yapo mambo ambayo yanafanywa na wanawake yanawaingiza *automatically* kwenye ukatili wa kijinsia na nitayataja hapa na wao wanawake watakuwa mashahidi kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, huwezi kuwa umeishi na mwanamke ndani, anakusingizia ujauzito, unaulea

miezi tisa, anazaa mtoto, unamlea mtoto anafikisha miaka 10, baadaye mnagombana kidogo anakwambia hata huyu mtoto mwenyewe sio wako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo namna mwanaume yeyote anaweza ku-*react* katika hasira. Kuna namna kuna wanaume wanaweza wakavumilia hasira, na kuna wanaume wengine wakati wanapambana na hilo neno ulilomwambia unatokea ukatili wa kijinsia. Kwa hiyo, akina mama tuwe wa kweli. Kama mimba siyo ya mtum mwambie, usimbebeshe mzigo mwanaume ambao siyo wa kwake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanawake, wapo wakina mama amesomeshwa, mtu anahangaika ameacha kusomesha ndugu zake, wadogo zake, anamsomesha binti kwa kuamini kwamba atakuja kufunga naye ndoa ili waweze kuendesha familia. Akishamaliza kusoma anamwona yule mwanaume hafai, anamgeuka. Ukimgeuka huyu mtu, familia yake yote inamwambia, "tulikwambia." Mwisho wa siku haya matendo yanaleta hasira kali sana kwa wanaume. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaongelea hapa mwanaume kupigwa, kwamba wanaume wanapigwa na wake zao, hayo mambo ya wanaume kupigwa hiyo ni nguvu ya mwisho, huyo ni mlevi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwawezesha vizuri wanawake, kuna baadhi ya matendo ambayo wanayafanya ambayo utanitafsiria baadaye kama ni utapeli au ni wizi, yataondoka. Kwa mfano, mwanamke hampendi mtu kabisa, hampendi hata kidogo, lakini anakaa naye baa, amemwita kama mpenzi wamekaa. Anajua kabisa hampendi, lakini yupo anamdanganya. Anakunywa pombe zake, anakula vitu vyake, mwisho yule bwana anaenda *toilet,* anarudi, anamwona yule mwanamke anakimbia kwenye bajaji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yanatokea kwa sababu wanawake kuna vitu wanavifanya kwa sababu ya uchumi tu. Mwanamke mwenye uchumi hawezi kwenda kula vitu

vya mtu ambaye hampendi. Mheshimiwa Dkt. Gwajima wasaidie wanawake wawe na fedha ili kupunguza hivi vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaimba mpaka nyimbo. Mtu anajua kabisa huko sitaenda. Unamwambia bwana unakuja saa ngapi? Tukutane wapi? Mnakubaliana. Nitumie nauli, unatuma shilingi 50,000, anazima simu, anaku-*block*. Si wizi huo! Huo ni wizi, na wanatumia kawimbo cha Zuchu, "siendi, nauli yake nakula, nasema siendi." Huu ni wizi mama. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huwa watu wana namna ya kukabiliana na mwizi. Kuna mwingine unampeleka Polisi na wengine unasikiaga wananchi wenye hasira kali wamemchoma mwizi moto. Haya matendo yanatokea kwa namna nyingine ni kwa sababu kuna wanawake bado kipato chao kipo chini, kwa hiyo, katika utafutaji wake anafanya mambo ambayo kiuhalisia yamekaa kama ni utapeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya twende basi kwa wale wenye kipato sasa. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Gwajima, nimemwona mume wako hapa. Wakati ametambulishwa nimeona alivyosimama, tabasamu lake nilikuwa ninamwangalia usoni, linatoka moyoni, na wewe ni Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwanamke akishapata fedha anabadilika kwamba yeye ndio mwanaume kwenye nyumba. Anataka kumpeleka mwanaume na kumzalilisha, kumwonesha kwamba wewe sio lolote, sio chochote. Jamani, jamani, Mwenyezi Mungu ametuumba tofauti. Mwanaume ni mwanaume tu. Kuna muda ukifika uwe na fedha, usiwe nazo mheshimu mume wako. Kuna ubaya gani? *(Makofi)*

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya matendo ...

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Hawa bila kutulia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa endelea.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya matendo yanayotokea katika familia yetu, ndiyo maana leo nimemletea Mheshimiwa Dkt. Gwajima, kitabu hiki hapa. Hiki ni kitabu kimeandikwa na Mheshimiwa Dkt. Mlenga Omary, nilikizindua juzi Kigoma, kinaitwa "Vijue Vyanzo vya Migogoro katika Ndoa na Familia." Huyu mzee kaandika kila kitu humu ndani kwenye kitabu hiki. Ninaomba wataalamu wa Bunge mumkabidhi Mheshimiwa Waziri hiki kitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wake zetu wanafundishwa namna ya kuja kutushambulia ndani ya familia. Ukisikia vipindi vyote, mwanamke ambaye amekubali kwamba mimi mume wangu acha atafute, mimi acha nikae na watoto nilee Watoto, anaonekana ni mjinga kwenye Taifa hili. Wanamtangaza kama mjinga. Unakubalije kukaa nyumbani eeh! Mwanaume anachagua mwanamke anayemtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwanaume anachagua mwanamke anayefanya kazi, kuna mwanaume anachagua mwanamke anayefanya biashara, na kuna mwanaume anataka mwanamke ambaye atabaki nyumbani na watoto wakati yeye yupo kwenye mapambano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa elimu nyingi zinatolewa kwenye vipindi vya redio, ni elimu ambazo zinamwonesha mwanamke kwamba lazima utoke. Sasa wakati anaanzisha vita ya kutoka kwenye familia ambayo mwanaume alioa mwanamke

ambaye atakaa nyumbani na familia, ndiyo hapo heka heka zinaanza kutokea, lakini manyanyaso wanayoyapitia wanaume ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Dkt. Gwajima atutengenezee *system*. Ndiyo maana umeona vinaanzishwa vyama sasa tujitetee wenyewe huko mitaani. Vyama vya wanaume, wazee wanaume, kwa sababu tumegundua mnatushambulia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mwanzo mwisho ni kutushambulia. Mimi nitakupa mfano mmoja. Unajenga nyumba ya ghorofa unampa hela mke wako kwamba simamia nyumba mimi ninapambana. Hakikisha nyumba inaisha ili tuweze kuishi na familia. Hela unazompa ananyofoa, anaenda kujenga na yeye kanyumba kake kadogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajenga nyumba ya familia ili muishi pamoja, yeye anatengeneza mazingira ya kujitegemea ndani ya ndoa, haiwezekani. Inakuwa ni kama familia mbili zipo ndani ya nyumba moja, haiwezekani. Unakuta bora hata ile nyumba ambayo anajenga basi ajiandike hata jina lake ili kwa namna moja au nyingine hata siku akifariki na mtoto wako ambaye umezaa naye aje arithi. Anaandika jina la mama yake. Mama yake akifariki wanarithi kaka zake, na ni hela zako, hela za watoto wako, haiwezekani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaunga mkono hoja, ninaomba sana Mheshimiwa Dkt. Gwajima, ukipata muda njoo Kigoma nikukutanishe na wakina mama wajasiriamali ambao wapo tayari kuwalea na kupambana na watoto pamoja na wanaume zao, lakini kwa heshima kubwa. Njoo nikupeleke Soko Marungu, kuna wakina mama zaidi ya 800; njoo nikupeleke Soko la kwa Noti kuna wakina mama zaidi ya 350; njoo nikupeleke Soko la kwa Kidala kuna wakina mama zaidi ya 300; njoo nikupeleke Soko la Gungu kuna wakina mama zaidi ya 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Dkt. Gwajima aje nimwoneshe wakina mama ambao wanajua maisha

na siyo haya mambo ya ujanja ujanja, anaitwa mwanamke anakuwa macho yapo juu juu tu muda wowote anaweza kunimaliza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabla sijamaliza, kuna wanawake wanatumwa. Hebu angalia hii hata ungekuwa kama mwanaume ni ukatili gani ambao ungeweza kuufanya? Kuna mwanamke anatumwa kwenda kumrekodi kiongozi hotelini, yupo utupu. Inawezekana kweli mimi nimeamua labda kuchepuka...

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuelewane vizuri. nimeamua kuchepuka, unaenda kwenye simu ya binti unakuta wakati unatoka kuoga unajifuta alikuwa anakurekodi, unaona kwenye simu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niambie ni tukio gani utalifanya? Waheshimiwa Wabunge, mniambie utachukua hiyo simu upeleke Polisi kwamba jamani huyu ananirekodi? Je, unawaamini Polisi kiasi gani? Waende wakaone hali yako uliyonayo? Au ni nini kitakachotokea? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana wakina mama, wakati tunawatetea kwenye suala la ukatili wa kijinsia, ninaomba na ninyi mjiondoe kwenye mazingira ya kupata huo ukatili. Nikikuta unanirekodi, nitakufanya nini? Nitakufanya kitu gani? Una roho gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, nina mengi, kwa sababu ninajua muda wetu umekwenda, lakini kwa leo ninaomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Gwajima, ninaunga mkono mama upewe fedha, lakini ninakukaribisha Kigoma, njoo Kigoma mama yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando. Ninakushukuru sana kwa mchango wako na kwa kupaza sauti kwa wanaume ambao pengine wanahisi wakisema ni aibu, lakini nikupongeze sana kwa ujasiri wako. Ninaamini wanawake wenye tabia hizo watajifunza, kwa sababu hatupo kwenye mapambano dhidi ya jinsia mbili, tupo kwenye

mapambano ya kuweka usawa baina ya jinsia zote mbili, na kuondoa mmomonyoko wa maadili.

Kwa hiyo, kama kuna vitendo vinafanywa na wanawake wenzangu wenye tabia hizo, ninafikiri ni wakati mzuri Mheshimiwa umezungumza kitu ambacho kitaweza kuifikia jamii, kwa sababu kesho, keshokutwa sisi wanawake tuna watoto wa kiume, wakienda kutendewa hivyo, sisi wazazi hatutaweza kuridhika. Ninakushukuru sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Kabla sijasitisha Shughuli za Bunge, nitataja wachangiaji ambao watachangia jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Amina Good Said, Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi, na Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.03 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Nilimtaja Mheshimiwa Amina Good Said

Mheshimiwa Charles Mhando Njama na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby ajiandae. Mheshimiwa Amina Good Said.

MHE. AMINA GOOD SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya na uzima na kuweza kusimama hapa mbele yako katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimshukuru kwa dhati ya moyo wangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa heshima kubwa aliyonipa yeye pamoja na vikao vyake vyote vya uteuzi na kunipa dhamana ya kugombea na hatimaye kuchaguliwa na kuwa Mbunge wa viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitakuwa mtovu wa fadhila nisipowashukuru wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuweza kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze katika hoja iliyopo Mezani ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba Waheshimiwa wenzangu wote tujue kwamba hiki tunachochangia humu ndani ni kitu ambacho kinagusa maisha yetu sisi wote. Tusiongee vitu kwa mihemko. Tusiongee vitu tunatolea mfano maisha yetu halisi, tutolee mfano wa vitu ambavyo vinaendelea sasa hivi katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu, sisi wote humu ndani tunakubali kwamba tumetokana na mama, lakini leo anasimama Mheshimiwa mmoja anakaa kumdhihaki mama. Kwa hilo kwa kweli tunamwomba sana, mihemko yake iishie huko huko. Hii siyo sehemu ya *kick*, wala siyo sehemu ya kutafuta mihemko. Hii ni sehemu ambayo tunachangia bajeti ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni kubwa. Bajeti hii imemgusa mwanamke, bajeti hii inamgusa mzee, vilevile bajeti hii inamgusa kijana na pia inamgusa mtoto. Kuna vitu vingi vya kuchangia vya mmomonyoko wa maadili. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu, tunapochangia bajeti hii twende kugusa kwenye vitu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba niweze kugusa kwenye suala la kuimarisha mafunzo ya ujasiriamali na matumizi ya teknolojia kwa wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana mama yangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima katika bajeti yake yote leo alioizungumzia hapa sijaona agusie Maafisa Maendeleo ya Jamii kugusa chini huku vijijini. Hali inazidi kuwa mbaya. Mmomonyoko wa maadili umezidi kuwa mkubwa sana. Mimi nina mifano michache katika mkoa wangu wa Dar es Salaam. Imefikia mahali tunaogopa hata kukaa na ndugu zetu, mzee wa miaka 80 ameenda kumbaka mtoto wa miaka nane, na mtoto huyu leo ndiye tunaenda kumzungumzia kwenye dira hii kumtengeneza na kumwandaa mpaka kufikia 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtoto huyu tunaenda kumwandaa nini kama tunaenda kumharibia maisha yake? Mtoto wa miaka nane akienda kufanyiwa vitendo vile vya ukatili haviwezi kutoka katika akili yake. Nimwombe sana mama yangu, Maafisa Maendeleo ya Jamii waweze kufika mpaka huko chini ili waweze kutusaidia, kwani hali siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ninaomba kuongezwe kwa vituo vya ushauri na msaada wa kisheria kwa wanawake na watoto wanaopitia ukatili ili haki zao ziweze kupatikana kwa haraka. Unakuta kesi ya ukatili wa mama au wa mtoto lakini kesi hiyo inachukua zaidi ya miaka mitano, miaka sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku jalada lake unaambiwa uchunguzi unaendelea. Ni uchunguzi gani unaoendelea ilhali kesi inaonekana iko wazi kabisa? Ninamwomba mama yangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, ninaujua uwezo wake,

ninajua tunashirikiana kwenye mengi sana kwenye suala hili la mmomonyoko wa maadili, ashirikiane na taasisi zisizokuwa za kiserikali, na wao pia wana mchango mkubwa ambao wanaweza wakasaidia kwenye suala hili la kuhakikisha mmomonyoko wa maadili unapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe pia Serikali yetu Sikivu, bajeti hii tuiongezee kutokana na hali ilivyo. Tuiongezee fedha ili fedha hizi ziweze kwenda kuongeza zaidi kuajiri Maafisa Maendeleo wa Jamii. Asilimia hii aliyosema ya kuajiri Maafisa Maendeleo wa Jamii 5,338 ninaona bado ni ndogo sana kutokana na hali ya mmomonyoko wa maadili ilivyo. Nimwombe sana mama yangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, ninaamini Serikali hii ni sikivu, tuongezewe bajeti kwenye hili suala, kwa sababu kila kukicha hali inazidi kuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa kuipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha sekta ya maendeleo ya jamii ambayo ndiyo msingi na ustawi wa familia, wanawake, vijana, na watoto nchini. Pia ninaomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, mama yangu, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima anajua biashara zetu wanawake, ni biashara ndogondogo tu, biashara ambayo haigharimu mtaji mkubwa sana, lakini leo kwenye mikopo hii ya 10% mnapokuwa vikundi unaambiwa ukaweke *collateral* ya nyumba. Mama anahitaji mtaji ambao ni wa shilingi 100,000 au shilingi 300,000, hii *collateral* ya nyumba anaenda kuitoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tutumie taasisi za Kiserikali na zisizokuwa za Kiserikali ambazo ziko *active,* hizi fedha ziweze kupitia kwao, ili waweze kuwasaidia hawa wanawake wa hali ya chini ili na wao waweze kukuza vipato vyao, kwa sababu ninaamini kabisa ukimwezesha mwanamke umeiwezesha jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pato la mwanamke huwa halina matawi kama la wenzetu akina baba. Mwanamke ukimwezesha pato lake linarudi ndani. Akina baba wana matawi mengi. Utakuta na nyumba tatu, nne tano. Leo wanajisifu na wana michepuko. Kwa hiyo, nimwombe mama yangu,

mwanamke huyu tumwangalie kwa jicho la huruma sana. Hii mikopo ya 10% ya kwenda kuweka dhamana ya nyumba kwa kweli tukae chini kwa mara nyingine tena tuiangalie na hicho kifungu kiangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Amina Good Said. Tulimtaja Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae.

Mheshimiwa Charles Mhando, hayupo; Mheshimiwa Ahmed Shabiby, hayupo; Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi, hayupo; Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia jioni ya leo kwenye hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ninaweza nikasema, kwamba hii ni Wizara ambayo ni muhimu kuliko Wizara nyingine zote kwa sababu, tunavyozungumzia ustawi wa jamii, huwezi kukwepa afya, huwezi kukwepa elimu, huwezi kukwepa miundombinu, na huwezi kukwepa ajira. Kwa hiyo hii ni Wizara ambayo mimi ninaitazama kwa jicho la kipekee zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwa ujumla wake kwa nini tuko hapa leo; yaani, ni kwa nini watu wote tunalalamika? Ni kwa nini watu wanalalamikia mambo ya elimu? Ni kwa nini watu wanalalamikia mambo ya unyanyasaji wa kijinsia? Ni kwa nini watu wanalalamika mmomonyoko wa maadili? Pia na mambo mengine kama ambavyo wenzangu wamechangia asubuhi, hasa wale wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiangalia matokeo zaidi badala ya kuangalia chanzo. Ukweli ni kwamba maisha yamekuwa magumu sana. Hakuna Mbunge anaweza

akasimama hapa kwa siku aniambie hajaombwa fedha na mwananchi wake, hayupo. Hakuna Mbunge anayeweza akasimama hapa akasema yeye hana changamoto ya kiuchumi. Basi, kama wapo hata 10% hawafiki. Tunashinda humu, licha ya kwamba sisi tunalipwa, lakini unaona binafsi bado *scarcity* ya maisha ni ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ambaye una kazi maalum kama hii, unaona kuna shida mahali, wimbi la *dependence* wanaokutegemea linazidi kuongezeka siku hadi siku. Sasa jibadilishe, nenda mtaani, *act* wewe ndiye uyeko mtaani, halafu hauna kazi, ndio unaweza kujua kwamba hali ipoje huko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia michango ya Waheshimiwa wenzangu, ninaiunga mkono yote. Hata hivyo, hebu tutafakari tunatokaje hapa tulipo? Bila kuumiza kichwa zaidi, ninaanza mfano kwenye *issue* ya elimu. Tanzania ni moja, Serikali ni moja, tuna mifumo ya elimu ya aina mbili. Mtoto wa Waziri, wa Mbunge anasoma *English Medium,* mfumo wa Kiingereza. Mtoto wa mama ntilie anasoma kwenye shule ya msingi ambao mfumo ni wa Kiswahili. Tunatarajia wakimaliza wakashindane kwenye soko kwenye *interview* moja mlango mmoja, kwenye *interview* moja mlango mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu kama hivi muhimu hatuzungumzi hapa. Huyo huyo mwananchi wa kawaida leo hii imesemwa kuwa wana mikopo ya 10% ndiyo, wamesema kuna shilingi bilioni 18 zimeweka *NMB* ndiyo. Ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, kinachoendelea huko *NMB* na huko kwenye 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnasajili vitambulisho *special* ambavyo mnasema ndio kitamsaidia mtu kupata mkopo. Ukienda benki huyu kijana mnayetaka mbadilishe maisha yake ili asiandamane, ukienda benki unadaiwa *TIN* namba, kitambulisho, *tax clearance* na leseni ya biashara. Huyu ambaye mnataka ndio aache kuandamana akajitegemee awaletee hivyo vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba moja, ukienda mikopo ya Halmashauri ya Mji ya Miji hii ya akina mama na vijana na watu wenye ulemavu, zile fedha licha ya kwamba masharti ni mengi, andiko la mradi, sijui Katiba, sijui nini, vikorokoro vingi ambavyo vinahitaji lazima umfuate mtu ambaye ana elimu ya *IT* akutengenezee hivyo vitu vyote. Licha ya kwamba kuna watu wamepambana kukidhi vile vigezo, fedha zile hazitolewi, hata kama umekamilisha vigezo vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyojua mimi, mwongozo unataka zile fedha zitolewe kila baada ya miezi mitatu na wenye taarifa ni wachache. Yaani wale wananchi hawapewi utaratibu kwamba hizi fedha ziko moja, mbili, tatu. Wewe Juma, John mtapata mwezi wa Pili, wewe Anna, Neema mtapata mwezi wa Tisa, huo utaratibu haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapata taabu kuulizia. Walisema, walisema, yaani hakuna *straight forward* kwamba hili jambo robo tatu ya mwezi huu kata fulani labda au vikundi fulani vitapata, haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba fedha leo. Umekamilisha *document* zote, unakuja kupata fedha mwakani. Kikundi kiliomba shilingi milioni 50, wanakuja kupata shilingi milioni tatu, na wameandika na andiko. Huo mchakato mzima ili ukamilishe *document* zote ambazo zinahitajika ni lazima shilingi laki tano, laki sita, laki nne na nusu utumie. Labda kama wakili ni mpenzi wako, maana yule anaweza akakugongea bure muhuri na katiba akakutengenezea bure. Huo ndiyo ukweli. Tuambizane ukweli. Huyu ambaye wanataka asiandamane, anatokaje kwenye mazingira kama hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Bandari ya Tanzania inapelekwa kwa mwekezaji, Serikali ilikuja na lugha kwamba hii ya kusimamia wenyewe imetuletea hasara sana. Sasa tumepata mwekezaji kwa sababu kabla ya mwekezaji tulishindwa kuiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa mtu namba moja nilifanya *press,* lakini waliuaminisha umma kwamba kwa kukodisha bandari kuna fedha nyingi tutaziokoa. Bahati nzuri nimeshiriki Wizara zote hapa. Kila Wizara inalalamika bajeti ndogo. Kila Wizara inalalamika bajeti ndogo. *What's the difference?* Utofauti wa kipindi tunaiendesha bandari yetu na kipindi ambacho tumekodisha, uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ugumu wa maisha waliosema kwamba tutapunguza baadhi ya gharama, uko wapi? Ninaenda kwenye kitabu ambacho Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilihutubia Bunge ukurasa namba 10. Alisema, "kuelekea matamanio ya wananchi ya kupata Serikali inayoshughulikia changamoto zao kama vile suala zima la gharama za maisha, kuongeza fursa za kazi na ajira ili waweze kujiendeleza kiuchumi na kuimarisha ustawi wa jamii zetu. Ninataka niwahakikishie kwamba Serikali itachochea upatikanaji wa fursa za kiuchumi na kujenga matumaini kwa vijana, wanawake na makundi yenye ulemavu." *The statement is too clear*.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, kuna taarifa ya Mheshimiwa Ulega.

TAARIFA

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Sigrada, unaohusu hotuba iliyopo Mezani ya Maendeleo ya Jamii ambayo ameihusianisha moja kwa moja na *performance* ya bandari yetu na kwamba Serikali ni kama iliwadanganya wananchi, ninaomba nimpe taarifa kwamba *performance* ya Bandari ya Dar es Salaam siyo jambo la kujificha, ni jambo la hadharani, kwamba tulichokisema ni ufanisi:-

(i) Meli itakapokuja kutoka nje, itakaa kwa muda gani?
(ii) Kasha litatolewa kwa muda gani?

(iii) Mapato ya bandari yatakuwa ni kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Sigrada, pamoja na lengo lake jema la kutaka kuona namna ambavyo mchango wa bandari kwenye pato la Taifa na mchango wa bandari kwenye pato la wananchi, mimi ningetamani sana, ikiwezekana nitakuwa tayari kumsaidia kumwonesha namna ya *performance* ya bandari ilivyochangia kwenye pato la Taifa letu na mchango wa mabadiliko ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukifika leo Dar es Salaam utaona namna ambavyo ongezeko la watu waliopata ajira, *either* ya moja kwa moja au iliyotokana na hizi *performance* za bandari. Kwa hiyo, mchango wake huu mzuri anaoutoa wa kuchangia namna ambavyo jamii yetu isiathirike na maadili na kadhalika, asiupotoshee katika *performance* ya bandari yetu na ahadi ya Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, unaipokea hiyo taarifa?

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kupokea hiyo taarifa kwa sababu, mzungumzaji yeye yupo kwenye mfumo, anajua. Mimi niko kwa wananchi, sijawahi kuingia kwenye huo mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, sijaona mpaka sasa hivi utofauti wa maisha kati ya kipindi tunaiendesha wenyewe na kipindi ambacho tumekodisha. Mimi nimeagiza gari juzi, wameingiza kodi inaitwa ukarabati wa bandari. Kuna maeneo yale ambayo tulibaki nayo sisi, sasa yanatakiwa yakarabatiwe magati sijui matatu. Kama mimi mwongo, nina *document* zenu hapa zote. Mmeingiza ambapo mtu ananunua gari, maana yake nini? Maana yake hapo umemkata kodi mama yangu, bibi yangu, shemeji yangu, hiyo gari si wanaenda kutumia wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *let us talk the truth,* mmeshindwa hata kurekebisha bandari kipande ambacho mmebaki nacho ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mbele. Mimi hoja yangu ilikuwa ni kwamba, sisi kama Wabunge, sisi kama Mawaziri, tuna-*reflect* alichosema Samia kwenye ukurasa wa 10 wa kitabu chake? Maendeleo hayapimwi kwa magari, au sijui *V8* au sijui barabara. Samia amesema, anataka maendeleo yapimwe kwa mtu mmoja mmoja, maisha ya mtu mmoja mmoja…

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu, kanuni gani imevunjwa?

KUHUSU UTARATIBU

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama kwa Kanuni ya 79, namna ya kum-*address* Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Mbunge anavyosema Samia amefanya au amesema, kwenye *Hansard* itashindwa kujua anayekuwa *addressed* ni Samia yupi? Ni vizuri anapo-*address* jina la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizungumze kwa ukamilifu wake ili kuweza kuweka taarifa vizuri kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sigrada ni kwa mujibu wa utaratibu utaje jina la Rais kwa urefu wake.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kitabu chake ukurasa namba 10 alionesha nia yake, licha ya maendeleo ya

majengo na barabara na vitu vingine alitamani tuhame, twende kwenye maisha ya kijamii ya mtu mmoja mmoja ikiwemo kubadilisha ugumu wa maisha. Je, Serikali hii *inareflect* hiki alichokiongea Mheshimiwa Rais? *That is my point.*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Hiyo ni kengele ya kwanza nakumbuka, mmemaliza muda wangu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea na hoja nyingine. Kuna watu wenye ulemavu kwenye hii Wizara. Tarehe 1 Januari, mwaka huu nilijaribu kukusanya walemavu wa Mkoa wa Njombe. Nikasema hebu nijifunze nile nao mwaka mpya, nikaita walemavu wote, nikafanya *party* fupi pale *Agreement Hotel*…

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, muda wako ulikuwa umekwisha, nimekuachia umalizie. Kwa hiyo, sitatoa nafasi ya taarifa. Mheshimiwa Sigrada malizia.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niliwaita, nilivyowaita nikataka kujua hawa watu wamewahi kufikiwa? Waliongea kwenye vyombo vya habari na mpaka leo zile *speech* zao zipo, wanasema toka dunia iumbwe hawajawahi kufikiwa, walemavu wote Mkoa wa Njombe. Sensa ya 2022 ilionesha Mkoa wa Njombe pekee yake tuna walemavu 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapozungumzia hii Wizara, ninatamani hebu tupanue akili, yaani twende mbali zaidi. Huyu mtu anayeandamana, yaani kwa nini anaandamana? Halafu mnasema, ninakumbuka *IGP* siku ya maandamano alisema, saa 48 ninataka watu wote wakae ndani. Wale vijana wanakaa ndani; hawana ndani. Wewe ndio una ndani kwa sababu, umezaliwa, umeona baba, mama, umeona nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana wengi ambao wako mtaani, ambao tusipokaa vizuri yale maandamano ya tarehe 29

mwezi wa 10 yatakuja kuwa mara 800. Hapa si tunataka kupongezana? Hatutaki kwenda kwenye uhalisia huko *ground*. Yale maandamano tusipoweka msingi mzuri yatarudia.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sigrada. Mheshimiwa Sigrada umeeleweka, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila ajiandae.

MHE. ASMA ALI MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii siku hii ya leo na mimi niweze kuchangia mada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipa nafasi, uwezo na afya ya kusimama hapa na kuweza kuchangia mada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue fursa hii kukushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi, lakini aidha nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar kwa kazi nzuri ya kuweza kusimamia ustawi wa jamii, maendeleo ya watu pamoja na kujumuisha makundi mbalimbali katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue fursa hii kumpongeza kwa kazi nzuri ambayo anaifanya Waziri, Mama Gwajima. Mimi ni mmoja wa watu wanaopenda kazi zake anazozifanya. Kwa kweli anafanya kazi nzuri, Mwenyezi Mungu ambariki na ampe nguvu kuendelea kufanya kazi nzuri ambazo anazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia katika mada ambayo nilikuwa nataka kuunga siku hii ya leo, ninaomba na niongee maneno machache kuhusu mada ambayo ilikuwa inaongelewa leo asubuhi, ambayo ni udhalilishaji wa kijinsia. Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ningeomba neno moja dogo. Wanaobaka

watoto wa kike pamoja na wa kiume wahasiwe hadharani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninaomba kuchukua fursa hii kujikita katika mada ambayo nilikuwa nataka kuiongelea. Katika jamii yetu mara nyingi kuna jamii ambayo husahauliwa. Nao sio wengine, kwa jina la kitaalamu ni jamii wanaoishi na *autism,* kwa Kiswahili inajulikana kama usonji na *down syndrome*. Kwa Kiswahili inajulikana kama *uso mfanano,* kwa kule visiwani wanaitumia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumeona ni *group* ambalo mara nyingi sana watu huwa wanalisahau na huwa hawawakilishwi kikamilifu katika mijadala ya kijamii. Hivyo, ninapenda kusimama siku ya leo na kuweka hadharani, kwa kuwa kuna uelewa mdogo ndani ya nchi yetu kutokana na hali hizi mbili za *autism* na *down syndrome* bado watu hawaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuweka hadharani katika Bunge lako Tukufu kuwa *autism* na *down syndrome* siyo afya ya akili, bali ni hali ya ukuaji mdogo tokea awali toka wakiwa watoto. Kutokana na huu upotofu ambao watu wako nao, afya ya akili au kutokufahamu kabisa imepelekea kuwa, jumuiya hii wanakuwa watu wanawanyanyapaa, wazazi kuwaficha watoto wao kiasi cha kwamba pia watoto wanakosa kufanyiwa ukaguzi wa awali na kupata matibabu yanayostahiki kwa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, imeendelea kuonekana kiasi cha kwamba hata kule kupata elimu inayotakiwa wao, hawapati wapate kutokana na miundombinu ya nchi ambayo bado haijasimama imara na kuwa sawasawa ili kuweza kupata haki yao hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni Watanzania wenzetu, wana ndoto, wana uwezo na wana haki ya kuishi kwa heshima kama Watanzania wengine wote.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ASMA ALI MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele yangu imelia, ninaomba uniruhusu niweze kutoa mapendekezo kwa Serikali nikiwa nimeyasoma ili niende kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kwanza, ninaomba Serikali iondoe upungufu mkubwa wa wataalamu wa afya na maendeleo ya watoto wakiwemo madaktari bingwa, wataalamu wa *speech therapy* na *occupational therapy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda kushauri Serikali kuimarisha huduma za uchunguzi wa mapema katika hospitali na vituo vya afya hasa kwenye kliniki za watoto, ili watoto waweze kugundulika mapema na kupata msaada unaostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuongeza mafunzo kwa walimu wa elimu maalumu na kuhakikisha shule zetu zinakuwa rafiki kwa watoto wenye mahitaji haya maalum. Elimu jumuishi siyo anasa, ni haki ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuangalia namna ya kuisaidia familia na walezi ambao mara nyingi hubeba mzigo mkubwa wa malezi bila msaada wa kitaalamu wa kutosha wala wa kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuanza kuweka mikakati ya kuwaandalia vijana hawa maisha ya baadaye, kupitia mifumo ya ufundi stadi ya maisha na fursa za ajira kulingana na uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninapenda kusema wazi kuwa watoto wenye *autism,* usonji, na *down syndrome* (uso mfanano) siyo mzigo kwa Taifa. Ni sehemu ya Taifa letu na wanahitaji nafasi, uelewa na mifumo bora ya kuwawezesha kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Asma Mwinyi. nilimtaja Mheshimiwa Fadhili Liwaka, Mheshimiwa Neema Mwandabila ajiandae.

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa rehema hii kubwa ya afya na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Gwajima pamoja na Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Maryprisca kwa kazi kubwa ya ku-*transform* Wizara hii, kutoka kuwa Wizara inayokwenda kujadili na kuhusika na mambo yaliyojificha na kuwa Wizara ya jamii inayogusa changamoto, inayounganisha Wizara nyingi zaidi na kuwa Wizara ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furaha kwa sababu, sisi kwenye Bunge letu hili tumepata bahati ya kuwa na vijana wengi sana ambao somo la maendeleo ya jamii, mmomonyoko wa maadili, umoja na mshikamano ndiyo sehemu ya *syllabus* pekee tunayopaswa kuisikia kila wakati. Nilikuwa nafanya utafiti kuona Bunge letu kama tukihesabu idadi ya vijana wenye umri chini ya miaka 45 tunaweza kufika wangapi, nikapata idadi isiyopungua Wabunge 103 ambao ni chini ya umri wa miaka 45. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni tafsiri kubwa ya mabadiliko makubwa ya kimfumo na namna ambavyo Taifa letu limeendelea kuwaamini vijana, kuwakuza na kuwaimarisha. Tunajivunia sana jitihada za Rais wetu katika kujenga imani hiyo, na kwa vyovyote vile dunia itakavyokuwa iwe jua limezama, maji yamekupwa na mvua inanyesha tutaendelea kumwombea kwa Mungu kwa sababu ametuthamini na sisi tunamthamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la malezi. Suala malezi ndiyo jambo ambalo sisi Watanzania leo tuko hapa tunazungumza kwa lugha tofauti tofauti za uchungu. Hata hivyo, ninataka niweke sawasawa kabisa mtazamo wangu juu ya namna tunavyoweza kuyapokea mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu, na Wabunge wenzangu ninataka wafahamu jambo moja. Leo ukinipa Wabunge 10 humu ndani uniambie mchague Mbunge

unayempenda sana, Mheshimiwa Sigrada atakuwa namba moja, mbili na namba tatu. Upendo wangu kwake hauna kipimo, kaka yake Ado Shaibu anajua, na hata Mwenyekiti wake wa chama anajua kuwa ninampenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nilikuwa nina jambo moja na hii wakati ninaelekea kwa sababu ni Wizara inayozungumzia masuala ya maadili na mmomonyoko wa maadili yenyewe, ni dhahiri hatuwezi kuondoka bila sisi vijana kukubali kujifundisha kwenye msingi wa jambo tunalolitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani kwenye hili jengo, wako Wabunge wa Walio Wachache wamewahi kupita na wakajenga historia yenye mashiko na mafanikio makubwa. Ukiridhia bila kumpa maumivu rafiki yangu Sigrada, Mheshimiwa Mbunge nitawataja wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge alikuwa anakaa kwenye kiti hicho anaitwa Mheshimiwa Halima James Mdee, kuna Mbunge alikuwa anakaa pembeni yako kwa Mheshimiwa Ado Shaibu anaitwa Mheshimiwa Kunti Majala, kuna Mbunge alikuwa anakaa hapo pembeni anaitwa Mheshimiwa Esther Matiko, kuna Mbunge alikuwa anakaa hapo nyuma anaitwa Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Naibu Waziri; na kuna Mbunge alikuwa anakaa huko pembeni kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Afya anaitwa Mheshimiwa Mama Kaboyoka mtaalamu wa hesabu na Mwenyekiti wa Kamati nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wote wameacha alama ambayo leo Tanzania tukiizungumza mnajua tuliwahi kupita na Walio Wachache, wenye hoja. Sababu ni nini? Leo ninataka nitoe msaada wa bure kabisa; walichagua kujenga hoja ili kutengeneza rekodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, mimi najua nia njema ya rafiki yangu, na dada yangu Mheshimiwa Sigrada ni kutengeneza rekodi. Sasa leo ninataka nimshauri achague njia mbili kati ya hizi nitakazomtajia. Moja, asome, ajifunze, akubali hoja na akubali

kwamba ni lazima tumsikilize kwa mashiko na upendo kama anavyofanya Mheshimiwa Ado Shaibu katika hoja zake…

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya pili, achague kutengeneza hoja zake katika mfumo wa mihemko na kuwa kituko ndani ya Bunge…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Liwaka kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Sigrada.

TAARIFA

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Liwaka anazunguka sana kuhusu Sigrada, lakini sisi tuna *personal issues* zetu. Kwa hiyo, asichanganye kuchangia mchango na mambo yetu binafsi, namba nilishampa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie, namba nilishampa, lakini hajawahi kunitafuta, ahsante. *(Kicheko/Makofi))*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Liwaka unaipokea hiyo taarifa?

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa, nimeikubali na ninataka nikihakikishie Kiti chako kwamba na hili ndiyo moja ya udhaifu wa mambo ambayo tunashauriana kwenye *personal issues,* lakini hasikii akija kwenye kadamnasi. Hapo tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa nini nimesema haya? Malengo yangu ni kujenga kwa sababu Mheshimiwa Sigrada anabeba taswira ya wanawake na vijana wengi huko nje watakaokuja humu ndani siku moja siyo kupitia Chama cha Mapinduzi pekee, bali chama chake na vyama vingine. Wakiona mfumo wa kuendesha Bunge na kuwa upande wa Walio Wachache Bungeni ni lazima ujenge ukuta wa hoja, basi

hatutajenga Taifa, tutatengeneza mpasuko utakaotufanya tusifanye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, leo Mheshimiwa Sigrada amemtaja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jina lake, "Samia". Jina ambalo mtoto wa Mbunge mwenzangu amezaliwa juzi ameitwa pale hospitali ya Mwananyamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yangu ni nini? Akiachilia mbali Kiti cha Urais na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, huyu ni mama yake. Huyu anaweza kuwa bibi yake. Nilikuwa na lengo moja tu zuri kwa Wabunge wenzangu na Watanzania... *(Makofi)*

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Liwaka, endelea.

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ndiyo inavyokuwa, inanoga eeh? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nami lengo langu hapa ni moja, kwamba vijana wa Kitanzania, leo tunapozungumza kuhusu maadili, tunapozungumza umoja wa Kitaifa, tunapozungumza kuhusu maendeleo ya jamii, ni pamoja na kutambua namna ya vijana na Watanzania kuzijua ajenda za kujadili ili kujenga umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa, tunazungumzia makuzi ya watoto wetu. Tunazungumza mifumo ya ufundishaji shuleni, na tunazungumza namna ya kuenenda katika kutatua changamoto kupitia misingi ya maendeleo ya jamii. Hatuwezi kuacha nyuma ukweli kwamba, ili umoja wa Kitaifa uweze kwenda mbele, lazima tudhibiti maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hatuwezi kukwepa kwamba ili watoto wetu wakute alama njema, lazima wakute umoja wa Kitaifa. Pia ili tuweze kuyakuza maadili tunayoyataka, tusifanane

na watu wengine, lazima hoja zetu zijikite kwenye kuivusha Tanzania inayozungumza lugha moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati tunazungumza kwenye hotuba ya Waziri wa Michezo, tulisema, tunahitaji lugha. Siyo tulihitaji lugha ili tutamke maneno ya Kiswahili na Kiingereza, tulihitaji lugha ili tuwe na tafsiri inayoendana kwenye maana. Nami ombi langu, Waheshimiwa Wabunge leo wamezungumza vizuri hapa kwamba tuna wajibu mmoja tu wa kutotengeneza alama au kuacha vivuli vya watoto wetu kuishi maisha magumu. Watu watakaofanya hiyo kazi ni sisi Wabunge na Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya malezi haiwezi kukwepeka, hoja ya umoja wa Kitaifa haiwezi kukwepeka, hoja ya maadili yetu kuanzia katika namna tunavyoendesha shughuli zetu kiuongozi na namna tunavyoenenda, lazima tuizingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja. Humu ndani kila Mbunge ametokana na chama chake cha siasa. Sisi Chama cha Mapinduzi tunayo maadili, malezi, misingi, na tanuri la kutupika. Huu ni ushauri wangu, na usibebwe kwa chuki. Kila chama cha kisiasa, kabla hakijakubali kuleta Mbunge humu ndani, lazima apimwe kwenye misingi ya kimaadili, malezi yake, mapito yake na lugha zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni moja tu, leo hii humu ndani tunaweza kupata mwakilishi kutoka chama chochote kwenda kutuwakilisha nje. Tukipata watu wa aina ya Mheshimiwa Sigrada kwenda kuongea haya huko Marekani, tumekwisha. *We are total finished. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Liwaka, ahsante sana. Hiyo ni Sheria ya Vyama vya Siasa, Kifungu namba Sita. Kwa hiyo, uko sahihi, kila kiongozi anayetakiwa kuja, awe na maadili kwa Kifungu cha Sita.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Hawa Chakoma, Mheshimiwa Janeth Mahawanga ajiandae.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, niendelee tu kuwashukuru wote ambao wameweza kutupa burudani na kutufurahisha leo. Ninadhani kila Mbunge leo anayo sababu ya kusema amefurahi na amecheka. Kama kucheka ni kuongeza siku za kuishi, basi wengi leo wameongeza siku za kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tu kusema ninashukuru kupata nafasi ya kuchangia jioni hii, hasa katika Wizara hii ya dada zangu wazuri wote wawili; dada yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima na dada yangu Mheshimiwa *Engineer* Mahundi. Ninamshukuru Mungu kwa kuwa ninafahamu ni watu wenye uwezo mzuri na wana uwezo mzuri wa kuweza kupunguza changamoto zetu kama Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu masikitiko yangu ya wazi kwamba katika Wizara haitendewi haki, ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Ninayasema haya kwa kuwa ni Wizara inayopata fedha ndogo kuliko Wizara zote, lakini ndiyo Wizara yenye majukumu makubwa kuliko Wizara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukaongelea shilingi bilioni 79 kwa Wizara, halafu tukae kama Wabunge tunafurahia kwamba hii ni fedha ya kuiongoza Wizara iweze kufanya kazi, itusaidie kupunguza matatizo yetu yote yaliyopo kwenye jamii kama tunavyoona. Tunaongea sijui ubakaji, ni wao; tukiongea sijui kwenda kuhamasisha maendeleo, ni wao; tukiongelea ukatili wa aina mbalimbali, ni wao. Sidhani kama hizi kazi zinaweza kufanyika kama hawatapewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasilishe ombi langu maalum kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake. Hebu waangalie namna ya kuwaongezea fedha watu hawa. Watu hawa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu. Ni kweli keki ni ndogo, lakini keki ya shilingi milioni 79 na watu wengine wanapata trilioni, kuna uwiano hapo? Kazi tunazoenda kufanya zote ni za Watanzania. Tunapoongelea Wizara nyingine kushirikiana na maendeleo ya jamii, basi wangekuwa hata wanagawa fungu wanawapelekea maendeleo ya jamii wafanye kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo kwenye maeneo yetu wanateseka. Ndiyo idara ambayo inaishi kinyonge, ndio idara ambayo kule chini wanaogopa hata kujadili ujenzi wa nyumba za watumishi wao kwenye kata, ndio Wizara ambayo watu wao hawana hata pikipiki. Afadhali wenzetu wa kilimo waliweza kufanikiwa kupata pikipiki. Hawawezi kwenda *site* kama tunavyotarajia. Changamoto zinatokea hawawezi kufika *on time* kwenye matatizo. Kwa hiyo, ninaomba tu Waziri Mkuu atusaidie kuongeza fedha kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kupitia Bunge hili wawapatie pikipiki Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo kule kwenye ngazi za kata. Ninatambua kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii; nami ninapenda kuwataja wote japokuwa kwenye takwimu leo humu nimeona ya Maafisa Maendeleo ya Jamii tu, kwamba ndiyo, wameajiri, wamefikia 89%. Nimetafuta ya Ustawi sijaipata, labda huenda macho yangu yalikuwa hayako vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Maafisa Ustawi wa Jamii na Maafisa Maendeleo ya Jamii hawatoshi kwenye maeneo yetu. Hivi ninavyoongea kwenye Mkoa wangu wa Songwe, ninafahamu kuna baadhi ya kata hazina Maafisa Maendeleo ya Jamii. Sasa zile changamoto tunazosema watu wa maendeleo ya jamii watatue kwenye hizo kata, ni nani atafanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afisa Wilaya wa Maendeleo ya Jamii hana gari, na Afisa wa Mkoa hana gari. Yaani Kitengo cha *TASAF* kinaweza kuwa na gari, lakini idara kamili haina gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vitu kama hivyo pia tuombe Waziri Mkuu atusaidie, kwa sababu tunajua yeye ndiye mwezeshaji wa hawa Mawaziri wetu. Maafisa Maendeleo ya Jamii wapate magari ili waweze kutuhudumia na kufika kwenye changamoto zetu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa kuongelea, Maafisa Maendeleo ya Jamii ifikie hatua nao waanze kuwa na mikakati ya kuwajengea watumishi nyumba kama wanavyojengewa walimu na watumishi wa afya; na wao kazi wanayofanya kule ni ngumu. Tena unakuta mtumishi wa afya ana kipato kikubwa kuliko Afisa Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, wao pia kama watumishi wa Taifa hili, hoja ya ujenzi wa nyumba ionekane kwenye bajeti zao. Watumishi wote katika Taifa hili wana haki sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ninatamani kuchangia jioni hii, kuna mikopo ambayo imepelekwa NMB. Ushauri wa wadau kule chini wanasema hizi fedha kungekuwa na *distribution* kwenye benki zaidi ya moja. Halafu wawekee *target* ya utoaji wa hizo fedha ili wananchi waweze kupata hizo fedha, kwa sababu imeonekana waliopewa hawa, hiyo benki moja waliyopewa, wame-*relax*. Hawajitumi kuweza kutoa hizo fedha kwa sababu wananchi hawana pengine kwa kukimbilia, watakuja tu na masharti mengine ni magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nina wazo. Kwa kuwa tunafahamu vijana wengi hawana mitaji, tutengeneze fedha ya kuwafundisha *starting point* ya ufanyaji wa biashara. Ili tunapokuja kuwakopesha, hizi walizofundishiwa kutengeneza biashara, iwe kama sehemu yao ya kianzio. Kijana hajawahi kufanya biashara, tunataka aende kukopa moja kwa moja, huku tukimtaka awe na uzoefu wa biashara, atajifunza na nini? Kwa hiyo, hilo nalo lilikuwa ni ombi langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, tunawaomba vitambulisho hivi vya machinga vinavyovyotolewa, wavishushe kwenye ngazi za mikoa. Hebu fikirieni, tumeweza kusajili watu 56,000 tu. Taifa hili lina Watanzania wangapi? Taifa hili lina wamachinga wangapi? Tunaomba vitambulisho vishushwe kwenye ngazi za mikoa ili watu wapate huduma kwa wakati. Wanashindwa kupata huduma zile kwa sababu vitambulisho haviendi kwa wakati na hatuwezi kuwafikia wananchi wote kuweza kutoa hiyo huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mikopo hawapati kwa sababu ya hizo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia kitu kidogo tu. Nilikuwa ninaishauri Wizara, kwa kuwa ina shida ya fedha, Kituo cha Kurasini pale kimeshapoteza hadhi ya kuendelea kuwahudumia watoto. Wauze lile eneo wakajenge sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashauri tu kwa nia njema, kwa sababu kule bandarini tena eti wanaendelea kulelea watoto. Kumechafuka, yaani uchafuzi wa mazingira ni mkubwa. Kuna maeneo bado ni mazuri mengi eneo la Dar es Salaam kule. Wakauze lile eneo, wajenge sehemu nyingine, watoto wakae kwenye mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tujali muda, kwa sababu wachangiaji ni wengi. Ninajua mna mengi ya kuongea, lakini jitahidini kupunguza, kengele ya pili ikilia ili mwingine aweze kuchangia. Tunaendelea na Mheshimiwa...

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mwongozo.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mwongozo.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninasimama kwa Kanuni Na. 79 inayohusu Mwongozo wa Spika au Mwongozo wa Mwenyekiti. Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nachingwea, ambaye ni Mheshimiwa Liwaka, wakati anamalizia mchango wake, amezungumza kuwa "na Wabunge kama Sigrada ambao hawana maadili." Nilikuwa ninaomba Mwongozo wako kuhusu *statement* yake ya mwisho, kuhusu mimi kutokuwa na maadili. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Sigrada, amesimama kwa Mwongozo, Kanuni Na. 79 ambayo inamtaka au inamruhusu kusimama na kuomba Mwongozo. Wakati Mheshimiwa Liwaka anachangia, nilikuwa ninamsikiliza alikuwa anazungumzia maadili ya viongozi. Alikuwa anashauri, kwamba Vyama vya Siasa wanapoleta Wabunge wajaribu kuwapima maadili. Sikuwa nimesikia kama ametaja jina lako. Kama atakuwa ametaja jina lako kwamba huna maadili, basi anaweza kufuta hiyo kauli.

Mheshimiwa Liwaka, Mheshimiwa Sigrada ameomba Mwongozo, kwamba umesema yeye, Sigrada, hana maadili humu ndani. Kama umesema hivyo, ni lugha ambayo ni ya maudhi, naomba uifute. Kama mimi nilivyosikia ni sawa, kwamba umesema viongozi wa Vyama vya Siasa ambao wanatakiwa waje hapa wapimwe maadili, kama ni hivyo uko sawa. Lakini kama umemtaja yeye itabidi ufute kauli yako.

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia mwanzo wa mchango, ni Mbunge wa karibu yangu, na ukaribu na mimi ninaamini maadili yake yanatosha. Sikutamka kuwa hana maadili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, kwa vile Mheshimiwa Liwaka amesema kwamba hakutamka kwamba wewe huna maadili, na nilichosikia mimi ninafikiri ni sahihi kwamba amesema viongozi wa Vyama vya Siasa kabla ya kuchujwa, waangaliwe maadili yao, ninafikiri hajakukusudia wewe. Kama atakuwa amesema hivyo, ameshasema yeye kwamba hajasema.

Kwa hiyo, kwa Mwongozo wangu ni kwamba, alichozungumza yeye ni kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Kifungu namba Sita, ambacho kinataka Chama chochote cha Siasa kiwaangalie katika maadili viongozi wao kabla ya kuwaleta popote. Huu ndiyo Mwongozo wangu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Chakoma, Mheshimiwa Janeth Mahawanga, Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, ajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Awali ya yote ninapenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Ukarimu aliyetujalia siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuanza mchango wangu kwa kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya kustawisha maendeleo endelevu ya Taifa lake la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda kumpongeza Waziri wetu, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, na Naibu wake, Mheshimiwa *Eng*. Maryprisca Mahundi bila kusahau timu yote ya Wizara inayoongozwa na Katibu Mkuu, Eliakim Maswi, pamoja na Manaibu Makatibu Wakuu wake Ndugu Amon Mpanju, pamoja na Ndugu Felister Mdemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakubaliana sote, Wizara hii ni kubwa na ina mambo mengi, lakini Waziri huyu na timu yake wamekuwa hawalali, wanafanya kazi usiku na mchana, kuhakikisha maadili ya nchi hii yanalindwa, watoto wa Taifa hili wanatunzwa, wazee wa Taifa hili wanahifadhiwa, Wafanyabiashara ndogondogo wananufaika, wakina mama

wanapata fursa ya mikopo, *NGOs* zetu zinasimamiwa ipasavyo, bila kusahau usimamizi wa Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii vinasimamiwa kwa kutoa wataalamu wa kada hii ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakubaliana sote, hii ni Wizara mtambuka. Wizara hii ili ifikie *performance* yake, ama ifikie malengo yake, inahitaji Wizara nyingine waweze kushirikiana nao ili waweze kufanya kile kinachostahili. Yupo mchangiaji asubuhi alizungumza kwamba ili Wizara hii iweze kufanya kazi yake sawasawa, inazihitaji Wizara nyingine nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaomba sana Serikali ama Wizara hizo ambazo zina-*connection* na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, waweze kufanya kazi bega kwa bega na Wizara hii ili mambo yaweze ku-*happen*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza nitaanza na suala la bajeti. Mtiririko wa bajeti kwa Wizara hii, umekuwa ni wa kutokuridhisha. Kwa miaka miwili mfululizo, bajeti inayotengwa ni kidogo na haitoki yote. Mathalani, Mwaka wa Fedha 2024/2025, bajeti ya Wizara nzima ilitengwa shilingi bilioni 67.9, lakini kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kilitengwa kiasi cha shilingi bilioni 76.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua michango ya asubuhi iliyochangiwa hapa, mambo yaliyojazana kwenye Wizara hii utaangalia kwa shilingi bilioni 76. Nini kinaenda kufanyika? Mbali ya kwamba kiasi hicho tumesema ni kidogo, na bado hakitoki chote, kinatoka kwa uchache, kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali na kwa mwaka huu wa fedha 2026/2027 tunaoujadili awali bajeti iliyopendekezwa ilikuwa shilingi bilioni 83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunaipongeza Serikali na tunaishukuru kwa kuongeza shilingi bilioni 24.5. Hivyo kufanya bajeti nzima ya Wizara kufikia shilingi bilioni 108. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Rais ama tunaishukuru sana Serikali kwa kuona kilio cha Wizara hii, kwamba kwa muda mrefu tumepata

bajeti kidogo na safari hii wameamua kutuongezea na kufikia shilingi bilioni 108. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitaomba sana, tena sana hii ni rai yangu, lakini pia ni ushauri kwa Serikali. Tunaomba kiasi ambacho kinapendekezwa ambacho Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha na atakapoomba tumpitishie Waheshimiwa Wabunge, nitaomba tumpitishie kiasi hiki cha shilingi bilioni 108. Kutenga ni jambo moja na kutoka kwa fedha ni jambo la pili. Kwa hiyo, tunaomba kinachotengwa na kuidhinishwa na Bunge kiweze kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza asubuhi wakati ninawasilisha kwamba katika Bunge hili tulitunga sheria na tukajiwekea kwamba kila halmashauri itatenga asilimia tatu ya makusanyo yake kwa ajili ya malezi na makuzi ya mtoto. Tukasema fedha hizi zitaenda katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii ambayo wao ndio wana jukumu la kuratibu zoezi zima la malezi na makuzi ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamechangia hapa asubuhi. Watoto wanalawitiwa, watoto wanabakwa, watoto wanatelekezwa. Tunapata watoto wa mitaani, panya *road*, wanakuwa wanatokea huko kusikojulikana. Hilo ni kwa sababu malezi na makuzi hayajaendewa sawasawa. Kwa hiyo, ni rai yangu, tuziombe halmashauri kutekeleza hili takwa la kisheria. Watenge asilimia tatu na watoe ziwafikie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ili wafanye kazi yao ya msingi ya kulea na kukuza watoto katika maadili yaliyonyooka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kuzungumza ni mikopo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunampongeza sana Rais wetu kipenzi, mama wa huruma, aliyeamua kwa makusudi kuleta ustawi na maendeleo endelevu ya Taifa hili kwa kutoa mikopo ya aina mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mikopo ya 10%, lakini tunayo mikopo ya wafanyabiashara ndogondogo. Pia, tunayo mikopo ile ambayo inatolewa kwa vijana; tuna mikopo ya Mfuko

wa Maendeleo wa Wanawake. Kwa hiyo, mikopo hii imekuwa ya *category* tofauti tofauti kwa sababu inataka kuchukua makundi tofauti tofauti katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili nataka kumpongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuamua kuja na mtazamo tofauti wa kuamua mikopo hii kuipeleka ikatolewe na benki. Ninataka kuizungumzia mikopo inayotolewa na *NMB* ya wafanyabiashara ndogondogo ya asilimia saba, pia na mikopo inayotolewa na *CRDB* ya asilimia tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa maamuzi yake, kwa sababu wakati *NMB* wanakuja kutupa mafunzo, walituambia kwamba, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya kukopesha, walikikopesha kwa wakopaji, na mwisho wa siku, hii ninazungumzia ilikuwa mwezi wa Tatu. Walirejesha ikabaki shilingi milioni 70, lakini mpaka kufikia mwezi wa Tano, ile shilingi milioni 70 iliyobakia kwa wakopaji ikarejeshwa na yenyewe ikaenda ikakopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ukichukua mikopo hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia inayopitia benki ukilinganisha na ile 10%, hii mikopo imekuwa na tija kubwa, kwa sababu mikopo ya 10%, imekuwa na *defaulter* ya kutosha, lakini kwa mikopo hii hakuna *defaulters,* kwamba wanakopa na wanarejesha. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona umeshawasha *mic* yako. Ninakushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Chakoma. Nilimtaja Mheshimiwa Janeth Mahawanga, Mheshimiwa Kafiti, Mheshimiwa Asya Sharif, na Mheshimiwa Maryam Azan wajiandae.

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Nami nianze kama wenzangu waliopita kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Vilevile, nimpongeze Waziri Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng.* Maryprisca Mahundi, Katibu Mkuu na timu nzima kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakuwa na suala moja tu kuhusu majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi. Majukwaa haya mwasisi wake alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyaanzisha mwaka 2016 wakati akiwa Makamu wa Rais. Hayakufanya vizuri sana, lakini ilipofika mwaka 2022 waliyahuisha tena kwa kuweka miongozo mizuri kabisa, ambayo ndiyo inaishi mpaka sasa. Bado majukwaa haya kuna vitu vidogo vidogo ambavyo vinasababisha tusiuone huo uchumi wa wanawake huko mitaani kiasi kwamba, sasa tuna wasiwasi muda wa Mheshimiwa Rais utakwisha, halafu ile dhana na azma aliyokuwa anaitaka kupitia majukwaa haya isionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kila wilaya ina mratibu wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi na mkoa ina mratibu wake. Bahati mbaya sana huku mtaani kwenye kata zetu hawawafahamu hawa waratibu. Ninaiomba Wizara kupitia waratibu hawa, wahakikishe wanashuka kwenye kata, wanakutana na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi kwenye kata, wafanye kazi zao za kuratibu, kuwaunganisha wanawake hawa na benki, taasisi mbalimbali na wadau wa maendeleo kama ambavyo majukwaa haya yanataka iwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi kwenye majukwaa bado wana uelewa kwamba, kuna fedha zitakuja kwa ajili yao, lakini fedha ambazo zinatakiwa ziwaimarishe wao ni hizi fursa zinazoendelea za mikopo ya halmashauri, na pia mikopo kupitia Wizara, mikopo ya benki na taasisi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hawa waratibu wahakikishe wanaweka miundombinu na utaratibu mzuri, kwani wao ndio wana jukumu la kuwaunganisha wakina mama na

taasisi za kifedha, *TBS*, *SIDO* na wadau mbalimbali ili wakina mama hawa wazijue fursa ziko wapi. Wanaweza wakapata mikopo ya 10%, lakini kama hawajui wapi wakawekeze bado tutakuwa hatujawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara iangalie namna ya kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kule kuna mifuko ya uwezeshaji kama 75 hivi, lakini kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kuna maonesho yanaitwa Jua Kali. Tunaona kila mwaka kuna vikundi vya wajasiriamali vinakwenda nje ya nchi, kwenda kujifunza, kuangalia wenzetu wanafanyaje na kuleta ule ujuzi ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vikundi vinafanya vizuri, na vipo bado havijui utaratibu na mchakato mzima wa kushiriki maonesho haya. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara iangalie namna ya kuwaunganisha wanawake hawa wa vikundi na fursa hii. Tumekuwa tukiona vikundi vingine vinajirudia kwenda. Sasa inapoteza maana ya kwenda kujifunza na kuwa kama watu wanaenda *outing*. Tunatamani tuone vikundi mbalimbali, shughuli walizozifanya, wakalete ujuzi mpya waulete hapa ili majukwaa haya yaendelee kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia majukwaa haya ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, sisi Wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam tumeamua kuwaunganisha wanawake kuwa na jukwaa lao. Kila kitu wanachokifanya tunawaunganisha pamoja, kwa sababu kwa kufanya hivi tutaweza kusaidia hata wale wadau wa maendeleo kuja kuwafikia na kuwakuta kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ngumu sana kwenda ku-*convince* taasisi ya kifedha au mdau yeyote mkubwa kwamba, kuna wanawake wanafanya shughuli hii, anakuja anakuta wanawake 100, wanawake 50. Tuna majukwaa, kwa mfano, sasa hivi Dar es Salaam tuna majukwaa kama matano ukiacha jukwaa la Baba na Mama Lishe ambao nao wana jukwaa lao. Tunampongeza Mheshimiwa Rais na Wizara kwa kuhakikisha kwamba, wametoa karibu shilingi bilioni 94 kwa ajili ya jukwaa la Baba Lishe na Mama Lishe. Ni kitu kikubwa na kizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna majukwaa mengine. Dar es Salaam tuna jukwaa la wachuuzi wa mbogamboga na matunda, lina wanawake zaidi ya 3,000. Tuna jukwaa la wanawake wajane, tuna jukwaa la maafisa usafirishaji wa bodaboda, bajaji na magari makubwa na tuna jukwaa la wanawake wafanyabiashara wachuuzi wa bidhaa ambao ni machinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukwaa haya yote yana maelfu ya wanawake. Tunatamani walichofanyiwa Baba na Mama Lishe kishuke na kwenye majukwaa ya mengine. Hata kama siyo kwa kupata ile fedha japo nusu au kuwaunganisha na wadau wengine kutokana na shughuli wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Kampuni ya Simu *Vodacom*, iliweza kutushika mkono kupitia jukwaa la wakina mama wauza mbogamboga na matunda wa Dar es Salaam. Angalau imepunguza wingi wa wanawake wanaobeba mabeseni na kuuza matunda barabarani, bado wapo, lakini tumewapunguza. Lengo kubwa tunataka wakina mama wale wawe na *centers* zao, sababu watu wanaotaka kula matunda, wanahitaji mbogamboga, watawafuata kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana, unatoka Posta unakutana na mama na beseni la matunda. Kama kuna foleni, unafika Morocco mama yule naye ametembea mpaka Morocco. Hii haina afya na haipendezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Dorothy Gwajima, kwenye mchango wangu wa Bunge lililopita niliongelea hapa jukwaa la akina mama wajane wa Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakina mama wale wamenituma leo nije nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa alichokifanya. Ametusaidia kupata visima, kwa sababu wakina mama wale wajane wanataka kulima mbogamboga. Wao wamejikita kwenye kilimo, wana mashamba yao tayari eka 20. Mheshimiwa Waziri ametuelekeza tumeandika barua, ile barua

imeshakwenda TAMISEMI, TAMISEMI wameshatujibu. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri asituache, aendelee kutushika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla mwaka huu haujaisha, tunataka wakina mama wajane wa Kinondoni tuanze kulima mbogamboga. Pia, majukwaa mengine hawa nao wamenipa salamu zao, nitakwenda, tutakaa mezani, ninajua Mheshimiwa Waziri ni mtendaji na ni mfuatiliaji, twende tukahakikishe majukwaa haya yana vitu vya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kundi lingine ambalo nalo limesahaulika sana katika masuala ya kuwainua kiuchumi… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa malizia sentensi yako, ni kengele ya pili hiyo.

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ninashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mheshimiwa Asya Sharif na Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, wajiandae.

MHE. KAFITI W. KAFITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela nainaomba nitoe mchango wangu kwa Wizara hii muhimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuahidi tabasamu kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kumwamini dada yetu, Waziri wetu, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, kazi yake inaonekana. Ndugu zangu Wabunge wenzangu, kila mmoja anafahamu mchango wa mama huyu. Kazi anayoifanya ni kubwa, ndiyo maana Mheshimiwa Rais amekurejesha tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Wabunge tunaendelea kumpongeza. Tuendelee vilevile kumpongeza Naibu Waziri, Dada yangu Maryprisca. Nimpongeze Katibu Mkuu, kaka yangu Ndugu Maswi, ninaamini kuja kwake katika Wizara hii kutaleta maendeleo makubwa sana. Kaka yangu Ndugu Mpanju pamoja na Ndugu Felister ninawapongeza sana kwa kazi nzuri, pamoja na wataalamu wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite kwenye hoja yangu. Kwanza kabisa, ninaomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana wakina mama wa nchi hii ya Tanzania kwa malezi bora na makuzi mliyotupatia. Hata kaka yangu Baba Levo bila mama huyu asingekuwa humu Bungeni. Ni malezi mazuri na bora kutoka kwa wakina mama hawa, ndiyo yaliyotusababisha tuwe hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, ninaomba niwaambie, Taifa lililo bora na jema ni lazima lijengwe na Taifa lenye malezi na makuzi bora, pamoja na ustawi wa watoto ulioimarika. Ninaomba niwaambie, tuna Dira yetu ya 2025/2050. Dira hii bila kuwa na malezi bora na makuzi kwa watoto hatuwezi kuifikia. Kwa hiyo, Wizara hii ni Wizara muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa tumekuwa tukipambana na mikakati mikubwa ya kuhakikisha tunalikomboa Taifa hili, lakini tunasahau mikakati mikubwa ya malezi na makuzi ya watoto wetu. Kama tutakuwa na malezi na makuzi yasiyo bora katika Taifa hili, Dira hii hatuwezi kuifikia hata siku moja. Niwape mfano ndugu zangu Wabunge, ukiangalia nchi bora zenye ustawi mzuri wa malezi na makuzi kwa watoto, tuangalie nchi bora zinazoongoza kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia nchi ya Netherlands, Denmark, France, na kwa Afrika tunaangalia nchi ya Mauritius, na Seychelles; nchi hizi kubwa zina malezi bora na makuzi kwa watoto. Mataifa haya yana malezi mazuri kwa watoto hawa ambao yanachangia mchango mkubwa kwa maendeleo ya Mataifa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwape takwimu kidogo. Taifa letu kwa mujibu wa taarifa za *Early Childhood Development Network,* 47% ya watoto chini ya miaka miwili hadi mitano, ndiyo wako kwenye mwelekeo sahihi wa malezi. Maana yake ni nini? Kama Taifa, tuna kazi kubwa ya kuhakikisha tunaimarisha msingi wa malezi na makuzi bora ya watoto wetu. Tusipolifanya hili sasa hivi, maana yake tutakuwa na Taifa ambalo nitakuja kueleza hapa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, tunafahamu malezi na makuzi katika Taifa letu ndiyo msingi bora wa maendeleo yetu. Wizara hii tunatakiwa tuipe msukumo na tuipe *support*, mama anafanya kazi kubwa sana. Ukiangalia sasa hivi maadili, na mmomonyoko wa maadili yamezidi kuporomoka. Ndiyo maana nimetangulia kuwapongeza wakina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakina mama hawa ndio wanaokaa na Watoto. Sisi wakina baba tuko mtaani tunatafuta fedha na kula raha kama ndugu yangu Baba Levo. Ndugu zangu ninaomba niwaambie kitu kimoja, leo tuna watoto wanalawitiwa, tuna watoto majambazi, tuna watoto wanabakwa, tuna mateja, na tuna mashoga, ndugu yangu amenukuu mpaka mistari ya Biblia, lakini juhudi yote hii wanaopambana kuhakikisha wanaondoa haya ni ninyi wakina mama, mjipigie makofi jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Taifa tunatambua mchango wenu mkubwa. Kwa hiyo, tunahitaji mambo haya ya mmomonyoko wa maadili yaishe, maana yamekuwa mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie tu kitu kimoja ambacho ninakichukia, na niombe sana Mheshimiwa Waziri leo ukiangalia maudhui ya tamthilia tunazoangalia, wakina baba wengi wamejigeuza kuwa wakina mama. Sasa sijajua nia yao ni nini? Kwa hiyo, ninaomba wakina mama sijui wana vitu gani vinavyovutia wakina baba waweze kujigeuza. Tunaomba waendelee kutoa elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi kabisa, ninaomba sana Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kutunga Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Jamii. Maendeleo ya Jamii haina *govern body*. Kwa mfano, wenzetu wa *Law School* wana *professional board* yao, madaktari wanayo ya kwao, watu wa ugavi wanayo ya kwao, wahasibu wanayo ya kwao, na *auditors* pia wanayo. Kwa nini Maafisa Maendeleo ya Jamii wasiwe na *govern board* yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitachukua mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Wakati anakuja kuhitimisha, ninaomba aje na suluhisho la Serikali kutuambia ni lini na wakati gani tutakwenda kuwa na bodi hizi, ili Maafisa Maendeleo, hawa na watu wa Ustawi wa Jamii waweze kutenda kazi zao kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niongelee suala la ajira. Hapa Waheshimiwa Wabunge naomba wanisikilize vizuri. Kwanza, nitoe pongezi kwa Serikali na Mheshimiwa Rais wetu, kwa kuendelea kuongeza ajira kwa Maendeleo ya Jamii katika *level* ya kata. Nafikiri kata nyingi zina Maafisa Maendeleo ya Jamii. Hili ni jambo jema la kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *NGOs* nyingi ambazo ukiangalia nyingi hazina wataalamu ambao wanahusika kwenye mambo ya ustawi na maendeleo ya jamii. Sasa ninaomba tupitishe sheria na mwongozo, *NGOs* zote zinazoanzishwa ziwe na wataalamu wa maendeleo ya jamii katika *NGOs* hizo. Hii itasaidia maafisa hawa waweze kupata kazi kwa urahisi badala ya kwenda kukaa mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia hata zile *strategic project,* ile miradi ya kimkakati, sasa ifikie wakati na yenyewe ni lazima iajiri maendeleo ya jamii. Hao ukiangalia wana watu wa *health and safety*. Kwa hiyo, kwa nini wasiwepo watu wa maendeleo ya jamii katika kuhakikisha kwamba, wanam-*link* mkandarasi pamoja na jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa nafasi hii, wakina mama tunawapenda sana, wakina baba tuko kwa ajili yenu, tutawatunza na kuwahudumia siku zote. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kafiti. Nilimtaja Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mheshimiwa Rahma Kisuo na Mheshimiwa Salma Kikwete, wajiandae.

MHE. ASYA SHARIF OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na mimi jioni hii, nikaweza kusimama katika Bunge letu hili Tukufu na kuchangia bajeti yetu hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu, nianze kwa kutoa salamu kupitia Wizara yetu hii ya Maendeleo ya Jamii. Salamu kutoka kwa wanawake wajasiriamali, ninakusudia wafanyabiashara ndogondogo. Wanamshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuianzisha Wizara hii ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Gwajima pamoja na ndugu yangu *Engineer* Maryprisca. Kwa kweli, wanamtendea haki Mheshimiwa Rais, na Mheshimiwa Rais alikuwa na maono makubwa kuiona hii Wizara kuwapa watu hawa wakati huu. Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote ambaye hatamthamini na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia, ashindwe na alegee. Ashindwe na alegee ninasema popote alipo, kwa sababu ni ukweli na dhahiri usiofichika Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia amekwenda kubadilisha hali za wananchi wa chini, wakiwemo wenye kipato kidogo na sisi sote hapa ni mashahidi. Ameendelea

kutoa mikopo katika Wizara hii, mahitaji ni makubwa kwenye Wizara alizoziunda, lakini amezipa kipaumbele kwenye Wizara hii ya Maendeleo ya Wanawake, alikuwa na sababu zake za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 10 zilitoka hapa, Aprili mwaka 2025, lengo ni kuwakopesha wafanyabiashara wadogo wadogo waondokane na maisha tegemezi. Hali hiyo imeleta manufaa. Kwa nini tusimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia? Yeyote atakayembeza Mheshimiwa Dkt. Samia, huyo hana hofu ya Mwenyezi Mungu, na huo ndiyo ukweli. Mama amenyanyua hali za wanawake wenzetu, amenyanyua hali za vijana, amenyanyua hali za watu wenye makundi maalumu, mahitaji maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama kuna sensa itakayoweza kufanyika ya kuwachunguza wafanyabiashara ndogondogo, uende soko la Wamachinga watutazame wanawake tulivyojaa, watazame vijana, watazame watu wenye mahitaji maalumu, hawakukaa bure. Huyu ni Mheshimiwa Dkt. Samia kawawezesha kujinyanyua kiuchumi. Halafu watoke watu waseme mwanamke, mwanamke. Mwanamke ni nguvu kubwa, na tutaendelea kumlinda Mheshimiwa Dkt. Samia kwa nguvu zote, kwa sababu ametujengea heshima, ametuwekea tabasamu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiseme? Lazima tuseme, Mheshimiwa Dkt. Samia kaja kuwa mkombozi. Jamani tuwe na hofu ya Mwenyezi Mungu, Mungu akisema liwe, linakuwa. Alishapangiwa Mheshimiwa Dkt. Samia awe Rais wa nchi hii, lakini awe mkombozi wa wanyonge wa Tanzania wa nchi hii. Nani atabeza jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia? Hakuna, na huo ndiyo ukweli. Sasa hizo ilikuwa ni salamu. Ndiyo, mwanamke ni jeshi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu sasa ninajielekeza hivi kwamba Wizara hii ilipeleka maombi ya kuidhinishiwa fedha, lakini mwaka 2023/2024 iliweza kuidhinishiwa shilingi bilioni 74 siyo kidogo. Mwaka 2024/2025 Wizara hiyo

iliidhinishiwa shilingi bilioni 67; kama haitoshi, mwaka 2025/2026 ikaidhinishiwa shilingi bilioni 76.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wameomba shilingi bilioni 108 na tayari Mheshimiwa Rais amesharidhia, kutoka shilingi bilioni 74 mpaka shilingi bilioni 108. Siyo hatua ndogo ndugu zangu, na huu ndiyo ukweli. Hii ndiyo azma ya Mheshimiwa Dkt. Samia kuwanyanyua watu kutoka walipokwenda pengine kimaisha, kiuchumi lakini kujenga tabasamu kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeondokana na maisha tegemezi, tumeondokana na mikopo ya kausha damu, na tumeweza kusaidia wenza wetu. Halafu useme mwanamke hana heshima! Mwanamke ana nguvu, na mwanamke anaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tunajivunia Mheshimiwa Rais wetu mwanamke na anatuongoza vizuri na tunampenda na tutaendelea kumpenda na tutamlinda kwa nguvu zote. Mheshimiwa Dkt. Gwajima Fanya kazi msaidie Mheshimiwa Rais kwenye Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa kabla sijaunga mkono hoja, niseme Waheshimiwa Wabunge wenzangu niwaombe tuwaidhinishie ndugu zetu hawa Wizara waweze kufanya kazi zao vizuri, na mimi nipo tayari sasa kuwa balozi wa wafanyabiashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asya Sharif, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mheshimiwa Rahma Kisuo, Mheshimiwa Salma Kikwete, Mheshimiwa Khadija Taya ajiandae.

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima jioni hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya wanawake, vijana na wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi zake nzuri anazozifanya katika kujenga Taifa hili. Mheshimiwa Rais ni hodari, ni mchapakazi, ni mwenye maono. Pia, Mheshimiwa Rais huyu ametoa fursa kwa wanawake za kiuchumi, ndiyo maana amesimama katika mikopo ya aina mbalimbali katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii, Wizara yetu ambayo tunaipenda sana Wanawake, Vijana na Wenye Mahitaji Maalum. Mchango wangu utajikita kwenye mikopo iliyoko katika Wizara hii ya wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuweka mikopo yenye masharti nafuu katika Wizara hii. Wanawake wengi waliopo vijijini na mijini wengine hawajui fursa zilizoko katika Wizara hii ya wanawake na vijana. Katika Wizara hii ya Maendeleo na Jamii, kuna Mfuko wa Maendeleo ambao ni *WDF* mkopo wa wafanyabiashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii kuna mkopo wafanyabiashara ndogondogo ambao ni *WBN*, katika Wizara hii kuna mikopo ile ambayo inatolewa katika Halmashauri ya 10% wanawake wengi wanaona kuna mkopo huu tu wa 10%, lakini hii mikopo mingine ambayo ipo katika Wizara hii hawaifahamu, maana hawana elimu nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Mfuko wa Maendeleo wa *WDF* ambao upo katika Wizara hii ya Maendeleo na Vijana umetokana na Sera ya Maendeleo ya Wanawake, Jinsia ya mwaka 2000 iliyofanyiwa mapitio katika mwaka 2023. Mfuko huu wa *WDF* Serikali imeweka kwa malengo mahsusi ya wanawake, vijana na wenye mahitaji maalum. Mfuko huu Serikali imeweka malengo yanayofuatayo:-

(i) Kuimarisha uwezo wa kiuchumi wa wanawake na vijana;
(ii) Kukuza ustawi wa familia;
(iii) Kuchochea wanawake hasa wajasiliamali; na

(iv) Kuanzisha miradi ya sekta binafsi kama uvuvi, ufugaji pamoja na uchimbaji.

MHE. MARIAM M. NYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa inatoka wapi?

MHE. MARIAM M. NYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwa Mariam Nyoka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mariam Nyoka, taarifa.

TAARIFA

MHE. MARIAM M. NYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Mchangiaji anaongea vizuri sana kuhusu mifuko hii iliyopo kwenye Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii. Nilikuwa ninaiomba Wizara ishuke chini ikatoe elimu ya mifuko mbalimbali iliyoko kwenye Wizara yao. Kama leo hapa Waheshimiwa Wabunge tu wanashangaa hii *WDF* ni nini? Wananchi ndiyo kabisa! Ninaomba twende chini tukawaelimishe wananchi, wapi wanapata hii mikopo? Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maryam Azan, unaipokea hiyo taarifa?

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nimepokea taarifa yake. Mfuko huu unatoa mikopo ya miaka miwili au miaka mitatu. Mfuko huu ulipoanzishwa mwaka 1993 ulikuwa unatoa riba ya 10% kutokana na umuhimu wa wanawake wa Taifa hili na vijana pamoja na wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya maboresho na mwongozo wa Mfuko huu Toleo la Julai, 2022. Sasa mfuko huu unatoa riba ya asilimia nne. Wananchi waliopo vijijini hasa wale wanawake wakulima hawajui kama huu mfuko unatoa riba ya 4%. Ninaomba Mheshimiwa Waziri na watendaji wote muwape elimu wanawake hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali inayoimarisha mfuko huu, bado wanawake hawana uelewa wa hii mifuko hasa kule vijijini na huku kwenye miji pia kwa sababu wafanyabiashara ndogondogo wengi ni wanawake. Ninaomba sasa kushauri, Serikali itoe elimu katika Mfuko huu wa *WDF* hasa kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaiomba Serikali huu mfuko unatoa mkopo ufanye usimamizi maalumu kwa wale wanaokopa waweze kurejesha ili wengine wanawake wanaotaka kukopa kwa vile mfuko huu una riba ndogo, waweze na wao kupata mkopo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze katika Mfuko mwingine wa *WBN* ambao umo katika Wizara hii ya Maendeleo na Vijana. Mfuko huu unatoa 7% wa riba, ukiangalia wanawake wengi wafanyabiashara kuna mamalishe, wafanyabiashara ndogondogo, pia kuna akina mama wanaotembeza bidhaa mitaani. Wanawake hawa hawawezi masharti haya makubwa ambayo yamewekwa katika Mfuko huu wa *WBN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya mfuko huu ni lazima mama awe na leseni, awe na eneo la biashara, halafu mfuko huu unataka arejeshe *return* ya milioni tano kwa mwaka. Kweli mama anayetembeza maparachichi, hana sehemu ya kuweka bidhaa zake, hana mahali pa biashara, hana leseni na pia hawezi kurejesha *return* ya milioni tano kwa mwaka. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, hebu masharti haya ayapunguze kidogo kwa mfuko huu wa *WBN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda nichangie mfuko wa 10%. Mkopo huu una masharti magumu ambao unawataka wamama wanapotaka kuomba huu mkopo waende wakajaze fomu kwa kutumia mfumo kidijitali. Kweli mama yuko kijijini simu yake aliyonayo siyo simu janja ana simu ya tochi anaweza kujaza mfuko huu kwa kutumia kidijitali? Tunashauri kwamba haya masharti tunaomba yapunguzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri awawezeshe wale Maafisa Maendeleo waliopo katika vile vijiji waweze kuwasaidia hawa wakina mama kujaza zile fomu za mikopo, kuwajazia kwa usahihi ili na waweze kupata hii mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na michango yetu, tunao wageni ambao wapo Bungeni jioni hii ninaomba tuwatambue.

Wapo wageni waliokaa jukwaa la Mheshimiwa Spika wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, Naibu Waziri wetu wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake wa Makundi Maalum. Hawa ni Ndugu Devota Chacha, Afisa Tawala wa Halmashuri ya Wilaya ya Mbeya na mfanyakazi hodari wa mwaka huu ambaye amepata tuzo mwaka huu wa 2026, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Mwalimu Mgoza Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Chunya, Karibu sana. Ndugu Eveline Mwinuka mfanyakazi wa *Vodacom* Mkoa wa Mbeya, Ndugu Upendo Kiando Dada wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Prakseda Henjowele mdogo wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Daudi Kanani mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri. Ndugu Yusuf Kileo mtaalam wa usalama wa watoto mtandaoni, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Rahma Kisuo, Mheshimiwa Salma Kikwete, Mheshimiwa Khadija Taya jiandae.

MHE. RAHMA R. KISUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu kwa mara ya kwanza tangu niwe Mheshimiwa Mbunge wa Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza Mama yetu Jemedari sana, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa nguvu na kuipa kipaumbele ustawi na maendeleo ya jamii ndani ya nchi yetu. Tunampa heko kubwa tunajivunia sana yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwape heko Waziri, Naibu Waziri, Wizara nzima ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kuendelea kuchapakazi bila kuchoka hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu moja kwa moja leo kwenye bajeti hii nitauelekeza katika suala zima la *survival and maintenance of the child,* ama niseme matunzo ama malezi ama mahitaji ya msingi ya mtoto pale ambapo wazazi wawili wanapotengana; ama niseme mzazi mmoja anapoamua kukengeuka na kukwepa majukumu yake ya malezi kwa mtoto wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa sana zinazofanywa na Serikali, tunaziona na tunazitambua, lakini kwa bahati mbaya bado tunazo changamoto kubwa sana katika kutekeleza haki za watoto. Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2019 Kifungu Namba 41 - 43 kinaelezea wajibu wa mzazi katika malezi na matunzo ya mtoto. Vilevile katika sheria hiyo Kifungu Namba 51 (b) kinaelezea adhabu kwa mzazi ambaye atashindwa kushiriki kikamilifu katika malezi ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalisia wa maisha ya sasa na adhabu iliyokuwepo katika sheria hiyo ambayo ni kushindwa kumtunza mtoto wako, utalipa faini kiasi kisichozidi shilingi laki tano, ama utakwenda jela kwa kifungo kinachoanzia miezi sita, lakini kwa lugha rahisi niseme adhabu hii ni nyepesi sana kulingana na tatizo tulilonalo katika meza, niseme tu athari ya tatizo hili ni kubwa kuliko tunavyodhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna idadi kubwa ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu wakikosa haki zao za msingi

za elimu bora, afya bora vilevile lishe bora na hata makazi salama. Isivyo bahati na kwa kiasi kikubwa sana mzigo huu hubebwa na wanawake wanaobaki kulea watoto hawa pekee yao. Tumewapa jina la kiingereza tunawaita *single mothers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote haya hutokea kwa sababu tu mzazi mwingine kakimbia wajibu wake, ni aghalabu na nali-*stress* neno hili la 'aghalabu,' ni aghalabu mzigo huu kuachiwa mwanaume. Tatizo hili huchangia sana mmomonyoko huu wa maadili ambao tunahangaika nao sasa hivi na tunaipa Serikali mzigo mkubwa sana katika kutoa huduma za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema adhabu isiyopungua faini ya shilingi laki tano na kifungu kisichopungua miezi sita ni kwamba baadhi ya watu wata-*take advantage* ya adhabu hiyo kuona kwamba nina nafasi ya kulipa, kwa nini nihangaike na malezi ya mtoto mpaka atapokua, wakati shilingi laki tano ninayo mfukoni kulipa faini na kuendelea na maisha yangu? Ni lazima mtu huyo atakwepa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kuona umuhimu wa kurekebisha sheria hiyo ili kuwe na mfumo madhubuti na rasmi wa utekelezaji wa amri ya mafunzo ya mtoto, kwa wazazi wenye ajira rasmi, mahakama iwe na uwezo wa kuagiza fedha za matunzo kukatwa moja kwa moja kwenye mshahara kabla ya fedha hizo kumfikia mhusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili liko ndani ya uwezo wetu. Ninajua ni ngumu, ninajua ni jambo linalohitaji mjadala mpana wa kisheria na kiutendaji, lakini lazima tuanzie sehemu. Hata *Rome* haikujengwa kwa siku moja, ni lazima tuanzie mahali fulani. Tunaweza kuangalia mifumo iliyofanikiwa katika nchi nyingine, tuitumie kama *pari materia* na kuiboresha kulingana na mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima hili tuanzie mahali fulani tukubaliane kama ni 10% ya kukatwa ama nyingine, lakini litekelezwe kwa dhati ili ile dhana ya kwamba tunamlinda mtoto wa Kitanzania ije kwenye uhalisia. Kwa wale, wanaokwepa

makusudi matunzo ya mtoto na wakiwa hawapo katika ajira rasmi *le us say* wafanyabiashara, sheria iangalie ni kiasi gani inaweza kuwabana aidha kwa kuzuia na kukamata baadhi ya mali zao kwa ajili ya kulinda maslahi ya mtoto. Ugomvi wa wazazi, migogoro ya wazazi isiwe adhabu kwa watoto wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaona wakinamama kutwa, chungu nzima wakiendelea kuhangaika kwenye vyombo vya haki kutafuta utekelezaji wa agizo ama amri ya matunzo bila mafanikio maskini ya Mungu. Nachelea kusema sasa muda umefika tutoke kwenye hukumu twende kwenye utekelezaji wa hukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria kuja na mfumo wa marekebisho yanayoweka mifumo madhubuti ya utekelezaji wa matunzo ya mtoto ili haki za mtoto zilindwe kwa vitendo na siyo kwa maandishi pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Rahma. Nilimtaja Mheshimiwa Salma Kikwete, Mheshimiwa Khajida Taya, Mheshimiwa Ngwando, ajiandae.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Sambamba na hilo nitumie fursa hii kwa siku ya leo ambayo Mwenyezi Mungu amenipa kibali kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kusema ahsante sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye yeye ndiye mlezi nambari moja. Mlezi nambari moja nikiwa na maana kwamba yeye ndiye mkuu wa nchi wa Taifa letu la Tanzania. Ana wajibu mkubwa na kazi kubwa ya kulilea hili Taifa,

na kwa kweli Taifa liko vizuri. Anatulea vizuri, na anatuangalia vizuri. Pamoja na misukosuko michache inayojitokeza, lakini Mama ameendelea kusonga mbele katika kuliangalia Taifa lake la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Gwajima na Naibu Waziri wake na viongozi wote, akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia Suluhu Hassan, Daktari alipomteua Mheshimiwa Dkt. Gwajima, kuna vigezo maalum ambavyo ameangalia, na ndiyo maana aliendelea kukaa pale pale kwenye kile kiti chake. hongera sana kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninataka nijikite kwenye aya ya 68 ambayo inapatikana kwenye ukurasa wa 34; inayozungumzia masuala ya malezi, maadili, maendeleo na ustawi wa watoto. Haya maneno ni maneno makubwa na maneno ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia malezi, maadili, maendeleo na ustawi wa watoto, hii ndio injini; na hii ndiyo injini ya Taifa letu. Kana kwamba, ukiwa na gari, gari ikiharibika injini haiwezi kwenda. Ni sawasawa na mwili wa mwanadamu. Mwili wa mwanadamu moyo ukizimika, ndio mwisho wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye eneo hili ni muhimu sana. Ni nani anayewajibika kwenye suala la malezi, maadili, maendeleo hali kadhalika na ustawi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirejea nyuma tunaona kwamba Watoto, kwanza mlezi mkubwa ni Mwenyezi Mungu. Ukitoka kwa Mwenyezi Mungu unakuja kwa mzazi au wazazi, baba na mama. Ukitoka unakuja kwa walezi. Walezi wa mtoto huyu, kwa sababu mtoto anapokua baada ya miaka miwili, mitatu mtoto anatakiwa aende shule. Hapa tunawaangalia walimu ambao wamepewa

dhamana kubwa ya kuwalea hawa watoto. Halafu wa mwisho ni jamii inayozunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto zamani alikuwa sio wa baba na mama, alikuwa ni mtoto wa jamii, lakini mazingira ya leo mtoto tunamgeuza kuwa ni mtoto wa baba na mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na wajibu kama wanajamii. Mtoto anapofanya jambo ambalo siyo jema, anakanywa, anaonywa, anaelezwa, anaambiwa na anasikiliza. Leo ukifanya hicho kitendo, mama yake atakujia amejifunga kibwebwe anakwaambia kwa nini mwanangu unamfanyia hivyo? Hapa tunakosea na hapa tumekosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mlezi namba moja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akasema kuna mmomonyoko wa maadili katika Taifa letu la Tanzania. Hongera sana kwa Mama Samia kwa kuliona jambo hili ambalo ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tusipopakazania, maana yake hatuna Taifa. Leo tunazungumzia masuala ya elimu, vilevile tunazungumzia masuala ya afya, masuala ya maendeleo ya jamii, hali kadhalika masuala ya kila aina. Hii Wizara ni nyeti kuliko Wizara nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatujawalea watoto wetu vizuri, hatutapata watu watakaosoma hapa, hatutapata wataalamu, hatutapata maprofesa kwa sababu mmomonyako wa maadili umeendelea. Kama hatutawekeza kiasi kikubwa hapa, bado tutafikia hatua kama tunatwanga maji kwenye kinu. Kwa hiyo, ni lazima hapa tupaangalie kwa jicho la pekee kuliko ni kitu kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara hii kadiri siku zilivyokwenda imeendelea kuongezeka kutoka 67.9 ikaja mpaka 76. Leo hii tunazungumzia shilingi bilioni moja bilioni 108. Bajeti ni kitu cha kwanza lakini kupewa bajeti ikatosheleza ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu, hii Wizara ni nyeti, ni kubwa kuliko kitu kingine. Ninashauri tuipitishe bajeti hii na ikiwezekana Mwenyezi Mungu akitujalia uhai *inshaallah* tuiongezee iwe kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na huu mmomonyoko wa maadili unatokaje? Unakuwaje? Ndiyo, sisi siyo kisiwa, hatuwezi kukataa kwamba hatutaingia kwenye suala zima la utandawazi. Hayo ndiyo maendeleo yetu na ya dunia, lakini hata tunavyoviangalia viendane na utaratibu wa maadili yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi jukumu la malezi ameachiwa mama pekee yake. Malezi ni baba mama. Bila baba hakuna mtoto. Bila mama hakuna mtoto. Ni lazima tuhangaike na hili, kwani ni muhimu sana katika makuzi ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui muda umekwisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye suala la wanawake, na hasa wakina mama wajane, akina mama pindi wanapofiwa na waume zao wanateseka. Mwanamke akifiwa tu na mume wake kitu cha kwanza anachoambiwa katika mazingira ya kawaida, huyu mwanamke amemuua mume wake. Mbona mwanaume haambiwi amemuua mke wake? Hili ni lazima! Ndiyo maana inapotokea wakati mwingine anafikia hatua anasema hebu nichote kidogo nikajenge kule ili nikifukuzwa hapa niwe na sehemu ya kukimbilia. Ndicho kitu kinachojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaona muda sijui umeisha, sijui nilikuwa na mambo mengi, lakini sina; unaniangalia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa kuhusu mikopo ya wanawake, iongezwe kasi ya kulipa ile mikopo, hali kadhalika na ufuatiliaji kwenye suala la mikopo hapa watu wengi mikopo wanasema hatupati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia

kuhusu bajeti hii, ninawatakia kila la heri. Mama anastahili maua yake, asifiwe wakati yuko, hayuko hapa; siyo kesho, alifanya hiki, akafanya hiki, lakini tunakupongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Salma Kikwete. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Taya. Mheshimiwa Happiness Ngwando, Mheshimiwa Ramadhan Muhidini wajiandae.

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kupata fursa ya kuzungumza leo. Kwanza, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na leo hii tunasikiliza na kupitisha bajeti hii ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum. Pili, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais. Ninaendelea kumshukuru na sitaacha kumshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameendelea kutuheshimisha kwa kazi zake nyingi sana, na namna tu ambavyo ameweza kuongeza idadi ya watu wenye ulemavu hapa Bungeni. Hii ni pongezi ambayo tutamshukuru milele na tunaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu, juzi tu nilikuwa nimekaa na Wabunge kadhaa wanasema sasa hivi Wabunge wenye ulemavu wana michango mizuri sana. Ni kwa sababu wanasikika, kwa sababu wapo wa kutosha kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kadiri siku zinavyozidi Kwenda, ninaamini kabisa tutaendelea kuwa na Wabunge wenye ulemavu wengi humu ndani na wataweza kuendelea kusema changamoto zao na Serikali hii Sikivu, basi itaendelea kutetea na kusimamia kazi zote ambazo imepanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima. Yeye na Naibu Waziri wake wanafanya kazi nzuri sana. Ukweli usemwe, wanafanya kazi nzuri sana, *especially* yeye. Ninapenda namna ambavyo *she is*

very punctual kwenye mitandao ya kijamii. Amekuwa hodari wa kujibu hoja, amekuwa anasimamia kazi zake vizuri, na amekuwa akidadavua mambo yale ambayo yanaulizwa au yanaleta ukakasi fulani. Kwa kweli hongera sana. Ilitegemewa angeweza kuwa ni kijana ndipo angeweza kuwa *punctual,* lakini yeye *she is very punctual* kwenye mitandao ya kijamii. Ninaomba nimshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niungane na na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wamezungumza hapa leo. Ninaheshimu sana wanaume. Ninawaheshimu sana kwa sababu ndio baba zetu, ndio kaka zetu na wamekuwa pia ni watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina vijana watatu pale nyumbani. Nina baba yangu kipenzi ninayempenda Shabani Taya. Sitakuja hapa kusema ubaya tu wa wanaume wote, lakini nitasema baadhi ya wanaume kwa ubaya wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmomonyoko wa maadili chanzo kikubwa kabisa ni wanaume. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu ya namna ambavyo hawachukui majukumu yao, wanatelekeza familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini hakuna mwanamke anayependa kufanya kazi, huo ndiyo ukweli. Kama wanaume wangekuwa wanashika majukumu yao, sisi tusingekuwa hapa tunahangaika. Akina mama wale masokoni wasingekuwa wanahangaika. Kusingekuwa na *single mothers* kwenye dunia hii, lakini kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yao wanawake tumechukua hilo jukumu. *(Makofi)*

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Muislamu na katika Uislamu wangu kuna aya inasema *arrijalu qawwamuna alan nisai... (Makofi)*

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khadija kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

TAARIFA

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa taarifa mzungumzaji, anazungumza vizuri. Mimi ni Mkristo, tunapoenda Kanisani kuoa tunaambiwa tutashirikiana kwa taabu na raha. Sasa ikitokea kwenye majukumu yetu imekuwa tabu, tunatii yale maagizo ya dini kama majukumu yetu yameshindikana hasa kwenye maeneo labda ya uzalishaji na vitu vingine. Kwa hiyo, tuseme kwamba tumeshindwa majukumu, lakini inawezekana ukaugua na majukumu katika maisha yetu yakakushinda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khadija unaipokea taarifa?

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui niipokee. Ninaipokea kwa sababu ninamheshimu Mheshimiwa Getere, na yupo kwenye kamati hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia hakuna mwanamke mwenye akili timamu yuko tayari kumfanyia au kumuumiza mwanaume anayempenda na kumheshimu. Mwanaume anayemheshimu mwanamke, atampenda na kumheshimu zaidi. Kwa hiyo, ninataka niwaambie kwamba, haya maadili ambayo yana mmomonyoka sasa hivi msingi ni wa akina baba, kushindwa kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inapelekea wanawake tunatoka kwenda kutafuta fedha na wakati huo tunawaacha watoto wetu na wafanyakazi. Sasa watoto wetu wanajifunza kitu gani? Hawajifunzi kitu kizuri. Kwa wanaume, niendelee kusisitiza, watekeleze majukumu yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ninaendelea kusema wanaume hao wamekuwa wakitelekeza akina mama wale wanaozaa watoto wenye ulemavu. Wamekuwa ni viongozi wa kutelekeza wakiamini wao sio sehemu ya kuzaa watoto hao wenye ulemavu; wakiamini kuwa mwanamke ndio mwenye kuzaa watoto wenye ulemavu. Kitu ambacho hawakijui ni kwamba, mbegu zao ndizo zinazotoa watoto wenye ulemavu. Wanaacha majukumu, matokeo yake akina mama hawa wanahangaika, wanalea peke yao, familia zao zinawatenga, zinashindwa kulea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu kwa Serikali, Mheshimiwa Waziri ikiwezekana Serikali, kama Waziri Mkuu hapa angekuwepo, kwa sababu ninazungumza kwa ujumla, ninaomba kundi hili la akina mama wenye watoto wenye ulemavu liingie katika Wizara hii ili utekelezaji wake wa mambo yake iwe jambo kubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa akina mama wanahangaika sana, wanateseka sana. Kuna mama mmoja nilimwona katika shughuli yangu pale nilipokuwa ninafanya uzinduzi wa *NGO,* amembeba mtoto wa miaka 19. Anatembea naye, anahangaika naye. Huyu mtoto viungo vyake haviwezi kufanya kazi; na sasa hivi hakuna ndugu wa kumsaidia kulea mtoto wake. Kwa hiyo, Serikali ione namna ya kufanya na kuwasaidia akina mama wenye watoto wenye ulemavu ambao hawawezi kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwamini Mheshimiwa Waziri, ninampenda, ninafahamu juhudi zake, na hataweza kushindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yupo Mheshimiwa Rais, yupo mwanamke shupavu, yupo mwanamke namba moja ambaye ameleta Kazi na Utu, Tunasonga Mbele. Hili neno ni kubwa sana. Ni neno ambalo ukilitafsiri ndani yake, huyu mama ameonyesha ana nia ya dhati ya kusaidia hii Wizara. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama wanafahamu umuhimu wa hii Wizara, kipindi kijacho tuiongezee bajeti Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mtambuka. Wizara hii ina watu ambao wapo katika Wizara ya Madini, wapo katika Wizara ya Afya; ina maana wizara hii huyu mama akiweza kuwezeshwa vizuri, akaweza kushirikiana na Mawaziri wengine wanawake na makundi maalum yote yataweza kufanya kazi kwa namna ya kipekee kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ninashukuru sana, ninawapenda mno.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Taya. Nilimtaja Mheshimiwa Happiness Ngwando. Mheshimiwa Ramadhan Muhidin, Mheshimiwa Asha Omar Rashid, wajiandae.

MHE. HAPPINESS D. NGWANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nami nimshukuru Mungu kwa jioni ya leo. Nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwanamke namba moja mzalendo na mlezi. Sisi wote tuko hapa kwa kumwona yeye. Yeye ndiye mwanamke *role model*. Tunampongeza sana na Mungu aendelee kumbariki na kumlinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana pia Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima kwa kazi kubwa unayoifanya mama yetu. Tunatamani sana kazi anayoifanya hadi kule chini iwe kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushuhuda mdogo. Juzi nilimpigia simu mtoto ameng'atwa na mbwa aina ya *Germany Shephard,* amekatwa shingo nusu ya maututi kabisa. Nilipiga simu hii, *package* ile aliyoniletea pale ninaitamani iwe kwenye halmashauri yangu na Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi anayoifanya ni njema mno. Kila kata, kila kijiji nguvu hiyo ingeenda, hii Wizara ingekuwa ya moto na hayo mambo yasingekuwepo. Tunatamani sana hata halmashauri zetu wale Maafisa Maendeleo wawe na hizo *alternatives* za kupeana mawasiliano. Yaani badala ya Tanzania inaku-*dm* wewe, basi ingekuwa inam-*tag* mtu wa kwenye kata na wilaya kwa uharaka kama anavyojibia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kazi ni ngumu sana. Ustawi na maendeleo ya jamii ni ngumu, siyo kama tunavyosimuliana hapa. Unaenda kupambana na watu waliofanya uhalifu ambao ni matajiri, wana vihela vyao vya mboga. Tumefika pale, *package* uliyotupa, yule anatuuliza mko wangapi hapo? Hebu pata picha, anatuuliza maafande tuko wangapi pale ili atupe fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu leo aliowaleta wamemsifu sana, Ustawi wa Jamii wa Mkoa, Christa Mwaipopo pamoja na Christa Kayombo na Josephine Mwaipopo, walifanya kazi nzuri sana. Akamwambia tupo, tuletee tu tunakungoja. Kwa hiyo, ninamshukuru alifanya kazi nzuri sana. Ninaitamani kila maeneo timu kama ile ingekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niongelee moja kwa moja kwenye suala la ukatili. Mchana wa leo kuna mtu ametupiga vizuri sana anasema ukatili huu sisi tunajisababishia. Hakuna mwanamke mkatili bila kulipa kisasi. Mara nyingi mwanamke anakuwa katili pale ambapo mwanaume ameyumba. Mwanaume akiyumba anayumbisha dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaobaka ni wanaume, si wanawake. Wanawake hawana vibakio. Wanaobaka watoto wetu ni wanaume. Anabaka mdogo wako wa kiume; na ninayoyaongea hapa nina ushahidi nayo. Mara nyingi mimi nikiwa ninaongea humu ndani wanahisi ninaongea *petty issues*. *Petty issues* ndizo zinazoua kwenye jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita mwanaume amemuua mwanamke, amemtoa ubongo, watoto wamefungiwa ndani na mama yao wameloa damu usiku mzima hadi asubuhi. Watu majirani wanasema tumezoea kuona watu wanapigana, kwa hiyo tulijua ni kawaida. Asubuhi mtu amekufa, watoto wamelowa damu. Watoto wale wanakimbiza jeneza kama vichaa. Afisa ustawi hajaja, maendeleo hajaja. *May be* hawana usafiri. Kazi hii ni ngumu, mnaharibu saikolojia zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanaume anapiga mwanamke, anamtoa jicho, unafika Polisi wanasema haya ni mahaba. Hizo

siyo hisia tu, hisia kutoana jicho! Sisi mnatuharibu kisaikolojia, mahaba gani ya kututoa sisi macho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kaka mmoja ambaye yeye ni Polisi yuko pale Songea anaitwa Juma Baltazar, anatenganisha mahaba pamoja na *violence*. Anatenganisha kabisa. Tunaomba Sheria hii iwekwe vizuri. Wanaume wamepoteza *role* yao, niungane na Wabunge wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanaume ukikosea, tuanzie hapo; Adamu alimwacha Hawa, akaenda kuongea na nyoka. Adamu hakuwepo. Kama unaacha mwanamke anajilea mwenyewe, lazima ukatili utatokea tu. Atatafuta njia ya kutokea. Akina baba rudini kwenye nafasi zenu kuhusu maendeleo ya jamii, mnatutesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusianze hapa kuongea vitu kwa ajili ya kutaka rekodi, kutaka watu huko tuwe na umaarufu, hali ni mbaya mtaani. Wanaume wameacha *roles* zao. Kwa nini wafanye hivyo? Unakuta amezalisha mtoto wa watu, anaenda kuchukua mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe umezaliwa kipindi cha Nyerere, unakuja kuchukua mtoto wa kipindi cha JK, asikurekodi? Lazima atakurekodi tu. Kwa nini umeacha kiwanja chako unakuwa na *emergency landing?* Mnatuharibia watoto wetu, wanaume, niombe sana baadhi yenu, huko kwenye vikao vyenu mkumbushane. Hakuna mwanamke anayemtelekeza mwanaume wala mtoto anayempenda. Tuwaombe, mwanaume akiyumba, dunia imeyumba, hata tukeshe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wa Maendeleo ya Jamii wanafanya kazi kubwa sana kule. Ninaomba sana pajengwe *safe house*. Mtoto wa kiume analawitiwa, ukishamhoji anarudi tena nyumba ile ile aliyolawitiwa, hakuna usalama wa mtoto huyu. Tujenge *safe house* kila wilaya. Watoto wanaofanyiwa matendo maovu warudishwe wapelekwe sehemu salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuandai hiyo Dira ya 2050 kama rasilimali watu hakuna. Ninawaomba sana, kila mtu kwa nafasi yake a-*play part* yake. Tutoe miundombinu kule chini tucheze kwenye nafasi zetu, wanaume tufundishane jinsi ya kulea mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani ilikuwa ukienda shule giza limeingia, mwanaume anakusindikiza, lakini sasa hivi baba akikukuta anajua amepata nyama kwa sababu maadili yametoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi zifuatiliwe kwa makini. Kesi zinakuwa zinawekwa kawaida, kawaida; baba mzazi amebaka mtoto, mnasema akamalize nyumbani. Mnajua maumivu ya kubakwa na kulawitiwa? Kwa nini mtoto huyu atoke aondoke tena kule aachwe tu? Ushahidi gani mtoto mdogo mwenye miaka mitano anakuonyesha aliyenibaka ni huyu, unachunguza nini? Tunaomba Wizara mtambuka zile ambazo zinasaidia Wizara hii, tunaumia na hatutaacha kuongea *petty issues* humu ndani mpaka habari hii imetimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, niwaombe wanawake wote ambao tuko humu; Wabunge wa Viti Maalum, 2030, tukagombee kwenye majimbo ya wanaume ili wajue hatustahili kukaa nyumbani. Tunaenda kufanya vitu kwa sababu huwezi kuacha mwanao anaumia, hana ada, eti kwa sababu baba yeye amekataa. Ndio maana tunanyanyuka, lakini tumesema hivi, hata Mungu mwenyewe amesema, *a man must be a protector and a provider*. Anakuwa *protector* na *provider.* Kupewa mwanamke hela ni *Sunnah,* mnakataa nini kutupa hela? *(Kicheko/Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Happines.

MHE. HAPPINESS D. NGWANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu alisema mpende mkeo. Ukinipenda nitanyenyekea. Kaeni kwenye nafasi zenu, tuache hizi stori za kutaka majina makubwa bila sababu, jamii inateketea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, Mungu awabariki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Happiness Ngwando. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhan Muhidin, Mheshimiwa Asha Omar Rashid na Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa wajiandae.

MHE. RAMADHAN MUHIDIN RAMADHAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nimshukuru Mwenyezi Mungu, nami kwa kunijalia afya njema siku ya leo na kusimama hapa nikiwa mzima wa afya na kuweza kuchangia katika Wizara hii ambayo ina jukumu kubwa kwenye maendeleo ya jamii yetu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuendelea kutuletea maendeleo ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi naye kwa kufanya kazi kubwa ya kutuletea maendeleo kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Gwajima kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na wasaidizi wake wote. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wangu, wapiga kura wangu wa Jimbo langu la Chwaka kule Kusini Unguja kwa kunichagua kuwa Mbunge wao. Ni ahadi yangu kwao ni kwamba nitaendelea kushikamana nao katika suala zima la kuleta maendeleo ndani ya Jimbo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite zaidi kwenye suala zima la mmomonyoko wa maadili. Kwa kweli niseme kwamba msingi imara wa uzalendo wa watoto wetu, basi huanzia kwanza kwa baba yake na mama yake. Kwa maana baba na mama ndio wenye jukumu kubwa la kufinyanga watoto na kuwalea na kuwafahamisha nini wafanye, nini wasifanye, wapi waende, vipi wakae na Watanzania wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni kazi kubwa na mimi ninataka kusema kwamba tunasema elimu au shule ya awali ni shule ya chekechea, lakini mimi ninasema shule ya awali ni kwa baba na mama. Baba na mama ndiyo wanatoa elimu ya mwanzo kwa Watoto wao na niseme kwamba malezi mema kwa watoto wetu leo, yana tija kwao kesho yao. Watoto hawa watanufaika na malezi mema katika maisha yao lakini hata na Taifa letu litanufaika na malezi yao mema. Kwa hiyo, niseme kwamba wazee wana wajibu mkubwa kulea watoto wao na kulea kwa malezi mema, wala siyo hiari, ni wajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme vile vile kwamba vijana wengi waliopata elimu, wanakwenda vizuri, lakini ni wachache, wamepata elimu, lakini wana athari za mmomonyoko wa maadili. Hili lipo kweli na sisi tumeona. Kuna baadhi ya vijana wamepata mmomonyoko wa maadili, lakini kwa bahati huku juu wakapata kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukitazama, wamesoma lakini maadili yameyumba. Sasa hili ni tatizo na kiukweli unaweza ukakuta ikawa ni hatari kweli kweli kwa sababu unamkuta mtu kakosa maadili, lakini kasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na kukosa kulelewa vyema, kama nilivyosema, malezi mema kwa wazee ni shule ya awali. Maana yake kama hawajalelewa vyema, maana yake wamekosa elimu hiyo kutoka kwa wazee wao na kukosa elimu siyo maneno yangu. Tumesema kwamba ukikosa elimu, kuna ujinga, maana yake hukufuta ujinga. Sasa maana yake umekosa elimu ya awali kabisa ya kupewa na wazee wako, maana yake tayari kuna ujinga ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa bahati mbaya sana, unaweza ukakuta vijana baadhi, yaani wachache tu, wapo wamesoma, lakini malezi hayapo na ndiyo maana unakuta leo baadhi ya vijana wanakesha kwenye mitandao ya kijamii. Unamkuta kasoma sana tu, lakini maadili yameyumba. Sasa ina maana ule ujinga bado unaendelea kufanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mtu huyu mmemwamini, anakaa kwenye mitandao ya kijamii, anaanza kutukana na watu wakubwa zake, anatukana na viongozi, anawavunjia heshima wenzake, sasa hili ni tatizo kubwa. Unamkuta mtu namna hiyo, maana yake anafanya ujinga kisayansi, si kasoma. Basi atakaa atahadaa wenzake. Kuna msemo wanasema, "*ikate utakavyoikata kashata, lakini utamu ndiyo ule ule*." Bado unakuta ni ujinga unaendelea kumla kwa kutokaa vizuri na wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikiendelea kuchangia katika Wizara hii ya Mheshimiwa Dkt. Gwajima, niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametoa mkono wa faraja. Amepeleka shilingi bilioni 200 katika Wizara ya vijana katika hatua ya kuwaunga mkono vijana, lakini ukiangalia kwa kina, unaweza ukakuta tatizo lipo kwa vijana wetu ambao tayari wana athari ya mmomonyoko wa maadili. Je, vijana hawa wanaweza kufanikiwa kupata hizi fedha? Kama hawakufanikiwa, tunafanyaje? Hili nitalisema baada ya kuhitimisha mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watoto wana haki zao za msingi kutoka kwa wazee wao. Tusidharau, maana yake watoto ukiwakosesha haki hii ya msingi katika suala zima la kuwalea vyema leo na kesho, watadai haki zao, lakini haki zao wanazo, ziko wapi? Ziko kwa baba na mama; palepale tunarudi. Lazima wapatiwe haki zao kwa baba na mama ili waweze kuja kuingia kwenye ushindani wa masoko ya ajira waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama hakuna maadili mema, hawajafunzwa vyema kuishi na wenzao, hawakupelekwa shule, hawakusoma, sasa inafika wakati wa kupata nafasi za ajira hawapati. Maskini wanakwenda na wenzao ambao wamepata elimu, wamefunzwa vizuri wao hawapati, hawana vigezo. Sasa ninawahurumia sana vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa maskini mimi mfano wake ninatoa kama vile mfano wa nyaya za umeme za majumbani kwetu zilizochunika; huu umeme mdogo ambao

tunautumia. Watoto ambao wako kuanzia miaka 10 hadi miaka 30 ni nyaya za umeme ambazo zimechunika. Ukiachia hapo, hawa wa miaka 10 mpaka 30 ambao wameathirika na mmomonyoko wa maadili, kuna wengine ambao wana umri kuanzia miaka 30 mpaka 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Mheshimiwa Waziri Dkt. Gwajima anapiga kelele nao ndani ya mitandao. Sasa hili nalo ni tatizo. Ndiyo pale zinapokutana nyaya hizi ndogo za watoto hawa ambao wamepata athari hii, na nyaya kubwa ambazo hao wakubwa, mimi ninasema ni zile *main line*. Hizi usiombe kukutana nazo, shoti yake kubwa sana na ndicho kinachoendelea. Wanajaribu kupiga shoti wakikaa kwenye mitandao ya kijamii wanasema ovyo, mambo ambayo hayaendani na maadili yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yake, ashirikiane na wasaidizi wake wote, nimpe ushauri. Kupitia Wizara yake ni vyema wakaanzisha mamlaka ambayo itakuwa inaweza ikatoa ushauri nasaha. Kukawa kuna kitengo ndani yake kinatoa ushauri nasaha kwa vijana na watu wazima ambao wamepata athari hii ya mmomonyoko wa maadili. Siyo vibaya kwa sababu tayari... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ramadhan.

MHE. RAMADHAN MUHIDIN RAMADHAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Asha Omar Rashid, Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa na Mheshimiwa Eric Shigongo wajiandae.

MHE. ASHA OMAR RASHID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia leo katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza kwa moyo wa dhati, kwa upendo mkubwa kipenzi chetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake na juhudi anazozifanya kuhakikisha nchi hii ama Wizara hii inaenda vizuri, na wananchi wanapata huduma zao stahiki na haki zao kisawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue fursa hii kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo, pamoja na Naibu wake na Makatibu Wakuu wake. Dada yangu, hongera sana, pambana, tupo nyuma yako, hatukuachi mkono. Ninakuomba dada jitahidi sana, mama anapambana, na wewe jitahidi, amekuchagua kwa moyo wa dhati na twaona jitihada zako. Dada pambana, tuko pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nianze kwa kuchangia moja kwa moja, michango yangu kwenye udhalilishaji wa wanawake. Kila anayesimama hapa jamani, anasema kuhusu udhalilishaji; kila anayesimama hapa mwanaume anasema kwa upande wake na sisi wanawake tunasema kwa upande wetu. Jamani udhalilishaji, anayedhalilika ni mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia wanawake sasa hivi imekuwa ni gumzo, wanadhalilika kupitia *social media*. Kuna *post* nyingi zinazorushwa saa hizi picha za wakina mama za utupu, hili tusifichane, tuambiane ukweli. Mitandao ya kijamii inatumiwa vibaya, na hususan wanaotumiwa ni wanawake. Sijaona picha za udhalilishaji za wakina baba. Wanawake ndio tunaodhalilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha picha za utupu, sasa hivi kuna utaratibu wa midoli ambayo imewekwa madukani. Midoli ile inapachikiwa nguo, badala ya kupachikiwa nguo sasa hivi wamegeuza mtazamo wanapachika nguo za utupu na vitu vingine vya ziada ambapo hapo nyuma wazazi wetu wanajua vitu vile wapi vinapatikana na walikuwa wanatumia na wapi pa kwenda kuvitafuta na kuanza kuvinunua na kwa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iweje leo sisi tumebadilishiwa mtazamo, tunawekewa midoli ile na vitu vile vya udhalilishaji, mbele ya maduka? Kutembea na mtu wako wa karibu wa familiai yako, unashindwa. Ile ni hali mbaya, tunadhalilika wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali. Niiombe Serikali yangu Tukufu, iweke sheria kali ya kupambana na masuala yale ya udhalilishaji. Pia, Serikali iweke nguvu kwenye Sheria iweze kudhibiti hili janga, ambalo linapoteza utu wa mwanamke. Pia, ipige marufuku kwa ile midoli inayowekwa madukani, inatudhalilisha na kutupotezea utu sisi wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na suala lingine. Uuzaji wa pombe kiholela. Unywaji wa pombe kiholela ni udhalilishaji ambao sasa hivi umeenea ndani ya nchi yetu. Kuna ongezeko kubwa la uingizaji wa pombe kali kiholela ndani ya nchi yetu lakini pombe hizi ambazo ni kali sasa hivi zinafungwa kwenye vifurushi vya *package* ndogo, ambavyo vinauzwa madukani kiholela ambapo sasa hivi inapelekea vijana wetu wadogo, wa kike na wa kiume wanavipata vileo vile vikali na wanavitumia kwa sababu wamefanya mbinu sasa hivi, hawauzi kwa bei kubwa, wanavi-*package* kwenye vifurushi vidogo, vya bei ndogo. Watoto wetu wanaenda wananunua na kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali. Ninaiomba Serikali yangu Tukufu kwanza iondoe ongezeko la uingizaji wa pombe mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mwaka 2017, Serikali ilidhibiti utumiaji wa pombe kiholela mitaani, lakini hivi sasa imejirudia hali hii na imekuwa imeshamiri, na sasa hivi vijana wetu wanapotea. Unapopita vichochoroni sasa hivi vijana wetu wanakujibu majibu ya ovyo. Ukimwangalia kijana yule ni mdogo na kashatumia kilevi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hili suala tuliangalie sana. Dada yangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, ninamwamini. Chonde chonde, kama anavyopambana

Mheshimiwa Rais kwenye suala hili la kulinda mmonyoko wa maadili. Ninamwomba sana dada yangu pambana! Hili suala, vijana wetu wanapotea, tena wanapotea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuzungumzia kuhusu mmomonyoko wa maadili wa vijana wetu. Vijana wetu wanaharibiwa, maadili haya yamepotea. Vijana wetu wadogo wanaingiliwa nyuma ya maumbile. Hili tusikatae, lipo na linaendelea. Jambo la kusikitisha, tunaambiwa wazazi ama jamii haitoi Ushahidi, lakini yanapotoka jamii ama mzazi kutoa ushahidi ule anakamatwa jangili yule anawekwa ndani kwa muda mfupi maana miaka mitano sita hajafungwa huyo huyo. Huyo sio wa kutolewa tena nje anarudi nje jambazi yule, jangili yule, adui wa Watanzania anadunda tena mitaani, anakuja kudhalilisha vijana wengine na yule aliyemdhalilisha hana thamani, anaendelea kuwadhalilisha wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iweke mikakati atakapothibitika mtu huyu na kupatikana ushahidi wa kwamba kweli kadhalilisha awekwe kifungo cha maisha asitoke tena, hatumtaki tena mtaani. Ninaiomba sana Serikali niwashauri Wabunge wenzangu hususan wakina mama. Jamani wakina mama tunaumia, wakina mama tuna wakati mgumu, wakina mama tushikamane na tushirikiane na hii Wizara tuhakikishe udhalilishaji huu tumeuondoa kwa mikono yetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Asha Omar. Nilimtaja Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa, Mheshimiwa Eric Shigongo ajiandae.

MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Makundi Maalum na Watoto. Ninachukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima. Hata hivyo, kwa namna ya kipekee nininataka niwaambie Watanzania, Serikali mbalimbali duniani zilikutana Umoja wa Mataifa mwaka 1948 kujadili masuala mazima yanayohusiana na usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona kikao kile azimio lake linasuasua wakakutana kule Beijing wakaja na Azimio la Beijing ambalo linataka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhakikisha wanatekeleza azimio hilo kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka mwaka huu wa 2026 kwa takwimu ya masuala ya usawa wa jinsia na ushirikishwaji wa wanawake kwenye nafasi za uongozi kwa nchi mbalimbali duniani ni 27% tu ya wanawake wanashirikishwa kwenye nafasi mbalimbali za uongozi kwenye nchi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa muktadha huo huo, Tanzania ime-*break records,* imevunja rekodi ya Kimataifa kwamba sasa Tanzania ushiriki wa wanawake kwenye nafasi za siasa na uongozi ni zaidi ya 45%. Haijawahi kutokea kwenye historia ya Bara la Afrika. Hili limechochewa kwa kiasi kikubwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwanamke ambaye ameweka historia ya kuwa Rais wa kwanza Tanzania mwanamke, lakini kupambana kuhakikisha anawainua wanawake kwenye nafasi mbalimbali za siasa na uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa niaba ya vijana wenzangu tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo kubwa na nzuri ambayo anaifanya. Kipekee, nimpongeze Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima, mama unafanya kazi kubwa na nzuri sana. Tumeona kazi zako kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa, eneo ambalo umefanya mageuzi makubwa ni kwenda kufanya *reform* kwenye Sera yetu ya Maendeleo ya Jamii ambayo toka mwaka 1996 tunaenda kufanya marekebisho mwaka huu wa 2026, miaka 30 imepita. Kwa hiyo, tunakupongeza sana kwa sababu mambo yamebadilika, na mahitaji yamebadilika ipo haja ya kufanya maboresho ya sera yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza kwa kupambana kuhakikisha kwamba tuna Kitengo cha Idara ya Maendeleo ya Jamii kwenye Sekretarieti zetu za mikoa. Ninaamini

kuwepo kwa kitengo hiki kunatoa *room* sasa kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenye mikoa kuweza kuwajibika ipasavyo na kuweza kupewa kipaumbele. Kwa hiyo, ninakupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, Katibu Mkuu pamoja na Menejiment ya Wizara na Maafisa Maendeleo ya Jamii nchi nzima. Hongereni kwa kazi kubwa na nzuri ambayo mnaifanya. Ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mwanamke siyo kiumbe dhalimu kama wengi ambavyo wanaweza kutafsiri. Kwenye Dini yetu ya Kiislamu mwanamke wa kwanza kipenzi cha Mtume Muhammad Ṣallallāhu ʿalayhi wa sallam *(S.A.W),* Bi. Khadija Alayhis-salām *(A.S)* alikuwa ni mfanyabiashara mkubwa sana, mwanamke mchapakazi, na mpambanaji ambaye alimsaidia Mtume kuweza kuutangaza Uislamu. Hicho ndicho kielelezo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaye kipenzi cha pili cha Mtume wetu Muhammad Ṣallallāhu ʿalayhi wa sallam *(S.A.W),* Bi. Aisha Alayhis-salām *(A.S),* msomi na mwanazuoni mbobezi aliyebobea kwenye masuala ya sheria, siasa na uongozi. Kwa hiyo, mwanamke siyo tu chombo cha starehe au chombo cha kukaa nyumbani kwa ajili ya kulea watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke ni kiungo mchezeshaji kwenye familia. Kwa maana mwanamke akipewa elimu, na akawa na ujuzi, ana msaada mkubwa sana kwenye familia na ana msaada mkubwa sana kwenye Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa ya malezi na kila Mbunge ambaye amezungumza hapa amekuwa akiligusia suala hili, malezi yamekuwa ni changamoto kubwa sana kwa watoto wetu. Nami ninaomba nije na *solution.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *solution* ya kwanza Mheshimiwa Waziri niombe sana, nimeona kwenye bajeti yako mmesema mtapitia vikao vya *RCC* na *DCC*. Ni ukweli nami nimeshakuwa Mkuu wa Wilaya kwa miaka 10. Vikao hivi vya *RCC* na *DCC* vina mambo mengi sana ya kujadili ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, leo hii kwenye Kamati za Wilaya za *DCC* na kwenye mkoa tunazo Kamati nyingine; tuna Kamati ya Ushauri ya Mahakama, na kuna Kamati ya Uvunaji wa Misitu. Kwa nini tusiwe na kamati maalum ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwenye ngazi za wilaya na kwenye ngazi za mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu suala la ukatili wa kijinsia ni suala mtambuka, siyo tu la maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii. Tunahitaji ku-*engage* Sekta ya Elimu, tunahitaji ku-*engage* TAMISEMI kwenye masuala ya watendaji wetu, tunahitaji ku-*engage* Polisi kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tunahitaji ku-*engage* watu wetu wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zikiwepo hizi kamati za kupambana na ukatili wa kijisa kwa mujibu wa sheria, maana yake tuna uwezo sasa wa kuunda *tracking system* hata Mheshimiwa Rais akiwepo Ikulu awe ana uwezo wa kujua kesi ngapi zimeingia leo kwenye mfumo, zimesikilizwa ngapi, ziko wapi, zimekwamia wapi, aliyekuhamisha ni nani, na kwa nini amekwamisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kesi nyingi watu wanaogopa kwenda kuzipeleka kwenye vyombo vya sheria kwa sababu nyingi zikienda hazifiki mwisho. Hata zikifika mwisho, wahusika wanarudi mtaani na bado kazi ile ile inaendelea. Kwa hiyo, nami ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri hili jambo tulifanyie kazi kwa uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunajua Wizara inasajili taasisi zisizo za kiserikali na tunajua tuna mkakati wa kuhakikisha tuna-*engage private sector* 70% kwenye maendeleo ya nchi, lakini, kwa mujibu wa taarifa ya bajeti 93% iliyoiwasilishwa, 93% ya fedha ambazo zinaingia kwenye haya mashirika yasiyo Serikali zinatoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa maslahi na mustakali wa usalama wa Taifa letu ipo haja ya kufanya *due diligence,* siyo tu afisa maendelee kuangalia juu juu. *Due*

diligence kuhakikisha kwamba hizi fedha kweli zinakuja kwa malengo na mustakabali wa usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho Mheshimiwa Waziri ninaomba sana kwenye suala la maendeleo ya jamii, leo tunaona kuna miradi ya kimkakati inakuja kwenye mikoa yetu, kampuni ambazo zinakuja kufanya hizi shughuli kwa kweli wanakuja na Maafisa Maendeleo ya Jamii wanaotoka kwenye kampuni zao. *Engagement* ya hao maafisa ya maendeleo ya jamii kwenye kata, ushiriki wao umekuwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninafikiri ipo haja ya kukaa chini na wenzetu labda wa Wizara hizi za kimkakati, za uzalishaji, za biashara, na za viwanda kuona umuhimu wa ku-*engage* wenzetu maafisa maendeleo ya maendeleo kwenye kata na kwenye wilaya ili washiriki kikamilifu kwenye kutekeleza hiyo miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mheshimiwa Waziri tuna mifuko zaidi ya 74 ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, lakini kule kwenye ngazi za vijiji wanajua 10%, na *TASAF,* lakini, ile mifuko mingine ya kuwawezesha kiuchumi, kuna Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali, kuna mfuko mkoani kama *SIDO*.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

TAARIFA

MWENYEKITI: Mheshimiwa *engineer,* taarifa.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa mzungumzaji. Amezungumza vizuri sana na amenifanya nitoe taarifa hii kwamba fursa kubwa ya mfuko ya 30% ambayo ingeweza sana kusaidia jamii katika manunuzi ya umma haijawahi kufanyiwa kazi ipasavyo na Wizara hii. Ndugu yangu ongezea hii na wala haijasemwa katika hotuba hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Abdallah, unaipokea hiyo taarifa?

MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa hiyo na kwa kuhitimisha, nimwambie Mheshimiwa Waziri ipo haja sasa ya Wizara Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ku-*integrate* na Wizara zote zenye mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, ili Maafisa Maendeleo ya Jamii huko chini waweze kuifahamu hiyo mifuko na iweze kuwashirikisha wananchi wetu ipasavyo ili kweli mifuko hii iweze kuwanufaisha kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Zainab Abdallah. Nilimtaja Mheshimiwa Eric Shigongo na tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Naibu Waziri na mtoa hoja wajiandae.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza nianze kwa shukrani kwa watu watatu. Kwanza, nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini kwa jambo moja kubwa kabisa alolifanya, kumkinga mtoto wangu dhidi ya *pornography,* dhidi ya picha za ngono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hii hauwezi ku-*access* mitandao ya ngono kabisa na haya yalitokea tu mara baada ya Mheshimiwa Rais kuingia madarakani. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kumpongeza sana Rais wangu. Ni jambo jema tumewalinda watoto wetu. Ninaishukuru sana nchi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, na Katibu Mkuu. Kipekee ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana. Waheshimiwa Wabunge, tupitisheni bajeti yake, fedha ni kidogo, lakini, bajeti ijayo

ninaomba tumwongezee fedha, ana kazi kubwa, anahitaji msaada wetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita nilienda Wizarani kwake. Hili lazima niliseme, nilikuwa ninafuatilia cheti cha usajili wa *NGO* ofisini kwake. Katibu muhtasi wa Mkurugenzi wa Usajili wa *NGO* hakunitendea vizuri, nilipotoka pale nilimpigia simu Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri mwenyewe aliamua kwenda kwenye ile ofisi akakichukua cheti akaniletea mpaka hapa Bungeni. Kwa kweli dada yangu unafanya kazi nzuri, Mungu aendelee kukubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa tatu ninayetaka nimpongeze ni Mkurugenzi wa Halmashauri yangu ya Buchosa, kwa kukusanya fedha nyingi sana kwenye jimbo langu na hatimaye kupata ile 10% ya kuwahudumia akina mama, vijana pamoja na walemavu. Nina mambo mawili ya kuchangia. La kwanza, upo uhusiano mkubwa sana kati ya idadi ya watu na maendeleo ya Taifa. Upo uhusiano mkubwa. Wazungu wanasema, *the larger the population the larger the economy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lina ushahidi. China ina watu wengi na uchumi wake ni mkubwa. Marekani ina watu wengi, uchumi wake ni mkubwa. India ina watu wengi, uchumi wake ni mkubwa. Pia Nigeria ina watu wengi, uchumi wake ni mkubwa. Ninalisema hili kwa sababu ninaona sasa dunia inaelekea kwenye ku-*collapse* kwa *population,* kuanguka kwa idadi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo juhudi zinafanywa na matajiri wa dunia hii kuhakikisha kwamba idadi ya watu inapungua kutoka shilingi bilioni saba mpaka shilingi bilioni sita. Wanapozungumza kupunguza watu wanazungumzia Afrika. Kupunguza watu Afrika siyo kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushahidi hapa, ningependa niisome hii *data* hapa bila Waheshimiwa Wabunge waweze kuelewa, "Uwiano wa mwanamke kwa idadi ya watoto wanaozaliwa." Ninarudia tena, "*fertility rate* kati ya mama na

watoto wanaozaliwa hapa Afrika mwaka 2022 ilikuwa mwanamke mmoja watoto wa 4.21, mwaka 2023 ilikuwa mwanamke mmoja, watoto wa 4.16, mwaka 2024 ilikuwa mwanamke mmoja watoto wa 4.10 na mwaka 2025 ilikuwa watoto wa 4.05." Hiyo inaashiria kwamba watoto wanazidi kupungua kwa mwanamke mmoja, idadi ya watu inazidi kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania, mama, watoto wangapi? Mwaka 2022 mwanamke mmoja alikuwa ni watoto wa 4.67. Mwaka 2023 ni mwanamke mmoja ya watoto wa 4.61. Mwaka 2024 mwanamke mmoja 4.457, mwaka 2025 mwanamke mmoja watoto wa 4.52. Ukiangalia hizi data idadi ya watoto inazidi kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena kusema, uko uhusiano mkubwa sana kati ya idadi ya watu na ukuaji wa uchumi. Ninaomba nisimame hapa kwa ujasiri kabisa niseme tunahitaji kuongeza idadi ya watu kwenye Taifa letu. Tunahitaji kuzaa watoto wengi sana kwenye Taifa hili. Kampeni iliyoko ni kupunguza idadi ya watu. Ziko chanjo zinaletwa, watoto wetu wanachanjwa kuzuia wasizae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya P2. Mwanamke anatakiwa anywe P2 mara nne kwa mwaka. Watoto wetu wanakunywa karibu kila siku, wanaharibu homoni zao wanashindwa kuzaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme, iko sababu ya kuhakikisha idadi ya watu inaongezeka. Kazi ya Serikali itabaki moja kuhakikisha kwamba hawa watu wanaozaliwa wanapata elimu na wanawezeshwa ili kiweze kuwa kizazi kazi chenye uwezo wa kuchangia maendeleo ya Taifa. Tukiendelea kupungua hamwezi kunielewa lakini iko siku nitakuja kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina walikuwa wanazaa mtoto mmoja. Sasa hivi wamebadilisha sera, wanazaa watoto wawili kwa sababu wameshajua umuhimu wa kwamba idadi ya watu lazima iongezeke ili uchumi uendelee kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme neno? Ninaomba niseme mambo yafuatayo: La kwanza, wazazi katika Taifa langu mimi ni mzazi, nina watoto, tutimize wajibu wetu kwa familia zetu. Tutimize wajibu wetu kwa watoto wetu. Wazazi tukae na watoto tuwafundishe watoto wetu, tusiiachie Serikali kutulelea watoto wetu. Mimi ni baba, lazima niwepo nyumbani kulea watoto wangu pamoja na u-*busy* nilionao. Tuwanyang'anye watoto *device* za mkononi. Tuwanyang'anye watoto kompyuta mpaka watakapotimiza umri wa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyetengeneza *iPad* mwenyewe *Bill Gates* mwanaye haruhusiwi kuishika kompyuta mpaka atakapokuwa na miaka 14. Kompyuta na *gadgets* zinaharibu akili za watoto wetu. Tujiulize tunataka Taifa la namna gani? Tunataka Taifa lenye uweza wa kushindana na wenzetu, tufanye mambo mawili. Tuzae watoto na watoto wetu tuwalee vyema. Akina baba tutimize majukumu yetu nyumbani, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sheria zisimamiwe. Ninamwona dada yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima anapambana kila siku. Tuna sheria nzuri sana tuzisimamie wanaozivunjwa waadhibie kwa mujibu wa sheria, hakuna mtu yuko juu ya sheria. Ukimbaka mtoto wetu, ukimnajisi mtoto wetu, na ukitembea na mtoto chini ya umri ushtakiwe kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine, sijui hili litawafurahisha wangapi, siwezi kuelewa. Nimefanya utafiti huko tunakopita kote kwenye baa na sehemu za hoteli wanaohudumia wengi ni mabinti wadogo wadogo na wengi ni *single mothers.* Wengi wamepata mimba wanahudumia hawana baba nyumbani na wana watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Bunge lako Tukufu litafakari jambo hili. Nilipokwenda Marekani juzi juzi nikakuta sheria ya *tip* kwa mhudumu ni *compulsory by law;* ni lazima kisheria. Ninaomba Bunge lako Tukufu litafakari, wanalipwa shilingi 5,000 kwa siku. Matokeo yake wanashindwa kulea watoto, wanaingia kwenye mambo yasiyo sahihi. *Tip* iwe kisheria, *tip by law*.

Ukihudumiwa chini kule iandikwe *tip percept,* hii itasaidia kuwasaidia akina dada hawa. Pia, itawasaidia akina dada kukusanya fedha zao kwa sababu watalazimisha katika ile risiti hatimaye Serikali itakusanya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana. Ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunamalizia na Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Naibu Waziri na mtoa hoja wajiandae. Waheshimiwa ninaongeza muda hadi tutakapomaliza shughuli za leo.

MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye jioni hii ya leo tunajadili hoja muhimu sana ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii na *package* yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tumpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mapenzi yake makubwa na hasa kipindi kile alipoivunja Wizara hii ilipokuwa imechanganyika na Wizara ya Afya kutengeneza Wizara inayojitegemea ya Maendeleo ya Jamii na kumpa dada yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima, kuweza kuiongoza Wizara hii. Dada yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima unafanya kazi nzuri, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Eng. Maryprisca kwa kazi kubwa, na nimpongeze Katibu Mkuu Maswi, ninamfahamu sana. Hii ni *encyclopedia* ya Serikali katika mambo mbalimbali. Imani yangu ni kwamba Wizara hii itaendelea kufanya vizuri, lakini, na Amon Mpanju na dada yangu Felister, Timu imekamilika na Wakurugenzi wao na timu yote ya kiwizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe kwa kunipa hii fursa. Yangu ni machache sana siku hii ya leo. Maafisa Maendeleo ya Jamii ndio *agent of change* katika maendeleo ya nchi. Leo hii tunaona Maafisa Maendeleo ya Jamii wako katika

Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako huko kwa hakika wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni shahidi kwa sababu kazi yangu ya kwanza nilikuwa mtumishi wa Serikali nikiwa kama mtaalamu katika Idara ya Kilimo, lakini, wenzetu wengine wako katika Idara ya Maendeleo ya Jamii. Ninaishukuru Wizara, hivi karibuni ilifanya kazi kubwa ya kuwasaidia Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na TAMISEMI kuwapatia angalau pikipiki, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme, tukitaka maendeleo yaende kwa kasi lazima tufanye maamuzi. Jambo la kwanza, tuhakikishe tunawawezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii tuliokuwa nao. Bahati mbaya sana ukienda kila halmashauri, Afisa Maendeleo ya Jamii amekuwa kama ombaomba wa gari ya afisa mwenzake katika idara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Wizara ya TAMISEMI na Maendeleo ya Jamii wameanza kufanya kazi hii kubwa, lakini niwaombe, sasa twende tukawawezeshe vya kutosha. Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii awe na gari yake, kwani kazi yao ni kubwa sana. Wakati mwingine wanakuwa kama *spare tyre*, *spare tyre* haitumiki mpaka gari imepata pancha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ikitokea tatizo lolote ndiyo anaambiwa. Siku ya Mwenge, Afisa Maendeleo ya Jamii, sijui kichocho Afisa Maendeleo ya Jamii, sijui jambo lolote Afisa Maendeleo ya Jamii. Hawa ndio *agent of change*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kubwa sana, Wizara inafanya kazi vizuri na TAMISEMI inafanya kazi vizuri. Sasa twende tukawaangalie Maafisa Maendeleo ya Jamii tuwawezeshe vitendea kazi; na ofisi zao zisomeke vizuri. Sehemu nyingine ndiyo utakuta vichochoroni huko iko katika karakana, haipendezi hata kidogo. Ninadhani hili tukilifanya hivi tutawasaidia sana Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tuna Wizara na taasisi jumla ya takribani 325. Mimi siamini hata kidogo, hakuna Wizara

ambayo haifanyi na masuala ya maendeleo. Ombi langu ni kwamba Serikali tufanye mapinduzi makubwa katika kila Wizara, katika kila taasisi tuanzishe dawati la maendeleo ya jamii, lakini Wizara ya Maendeleo ya Jamii tuanzishe Kitengo cha *Sector Coordination Unit* kinachohusu maendeleo ya jamii. Kitakuwa kinapata taarifa kutoka Wizara zote kwa ajili ya mustakabali wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata siku Rais akitaka taarifa ya jambo fulani, akiuliza Waziri wa Maendeleo ya Jamii atampa taarifa zote za umeme, maji, kilimo, na sekta ya maendeleo ya jamii. Wizara hii kazi yake ni kubwa. Kwa hiyo, ombi langu kubwa, Wizara zote ikiwezekana tuwe na dawati maalumu la mtaalamu wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu sehemu nyingine wapo, lakini siyo Wizara zote. *TANROADS* tunamtaka, *TARURA* tunamtaka, *TRA* wawepo, watawanyike huko Maafisa Maendeleo ya Jamii wapeleke taarifa Wizarani. Waziri akisimama hapa anatoa taarifa ya maendeleo jinsi gani watu wake wamefanya na Wizarani kwenyewe kuwe na hicho kitengo, Mkurugenzi au Mkurugenzi Msaidizi wa *Sector Coordination Unit*. Tukifanya hivi tutakuwa tumeisaidia sana nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja yote hii ya Wizara hii kwa ukubwa wake, lakini ombi langu ni lile, sitaki kuwaona, ninatamani sana wale dada zetu huko na vijana wenzetu sasa yale mawigi yasiwe yanaingia vumbi peke yake. Wawe na magari mazuri ya kiyoyozi, kazi yao ni kubwa, lazima tuitukuze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge hapa tunajua ndio wanatusaidia sana huko katika halmashauri zetu. Tuwasimamie watu hao wawe na heshima kubwa, thamani yao ionekane kwamba wao ndio *agent of change* katika Taifa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono Hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ni Wizara mtambuka inayobeba maisha ya mwanadamu ya kila siku na hivyo basi, ina umuhimu wa kipekee sana katika kuratibu ukuaji wa mtoto kuanzia wazo la kupata mimba, kutunga kwa mimba, ukuaji wa mimba, kuzaliwa mtoto mpaka kufika umri wa kujitambua mtoto wa miaka nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu, ukamilifu wa mtu unajengwa kuanzia miaka sifuri hadi miaka nane. Hiki ni kipindi muhimu sana katika ku-*shape* maisha ya binadamu kitabia, malezi na makuzi. Kutokana na umuhimu wa kipindi hiki cha makuzi, ni muhimu sana Serikali kuendelea kuwekeza katika huduma muhimu zitazochochea makuzi endelevu na salama, ikiwemo huduma za afya kwa mama na mtoto, ushauri nasaha kwa wazazi watarajiwa na hapo Serikali ishirikiane na wadau mbalimbali kama vile viongozi wa dini, mashirika yasiyo ya kiserikali, na watu wenye taaluma ya saikolojia ya binadamu katika kutimiza azma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii, ninaomba kuipongeza Serikali kwa kuiongezea Wizara hii shilingi bilioni 24.5 katika bajeti hii, lakini bado ninatamani kuona bajeti ya Wizara hii ikiongezwa kadri fedha zinapopatikana ili kukidhi mahitaji ya Wizara katika kuhudumia jamii ili kujenga kizazi imara na chenye weledi, kuelekea Dira ya 2050, hasa katika kipindi hiki ambacho tunashuhudia mmomonyoko mkubwa wa maadili kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya ya utangulizi, ninaomba nichangie kwenye mambo machache, nikianza na ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na mabinti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wanawake wengi nchini ambao wanapitia unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa wenza hao,

na wakati mwingine hata kutoka kwa ndugu wa wenza wao na waathirika wengi ni wanawake wa vijijini. Baadhi ya matukio haya yanaripotiwa aidha kwa Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa, Madawati ya Jinsia au Polisi, lakini baadaye wanawake hawa wengine huamua kufuta kesi hizi au hawaonekani wala kutoa ushirikiano na mwisho wa siku kesi hizi huishia hewani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili inabidi liangaliwe kwa jicho la tatu na Serikali, kwani kesi hizi nyingi zinafutwa au mhanga wa ukatili anaamua kutotoa ushirikiano, siyo kwa kupenda bali kutokana na ukweli kuwa hana *option* nyingine bali kukubali yaishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria mama wa kijijini ambaye hana kipato chochote na ana Watoto, akiondoka kwa mweza wake anaenda wapi? Hana pesa ya kujikimu yeye mwenyewe licha watoto wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaiomba Serikali iongeze Maafisa Ustawi wa Jamii kwenye ngazi zote ili waweze kutoa ushauri nasaha kwa wanawake hawa ili watambue kuwa maisha yao yana thamani kubwa sana na kwamba unyanyasaji haukubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwenye eneo hili niishauri Serikali iongeze nyumba salama *(safe houses)* kwa ajili ya wahanga hawa, na siyo kuongeza tu, pia iboreshe mazingira ya hizi *safe houses* na kuweka wataalamu wa ushauri nasaha ili kuwasaidia wahanga hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapokuwa kwenye hizi *safe houses* wakipatiwa hifadhi na ushauri nasaha, Serikali iwekeze pia katika kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali ili hapo baadaye angalau waweze kufanya kazi za kuwawezesha kupata kipato cha kujikimu, na hapa niombe wawekwe kwenye mpango wa kupatiwa mikopo isiyo na riba ili waweze kuanzisha miradi itakayowafanya wasiwe tegemezi hata kama hapo baadaye wataamua kurudi kwa wenza wao, kwani tunatambua umuhimu wa malezi ya watoto familia inapokuwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la ubakaji kwa mabinti zetu na mimba zitokanazo na ubakaji. Wapo mabinti wanabakwa na baba zao wa kuwazaa au kaka zao na wengine wanapata ujauzito. Familia nyingi zimekuwa zinaficha matukio haya kwa kisingizio cha kuificha aibu kwa familia. Matendo haya yanaacha makovu ya kisaikolojia kwenye akili za mabinti hawa hasa wanapokosa ushauri wa kitaalamu kutibu majeraha haya ya kisaikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria binti aliyebakwa na baba yake wa kumzaa na kupata ujauzito, akizaa anamwangaliaje mtoto huyu? Katika mahangaiko yake anaweza kuamua kumuua mtoto huyu au kumtupa kama njia ya kuondokana kwa fedheha hii, na kwa bahati mbaya binti huyu akikumbana na mkono wa sheria, basi atapelekwa mahakamani na atahukumiwa kwa kosa la jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kovu kwenye akili ya binti huyu haliwezi kupona. Binti huyu hata asipokumbana na mkono wa sheria na akabahatika kupata mwenza wa kumuoa, ndoa yake itakuwa ya mashaka sana na dosari nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo muumini wa utoaji mimba kwani ni dhambi na inapingana na imani ya dini yangu, lakini katika hili huwa ninajiuliza sana kwa nini katika jambo hili binti huyu asiwe na *option* kama mkataba wa *Maputo Protocol* unavyoelekeza na sisi tulisaini mkataba huu Novemba 5, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kisaikolojia binti huyu ameshavurugwa sana, lakini sheria hairuhusu kutoa mimba kihalali kwa maana ya kwenye hospitali zinazotambulika, mwisho wake anaweza kuamua kwenda vichochoroni kutoa mimba hii, na hapa anahatarisha maisha yake kwani anaweza kufa au kupata *complications* zinazoweza kumpelekea ashindwe kupata watoto baadaye au kizazi kuharibika na hivyo kubidi kitolewe kuokoa maisha yake. Kosa la mzazi wake linaenda kuharibu maisha ya binti huyu maisha yake yote. Anakuwa *victim* na huku baba mzazi akibaki huru bila hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ilisaini mkataba wa *Maputo protocol,* ninadhani ni wakati mwafaka sasa wa kuangalia Sheria yetu ya *Abortion* na kuifanyia marekebisho kuwaokoa mabinti zetu wanaobakwa na hii iendane na kuhakiki taarifa za ukweli kwa waathirika kama ni kweli pasi shaka walibakwa, ili wasichana wengine wasije wakatumia vibaya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, hivyo ninaomba pia nichangie pia kwenye maeneo ambayo tulitembelea kama Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na vituo vya kuhudumia wazee. Niiombe Serikali iharakishe ujenzi wa vituo vya wazee kikanda ili kusogeza huduma karibu na kupunguza mtapanyo wa rasilimali fedha kuhudumia vituo vilivyopo kwa sasa. Hapa ninaomba kuishukuru Serikali kwa kukubali kuongeza bajeti ya Wizara hii shilingi 24,500,000,000 ambapo shilingi bilioni tano zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa makazi mawili ya kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mahabusu ya watoto Upanga Dar es Salaam. Kituo hiki kiko kwenye *prime area* na matumizi yake kwa sasa hayana tija kwa Wizara wala kwa Serikali. Nishauri kuwa ijengwe mahabusu nyingine kwenye eneo lenye nafasi kubwa ili vijana wanaotunzwa hapa waweze kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na eneo la sasa litafutiwe mwekezaji wa kuliendeleza ili kuongeza mapato ya Serikali. Tuna mifuko ya hifadhi ambayo inaweza kutumika kuwekeza kwenye eneo hili lenye *potential* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Arusha na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kijitonyama Dar es Salaam. Niiombe Serikali iviangalie vyuo hivi kwa jicho la tatu, maana ndiyo vyuo vinavyotoa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii, fani muhimu sana katika makuzi na malezi ya watoto hasa kuelekea Dira ya mwaka 2050 ili tuwe na kizazi chenye uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sera ambayo halmashauri zetu zinapaswa kutenga asilimia tatu ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya ulinzi wa watoto. Ninaomba sera hii itiliwe mkazo ili fedha hizi zitumike kujenga maeneo ya kulelea watoto, kwa mfano kwenye stendi za mabasi au kwenye masoko ili kuwasaidia kina mama kuweza kufanya kazi za kiuchumi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la Sheria ya Mtoto. Kwa kuwa Wizara hii ndiyo ina jukumu la malezi ya watoto na kuhudumia wanawake, niombe ione umuhimu wa kuhakikisha sheria ya mtoto inafanyiwa marekebisho ili kumlinda mtoto, ikiwa ni pamoja na sheria inayoruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 au 15 kwani imepitwa na wakati, na hapa niombe umri huu uongezwe mpaka miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningeomba Wizara ishirikiane na Wizara ya Sheria, ni kwenye Sheria ya Ndoa na Mirathi. Tumeshuhudia wajane wengi wakisumbuliwa na watoto waliozaliwa nje ya ndoa kipindi wenza wao wanapofariki. Watoto hawa huwa wanatambulika kama warithi halali wa marehemu na hivyo kupata mgao wa mali, lakini mali zilizopatikana wakati marehemu alipokuwa na mahusiano na mama zao kipindi cha uhai wake hazihesabiki wala kuguswa kwenye mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani hii ni kumtesa mama mjane kisaikolojia, hivyo ninashauri sheria hii ifanyiwe marekebisho ili mali za mama huyu nazo ziingizwe kwenye mirathi ili watoto wote wapate haki sawa ya mali za Marehemu baba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, kuna mali ambazo mama mjane na mwenza wake walizipata kabla watoto wa nje ya ndoa hawajazaliwa, nazo hizi zisiwe sehemu ya mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watalaamu wote kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inafanya kazi nzuri sana, lakini jukumu la Wizara ni kubwa sana. Ninaomba kushauri ili hali ianze kuleta mafanikio Chanya, ni muhimu Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii waliopo kwenye kata wapatiwe usafiri ili waweze kuwazungukia wanajamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya watoto wa mitaani inaongezeka kila kukicha. Kama elimu kwa wazazi na walezi isipotolewa, watoto watapoteza maadili. Pia kwa sasa watoto wa kike na kiume wanafanyiwa matendo yasiyo sahihi. Tuje na sheria mpya na kali ya kuwalinda watoto wetu wote, tuanze kuandaa kuunda mamlaka ya kulinda haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri tusimamie kikamilifu upatikanaji wa asilimia tatu kutoka halmashauri zetu ziende kulinda haki za watoto kwa kuzingatia kwamba fedha kutoka nchi nyingine hasa *USA* hatutapata hivyo *NGOs* nyingi zitashindwa kutekeleza majukumu yake. Watoto ni wetu na fedha zitoke kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, pawepo na sheria ya kuwabana wazazi hasa baba ahudumie mtoto wake. Imeshakuwa tabia ya kuzalisha kisha kukana au kutokutoa huduma kwa ajili ya mtoto. Siku hizi bodaboda wanazalisha sana, lakini hawatoi matumuzi wala malezi kwa mama na mtoto, hili linatakiwa kuwa na sheria kali ya kuwalinda watoto na mama pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ikiendelea baada ya miaka 20 ijayo tutakuwa na Taifa lililolegea kabisa na wengi hawatakuwa na uwezo wa kufikiria na kuitumikia nchi. Hatma ya nchi yetu iko kwenye mikono ya Wizara hii. Hivyo tuangalie namna bora na shirikishi ya kuwatumia viongozi wa kidini, lakini pia tuboreshe mitaala hasa kwa shule za msingi, watoto wafundishwe namna ya kumtambua mtu mwenye nia ovu, wafundishwe kwamba wasikubali kuguswa sehemu nyeti na mtu yeyote. Vilevile

mtu akibainika, lazima sheria ishike mkondo wake kuhakikisha anapata adhabu kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijijini imeshawahi kutokea mwalimu mwenye UKIMWI kwa kutumia nafasi yake aliambukiza wasichana wengi kisha baada ya kubainika akakimbia na hajapatikana mpaka leo, kwani kumfatilia tu Polisi wanahitaji hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Mungu atubariki tuokoe watoto wetu na vizazi vijavyo kuanzia sasa ambapo pia tumeshachelewa.

MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya na uhai siku hii ya leo. Kipekee, ninampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuhakikisha tunaunda jamii ya watu wenye ustawi na iliyostaarabika kwa kuweka mipango kabambe kama inavyoainishwa katika Mpango wa Taifa 2025/2050 na Dira ya Taifa 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuifikia mipango hiyo na kuiishi Dira ya Taifa 2050 ni lazima tukubaliane kuwa Wizara hii ni mtambuka na muhimu sana katika mustakabali wa Taifa letu katika nyanja zote za maendeleo na ustawi wa jamii yetu. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii chini ya Waziri shupavu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, lazima tuhakikishe kuwa mipango ya Wizara nyingine zote zinazingatia usawa katika kuendesha shughuli zake. Taasisi nyingine kama vile Polisi, Magereza, Asasi za Kiraia nazo haziachwi nyuma ili kusimamia maadili ikiwa ni pamoja na kuzuia vitendo vya ukatili kwa jinsia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa elimu kwa umma liwe ni jambo la kipaumbele kwa Wizara hii ili kuifahamisha jamii haki na wajibu wa msingi katika kujenga jamii yenye usawa na inayoheshimiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu zote na vyuo turejee mitaala yetu ili kuhakikisha kuwa mafunzo yetu ya kimaadili, mila na desturi zetu vinatoa mchango katika kujenga jamii yenye ustaarabu na usawa ikiwepo kuthamini utu na hadhi ya binadamu. Kupiga marufuku ulevi, matumizi ya dawa za kulevya na uzembe kwani tusipokuwa na mkakati mahsusi tutazalisha Taifa goigoi hasa vizazi vijavyo na watu goigoi hawawezi kusimamia tunu za Taifa ikiwemo mila, tamaduni, maadili na mengineyo ambavyo ni muhimu sana katika kuleta maendeleo na ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ADONIS A. BITEGEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri, Naibu Waziri na watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na wale waliopo katika Sekretariat za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa yafuatayo:-

(i) Mageuzi makubwa na mafanikio katika utoaji huduma za maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake na makundi maalumu;

(ii) Kuimarisha rasilimali watu kwa kuajiri watumishi wapya na kuwapa mafunzo Maafisa Ustawi wa Jamii na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali wakiwemo wa halmashauri;

(iii) Kuendelea kuimarisha Taasisi za Maendeleo ya Jamii ya Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii;

(iv) Kwa kazi nzuri ya utambuzi, uratibu na uendelezaji wa wafanyabiashara ndogondogo; na

(v) Kwa jitahada zinazofanywa za kuimarisha malezi, maadili, maendeleo na ustawi wa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri yafuatayo: Serikali ifanye mapitio/kukamilisha mapitio ya sera, sheria na miongozo ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake na makundi maalum ili yaendane mahitaji ya sasa, vipaumbele na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050; na Serikali iwekeze zaidi katika kutoa ajira mpya za Maafisa Maendeleo na Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa/Halmashauri pamoja na kuwawezesha vitendea kazi kama pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Muleba ina kata 43; Halmashauri ya Muleba ina kata 43 na ina Maafisa Ustawi wa Jamii 12 wa kata na ina upungufu wa mkubwa wa Maafisa Ustawi wa Jamii 31. Halmashauri ya Muleba ina Maafisa Maendeleo 38. Tunaomba kuongezewa Maafisa Maendeleo 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI katika kufuatilia na kupeleka watumishi wapya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii katika halmashauri, kuendelea kuwapa mafunzo na kuwawezesha usafiri. Hatua hii itaongeza ufanisi katika kazi za maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe elimu nchi nzima ya uwepo wa fursa za kuwezesha kiuchumi ikiwemo mikopo makundi mbalimbali kupitia Wizara husika ili wananchi waweze kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara iimarishe utoaji elimu utakaowafikia wananchi wengi kwa njia mbalimbali ikiwemo runinga na redio kuimarisha usalama wa mtoto katika matumizi ya teknolojia na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijenge vituo vizuri vyenye miundombinu rafiki zaidi vya malezi ya watoto wakiwemo yatima katika wilaya/halmashauri zote ili maeneo mengi yafikiwe na huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ongezeko la mashauri ya matunzo ya watoto na mmomonyoko wa maadili; Serikali iweke

mkakati maalum wa kukabiliana na kuongezeka na mashauri ya matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa, mmomonyoko wa maadili katika ngazi ya familia unaosababisha watoto wengi kukosa malezi bora ya msingi na kusababisha migogoro ya kisheria na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za Wizara za kujenga usawa na haki kwa jinsia zote zisielemee upande mmoja wa jinsia ya kike. Zijikite katika kujenga jamii inayoheshimiana na kukemea unyanyasaji wowote wa aina yote hata ule dhidi ya jinsia ya kiume. Jinsia ya kiume pia iwezeshwe kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa mmomonyoko wa maadili na kushuka kwa uzalendo katika baadhi ya jamii, kuna umuhimu Serikali kupitia Wizara husika ikafanya tathmini au utafiti na kuunda taasisi au baraza au kujenga mfumo imara zaidi ya kusimamia masuala ya ustawi wa jamii kuanzia ngazi ya Taifa, Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda za maendeleo ya jamii ziwe za kudumu katika mabaraza ya ushauri ya mikoa, wilaya na madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke utaratibu wa kutoa elimu kwa wanandoa watarajiwa au wapya kuhusiana na masuala ya ustawi wa jamii yakiwemo malezi bora ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuweka msisitizo katika ustawi wa wananchi, maendeleo ya wanawake, vijana, watoto pamoja na makundi maalum nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayoendelea kuifanya katika kuratibu ajenda zinazogusa moja kwa moja ustawi wa jamii na maendeleo ya rasilimali watu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza katika maeneo matatu ambayo ninaamini yana mchango mkubwa katika uthabiti wa jamii na uchumi wa Taifa. Kwanza, kuhusu malezi na maendeleo ya vijana, leo Taifa letu linapitia mabadiliko makubwa ya kijamii na kiteknolojia. Matumizi ya mitandao ya kijamii yanaongezeka kwa kasi huku changamoto za malezi, afya ya akili, matumizi ya dawa za kulevya pamoja na mmomonyoko wa maadili nazo zikiongezeka katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *TDHS 2022,* takribani 27% ya wasichana wenye umri wa miaka 15 hadi 19 wameanza kuzaa. Aidha, vijana wengi wanaomaliza elimu bila stadi na ajira hujikuta kwenye mazingira hatarishi yanayoathiri ustawi wao pamoja na nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hizi, kuna haja ya kuendelea kuboresha sera za maendeleo ya jamii ili malezi, afya ya akili, maadili pamoja na maendeleo ya vijana, viwe sehemu ya ajenda ya maendeleo ya Taifa. Tanzania tayari ina wataalam wa maendeleo ya jamii pamoja na ustawi wa jamii, lakini mfumo huu bado haujatumika kikamilifu kama sehemu ya mfumo wa kinga na ustawi wa familia katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania ina takribani kata 4,000, ninaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mfumo wa Maafisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Ustawi wa Jamii katika ngazi ya kata ili wawe sehemu ya mfumo wa kusaidia malezi, afya ya akili, maendeleo ya vijana pamoja na ulinzi wa watoto katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi itasaidia kujenga mfumo wa mapema wa kinga ya changamoto za kijamii, kuimarisha familia pamoja na kujenga kizazi chenye maadili, nidhamu na uwezo mkubwa wa kushiriki katika maendeleo ya Taifa. Aidha,

kuna haja ya kuimarisha ushirikiano kati ya wataalam hawa, shule, vituo vya afya, viongozi wa dini pamoja na Serikali za Mitaa ili kujenga mfumo shirikishi wa malezi na maendeleo ya jamii unaoweza kutoa msaada wa mapema kabla changamoto hazijawa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili nitakaloliongelea ni uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Wanawake wa Tanzania wana mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa hususan katika kilimo na biashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wanawake wengi bado wako kwenye uchumi wa kujikimu kutokana na changamoto za taarifa za masoko, matumizi ya teknolojia, urasimishaji wa biashara pamoja na upatikanaji wa huduma rasmi za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili bado kuna fursa kubwa za kimfumo zinazoweza kuongeza tija na ushiriki wa wanawake katika uchumi rasmi. Kwa mfano, Serikali inaweza kuimarisha matumizi ya mifumo iliyopo ya Serikali za Mitaa, Maafisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Vituo vya Maendeleo ya Wanawake kama njia ya kuwafikia wanawake kwa karibu zaidi katika elimu ya kifedha, matumizi ya teknolojia, urasimishaji wa biashara pamoja na taarifa za masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, bado kuna fursa kubwa katika matumizi ya teknolojia na mifumo ya kidijitali kuwaunganisha wanawake na huduma za kifedha, biashara za mtandaoni pamoja na masoko mapana zaidi. Kadhalika, utekelezaji wa sera ya 30% ya zabuni za umma kwa makundi maalum bado unaweza kuimarishwa zaidi ili wanawake wengi zaidi waweze kushiriki katika uchumi rasmi kupitia zabuni na manunuzi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali iendelee kuboresha sera za uwezeshaji wanawake ili zisijikite zaidi kwenye mikopo pekee, bali ziweze kuwaunganisha wanawake na masoko, teknolojia, urasimishaji pamoja na shughuli za uzalishaji zenye tija. Hatua hizi zitasaidia kuongeza kipato cha familia,

kupunguza umaskini pamoja na kuongeza mchango wa wanawake katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ninalochangia ni kuhusu makundi maalumu. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha ujumuishi wa makundi maalum, bado kuna changamoto katika matumizi ya teknolojia saidizi, mifumo jumuishi ya kidijitali pamoja na ushiriki wa watu wenye mahitaji maalum katika elimu, ajira na uchumi wa kisasa. Kadri Taifa linavyoendelea kuhamia kwenye mifumo ya Serikali Mtandao pamoja na uchumi wa kidijitali, kuna hatari ya makundi maalum kubaki nyuma zaidi iwapo mifumo hiyo haitajengwa kwa kuzingatia ujumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, bado kuna fursa kubwa ya kuimarisha matumizi ya teknolojia saidizi, mafunzo ya stadi pamoja na mifumo rafiki ya utoaji huduma katika ngazi za jamii na Serikali za Mitaa ili kuongeza ushiriki wa makundi maalum katika elimu, ajira pamoja na shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali iendelee kuboresha sera za ujumuishi pamoja na viwango vya utoaji huduma za kidijitali ili taasisi za umma na binafsi ziweze kuzingatia zaidi matumizi ya teknolojia saidizi na mifumo jumuishi ya TEHAMA kwa watu wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanyika chini ya Wizara hii ikiwemo kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia na mengine mengi nina ushari mdogo kwa habari ya watoto waishio mazingira magumu, maarufu watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali ione namna ya kutenga fedha ya kuwatambua; pili, kutoa elimu ya kujitambua; tatu, wapo waotamani kusoma. Serikali pamoja na wadau waone ni jinsi gani ya kuwasaidia kufikia ndoto zao wakiwa kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Serikali ione jinsi ya kuwapatia hata ujuzi ili waweze kumudu maisha yao. Hii itawasaidia kutokuwa kizazi cha uhalifu ama kujipatia kipato halali.

MHE. SHEILA E. LUKUBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake wenye maono makubwa. Ninamwombea afya njema na Mwenyezi Mungu amtunze kiongozi wetu wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Jitihada za kuwakomboa wananchi na hasa wanawake na kulinda maadili ya watoto wetu zinaonekana. Ni imani yangu mtaleta tabasamu kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwani miradi mingi ya kimkakati iliyofanyika na inayoendelea kufanyika nchini ni moja ya mikakati aliyoiweka katika utendaji wake kwa kipindi chote cha uongozi wake na hakuna mkoa ambao haujatekeleza miradi. Miradi hii inasaidia wananchi kupata huduma kwa karibu ikiwemo makundi maalum kufanya shughuli zao kwa uhakika kwani zimejengwa barabara rafiki, shule, hospitali, Bwawa la Kidunda, Bwawa la Mwalimu Nyerere, Daraja la Busisi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kurudisha mikopo ya asilimia 10 kwa mfumo ulioboreshwa ambapo kupitia mwongozo wa utoaji na usimamizi wa mikopo wa

mwaka 2024 umeboreshwa na makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wamenufaika na mikopo hii. Kundi la wanawake linaguswa pande zote kwani wanawake wanapatikana katika kundi la vijana kwa vijana wa kike na pia wanawake wanapatikana katika kundi la watu wenye ulemavu. Hivyo kipekee wanawake wananufaika kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia majukwaa ya wanawake, wanawake wengi wameanzisha biashara na wanatengeneza bidhaa bora na wanapata masoko ndani na nje ya nchi na zoezi la uhamasishaji wa kuunda vikundi kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ushauri kuhusu kuboresha upatikanaji wa mikopo kwa wanawake, vijana na makundi maalum. Pamoja na uwepo wa mikopo ya 10% inayotolewa na halmashauri, bado wapo wananchi wengi wanaoshindwa kufikia mikopo hiyo kutokana na masharti, ukosefu wa elimu ya fedha na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naiomba Serikali kuongeza kiwango cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwenye taasisi rasmi za fedha; kurahisisha masharti ya upatikanaji wa mikopo hiyo ili kuwafikia wananchi wengi zaidi; kutoa elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa fedha kwa vikundi vinavyopokea mikopo; na kuhakikisha mikopo inatolewa kwa wakati ili iweze kusaidia shughuli za uzalishaji na kuongeza kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ushauri. Kamati za Mikopo kuanzia ngazi za kata hadi Kamati ya Uhakiki ngazi za wilaya ziunganishwe na kufanya kazi kwa pamoja ili kupunguza muda mrefu wa ukaguzi wa vikundi vinavyoomba mikopo. Mikopo itolewe hata kwa mtu mmoja mmoja kwa makundi yote ili kuepukana na changamoto za wanakikundi pale mmoja wao amepata changamoto. Pia kuongeza idadi ya mabenki ili kurahisisha utoaji wa mikopo hasa halmashauri zinazofanya mfumo jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuimarisha mfumo wa utengenezaji vitambulisho vya wajasiriamali ndogondogo ili kuepusha malalamiko na kusubiri muda mrefu wa maombi ya mikopo ya riba asilimia saba kwa wajasiriamali; kujenga uwezo kwa wataalam katika Idara ya Maendeleo ya Jamii, Idara ya TEHAMA na Idara ya Ugavi kwa waratibu wa madawati yanayohusika na usajili wa vikundi katika mfumo wa *NeST* na kuwapa vikundi elimu ya Sheria za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, namna ya kuona *tender* na kuomba *tender* zinazotangazwa kwenye mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya biashara. Rais ameboresha masoko na miundombinu inayosaidia wajasiriamali wadogo na wa kati kufanya biashara zao kwa kuongeza kipato cha kaya na pato la Taifa kwa ujumla kupitia mikopo ya wajasiriamali wadogo walioko masokoni wa asilimia saba ya mama na baba lishe, wamachinga, waendesha bodaboda na bajaji inayotolewa na Serikali kupitia benki ya *NMB*. Mikopo hii imekuwa mkombozi kwa mjasiriamali mdogo mdogo kukopa mikopo hii, kwani riba yake ni ndogo na imewainua wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie 30% ya ununuzi wa umma ya Sheria ya Ununuzi wa Umma. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha makundi maalum katika mfumo wa 30% wa ununuzi wa umma. Hii inasaidia sana kuwainua wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana changamoto zifuatazo zifanyiwe kazi. Kwanza, uelewa mdogo na ukosefu wa habari juu ya Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 kwa makundi ya wanawake, vijana, wazee na makundi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uchambuzi wa zabuni. Wajasiriamali wengi hawajui namna ya kusoma na kujaza nyaraka za zabuni kikamilifu. Tatu, mawasiliano vijijini: taarifa za zabuni zinazotangazwa na taasisi nunuzi haziwafikii walengwa maeneo ya pembezoni mwa mkoa. Nne, ugeni wa mfumo wa ununuzi wa

umma *(NeST)* unahitaji ujuzi wa kompyuta ambao makundi mengi hayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imeendelea kuwa nguzo muhimu katika kujenga jamii yenye usawa, mshikamano na ustawi kupitia utekelezaji wa programu mbalimbali za uwezeshaji wa kiuchumi kwa wanawake, vijana na makundi maalum, kuimarisha majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, mabaraza ya watoto, wazee, majukwaa ya kijamii, kukuza usawa wa kijinsia pamoja na juhudi za kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, ninapenda kueleza kuwa utekelezaji wa majukumu haya muhimu unafanywa kwa kiwango kikubwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Maafisa Ustawi wa Jamii ambao wako karibu sana na wananchi wetu huko vijijini na mijini. Wataalam hawa wanafanya kazi kubwa na yenye matokeo chanya, lakini mazingira yao ya kazi bado ni magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa jinsi wanavyohangaika na kusaidia makundi yetu kwenye vikundi, kutengeneza katiba na kusimamia upatikanaji wa mikopo ya 10%, mikopo ya wafanyabiashara ndogo ndogo, kufuatilia marejesho, kuwaunganisha na taasisi za fedha kupata mikopo, lakini pia ulinzi na usalama wa watoto wetu kupitia mabaraza, Kamati za MTAKUWWA na masuala mengine yahusuyo maendeleo ya jamii na ustawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, maafisa hawa hawana vitendea kazi vya kutosha vinavyowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Pili, kumekuwa na uhaba mkubwa wa bajeti za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii na ustawi katika maeneo yao ya kazi (halmashauri), hali inayosababisha baadhi ya shughuli muhimu kutotekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Idara ya Ustawi wa Jamii katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za

Serikali za Mitaa ili kuweka vipaumbele vya bajeti zinazotekelezeka ili kuimarisha huduma za ustawi wa jamii? Wakati wa majumuisho nitaomba nipate majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa Idara ya Ustawi wa Jamii hususan ngazi za halmashauri kunasababisha kutokuwekwa vipaumbele na kuzingatiwa kwa afua za ustawi wa jamii ambazo ni muhimu kwa ustawi wa makundi maalum, kwani kwa sasa zipo chini ya Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambao kimsingi wanaelemewa na majukumu ya afya na kushindwa kuzibeba huduma za ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, changamoto ya usafiri bado ni kubwa, maafisa wengi hawana usafiri wa kuwafikisha kwenye maeneo ya wananchi, hasa vijijini ambako mahitaji ya huduma hizi ni makubwa zaidi na kiukweli wananchi wanawahitaji maafisa hawa kwa karibu. Kama tunataka kuondoa umaskini na kuwa na maendeleo endelevu, lazima tuwekeze kwa wataalam hawa ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiyopingika kuwa hatuwezi kutarajia matokeo makubwa kutoka kwa wataalam hawa bila kuwapatia mazingira bora ya kazi. Kama Taifa tunapaswa kuhakikisha kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wanapewa kipaumbele kwa kuboreshewa maslahi, vitendea kazi, usafiri na bajeti za utekelezaji ili waweze kuwafikia wananchi kwa wakati na kutoa huduma bora ili kuwa na matokeo yanayopimika katika jamii zetu, lazima tuwekeze kwa wataalam hawa ambao watafanya sekta hii kuwa *engine* ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ukatili wa kijinsia, bado jamii yetu inaendelea kushuhudia matukio ya ukatili dhidi ya wanawake, watoto na makundi maalum. Matukio haya yanaathiri ustawi wa jamii na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Hivyo ninashauri Serikali kuongeza kampeni za elimu kwa umma kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia; kuimarisha mifumo ya ulinzi na utoaji wa haki kwa waathirika; kuweka vituo rafiki zaidi vya

huduma kwa manusura wa ukatili; na kushirikisha viongozi wa dini, mila na jamii katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hoja za Mheshimiwa mmoja, mchango wake ni kama anataka kuturudisha nyuma enzi za mfumo dume. Hakuna mwanamke mjeuri kwenye ndoa yake kama baba anasimama vizuri kwenye nafasi yake na ndiyo maana Serikali kwa kuliona hilo ilianza kutoa mikopo kwa wanawake na kuanzisha majukwaa ya kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kina mama wanasomesha, wanafanya biashara, wanajenga na kadhalika. Maisha ni kusaidiana, kukaa ndani kama golikipa imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa wasaa wa kuchangia katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuzidi kuendelea kuwa Rais wa maono kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapenzi makubwa ninaipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum hasa Waziri Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa *Eng.* Maryprisca Mahundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia watumishi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote walioko chini yao. Pongezi hizi kwa Wizara ni kwa sababu ya maandalizi makini ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

yenye maono, iliyoandaliwa kwa weledi na inayoakisi mahitaji halisi ya kila Mtanzania katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla (Kitaifa). Ili kuongeza tija, ufanisi na matokeo yanayoonekana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ni muhimu kuweka mkazo katika uratibu madhubuti, matumizi ya takwimu na ushahidi, ushirikishwaji wa wadau mbalimbali, pamoja na ufuatiliaji na tathmini endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ufuatao unaweza kusaidia katika maeneo husika. Kwanza kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia, kutokomeza ukatili wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kwa kuimarisha uratibu wa sekta mtambuka; kuanzisha na kuimarisha mifumo ya uratibu inayoshirikisha Wizara, taasisi za umma, sekta binafsi, asasi za kiraia, viongozi wa dini na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuweka majukumu na viashiria vya utendaji vinavyoeleweka kwa kila mdau ili kuondoa urudufu wa shughuli na kuimarisha matumizi ya takwimu na mifumo ya taarifa; kuanzisha kanzidata jumuishi ya masuala ya kijinsia na ukatili wa kijinsia kwa ajili ya kupanga, kufuatilia na kutathmini afua; na kutumia takwimu zilizogawanywa kwa jinsia, umri na eneo ili kufanya maamuzi sahihi ya sera na mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kukuza uwezeshaji wa wanawake kiuchumi; kuongeza upatikanaji wa mitaji, mikopo nafuu, huduma za kifedha na masoko kwa wanawake; na kutoa mafunzo ya ujasiriamali, ubunifu, matumizi ya teknolojia na stadi za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutokomeza ukatili wa kijinsia; kuimarisha kampeni za mabadiliko ya mitazamo na tabia katika jamii; kupanua huduma za msaada kwa manusura ikiwemo ushauri nasaha, msaada wa kisheria na huduma za afya; na kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa na rufaa kwa manusura wa ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuimarisha uwajibikaji kwa kuweka mfumo wa kupima matokeo ya afua za kijinsia na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwa kipindi maalum. Pia kufanya tathmini za mara kwa mara ili kubaini changamoto na maeneo yanayohitaji maboresho; na kuratibu afua za upatikanaji wa haki, ulinzi, malezi na matunzo ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha mifumo ya ulinzi wa mtoto; kuanzisha na kuimarisha Kamati za Ulinzi wa Mtoto katika ngazi zote za utawala; na kuweka mifumo ya haraka ya kuripoti na kushughulikia vitendo vya ukatili, unyanyasaji, ajira za watoto na ndoa za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha malezi chanya na matunzo ya watoto; kutoa elimu ya malezi bora kwa wazazi, walezi na jamii; na kuendeleza programu za malezi chanya zinazozingatia ukuaji wa mtoto kimwili, kiakili na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha uratibu wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi; kuimarisha ushirikiano kati ya sekta za afya, elimu, ustawi wa jamii, Polisi na Mahakama; na kuweka mfumo wa pamoja wa usimamizi wa mashauri ya watoto na huduma za rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanua upatikanaji wa haki kwa watoto; kuongeza uelewa wa sheria na haki za mtoto kwa jamii; kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa watoto na familia zao; na kuhakikisha watoto wanapata huduma rafiki katika mifumo ya haki jinai na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia matumizi ya teknolojia kwa kuanzisha mfumo wa kidijitali wa kufuatilia watoto walio katika mazingira hatarishi na hatua zinazochukuliwa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa kuongeza rasilimali watu na uwezo wa watumishi; kuajiri na kusambaza wataalam wa ustawi wa jamii kulingana na mahitaji ya maeneo husika; na kutoa

mafunzo endelevu kuhusu mbinu za kisasa za utoaji huduma na usimamizi wa mashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuimarisha mifumo ya utoaji huduma kwa kuandaa viwango na miongozo ya utoaji huduma za ustawi wa jamii vinavyotumika nchi nzima na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa ubora wa huduma katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha uratibu wa wadau kwa kujenga ushirikiano madhubuti kati ya Serikali, sekta binafsi, mashirika ya kiraia na washirika wa maendeleo na kuanzisha majukwaa ya mara kwa mara ya kubadilishana taarifa, uzoefu na mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuongeza matumizi ya TEHAMA kwa kuweka mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa taarifa za ustawi wa jamii na kurahisisha ukusanyaji wa takwimu, utoaji wa huduma na ufuatiliaji wa matokeo kwa kutumia teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwa kuweka viashiria mahsusi vya kupima ubora, ufanisi na athari za huduma zinazotolewa na kutumia matokeo ya tathmini kuboresha sera, mipango na utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Ili Wizara iweze kufikia matokeo makubwa zaidi, inashauriwa kujenga mfumo imara wa uratibu unaozingatia ushirikiano wa sekta mbalimbali, matumizi ya takwimu na teknolojia, uwajibikaji wa wadau, pamoja na ufuatiliaji wa matokeo. Aidha, uwekezaji katika rasilimali watu, mifumo ya taarifa na uwezeshaji wa jamii utakuwa msingi muhimu wa kukuza usawa wa kijinsia, kulinda haki za watoto na kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na fadhila kwa kutujaalia afya na hekima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika Wizara hii ninataka nijikite kwenye mikopo. Tunaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuweka mikopo yenye masharti nafuu. Wanawake wengi hawazifahamu fursa ambazo zinapatikana chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF),* kuna Mkopo wa Wafayabiashara ndogo ndogo *(WBN)* na Mkopo wa 10% inayotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)* umetokana na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 Iliyofanyiwa mapitio katika mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu wa *WDF,* Serikali imeweka malengo mahsusi. Malengo hayo ni kuimarisha uwezo wa kiuchumi kwa wanawake; kuongeza ajira ili kupata kipato; kukuza ustawi wa familia; na kuchochea wanawake kwa kujihusisha na miradi ya uzalishaji hasa katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi na uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu unatoa mikopo miaka miwili na miaka mitatu, mfuko huu ulipoanzishwa mwaka 1993 ulikua unatoa riba 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa wanawake wa Taifa hili, Wizara ilifanya maboresho ya mwongozo wa mfuko huu Toleo la Julai, 2022. Sasa mfuko huu unatoa riba asilimia nne ambayo ni nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali za kuimarisha mfuko huu bado wanawake hawana uelewa wa

mfuko huu, kwani bado wanafahamu kwamba kuna mfuko wa halmashauri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuhauri. Ninaiomba Serikali ifanye juhudi za makusudi za kutoa elimu kuhusu mfuko huu wanawake *(WDF)* Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ili lile lengo liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uwepo usimamizi wa marejesho ili wale wakopaji na warudishe kwa wakati mikopo hiyo ili wanawake wengi zaidi waweze kupata mkopo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kuhusu mikopo ya wafanyabiashara ndogo ndogo *(WBN)* wenye riba ya asilimia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wanawake wengi nchini wanafanya biashara ndogondogo kama mama lishe, wauza mbogamboga na kimama wanaotembeza bidhaa mitaani, hivyo wanawake hawa hukumbana na masharti magumu ya mkopo huu na wanashindwa kumudu masharti hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya mkopo huo ni lazima uwe na leseni ya biashara, eneo la biashara na *return* ya milioni tano kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho ni kuhusiana na mkopo wa 10%. Mkopo huu una masharti magumu ya uombaji wa mikopo hiyo inayotolewa na halmashauri nchini ambayo inawataka waombaji wa mikopo kupitia njia ya mfumo wa kidigitali, wanawake wa vijijini hawawezi, na wanajikuta fursa hii inawapita kwani wengi wao hawatumii simu janja, wanatumia simu za tochi na hawatumii *computer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Serikali ifanye mkakati maalum wa kuwataka Maafisa Maendeleo kushuka ngazi ya vijijini na kuwasaidia wanawake kujaza fomu za maombi ya mikopo kwa kuwa hawana uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuwepo mahali hapa nami niweze kushiriki kikao hiki cha kupitisha bajeti hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Wizara hii ndiyo *engine* ya kuinua maisha ya mwananchi wa kawaida. Ikiwa mama kijijini hana mtaji, mtoto mwenye ulemavu haendi shule, na vijana wamekosa ajira, basi maendeleo ya nchi yanakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kibaha Vijijini ni jimbo linalokua kwa kasi kutokana na uwekezaji wa *TAMCO, Expressway* na Bandari Kavu ya Kwala, lakini kasi hiyo imeacha nyuma makundi maalum. Hivyo bajeti hii ni lazima iwaguse moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya msingi ya Kibaha Vijijini katika sekta hii ni kama ifuatavyo: uwezeshaji wa kiuchumi kwa wanawake na vijana. Jimbo lina vikundi zaidi ya 400 vya akina mama na vijana vinavyojishughulisha na kilimo cha muhogo, korosho, ufugaji wa kuku na biashara ndogo Mlandizi, Ruvu na Kwala, lakini vikundi nane kati ya 10 havijapata mkopo wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake tangu mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki zinawadai dhamana ambazo hawana. Mahitaji ya haraka ni mtaji usiyozidi shilingi milioni tano kwa kila kikundi, mafunzo ya usimamizi wa fedha na kuwaunganisha na masoko ya uhakika *TAMCO* na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na ustawi wa mtoto. Kata za Gwata, Bokomnemela na Dutumi zinaripoti ongezeko la mimba za

utotoni kwa sababu ya umaskini na kukatisha masomo. Shule za Mlandizi A, Ruvu Sekondari na Gwata Sekondari zina wasichana zaidi ya 60 walioacha shule miaka miwili iliyopita. Pia watoto wa mtaani wameanza kuonekana Mlandizi Mjini kutokana na kuvunjika kwa familia. Tunahitaji madawati ya jinsia na watoto kwenye kila kata, vituo vya malezi ya mchana kwa watoto wa akina mama wanaofanya biashara sokoni na mpango maalum wa kuwarudisha shule wasichana walioacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwa watu wenye ulemavu na wazee. Kibaha Vijijini ina watu wenye ulemavu zaidi ya 1,800 lakini Kituo cha Afya Mlandizi hakina vifaa rafiki kwao. Hakuna njia za magongo, na hakuna mkalimani wa lugha ya alama. Walemavu wa viungo wanashindwa kufika kwenye mikutano ya maendeleo kwa sababu ya miundombinu mibovu. Wazee zaidi ya 2,500 hawajapokea pensheni za jamii kwa miezi minne. Tunahitaji vitambulisho vya walemavu vitolewe kwa haraka, vifaa saidizi kama magongo na viti mwendo vigaiwe na pensheni ya wazee ilipwe kwa wakati kupitia mawakala wa simu vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kupambana na ukatili wa kijinsia na ulevi. Kutokana na wimbi la wafanyakazi *TAMCO* na madereva wa malori, pombe haramu na ukahaba vimeongezeka *Ruvu Station* na Kwala, matokeo yake ni ongezeko la ukatili kwa wanawake na maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Mlandizi kinaripoti kesi 12 za ubakaji kila mwezi, lakini nyingi hazifiki Mahakamani kwa kuhofia unyanyapaa. Tunahitaji nyumba salama ya dharura Mlandizi kwa wahanga na kampeni za mlango hadi mlango kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara imejitahidi sana kusimamia sekta mbalimbali zilizopo chini ya Wizara hii hasa masuala ya jinsia, wanawake, jamii na makundi maalum, tumeona namna Wizara inavyofuatilia kwa kina masuala ya kijinsia na kuchukua hatua stahiki kwa kuwaita wahusika na kuvishirikisha vyombo vingine vya sheria kwa hatua zaidi. Ni wajibu

wetu kupongeza kwenye mazuri yanayofanywa na Serikali kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kibaha Vijijini tuna changamoto mbalimbali tunazokabiliana nazo, ninaomba kwenye bajeti hii Wizara iende kuzitatua na kuzipatia ufumbuzi wa haraka.

(a) Ucheleweshaji wa fedha za mikopo ya 10%. Sheria inataka halmashauri zitenge 10% ya mapato ya ndani kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu, lakini Halmashauri ya Kibaha imetenga 6% tu mwaka 2025/2026 na hadi sasa vikundi 70% havijapata fedha. Sababu zinazotajwa ni ukusanyaji mdogo wa mapato na urasimu wa kujaza fomu. Hii inavunja moyo wa wananchi.

(b) Mila na desturi zilizo pitwa na wakati; baadhi ya Vijiji vya Dutumi na Gwata bado vina mila ya kuwanyima wanawake haki ya kurithi ardhi. Wasichana wanaozwa kwa vijana wa bodaboda kwa mahari ya shilingi 200,000. Pia imani potofu kuwa mtoto mwenye ulemavu ni laana inafanya familia kuwaficha ndani wasipelekwe shule. Maafisa Maendeleo ya Jamii ni wachache, kata zetu zote zina Maafisa Maendeleo Jamii wa tatu tu, hivyo elimu haifiki vijijini.

(c) Ukosefu wa takwimu sahihi za makundi maalum, hatujui idadi kamili ya wajane, yatima, walemavu na wazee wanaohitaji msaada. Matokeo yake bajeti inatengwa bila kuangalia uhalisia. Mfano, *TASAF* imesajili kaya maskini 1,200 lakini viongozi wa vijiji wanasema wahitaji ni zaidi ya 3,000. Bila *data*, tunapanga kwa kubahatisha na kutokufika malengo kwa wahusika.

(d) Uwezo mdogo wa mabaraza ya kata ya Watoto. Mabaraza ya watoto yameundwa shuleni, lakini hayana fedha wala mafunzo. Walimu wasimamizi hawajapewa posho, hivyo mabaraza yamekufa. Mtoto akipata shida hana pa kusemea.

(e) Miundombinu isiyokuwa rafiki. Sokoni Mlandizi hakuna vyumba vya kunyonyeshea. Mama mwenye mtoto mchanga analazimika kuuza chini ya jua au kumwacha mtoto nyumbani.

Shule nyingi hazina matundu ya vyoo kwa watoto wenye ulemavu. Hii inawakwaza kushiriki maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kwenye kutoa ushauri. Maoni yangu, nini Serikali kifanye kwenye bajeti hii ya mwaka 2026/2027 kwenye Jimbo letu la Kibaha Vijijini?

(a) Kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

(i) Ongezeko mgao wa mfuko wa wanawake. Serikali itenge shilingi bilioni 2.5 kwa Kibaha Vijijini pekee kwa mwaka 2026/2027. Kila kata ipate angalau shilingi milioni 300. Mkopo utolewe bila riba kwa mwaka wa kwanza na vikundi vifundishwe kwa vitendo jinsi ya kuendesha biashara ya korosho, kuku na usindikaji wa muhogo.

(ii) Serikali ijenge Kituo cha Mkono kwa Mkono Mlandizi. Hiki kiwe kituo cha pamoja chenye nyumba salama kwa wahanga wa ukatili, chekechea ya mama lishe, ofisi ya mkalimani wa lugha ya alama na darasa la ufundi stadi kwa walemavu. Wizara itenge shilingi milioni 800 kukijenga.

(iii) Zindua Operesheni Rudi Shule Binti. Serikali itenge shilingi milioni 400 kuwatafuta na kuwarudisha shule wasichana 200 walioacha shule kwa sababu za mimba au umaskini. Wapewe vifaa vyote, sare na posho ya shilingi 30,000 kwa mwezi. Shule ziwe na vyumba vya kusoma mama na mtoto.

(iv) Serikali igawe vifaa saidizi 500. Serikali inunue na kugawa viti mwendo 200, magongo 200 na miwani 100 kwa walemavu wa Kibaha Vijijini kabla ya Desemba, 2026. Zitolewe moja kwa moja kijijini badala ya kusubiri ofisini.

(v) Ajira za Maafisa Maendeleo. Serikali iajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenye kata zote ili kila kata iwe na afisa wake. Wapewe pikipiki na posho ya mafuta ili wafike vijijini kutoa elimu dhidi ya mila kandamizi.

(vi) Wizara ihakikishe halmashauri inatekeleza 10% kwa ukamilifu. Mwaka 2026/2027 halmashauri itenge 10% kamili ya mapato ya ndani sawa na shilingi bilioni 1.1. Asilimia nne, wanawake; asilimia nne, vijana; na asilimia mbili, walemavu. Orodha ya vikundi vilivyopata itangazwe kwenye ubao wa matangazo kila kata.

(vii) Sensa ya makundi maalum. Ndani ya miezi mitatu, ifanyike sensa ya wazee, walemavu, yatima na wajane wote. *Data* itumike kupanga bajeti ya mwaka 2027/2028.

(viii) Vyumba vya Kunyonyeshea sokoni. Wizara ishirikiane na halmashauri kuhakikisha inajenga chumba kimoja cha kunyonyeshea na kubadilishia watoto katika soko la Mlandizi na Ruvu. Hii itaongeza ushiriki wa kina mama kwenye biashara.

(ix) Kuanzishwe Kampeni ya Kataa Mila Kandamizi. Wazee wa kimila wa Dutumi na Gwata wakae na kuweka azimio la katazo la ndoa za utotoni na kunyima wanawake urithi. Wakikiuka wafikishwe mbele ya sheria na adhabu kali itolewe.

(x) Serikali isimamie vikundi. Mwenyekiti wa Kijiji asaini kila mkopo wa kikundi na ahakikishe fedha zinatumika kwa mradi, siyo kugawana.

(xi) Ripoti kuhusu ukatili. Kila mtaa uwe na Mjumbe wa Dawati la Jinsia, mtoto au mama akipigwa, ripoti ifike Polisi ndani ya saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya kweli ni yale yanayomgusa mama anayeuza mboga Mlandizi, mtoto mwenye ulemavu wa Gwata na binti aliyeacha shule Ruvu. Bajeti ya mwaka 2026/2027 ikitekeleza haya, Kibaha Vijijini itakuwa mfano wa Tanzania inayojali watu wake wote. Tusipowainua hawa na kwa jinsi mji wetu unavyozidi kukua basi umaskini vijijini utaongezeka na vitendo vya unyanyasaji kijinsia vitaongezeka pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Sasa nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, Maryprisca Mahundi.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote ninapenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye amenijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuchangia Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum aliyoiwasilisha leo tarehe 1 Juni, 2026 hapa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru kwa dhati ya moyo wangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini na kunipa kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Ninachoweza kusema, ninamwahidi Mheshimiwa Rais kazi hii ninaiweza, ninaipenda, na nitaifanya kwa moyo wangu wote kuhakikisha lile tabasamu analotamani wananchi wake kulipata na mimi ninakuwa sehemu ya kuona ninaifikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Balozi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri namna ambavyo anaiwezesha Wizara yetu pia kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake, maelekezo na katika kuhakikisha ninatimiza majukumu yangu ya Wizara kwa nafasi yangu ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Vilevile, Mheshimiwa Daniel Sillo kuwa Naibu Spika na wewe

na Mwenyekiti na wenyeviti wote wa Kamati za Bunge kwa uongozi wenu imara unaotuwezesha kutimiza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na kuipongeza Kamati yetu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii ambayo inaongozwa na mwanamke hodari. Mwanamke huyu Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, Pwani, amekuwa Mwenyekiti wa mfano. Anafanya kazi yake vizuri kwa ushirikiano mkubwa kabisa na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati. Wamekuwa wakitushauri, wakitupa maelekezo na hayo maelekezo tunavyoyafanyia kazi ndiyo uimara unaouona katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa dhati ya moyo, Waheshimiwa Wabunge ninawashukuru sana, ninawapongeza sana, ushirikiano wenu kwangu mmekuwa mkiendelea kunifanya niwe imara katika jukumu ambalo Mheshimiwa Rais amenipa, lakini vilevile nafasi ya namna mmechangia toka asubuhi mpaka muda huu, mmeweza kutupa dira na mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawahakikishia yote mliyoyaongea kwa nafasi yangu nitamsaidia kwa karibu kabisa Mheshimiwa Waziri wangu kuona kwamba tunayafanyia kazi na yanakuwa yenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, ninaomba nimshukuru Waziri Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima. Huyu kwangu ni dada, ni mama, ni mlezi, na ni rafiki. Hakika amekuwa na msaada mkubwa. Yeye amekuwa mbobezi kwenye hii Wizara kwa miaka mingi. Amefanya kazi nzuri, ma-*Gen Z* huko mtandaoni huyu ni shangazi yao, ni bibi yao, wanaweza wakaongea lugha wakaelewana na mambo yanakwenda vizuri na mihemko anaituliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuwarejesha kimaadili anafanya hivyo na nyote mmeongea hivyo. Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ninakushukuru sana kwa ulivyonipokea katika

Wizara hii na ninaendelea kujifunza nikikusaidia kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishukuru sana familia yangu hasa mume wangu na binti yangu Maureen pamoja na wadogo zake na ndugu zake wote, wameweza kunivumilia, nimeweza kutimiza majukumu yangu na leo baadhi yao walikuwa hapa na wengine wameendelea na masomo na wengine kazi zao, lakini ninashukuru sana familia yangu, niko imara kwa sababu ya upendo wenu kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wanawake wa Mkoa wa Mbeya, waliweza kunipa kura za kishindo, za heshima na mimi nikaweza kuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya na hatimaye Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndipo aliponiona na kunipa nafasi hii. Wanawake wa Mkoa wa Mbeya, Mwenyezi Mungu aendelee kuwatunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Diwani, ninayetokea Halmashauri ya Wilaya ya Chunya. Leo asubuhi umeweza kuona *crew* nzima iliyotoka Wilaya ya Chunya. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, kaka yangu Mbaraka pamoja na Kamati yake ya Usalama nzima ilikuwepo hapa. Katibu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya alikuwepo hapa na Kamati yake ya siasa. Vilevile, Mwenyekiti wa Halmashauri alikuwepo hapa na Waheshimiwa Madiwani wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nimepata bahati kubwa sana ya kuweza kuja kutiwa moyo pia na Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Beno Malisa naye alikuwepo hapa hapa. Pia, ninatokana na dirisha la UWT. Mwenyekiti wangu wa mkoa alikuwepo hapa, Bi. Edina Mwaigomole na aliongozana na katibu wake, Agnes Bashem. Wote hawa maana yake ni nini? Wananitia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtoto wao, wananilea na ndiyo maana walifunga safari kutoka Mbeya na Chunya mpaka hapa kwa lengo la kunitia moyo na kuhakikisha ninafanya vizuri katika majukumu yangu. Ninawashukuru sana viongozi wote

mliotoka Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Chunya kuja kunitia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru pia familia yangu ya taasisi isiyokuwa ya Kiserikali, *Maryprisca Women Empowerment Foundation*, na wenyewe hawakuwa nyuma, walikuja hapa kuhakikisha wananitia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema ninawashukuru wote kwa namna mnavyonisaidia kutimiza majukumu yangu. Ninapenda kusema nitaongea kwenye maeneo mawili matatu hivi, na nikimpa muda wa kutosha Mheshimiwa Waziri Dkt. Dorothy Gwajima, ana nondo za kutosha, ikiwa ni darasa ataelimisha, lakini vilevile akiwa anajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na ninaamini wote mtatuunga mkono kwa kupitisha bajeti hii muhimu ili tuweze kwenda kutimiza majukumu haya. Vilevile, mtakuwa mnaendelea kupata elimu taratibu kadiri ya atakavyokuwa anatoa maelezo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda kusema kwamba Wizara hii Mheshimiwa Rais aliyoiunda kutoka kwenye Wizara ya Afya alikuwa na maono makubwa sana. Inabidi tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono haya yenye upendo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuianzisha hii Wizara, maana yake alikuwa anataka kuongeza msukumo kwa jamii kushirikishwa katika kubuni, kutekeleza na kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na wananchi waweze kuona shughuli hizi zote zipo kwenye vidole vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, alipenda kuanzisha Wizara hii ili kuhakikisha tunaweka mazingira wezeshi na jumuishi kwa makundi yote. Hakuna kundi ambalo linaachwa katika Wizara hii. Lengo ni kuhakikisha kwamba wale walio katika mazingira hatarishi, basi wanapelekewa huduma za ustawi wa jamii kwa karibu na kuona kwamba maendeleo ya jamii yanaweza kufikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Wizara yetu kubwa ni kubadili fikra. Tunafanya *mindset setup* kuona kwamba tunakwenda kwenye uelewa wa pamoja ili jamii nzima iweze kujikita na kuona kwamba inachangia na kushiriki katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja chache ambazo nimezichagua moja ni eneo la huduma kwa wazee wenye uhitaji. Waheshimiwa Wabunge hapa wameelezea vizuri mambo kadhaa kuhusiana na wazee. Wazee ni tunu ya Taifa na sote tunafahamu na tunaheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba wazee hawa wenye uhitaji, sisi kama Wizara tunatambua na kuthamini mchango wa wazee hawa, lakini vilevile dhamira hiyo imeweza kuainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2024 inayosisitiza kuhusu ulinzi wa wazee, matunzo ya wazee, hifadhi ya jamii na ustawi wa wazee. Taifa lisilojali wazee linapoteza hazina ya maarifa, uzoefu, historia, utamaduni, mila na desturi ambavyo vyote hivi ndivyo msingi wa mshikamano na maadili ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa maeneo yatakayopatiwa kipaumbele ni kuimarisha huduma na matunzo na malezi, upatikanaji wa huduma bora za afya, msaada wa kisaikolojia na kijamii pamoja na ulinzi dhidi ya ukatili na unyanyasaji wa wazee, lakini vilevile ubaguzi katika malezi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama jamii tunapaswa kuwaheshimu, kuwapenda na kuwalinda wazee hawa kwa sababu na wao enzi ya ujana wao sisi walitulea vizuri ndiyo maana tupo hivi tulivyo leo. Kwa hiyo, leo ni zamu yao na wao tuweze kuwalinda, tuwaheshimu na tuwatunze ili waweze kufurahia matunda ya uzao wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali itaendelea kuhamasisha ushiriki wa wazee katika shughuli za maendeleo kwa kuimarisha mifumo ya utoaji huduma kwa wazee katika ngazi zote na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuboresha maisha

yao. Hatua hizi ni sehemu za utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo inaweka msingi wa kujenga jamii jumuishi inayotambua, inayoheshimu, na inayolinda na ustawi wa wazee ili waishi maisha yenye heshima, usawa, usalama na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara zangu nilizozifanya mikoani nimejifunza mambo mengi na mazito. Katika hizi nyumba tunazotunza hawa wazee ukianza kuwahoji na wao walikuwa watumishi kama sisi, walisoma kama sisi, lakini kilichowakuta ndugu zangu hawakutimiza majukumu yao. Unakutana na baba yupo pale unamwuliza, mzee imekuwaje? Ujana wako Mungu hakukujalia watoto? Ujana wako Mungu hakukujalia kuwa na mke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, anakwambia nilikuwa nao. Mtoto wangu yuko mahali fulani, ni kiongozi, ni bosi, ni mtu anayefanya shughuli zake na anafanikiwa kiuchumi, lakini kilichonikuta mwanangu sikutimiza majukumu yangu. Nilimtelekeza labda mama mwenye ujauzito wangu, akazaliwa mtoto na yeye nikamtelekeza. Kwa hiyo, mama na mtoto wameleana, sasa hivi wameshikamana mimi nimeishiwa nguvu sina pa kwenda ndiyo maana ninamwomba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia aweze kunifadhi katika makao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Ndugu zangu kwa umoja wetu huu tuendelee kutoa elimu katika maeneo yetu ya uongozi, tuone kwamba kila mzazi atimize majukumu yake. Alee watoto wake na mkewe ili kesho atakapoishiwa nguvu asiwe mpweke aweze kulelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee hawa kulelewa katika nyumba hizi za Serikali ni hatua ya mwisho. Sisi kama Wizara tunatamani kuona kwamba mzee analelewa kwenye ukoo wake. Kama ni watoto wake, kama ni mkewe, kama ni ndugu aliozaliwa, kama ni ndugu wa kiukoo, basi alelewe kule kwa sababu mila na desturi na tamaduni zao wanazifahamu. Kulikoni kuja kuishi huku anakuwa mpweke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la wazee, ninaomba niseme hapo kwa ufupi, niende kidogo kwenye mikopo. Nitaongea haya mawili na mengine yote nitamwachia Mheshimiwa Waziri aje atupe somo, naamini tutafurahia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la mikopo, kuhusu fursa za mikopo kwa wajasiamali wadogo, ili kuhakikisha kuwa wanakua kiuchumi na kuchangia pato la Taifa, Serikali inaimarisha mfumo wa uwezeshaji na upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kama ambavyo tumesikia wachangiaji mbalimbali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kusikia Mheshimiwa Maryam Mwinyi, Mheshimiwa Janet Mahawanga na wengine wengi wameongelea sana suala la mikopo. Sisi kama Wizara kwa kweli tutaendelea kusimamia kuhakikisha mikopo hii inatoka kwanza kwa wakati, lakini vilevile warejeshaji tutawafuatilia ili waweze kurejesha kwa wakati ili na wengine ambao wanasubiri, waweze kunufaika na mikopo hii ambayo Mheshimiwa Rais lengo lake ni kuona tunabadilisha mifumo ya kiuchumi na wenzetu wengi watoke kwenye uchumi ule wa kujikimu tu, lakini wawe na uchumi wa kibiashara na kujitanua zaidi kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Women Development Fund,* huu ni Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, uko katika Wizara yetu na mpaka sasa zaidi ya shilingi bilioni moja tumeshaitoa, wanawake wengi wamepata na riba yake ni ndogo haizidi asilimia tano. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa elimu Kadiri ya ambavyo mmetushauri kwa lengo la kuona kwamba wengi waendelee kufahamu na nyinyi mkiwa wawakilishi wa wananchi Waheshimiwa Wabunge ninaamini hili kwa sababu nyinyi mmeelewa, mtaenda kulipeleka katika maeneo yenu na Maafisa Maendeleo wa Mikoa mtawafikia ili waweze kuwasiliana na mkuu wa idara anayehusika na mkopo huu kwa huku Wizarani ili watu wengi waweze kunufaika na mkopo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mkopo ule wa wafanyabiashara ndogondogo kwa jina maarufu machinga, nimekuwa nikijibu maswali haya hapa ndani ya Bunge lako Tukufu na nimesisitiza, Waheshimiwa Wabunge niwaombe, mnapokuwa

kwenye maeneo yenu mkopo huu ni rahisi kwa wale wananchi wetu. Kigezo kikubwa ni kitambulisho cha mfanyabiashara mdogo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, vile vitu vingine ambavyo vilikuwa ni vikwazo pale awali kwa sababu kwanza mkopo huu tumeingia mkataba na Benki ya *NMB*, wanachukulia kule. Kwa hiyo, wanapofika kule kulikuwa kidogo na masharti ambayo yalikuwa yanakera, lakini kwa mawasiliano ya Wizara na benki yameweza kuondolewa. Vimebaki vipengele vichache ambavyo wengi wanaviweza na tayari wananufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito, wajasiriamali wadogo wadogo wote fikeni kwenye halmashauri zenu, onaneni na maafisa biashara ndiyo wanaotoa hivi vitambulisho vya mfanyabiashara mdogo. Baada ya hapo unapeleka pale kwenye dawati la mikopo kwenye Benki ya *NMB*, matawi yote nchini wanatoa huduma hii na Mheshimiwa Rais ametupatia fedha tayari zipo kule benki ili tuendelee kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mkopo huu wa 10% kama ambavyo umekuwa ni maarufu, tutaendelea kuhakikisha tunasimamia na tutaendelea kuwaelekeza Maafisa Maendeleo wa Kata ili wawasaidie wanawake kupunguza kero za kwenda na kurudi na gharama ndogondogo ambazo zinapelekea kuwaharibia mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi tunatamani kuona kwamba wale wanawake wa kule chini wanasaidiwa. Vilevile, tumekuwa tukitoa maelekezo kwa hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii kule kwenye kata waweze kutumia taasisi zisizo za Kiserikali, hizi *NGOs*. Wanaweza wakasaidia wananchi wetu kutoa hizi gharama ndogondogo labda muhuri wa mwanasheria ikawa kwa nafuu. Siyo tena mtu anatafuta mtaji wa shilingi laki 5, muhuri unagongwa kwa shilingi 50,000. Wataendelea kusaidiwa hata kwa shilingi 5,000 hata kwa shilingi 3,000 ili tu yule anayegonga mihuri aweze kununua *stationary* zitakazomwezesha kugonga mihuri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwe nimeongea kwa ufupi ili niweze kutoa nafasi kwa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, ana nondo za kutosha. Waheshimiwa Wabunge niwakaribishe tumsikilize Mheshimiwa Waziri, ana mambo mengi mazuri. Baada ya kuongea hayo hoja nyingine zitajibiwa na Mheshimiwa Maziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, na ninaunga mkono Hoja. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa ninamwita mtoa hoja aweze kuhitimisha hoja yake. Karibu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima kwa ajili ya kuhitimisha hoja yako.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja niliyoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitoa shukrani za pekee kwa Mungu wangu, Mwingi wa Rehema, aliyenipa uzima na uhai kuwepo siku hii ya leo mahali hapa. Aidha, ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini nitumikie Wizara hii. Nami ninamwahidi nitaendelea kupambana niwezavyo nikishirikiana na timu yangu ili maono yake na matamanio yake yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao waliyoitoa kuhusu hotuba yangu. Kipekee ninawashukuru sana na kwa pongezi nyingi mlizozitoa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri kwa Taifa letu na hususan kwa kuipa Wizara hii kipaumbele kwamba iwe msingi wa mabadiliko ya fikra na mtazamo wa jamii katika kujiletea maendeleo na ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais ameendelea kuikuza hii Wizara kidogo kidogo, tumetoka mbali kama tutakumbuka mwaka 2022 Juni, wakati ninasoma bajeti hapa, fedha yake ilikuwa ni chini ya shilingi bilioni 50, leo tunaongelea kuomba shilingi bilioni 108, siyo kitu kidogo hiki na ataendelea kuikuza ipasavyo kadri tunavyompelekea mapendekezo tunayoyatoa kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma Mbunge, kwa maoni, ushauri na maelekezo yao yanayotuwezesha kuboresha utekelezaji wa majukumu yetu kwa ufanisi. Kamati imekuwa ikichambua mambo kwa kina sana na kila siku nimekuwa nikisema, ninajifunza sana kwao kwa *positive criticism* wanazotupatia tukirudi kule huwa tunaboresha mikakati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Injinia Maryprisca Mahundi kwa kazi nzuri anayoifanya kunisaidia kuibeba hii Wizara. Peke yangu siwezi. Mchango wake umekuwa siyo mdogo, hakika ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Mahundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuacha kuipongeza *Management* ya Wizara yangu chini ya Katibu Mkuu Eliakimu Maswi, hakika amekuja ana muda mdogo sana lakini amenishangaza kwa jinsi ambavyo ameweza kwa muda mfupi kubeba Wizara hii kitendaji hadi mimi ninatabasamu, ninasema sasa nimepata Naibu *Field Marshal*. Hakika anafanya kazi nzuri kuiongoza Wizara hii akiunganisha watendaji wote na *tone* yake ina-*align* vyema na Dira ya 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kuwa kiu ya wananchi siyo nyingine bali ni kuona mabadiliko ya maisha yao pamoja na Taifa kwa ujumla ambayo ni malengo ya Dira ya 2050 na matamanio ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Taifa lenye amani, utu, umoja na mshikamano. Wizara ninayoiongoza itaimarisha ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge na ninawahakikishia kwamba, michango mnayotupatia sisi kila tukienda kule tunafumua mikakati yetu kuboresha zaidi ili kuweza kufika mbele. Maana hatuwezi kujiona sisi, bali ninyi mnatuona na mnawaona wananchi. Mkituletea michango yenu ni ya thamani sana kuliko kwenda hata ziara. Ninyi mnakuwa mmeshaenda ziara huko, mkileta ni vitu ambavyo vinatufanya sisi tutafakari ku-*align* na *program* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijielekeze kutoa ufafanuzi wa hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambapo hapa hesabu inasoma ni hoja 64. Kutoka kwenye Kamati yetu hoja 22, hoja za kuongea au kuzungumza Waheshimiwa Wabunge humu ndani 24 na 18 ni za maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika huu siyo mchango mdogo, huu ni mchango mkubwa sana utakaoweza kwenda kutuboreshea yale ambayo sisi tunapanga kuyafanya. Michango hii inajumuisha maeneo mbalimbali. Mengine ni maswali, mengine ni ushauri, michango mingine ni hoja nzito za kufanya *transformative changes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mdogo, lakini ukiniruhusu nijielekeze kwenye hoja moja ya kwanza ambayo itabeba karibu nyingi sana majibu yake au ufafanuzi wake. Hii siyo nyingine ni ile ambayo imesemwa kwa sauti kubwa na wengi zaidi kuhusu mmomonyoko wa maadili pamoja na malezi na makuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimeshika mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kwa miaka 10 ijayo kuanzia 2026/2027 hadi 2036/2037. Mkakati huu ni wa kisekta, umeshirikisha wataalam bobezi pia kutoka sekta binafsi. Mkakati huu umezinduliwa Aprili, 2026 kupitia Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo aliyeturatibu sisi wote kwa mujibu wa Wizara yake kwamba ni ya utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni unaendana na mila na desturi ambazo ndiyo zao la maadili yetu. Kwa hiyo, kwa dhamana yake alituratibu sekta zote tukapata huu mkakati.

Hivyo, niseme mkakati huu uko *online*, utapatikana kwa Waheshimiwa Wabunge wote na ninawasihi sana muusome ili tuweze kwenda na *shared vision*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kilichoandikwa humu, maana ya mmomonyoko wa maadili ni hali ya kuporomoka au kukiukwa kwa tabia njema, misingi, kanuni na mienendo inayokubalika katika jamii ambayo hujidhihirisha kupitia vitendo na mienendo inayokiuka matarajio ya kijamii na misingi ya maisha, ikiwa ni pamoja mfano matumizi yasiyofaa ya lugha, malezi duni ya watoto na vijana, mitindo ya mavazi isiyozingatia staha pamoja na kuongezeka kwa vitendo vya ukiukwaji wa sheria na maadili ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maadili yanaweza kujengwa kupitia malezi ya familia, tamaduni, dini na hata sheria zinazosimamiwa na Serikali. Kwa upande wa utumishi, tunayo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Tanzania, lakini urithishaji maadili ni utekelezaji wa afua zote zinazolenga kurithisha fikra na mienendo sahihi kwa watoto, vijana na wanajamii kupitia malezi, makuzi, mafunzo na mazingira yote ambayo humjenga mtu kuwa na mtindo wa maisha unaokubalika. Afua hizi zinatekelezwa na taasisi za kijamii zenye wajibu wa malezi na makuzi pamoja na ushawishi kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo ushawishi kwa watoto tu, pamoja na vijana na wanajamii wengine wote na taasisi ya msingi ni ya familia ambayo ina nafasi ya kwanza kabisa katika ukuaji wa mwanajamii yeyote na ina wajibu wa kutoa fursa za mwanajamii kujifunza na kufundwa fikra na mienendo sahihi hususan wakati wa utoto umri miaka sifuri mpaka saba. Hapa ndiyo kompyuta tunaiwekea *program* iweje, itusaidieje mbele ya safari. Sasa hapa ndipo ubongo unakuwa hadi kufikia 90%, kama ni nyumba umemaliza unakwenda *finishing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuje tuangalie hali ya familia zetu katika maisha ya sasa, lakini taasisi nyingine ni zile zinazotumia muda mrefu kukaa na watoto na vijana ikiwemo vituo vya malezi, shule, vyuo na jamii inayowazunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka kusema, akitoka mtoto nyumbani anakwenda shuleni hajafundwa vizuri kashavuka umri wa miaka mitano, haelewi jema na baya, haongei na wazazi wake, hana malezi yenye mwitikio, mtoto anajilea mwenyewe kwa *TV* kwenye ibada haendi. Akienda shuleni, akakutana na mwingine mbovu wanakuwa wabovu wawili wanaenda kuwaambukiza wengine matokeo yake darasa zima linakumbwa na ugonjwa wa ubovu. Hivyo familia lazima tuiangalie kwa kina, hivi sasa tuna familia za namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache kabisa, baadhi ya sababu za kuporomoka kwa maadili, kitabu hiki kizuri kinasema, sisi wote kama Taifa tumepuuza mila na desturi na taratibu za malezi ya asili zilizokuwa zikidhibiti mwenendo wa wanajamii. Pia athari hasi za utandawazi; hatujakaa na watoto wetu tuwaambie yule shetani tunayemsema, basi anaweza akawa amejificha kwenye huo mtandao, maana kuna mema na mabaya mle, watoto wetu muwe makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wanaingia mle wenyewe kimya kimya, hawana *foundation* katika ule ubongo wao wa umri wa miaka mitano. Mtoto ukimwambia usiku usitoke nje kuna nyoka, analishika lile ataenda nalo maisha yote, lakini mtoto hujamwambia kwenye mtandao ingia ukiwa na umri fulani, yeye anaingia tu kaoneshwa na rafiki yake, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunayo malezi holela. Ukiacha hapo, migogoro ya kifamilia, wazazi wanagombana mbele ya mtoto mpaka wana-*post* mitandaoni hawaoni kama ni shida. Hawakulelewa vizuri kipindi chao cha utotoni huko, wala Mwenyezi Mungu hayuko ndani yao, hatukuweka msingi mzuri. Mambo mengine ni haya ya umaskini na yenyewe mengine niyaache kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viashiria vyake ni nini? Ndiyo vyote vilivyosemwa leo na Waheshimiwa Wabunge kitabu hiki kimedadavua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapenzi ya jinsia moja, amesema Mheshimiwa Kampala, haya masuala ni dalili na viashiria vya kuporomoka kwa hayo maadili yenyewe kwa sababu sisi hatukuwekeza kuanzia kwenye familia mambo tuliyopaswa kuwekeza kwa watoto wetu. Tunayo madawa ya kulevya na pombe kupita kiasi na yenyewe ni mmomonyoko maadili, ni viashiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba za utotoni na kutupa watoto wachanga na yenyewe ni sehemu ya viashiria vya mmomonyoko wa maadili. Ukatili wa kijinsia, ubakaji, ulawiti na ukeketaji amesema Mheshimiwa Chipando, tena huko ndani wanagombana, ametoa ushauri mzuri sana hoja yake nzito na amenipa kitabu hapa nimeshaanza kukisoma, na chenyewe kimesema sababu za migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Chipando kutoka kwa *Rev*. Dkt. Mulenda Omary Kalama. Mimi nimemwambia Katibu Mkuu nitamkabidhi wakisome, wakichambue, wamwite tuje tuweke mikakati mizuri itokanayo na mawazo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la wanawake ambao wako kwenye ndoa au kwenye mahusiano kufanyiana vyote alivyovisema Mheshimiwa Chipando; ni kwamba wamekutana watu wawili ambao hawakulelewa kotekote. Wala hapa siyo kesi ya mwanamke peke yake, wala siyo kesi ya mwanume peke yake. Zinapokutana *positive* zote kwenye sayansi, huwa tunasema zinafanya *repulsion*. Zikikutana *negative* zote *repulsion,* hasa lazima ipatikane *positive* moja na *negative* zifanye *attraction*. Hili ni bomu litokanalo na malezi duni tuliyoyafanya kwa watoto wetu. Ndoa zaidi ya 40,000 kuelekea 50,000 huko ambazo zimeripotiwa zina migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume-*solve* wee, tukabaki na 31,000 tunaendelea nazo. Hii ina maana ni picha ya malezi ya watoto wetu wa kike na wa kiume. Hii ni hoja ambayo ananiambia kwamba Mheshimiwa Waziri kaangalie kwenye malezi na makuzi, jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia

hapa. Sasa wanakutana hawa *guest house*, wanapigana picha, huyu kamdanganya mkewe wameenda gesti, huyu naye kaja na video yake anamrekodi huyu. Hawa ni *negative* mbili zimekutana, hazitakaa zipatane, hawakulelewa wote hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema vizuri, katika sura ya wanaume, lakini wanawake pia tunao ambao hawalelewi vizuri. Suala la kuingia kwenye mahusiano linahitaji maandalizi. Kitabu hiki nimekisoma, nimeona hapa amesema mwenyewe huyu mwandishi kuwa makosa ya vijana katika ndoa; kutokuwa na maandalizi ya kutosha, kuingia kwenye ndoa kwa sababu ya tamaa, kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa kumchagua mume, mke wa kuishi naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anakwenda kumchagua mke na mume *Facebook*. Hii inakaaje? Aliambiwa na nani kwamba mapatano ya mahusiano ni mapatano yanayohitaji kumsikiliza Mwenyezi Mungu anasemaje? Ni mapatano ya kuweka urafiki mfahamiane na kufuata taratibu za mila na desturi mpaka ionekane hawa ni *positive* na *negative*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanguka anguko la malezi na makuzi kama Taifa, lazima turudi tukayatengeneze huko. Vinginevyo hapa utaona kwamba kwa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, 61.5% ya wakazi wa mjini wenye umri wa kuoa au kuolewa, hawajaingia kwenye ndoa. 55.5% ya wakazi wa vijijini walio kwenye umri wa kuoa au kuolewa nao hawajaingia kwenye ndoa. Hii ndiyo shida tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna athari nyingi kwa sababu ya muda sitaweza kusema zote, lakini tumefika mahali tunatengeneza kizazi kisicho na malezi bora na mwelekeo sahihi wa maisha ambacho kitazalisha wahitimu wenye ujuzi, lakini wasio na uadilifu wa kutumia ujuzi huo kwa manufaa ya umma, wanapigana, hasira na mihemko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wanaume, wanaofanyiwa hivi vitu, kwenye Dawati la Jinsia siwaoni, wanakufa na tai shingoni, lakini magerezani wamejaa kwa

sababu ya hasira. Mtu amekwambia huyu mtoto sio wako, na wewe tayari. Mwanamke ni kichwa cha familia, imeandikwa mahali. Je, tuwatengenezeje watoto wetu wa kiume na watoto wa kike ili waweze kushabihiana? Huu ndiyo mkakati wa malezi na makuzi ambao tunao kwa uchache. Tunahitaji kuongeza uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vikundi vya malezi na makuzi nimesema kwenye hotuba yangu. Azimio la Bogota tunahitaji vifike 200,000 ifikapo 2030 kule kwa wazazi. Tutakwenda kuhakikisha mkakati wa kuwekeza vituo vya kulea watoto kwenye jamii, acha hivi vya kwamba ana kesi, ameumizwa, mpelekeni makao, hapana. Kuna vile vya kwenye jamii, baba ameenda kazini na mama ameenda kazini, mtoto asiachwe nyumbani akalelewa na *TV* au na msaidizi yule asiye na hili wala lile kwenye malezi na makuzi, apelekwe kwenye vituo hivyo ambavyo vinamilikiwa na jamii vyenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tuna vituo karibia 250 na kitu, nimesema kwenye hotuba yangu kama sikosei, huu ndiyo mkakati tunaoendanao. Pia kuna malezi ya vijana balehe, mwili tu ukishaanza kuhamasika hivi, yeye anaona mimi tayari, haelewi hii jiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yatatufanya tutengeneze vijana ambao wana utulivu, wanaelewa mapito yao ya maisha, wanaelewa taasisi ya ndoa siyo ya kukimbilia tu hivi, wanaelewa kwamba inahitaji subira na kumcha Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya jitihada nyingi nyingine kama Serikali, muda hautoshi kusimulia tumefanya nini. Hizi *program* za malezi ya vijana nimezisema. Jambo jema kabisa somo la maadili limejumuishwa katika mitaala mipya ya shule za msingi. Hii itasaidia sana. Pia nyumbani lazima tulee wazazi, ukituletea shule mtoto wako ni mgumu, haendi na wengine, atawaharibu wenzake. Serikali itakusaidia kuweka mifumo ya malezi, lakini lazima mzazi ukishazaa, ukumbuke kuna kutunza na kuna kulea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili alilolileta, *challenge* na hoja nzuri Mheshimiwa Chipando, Ndugu wanaume wa Taifa hili niwaombe, tumeokoa watoto 6,000 na zaidi kutoka mitaani. Kila ukimwuliza mtoto baba yako yupo? Yupo, mama yako yupo? Yupo. Yuko wapi? Aliachana na baba, akaolewa. Baba naye? Yupo. Kaenda wapi? Kaoa kwingine. Kwa hiyo wewe? Mimi nikawa ninapigwa na mama wa kambo, na baba wa kambo, kotekote, nikakimbilia mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanaume tunatarajia tuwaombe sana tutafakari. Tunashukuru sana Vyama vya Wanaume vinasajiliwa kwa kasi, na ni ishara kwamba wameanza kuona umuhimu wa kukutana pamoja kutafakari. Tutawapa ushirikiano, kuwe na vyama vingi, mrudi kwenye mstari wenu ili mkikaa kwenye kile kichwa ambacho Mungu alikisema, mambo yote ninaamini yatakaa sawa huku chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake na ninyi, wako wanawake wazuri tu, wako wengine matata, hawa ndio watengeneza mmomonyoko wa maadili. Wengine wanaenda kukodi ngoma za rusha roho, ngoma sijui za vigodoro, wanaalika watoto wadogo wanapita nao kwenye *party*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wanawake wazuri na sisi tukae tuangalie malezi mpaka ya watu wazima, siyo ya watoto tu, ili hawa wanaofanya hivyo vitu waweze kuwa na mwisho wa kufanya.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikia kengele imelia. Kitabu hiki kinasema, baadhi ya changamoto za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili. Suala la maadili hatujalipa kipaumbele cha juu katika baadhi ya mipango ya maendeleo ya Serikali ngazi zote na jamii kwa ujumla, licha ya uwepo wa miongozo mbalimbali ya kisera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ikiulizwa, changamoto zao hivi leo hawataji zile zinazohusu asili ya maadili. Hivyo hata wawakilishi wao wanapoenda kwenye vikao rasmi hawazungumzi hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na Mheshimiwa Prof. Shemdoe, yupo safarini nje ya nchi. Kabla hajaondoka, yeye alikuwa Mkurugenzi wa Halmashauri, akawa Katibu Tawala wa Mkoa, akawa Katibu Mkuu wa TAMISEMI na sasa ni Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Humu ndani kuna Wakurugenzi wengi walikuwa wa Halmashauri, humu ndani kuna waliokuwa Makatibu Tawala, wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule hii ajenda, yaani siyo kipaumbele, haipo. Wanaongelea maji, wanaongelea afya, wanaongelea kilimo, wanaongelea kila kitu, lakini kwamba tuna shida ya mmomonyoko wa maadili kwa Gwajima, hapa ndipo shida inapoanzia, kwenye vipaumbele vinavyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee mazungumzo yangu ya awali. Ninaomba nirekebishe sentensi niliyosema, kwamba mwanamke ndiye kichwa cha familia, hapana. Nilitaka kusema mwanaume ndiye kichwa cha familia. Akikaa pale yeye, kama kichwa cha familia akajitambua vizuri sana na tukimsaidia kwenye malezi na makuzi ataweza kuhimili misukosuko ile; na inapotokea changamoto akaitisha kikao chake pale cha familia akasema mimi ndiye baba, wasipomsikiliza akaja ustawi wa jamii, sisi tutatoka ustawi wa jamii tutakwenda kwenye ile familia kutoa msaada wa ushauri nasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huenda binti yule ana tatizo la afya ya akili. Hivi tunaambiwa, katika watu 100, watu 25 wana afya ya akili. Kuna mambo mengi huko; ndugu wanaume wakipiganapigana na hawa mabinti au wake zao magerezani wamejaa tele. Haina afya, wala haina sababu. Watumie huduma za dawati la jinsia sisi tutawapa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nirejee nilikokuwa nimetokea, kwamba, kwa kuzungumza na Mheshimiwa Prof. Riziki Shemdoe, tumekubaliana, yeye kwa uzoefu wake tutahakikisha tunarudi

kule. Sisi Maendeleo ya Jamii kuwaelimisha wananchi waibebe hii ajenda, waione ina uzito sawa na kuomba barabara sawa na kuomba maji, sawa; na kuomba pembejeo za kilimo; lakini mabaraza yetu ya Madiwani tuone maswali mengi yanayohusiana na hatma ya malezi na makuzi kwenye Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhesabu maazimio mangapi yamepitishwa, lakini pia tuhesabu sheria ndogo zipi zimepitishwa za ku-*enforce* haya masuala ya malezi pamoja na mmomonyoko wa maadili yakawe sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingi tumechambua tumeona zinaongelea mapato ya Halmashauri, lakini malezi na makuzi ya mmomonyoko wa maadili siyo sehemu. Tunatarajia mwaka ujao tukija hapa tutahesabu sheria ngapi ndogo zimetungwa katika kuimarisha eneo hili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeniishia, siyo rafiki, nia ya kusema ni mengi. Tutaunda kamati za maadili katika kila Kijiji, kila kata, kila wilaya, na kila mkoa kwa mujibu wa mkakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa itoshe kusema, kwamba mambo ni mengi. Kulikuwa na hoja ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ambapo katika kuongeza mchango wa sekta ya maendeleo ya jamii kuelekea Dira 2050, ambayo inasisitiza mageuzi ya kuwa na Taifa lenye uwezo wa kumiliki na kutumia kikamilifu rasirimali zake kwa manufaa ya wananchi wote, Serikali inakamilisha Mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ya Mwaka 1996 ili kuakisi mabadiliko yaliopo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ya watalamu wa huduma za ustawi wa jamii pamoja na maendeleo ya jamii, ni kweli sheria hizi hazipo. Hapa taaluma hizo bado hazina mfumo mahsusi wa kisheria unaosimamia usajili, maadili, viwango vya kitaaluma na uwajibikaji kama ilivyo kwa taaluma nyingine za sheria, uhandisi, udaktari na nyinginezo. Hivyo basi, tunaamini sheria hizi zitasaidia kulinda hadhi ya taaluma, kuimarisha ubora

wa huduma zinazotolewa kwa wananchi na kuweka mfumo wa leseni za kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Wizara itaanza mchakato wa kuandaa sheria hizo katika mwaka ujao wa fedha kwa lengo la kuimarisha taaluma hizo, kuongeza uwajibikaji, kuboresha utoaji wa huduma na kuziwezesha kuchangia kikamilifu kuelekea Dira 2050. Idadi ya watalamu wa ustawi wa jamii kweli bado iko ndogo, wako 12% kati ya maafisa 18,481 wanaohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa watalamu wa maendeleo ya jamii waliopo ni 4,882 na kuna upungufu wa watamu 684. Wizara itaendelea kufuatilia utumishi ili kuendelea kuajiri watalamu hao kadri kibali kinavyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya vyuo na watalamu wa maendeleo ya jamii, kweli katika kuongeza thamani na ubora wa wahitimu wa taasisi wa vyuo vya maendeleo ya jamii Serikali inaendelea kuwezesha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Leo tumeomba tupitishiwe kwenye bajeti yetu ili ujenzi uendelee, hususan kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, hosteli ya wasichana katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Monduli na Uyole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetenga fedha za ujenzi wa miundombinu katika Vyuo vya Ruaha na Rungemba. Fedha za maendeleo zilizotengwa zitaendelea kuboresha miundombinu ya Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na vyuo vingine vya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukatili wa kijinsia, tunatekeleza Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 inayolenga kuhakikisha wanawake na wanaume wanapata fursa sawa za kushiriki na kunufaika na maendeleo yao. Sera haitetei jinsi moja dhidi ya nyingine, bali inakuza usawa wa kijinsia kwa kutambua mchango wa wanawake na wanaume katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, huduma zote tunazowapatia wanawake katika dawati la jinsia na wanaume wanatakiwa kuzipata. Hata hivyo, kwa bahati mbaya hawajitokezi kwa wingi. Wamejengwa hofu kwamba wao hawatakiwi kusikitika, majibu yao wao ni kupiga na kuishia jela. Tutaendelea kuwaelimisha watoke kwenye fikra hizo ili watumie huduma hizi, na sisi tuingie katikati ya maisha yao kurekebisha pale wanaposumbuliwa na jinsi ile nyingine ya kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua nafasi na umuhimu wa wanaume katika kufanikisha usawa wa kijinsia, Wizara imeunda Kikosi Kazi cha Taifa cha Ushirikishwaji Wanaume na Wavulana ambacho kinaratibu juhudi za kukuza ushiriki wao katika kuimarisha familia, kuzuia ukatili wa kijinsia, kukuza uwezeshaji wa kiuchumi na kujenga mahusiano yenye usawa. Pia tunaandaa Mwongozo wa Taifa wa Ushirikishwaji wa Wanaume na Wavulana katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuhakikishia kwamba Wizara haitajikita kutetea wanawake pekee, na hilo na wao wajue. Tutawasikiliza wote; wanaume na wanawake kwa usawa unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumziwa suala la afya ya akili na msaada wa kisaikolojia. Kama nilivyosema, kwamba hili ni tatizo. Tutaendelea kushirikiana na Taasisi ya *TAPA* ambayo wanashughulika na masuala ya afya ya akili kuona namna gani twende kulipunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umiliki wa maeneo yaliyo chini ya Wizara, upatikanaji wa hatimiliki wa maeneo yanayomilikiwa na Wizara hadi kufikia Aprili, 2026. Wizara imewezesha upatikanaji wa hati 18, hivyo kufikia hati 21 kati ya 39 sawa na 54%. Hati sita ziko kwenye hatua za mwisho kukamilishwa. Tumeunda Kamati maalumu ya kushughulikia maeneo ya Wizara yenye changamoto za mipaka ili kukamilisha upatikanaji wa hati hiyo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisikia kengele, na mambo mengi yapo ambayo ni mazuri ya kuzungumzia hapa, ikiwemo kuhusu mikopo, kwamba, baadhi ya wananchi wetu hawapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashirikiana na Mheshimiwa Waziri Prof. Shemdoe kwenda kuangalia nini kinaendelea pamoja na akina mama wenye watoto walemavu. Hawa tutapata takwimu zao tuone jinsi ya kushirikiana na Wizara inayoshughulikia masuala ya wenye ulemavu kwa Mheshimiwa Kabudi hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, eneo hilo. Wale wazee wenye ulemavu na wanawake wenye ulemavu tumesikia hoja ya Mheshimiwa Nassriya na yenyewe tumeichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zote nimeziandika, ziko humu. Kwa sababu ya muda ninaomba niseme nimezipokea. Tutazileta kwa maandishi ili Bunge lako Tukufu liweze kupata kumbukumbu sahihi za *response* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya mengi ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dorothy Gwajima, ahsante sana. Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi.

MWENYEKITI: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na kitabu cha pili, matumizi ya kawaida, Fungu 53, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Ukurasa wa 457 na kwenye kishikwambi ni ukurasa wa 515.

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Kifungu 1001 - *Administration and HRM*.....Sh. 6,062,588,917
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 974,480,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....Sh.1,849,945,600
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 684,544,664
Kifungu 1005 - *Government Communication Unit*.....Sh. 384,723,300
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.....Sh. 605,832,500
Kifungu 1007 – *ICT Unit*..... Sh. 558,271,800
Kifungu 1008 - *Legal Service Unit*.....Sh. 581,886,019
Kifungu 1009 – *Monitoring & Evaluation Unit* ..... Sh. 468,642,900
Kifungu 2001 - *Community Development Institutes*.....Sh. 15,179,461,100
Kifungu 2002 - *Community Development*..... Sh. 1,771,203,200
Kifungu 3001 - *Gender Development*.....Sh. 1,521,144,900
Kifungu 3002 - *Children Development*.....Sh. 1,153,664,300
Kifungu 3003 - *Special Groups*.....Sh. 1,471,709,600
Kifungu 4001- *Non-Government Organizations*……Sh. 2,386,934,300
Kifungu 5001 - *Social Welfare Division*..... Sh. 14,482,767,900

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*..... Sh. 20,475,013,417
Kifungu 1009 – *Monitoring & Evaluation Unit*..... Sh. 90,000,000
Kifungu 2001 - *Community Development Institutes*.....Sh. 14,200,000,000
Kifungu 3001 - *Gender Development*..... Sh. 2,047,315,099
Kifungu 3002 - *Children Development*.....Sh. 934,011,725
Kifungu 3003 - *Special Groups*.....Sh. 10,500,000,000
Kifungu 5001- *Social Welfare Division* .....Sh. 9,640,101,759

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja.

T A A R I F A

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Ninaomba kwamba Taarifa ya Kamati ya Matumizi, ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa ninatangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, baada ya kuwa tumeishapitisha, taratibu nyingine zitaendelea kufuata.

Nitumie fursa hii kumpongeza sana kwa mara nyingine Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na kuitenga Wizara hii kwa umuhimu wake ikawa Wizara peke yake inayojitegemea.

Nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi pamoja na Katibu Mkuu wao na Watendaji wote wa Wizara, bila kusahau Kamati yetu ambayo inashughulikia masuala hayo ya maendeleo ya jamii kwa kazi kubwa ambayo inafanya na ushirikiano ambao wanapeana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, kwa kweli, kama ambavyo wamezungumza wote, kazi hii siyo yao peke yao, ni ya Serikali nzima kwa maana Wizara nyingi zinaguswa. Wamesema hapa Waheshimiwa Wabunge, nami niseme pia kwamba, Wizara ya

Katiba na Sheria itusaidie katika maeneo machache ya kurekebisha sheria ambazo zimepitwa na wakati.

Waheshimiwa Wabunge, tuna Sheria ya Vileo ya Mwaka 1969, vijana wetu wengi walio chini ya umri wanatumia vileo vya aina mbalimbali. Hii inapelekea mporomoko mkubwa wa maadili katika eneo hilo. Kwa hiyo, niwaombe sana wenzetu wanaohusika na Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu na Ofisi yake, tujaribu ku-*review* tuone hii sheria tuiboreshe ili tuweze kuona vijana wetu wanaweza kunusurika na hili janga la vileo ambavyo vinatumika, ambavyo wanaruhusiwa kwa mujibu wa sheria hiyo ambayo ipo ambayo haijafanyiwa maboresho.

Waheshimiwa Wabunge, pia hii Sheria ya Ndoa ya Mwaka ya 1971; tukitaja Sheria ya Ndoa watu wengi wanafikiria ni lile suala la mke na mume tu, yaani tu kuoana, umri wa kuoana. Mle ndani ya Sheria ya Ndoa kuna mambo mengi yanayohusu wanandoa. Majukumu ya wanawake na majukumu la wanaume yote yameandikwa mle.

Tukiweza kufanya *re-view* vizuri, ninafikiri ndoa zetu zitanusurika, na utelekezwaji wa wanawake na watoto unaweza ukapungua kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, ninaomba sana vitengo vinavyoshughulikia na mambo hayo ya urekebishaji wa sheria waweze kuleta hapa Bungeni ili tuweze kufanya marekebisho na kulinusuru Taifa letu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla wake wote, niseme kwamba hili suala la wote, ni Wizara zinazohusika, nyingine zote nimetaja. Hata Wizara ya Elimu inahusika, hata Wizara hiyo ya Mambo ya Ndani ya Nchi yetu, Mheshimiwa Patrobas inahusu pale. Wizara ya Elimu pia, tumeona hapa amesema kwamba tumeingiza somo la maadili kwenye Wizara ya Elimu, linahusiana na masuala ya jamii.

Hata hivyo, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge, sisi wenyewe ni vioo vya jamii. Tukiwa tunaonyesha mfano bora, hata jamii itatuelewa na kusikia. Kwa hiyo, ninaomba tuanzie sisi

wenyewe, tuwe na maadili mazuri ili tunapozungumza na wale wananchi ambao tunawaambia waweze kutuelewa.

Waheshimiwa Wabunge, suala la kusikitisha sana ni kwamba, kwa mfano, jambo la ulawiti halifanywi na wanawake, ni vigumu mwanamke kumlawiti mtoto wa kiume. Linafanywa na wanaume wetu au baadhi ya wanaume wetu ambao tunawapenda na kuwaheshimu sana.

Kwa hiyo, ninaomba sana ndugu zetu wanaume tuchukue wajibu wetu tuone kwamba jamii yetu tunaenda kuipoteza. Mtoto wa kiume tunapomharibu tuondoa nguvu kazi ya mtoto wa kiume katika Taifa letu; na wanaofanya hivyo ni wanaume wenzetu. Ni kitu cha kusikitisha. Kwa hiyo, tuwalinde watoto wetu. Akina mama tujitahidi; na kinababa wenye tabia hizo tuwafichue tusione aibu. *(Makofi)*

Kuhusiana na suala la utelekezaji wa wanawake wenye watoto *(single mothers)* ni wengi kuliko *single fathers* tukifanya sensa. Hii inasikitisha sana. Pia wanawake tuwe na huruma na wenzetu. Unaona baba ameishatelekeza watoto watano na mke wake, wewe unampokea, unamkumbatia, na unampenda, wakati mwenzako kule anateseka.

Kwa hiyo, ninaomba sana wanawake kwenye hilo tuhurumiane, tusiwazoeshe hivyo ili waweze kujua kwamba kile walichokifanya kule ni kibaya, huku na wewe atakuja kukufanyia hivyo hivyo, aje akuache.

Kwa hiyo, tunaomba sana jamii nzima ituelewe hivyo. Hatuna nia ya kupambana katika jinsia mbili, nia yetu ni kuweka usawa wa kijinsia. Kwa hiyo, ninaomba sana tuelewane hivyo.

Nitumie fursa hii kwa mara nyingine kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote na kuwatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa bajeti yetu hii ya Wizara yetu muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwatakie jioni njema na ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 2.37 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 2 Juni, 2026 Saa Tatu Asubuhi)

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA